# MUUNDO NA USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA KIUPELELEZI YA KISWAHILI

**NA**

**IKUATHU SILAS THURANIRA**

**Tasnifu hii imewasilishwa ili kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamifu katika Idara ya Kiswahili**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2022**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolea kwa mahitaji ya shahada ya uzamifu katika chuo kikuu kingine chochote

Ikuathu Silas Thuranira — 28/10/2022 Tarehe

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza mahitaji ya Shahada ya Uzamifu kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na chuo kikuu cha Nairobi.

Prof Evans Mbuthia — 29-10-2022 Tarehe

(Msimamizi)

Prof Tom Olali — 29/10/2022 Tarehe

(Msimamizi)

Prof Wamitila. K.W. — 29/10/2022 Tarehe

(Msimamizi )

# Tabaruku

Tasnifu hii naitabaruku kwa mama yangu, Rosalia Kabitore, kwa kunionjesha utamu wa elimu katika miaka ya mapema katika shule ya msingi, kwa mke wangu, Mary Machaki na wanangu, Caleb, Boaz na Eva.

## Shukrani

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na afya nzuri wakati wa utafiti na kwandika tasnifu hii. Pili, kazi hii haingekamilika bila ushauri na uelekezaji wa wasimamizi wangu. Kwa njia spesheli nawashukuru Profesa Evans Mbuthia, Profesa Tom Olali na Profesa K.W. Wamitila kwa kunifaa kwa hali na mali. Walinielekeza na kunipa nasaha wakati wa utafiti na uandishi wa tasnifu hii. Wamenifaa kwa vitabu na makala mbalimbali kando na kutumia muda wao mwingi katika kusoma kazi hii na kutoa maoni.

Kadhalika, shukrani jazila ziwaendee wahadhiri wa idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi kwa msaada wao ulionifaa kwa njia mbalimbali. Nawashukuru Profesa Iribe Mwangi, mwenyekiti wa idara ya Kiswahili, Profesa John Habwe, Profesa Mwenda Mbatiah, Profesa Rayya Timammy, Daktari Zaja Omboga, Daktari Prisca Jerono, Daktari Amiri Swaleh, Daktari Ayub Mukhwana, Daktari Samson Ongarora, mwalimu Sanja Leonard na mwalimu Mary Ndung'u. Namshukuru pia daktari Timothy Kinoti Ngaruthi wa Chuo Kikuu Cha Embu kwa mawaidha yake kupitia mazungumzo tuliyofanya.

Nawashukuru pia wasomi wenzangu tuliosaidiana nao kupitia mahojiano na mazungumzo kupitia mitandao ya kijamii na mawasiliano ya simu. Hawa ni Shadrack Kirimi, Edward Lokidor, Victor Amenya, Rose Kawira, Hillary Kimeto, Rose Munyao, Sista Teresa, Josephat Gitonga miongoni mwa wengine. Mungu awasaidie katika safari hii ya kiusomi. Siwezi kuisahau aila yangu kwa kunifaa kwa njia mbalimbali. Katika muktadha huu shukrani za dhati zimwendee mke wangu, Mary Ngithi, watoto wangu, Caleb, Boaz na Eva kwa uvumilivu na maombi yao wakati wa utafiti huu. Namshukuru pia kakangu John Kobia kwa kunitia shime kumaliza kazi hii mapema pamoja na maombi yake. Rafiki zangu, Bwana Akwalu Morris, Bwana Miringo na walimu wenzangu wote nawashukuru kwa kunitakia mema katika safari hii. Mungu awabariki nyote.

# Ikisiri

Tasnifu inahusu uchunguzi wa muundo na usimulizi katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Ili kufanikisha uchunguzi huu, malengo matatu yalizingatiwa. Malengo hayo yalikuwa; kuchunguza usimulizi katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, kutathmini usawiri wa wahusika katika riwaya teule za kiupelelezi za Kiswahili na mwisho, kuchunguza mbinu za ujenzi wa msuko katika riwaya teule za kiupelelezi za Kiswahili. Kuhusu lengo la kwanza, utafiti huu ulichunguza vipengele vya usimulizi vya mtazamo na sauti za kisimulizi. Kuhusu lengo la pili, utafiti huu ulijikita katika utathmini wa jinsi wahusika wa riwaya ya kiupelelezi wanavyosawiriwa kwa njia maalum inayowapambanua na wahusika wapatikanao katika tanzu nyinginezo za riwaya. Ili kutekeleza lengo la tatu, mbinu za kimtindo zitumikazo kuukuza msuko wa riwaya teule zilichunguzwa. Data ya kimsingi iliyotumika ilipatikana kutoka kwa riwaya za kiupelelezi za waandishi mbalimbali. Hizi ni riwaya tatu za Mohammed Said Abdulla za *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960), *Kisima cha Giningi* (1968) na *Duniani Kuna Watu* (1974), riwaya mbili za Ben Mtobwa za *Tutarudi na Roho* Zetu (1984) na *Salamu Kutoka Kuzimu* (1987), riwaya mbili za Elvis Musiba za *Njama* (1984) na *Uchu* (2000), riwaya ya Godfery Levi ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wezi* (1975) na riwaya ya *Simu ya Kifo* (1960) ya Faraj Katalambulla na mwisho, riwaya ya John Simbamwene ya *Kwa Sababu ya Pesa* (1971). Ili kuafikia malengo ya kazi hii, tulitumia nadharia tatu ambazo ni nadharia ya utanzu, nadharia ya naratolojia na nadharia ya umitindo. Nadharia ya utanzu ilituwezesha kuhakiki sifa bainifu za utanzu wa riwaya za kiupelelezi. Nadharia ya naratolojia nayo ilitumika katika kuchanganua vipengele vya kisimulizi vya mtazamo pamoja na nafsi za usimulizi katika riwaya teule. Ili kushughulikia mbinu za kimtindo zinazofanikisha ujenzi wa msuko katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili, nadharia ya umitindo ilitumika. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa riwaya nyingi za kiupelelezi zimetumia mtazamo nje katika usimulizi wa matukio. Usimulizi wa aina hii unampa msimulizi uhuru wa kusimulia mengi na kwa njia yenye utendeti. Imegunduliwa kuwa suala la mtazamo linajitokeza katika sawia nne ambazo ni sawia ya kiitikadi, sawia ya kimwanda-wakati, sawia ya kisaikolojia na sawia ya kiisimu. Imebainika kuwa wahusika wakuu katika riwaya za kiupelelezi wanaweza kuwekwa katika makundi matatu ambayo ni; waahusika wahalifu, wahusika wahasiriwa na wahusika wapelelezi.Makundi haya yanaweza pia kujitokeza kwa mtindo wa uwili; yaani, mpelelezi na msaidizi wake, mpelelezi na mhalifu na mhalifu na mpelelezi. Kuhusu msuko, utafiti huu umebainisha kuwa riwaya ya kiupelelezi huwa na usambamba wa hadithi mbili zikiwa ni hadithi ya uhalifu na ile ya uchunguzi. Ili kufikia muwala wa msuko huu, mbinu kadhaa hutumika. Mbinu hizo ni taharuki, mbinu rejeshi, usambamba, sadfa, hotuba miongoni mwa mbinu nyinginezo. Muundo wa kimsuko wa riwaya hizi unasalia kuwa sahili, usiokuwa na hadithi tegemezi nyingi wala mbinu rejeshi changamano. Uwepo wa msuko sahili ni sifa kuu inayorahisisha usomekaji na kuzifanya riwaya za kiupelelezi kuainishika kama fasihi pendwa.Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusu riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili hususan kuhusu tanzu nyinginezo za kifasihi kama vile drama, hadithi fupi na mashairi kwa lengo la kubaini ikiwa kuna tamthilia au hadithi fupi za kiupelelezi katika fasihi andishi ya Kiswahili..

## ABSTRACT

This study focused on the structure and narration in the Kiswahili detective prose. Toward this end, the study pursued three objectives namely; to examine how narration is carried out in the Kiswahili detective prose, to analyse the construction and portrayal of characters in the Kiswahili detective prose, and thirdly, to investigate various styles used in the construction of plot in the Kiswahili detective prose. To achieve the first objective, the research dwelt on the narrative voice and facets of focalization while for the second objective the focus was on the unique portrayal of the detective character, the criminal and the victim. To achieve the third goal, the focus was on the stylistic devices that aid in the development of the plot structure of the select Kiswahili detective prose works. Primary data was collected from the following Kiswahili detective prose writers; Mohammed Said Abdulla's *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960) [The Ancestors' Grove], *Kisima cha Giningi* (1968) [The Well of Giningi] and *Duniani Kuna Watu* (1974) [The People of this World], Ben Mtobwa's *Tutarudi na Roho* Zetu (1984) [Shall we Return Safe?] and *Salamu Kutoka Kuzimu* (1987) [Greetings from the Afterworld], two detective novels by Elvis Musiba, namely, *Njama* (1984) [A Conspiracy] and *Uchu* (2000) [Excessive Greed], Godfrey Levi's *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975) [A Tough Detective and a Gang of Criminals], John Simbamwene's *Kwa Sababu ya Mapenzi* (1971) [Because of Love] and lastly, *Simu ya Kifo* (1965) [A Call of Death] by Faraj Katalambulla. An ecclictic theorical approach was used in the analysis of the selected texts. Narratogy was used to analyse perspective planes and narrative voice. The ideas of narratologists such as Rimmon-Kenan and Mike Bal were used. To achieve a proper study of the salient and disntictive features of the Kiswahili detective fiction, generic theory was used and finally, we used the stylistic approach in examining the structural and linguistic features employed in the construction of plot in the Kiswahili detective fiction. It was found out that the Kiswahili detective fiction is mostly narrated through the external perspective where an omniscient narrator gives an account of all events, thereby offering a very objective narration.On characterization, the study discovered that detective characters can be uniquely grouped into three categories namely, the criminal, the victims and the detective. These could in terms of actions be grouped further in pairs such as; the detective himself and his assistant, the detective and the criminal or the criminal and the victim. On plot construction, this study reveals that the plot of the Kiswahili detective prose is composed of two parallel story lines; the story of the crime and the story of the investigation. To achieve a cohesive and entertaining chronology of events, various styles are used. These includes suspense, coincidence, back referencing among other stylistic devices. The plot structure remains simple with minimal reversals and narrative embedments. It is this simplicity of the plot and usage of great suspense and surprises that makes detective prose works be classified as popular fiction. This research calls for more investigation of the Kiswahili written literature with a view to unearthing if there are detective plays, short stories and/or detective poetry.

## Orodha ya Jedwali na michoro ya Kielelezo

**Jedwali** **Ukurasa**

Jedwali2.1 Mifano ya wahusika wa kipelelezi na wasaidizi wao……………… 38

**Michoro**

Kielelezo 3.1 Kielelezo kinachoonyesha cha hadithi msingi na hadithi tegemezi …… 108

Kielelezo 3.2 Kielelezo kinachoonyesha hadithi tegemezi za daraja tofauti ………………………………………………………….…………… 108

Kielelezo 3.3 Kielelezo kinachoonyesha hadithi kadhaa tegemezi ambazo ziko kivyake……………………………………………………………………………… 109

Kielelezo 5.1 Mchoro ukionyesha mbinu rejeshi ndani …………… ………… 182

Kielelezo 5.2 Mchoro ukionyesha mbinu rejeshi nje…………………………… 182

## Orodha ya Vifupisho

**ANC-** African National Congress- Chama cha kisiasa kikubwa zaidi nchini Afrika Kusini

**CIA-** Central Intelligence Agency- Shirika la kiupelelezi la Marekani

**KGB-***Komitet gosudartvennoy bezopasnoti***-** (Committee for State Security’**)-** Shirika la Kiupelelezi la Urusi.

**NAM-**Non Aligned Movement- Vuguvugu la mataifa yasiyoegemea upande wowote wakati wa vita baridi vya ulimwengu.

**PAM**- Pan African Movement- Muungano wa kutetea haki na uhuru wa watu wenye asili ya Kiafrika kokote walipo duniani.

**OAU-**Organisation of African Unity- Umoja wa Nchi Huru za Afrika

**IQ**-Intelligence Quotient- Kipimo cha akili ya binadamu.

**PLF-**Peoples Liberation Front-Chama cha kutetea uhuru Afrika Kusini

## Orodha ya Dhana Muhimu Zilizotafsiriwa

**Secret Agent/Ajenti wa kisiri**………Afisa wa kijasusi anayetumwa nchi nyimgine kufanya upelelezi kisiri

**Style/Mtindo**………………………………………Upekee wa kifani katika kazi za kifasihi

**Popular Literature/Fasihi Pendwa**…………….Hutumiwa kuelezea fasihi Ambayo hudhamiria kuburudisha. Sifa kuu yake ni kuwa aina hii ya fasihi hupendwa na watu wengi.

**Popular Novel/Riwaya Pendwa**…………….Aina ya riwaya ambayo hushughulikia Masuala kama vile uhalifu, upelelezi, mapenzi na anasa ili kuburudisha.

**Detective Novel/Riwaya ya kiupelelezi**................Ni kijitanzu cha riwaya pendwa ambacho huhusu uchunguzi wa masuala mbalimbali hasa uhalifu.

**Committed Literature/Fasihi Dhati**…………Hutumiwa kuelezea fasihi ambayo huhusu masuala halisi yanayoiathiri jamii. Hulenga kuirekebisha, kuielekeza na kueleimisha jamii.

**Committed novel/Riwaya Dhati**…………aina ya riwaya inayohusu matatizo halisi ya kijamii na ambayo hulengwa na waandishi ili yatatuliwe au yaepukwe.

**Hard-boiled/Riwaya ya Kiupelelezi ya Kimarekani**…….Mtindo wa riwaya ya kiupelelezi ulioibuka Marekani katika miaka ya baada ya vita vikuu vya pili vya Ulimwengu.

**Golden age of Detective Fiction/Kipindi cha Urasimi cha riwaya ya kiupelelezi**……………………………..Kipindi cha baina ya miaka ya 1920-1930 ambapo riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi ilishuhudia mabadiliko mengi.

**YALIYOMO** **UKURASA**


UNGAMO....................................................................................**Error! Bookmark not defined.**

Tabaruku .......................................................................................................... iii

Shukrani .......................................................................................................... iv

Ikisiri .......................................................................................................... v

Abstract.......................................................................................................... vi

Orodha ya jedwali na michoro ya kielelezo.......................................................... vii

Orodha ya Vifupisho ………………………………… …………………….………...viii

Orodha ya Dhana Zilizotafsiwa..........................................................................viii

**SURA YA KWANZA: MSINGI WA UTAFITI ........................................................... 1**

1.1 Usuli wa Mada ................................................................................................ 1

1.2 Tatizo la Utafiti ................................................................................................ 5

1.3 Maswali ya Utafiti............................................................................................ 6

1.4 Malengo ya Utafiti ............................................................................................ 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ................................................................................ 6

1.6 Upeo na Mipaka ................................................................................................ 8

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Fasihi Pendwa na Riwaya ya Kiupelelezi ........................ 8

1.7.1 Masuala ya Kijumla Kuhusu Fasihi Pendwa na Riwaya ya Kiupelelezi ............ 9

1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Fani Katika Riwaya za Kiupelelezi ............................ 14

1.8 Msingi wa Kinadharia ...................................................................................... 19

1.9 Mbinu za Utafiti .............................................................................................. 23

1.9.1 Ukusanyaji wa data ...................................................................................... 23

1.9.2 Uteuzi wa Sampuli ........................................................................................ 24

1.9.3 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo ........................................ 24

1.9.4 Mbeko Katika Utafiti. ...................................................................................... 25

1.10 Hitimisho......................................................................................................... 25

**SURA YA PILI:UKUAJI NA MAENDELEO YA RIWAYA YA KIUPELELEZI............ 26**
2.1 Utangulizi................................................................................................................... 26
2.2 Vyanzo vya Riwaya ya Kiupelelezi katika Kifasihi Simulizi na Maandishi ya Mapema ...... 27
2.3 Chimbuko na Maendeleo ya Riwaya ya Kiupelelezi ya Kimagharibi .................................. 31
2.4 Riwaya ya kiupelelezi katika kipindi cha Urasimi (1920-1930) ......................................... 36
2.5 Sababu za Maendeleo Makuu ya riwaya ya Kiupelelezi Wakati wa Urasimi ........................ 42
2.6 Riwaya ya Kiupelelezi katika Nchi za Kimashariki ............................................................ 44
2.7 Riwaya za kiupelelezi Afrika............................................................................................ 46
2.7.1 Riwaya ya Kiupelelezi Afrika Magharibi ........................................................................ 46
2.7.2 Riwaya ya Kiupelelezi Kusini mwa Afrika...................................................................... 48
2.7.3 Riwaya ya Kiupelelezi ya Afrika Mashariki (Kiswahili)................................................ 51
2.7.3.1 Sifa za Riwaya ya Kiupelelezi ya Kiswahili ................................................................ 56
2.7.3.2 Sababu za Kuzuka na Kukua Kwa Riwaya ya Kiupelelezi ya Kiswahili ..................... 59
2.7.3.3 Wasifu wa Waandishi na Muhtasari wa riwaya zinazohakikiwa.................................. 61
2.8 Hitimisho......................................................................................................................... 64

**SURA YA TATU:USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA KIUPELELEZI YA KISWAHILI**
3.1 UTANGULIZI ................................................................................................................... 67
3.2 Sauti za Kisimulizi............................................................................................................ 67
3.3 Udhihirikaji wa Msimulizi................................................................................................. 68
3.3.1 Maelezo ya Kimandhari ................................................................................................. 68
3.3.2 Utambulishaji wa mhusika.............................................................................................. 69
3.3.3 Maelezo ya Mpito wa Wakati ......................................................................................... 69
3.3.4 Tathmini ya kisimulizi .................................................................................................... 70
3.3.5 Ripoti Kuhusu kile ambacho hakikusemwa wala kufikiriwa........................................... 71
3.3.6 Tafsili ya Mhusika........................................................................................................... 71
3.4 Dhima ya Msimulizi ......................................................................................................... 72
3.4.1 Dhima ya Usimuliaji ...................................................................................................... 72
3.4.2 Dhima ya Uelekezaji....................................................................................................... 73
3.4.3 Jukumu la Kumshirikisha msomaji................................................................................. 74

3.4.4 Jukumu la Kutoa Ushuhuda ........ 74
3.4.5 Jukumu la Kuendeleza Itikadi ya mwandishi ........ 75
3.5 Mtazamo katika Usimulizi ........ 76
3.5.1 Mtazamo wa Ndani ........ 77
3.5.2 Mtazamo wa Nje ........ 78
3.5.2.1 Mtazamo Katika Sawia ya Kiisimu ........ 79
3.5.2.2 Mtazamo Katika Sawia ya Mwanda-Wakati ........ 84
3.5.2.3 Mtazamo katika Sawia ya Kiitikadi ........ 90
3.5.2.4 Mtazamo Katika Sawia ya Kisaikolojia ........ 98
3.5.2.4.1Matumizi ya Maneno ya Mkabala (Verba Sentiendi) ........ 100
3.5.2.4.2 Matumizi ya Vitenzi Visaidizi vya Uwezekano, Idhini na Masharti ........ 103
3.6 Simulizi Tegemezi ........ 107
3.6.1 Dhima ya Hadithi Tegemezi ........ 110
3.6.1.1 Dhima ya Kiufafanuzi ........ 110
3.6.1.2 Dhima ya Kidhamira ........ 111
3.6.1.3 Dhima ya Kiutekelezaji (uwekaji msingi wa kimsuko) ........ 111
3.7 Hitimisho ........ 113

**SURA YA NNE:UHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KIUPELELEZI YA KISWAHILI 114**
4.1 Utangulizi ........ 114
4.2 Mbinu za Usawiri wa Wahusika ........ 116
4.2.1 Uwasilishaji wa Moja kwa Moja ........ 117
4.2.2 Usawiri wa Kiishara (Usio wa Moja kwa Moja) ........ 119
4.2.2.1 Vitendo vya wahusika ........ 120
4.2.2.2 Usemi wa Wahusika ........ 122
4.2.2.2.1 Dayalojia ya Kinathari na Uhusika ........ 125
4.2.2.2.2. Uzungumzi Nafsiya na Mkondo wa Ung’amuzi ........ 127
4.2.2.3 Mwonekano wa nje kama kiashiria cha Uhusika ........ 130
4.2.2.4 Mandhari na Uhusika ........ 134
4.2.2.5 Analojia katika ukuzaji wa Uhusika ........ 136
4.2.2.5.2 Analojia ya kimahali ........ 140

4.2.2.5.3 Analojia ya Kiulinganuzi wa wahusika ... 141
4.3 Uhusika wa Kimwingilianomatini ... 142
4.4 Uhusika wa Kifomyula katika Riwaya ya Kiupelelezi ... 144
4.4.1 Uhusika wa Mpelelezi ... 145
4.4.2 Usawiri wa wahusika Wahalifu ... 157
4.4.3 Usawiri wa Wahusika Wahasiriwa ... 164
4.5 Uhusika Usaidizi ... 167
4.5.1 Mhusika Msaidizi wa Kike ... 169
4.6 Ulinganisho wa Kihusika katika riwaya Teule ... 173
4.7 Hitimisho ... 174

**SURA YA TANO:MSUKO KATIKA RIWAYA ZA KIUPELELEZI ZA KISWAHILI . 176**
5.1 UTANGULIZI ... 176
5.2 Mbinu za Kimtindo na Msuko ... 179
5.2.1 Usambamba wa Hadithi Mbili ... 179
5.2.2 Anakroni na Msuko ... 180
5.2.2.1 Mbinu Rejeshi ... 181
5.2.2.2 Mbinu Elekezi ... 184
5.2.2.2.1 Mbinu Elekezi Yakini ... 186
5.2.2.2.2 Mbinu Elekezi Isoyakini ... 187
5.2.3 Mwingilianomatini na Msuko ... 188
5.2.3.1 Urejelezi wa riwaya za awali za mwandishi mmoja ... 189
5.2.3.2 Urejelezi wa Riwaya za Waandishi Wengine ... 191
5.2.4. Taharuki na Msuko ... 194
5.2.4.1 Vijenzi vya Taharuki katika Riwaya za Kiupelelezi ... 194
5.2.5 Sadfa na Msuko ... 202
5.2.6 Vyombo vya Habari na Ukuzaji Msuko ... 206
5.2.7 Barua na Maandishi Mengine katika Msuko ... 211
5.2.8 Hotuba ya Mpelelezi na Ukuzaji wa Msuko ... 217
5.3 Mbinu za Ucheleweshaji wa Msuko ... 220
5.3.1 Misukumo Pofu ... 220

5.3.2 Mazungumzo ........................................................................................................ 225
5.4 Hitimisho........................................................................................................................ 229

**SURA YA SITA:MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO................................. 231**
6.1 UTANGULIZI ................................................................................................................ 231
6.2 Muhtasari ...................................................................................................................... 231
6.3 Matokeo ya Utafiti ........................................................................................................ 232
6.4 Hitimisho........................................................................................................................ 236
6.5 Mapendekezo ................................................................................................................ 237
6.6 Changamoto za Utafiti Huu .......................................................................................... 238
**MAREJELEO ................................................................................................................ 239**

# SURA YA KWANZA

# MSINGI WA UTAFITI

## 1.1 Usuli wa Mada

Historia ya ukuaji wa nathari ya Kiswahili inaonyesha kwamba fasihi dhati imekua na kuendelezwa kwa kasi zaidi kuliko Fasihi Pendwa. Ushahidi wa kauli hii unatokana na kweli kwamba kuna idadi kubwa ya tahakiki na vitabu vilivyochapishwa kuhusu fasihi dhati na hasa utanzu wa riwaya. Mulokozi (1996:52) anasema kuwa fasihi ya Kiswahili iliyohakiki maisha ya kijamii ilijitokeza kuanzia karne ya kumi na tisa kupitia kazi kama vile za Muyaka Bin Haji huku Fasihi Pendwa ya Kiswahili ikijitokeza katika miaka ya sabini. Kauli hii ina maana kuwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili ni changa ikilinganishwa na riwaya dhati katika fasihi ya Kiswahili. Swaleh (2011:72) kwa mfano, anasema kuwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili ilichimbuka miaka ya sitini na kufikia upeo wake katika miaka ya themanini. Kwa maoni yetu, tangu Musiba na Mtobwa walipoandika riwaya zao za kiupelelezi miaka ya themanini, kumekuwa na kimya kirefu kutoka kwa waandishi hadi kufikia mwishoni mwa miaka ya tisini ambapo nyongeza kidogo ilipopatikana. Kwa mfano, Mtobwa aliandika *Roho ya Paka* (1996), *Nyuma ya Mapazia* (1996) na *Mtambo wa Mauti* (2004) naye Musiba akaongezea *Mkataa Pema* (1996) na *Uchu* (2000). Utafiti huu umezichunguza kwa kina baadhi ya riwaya za Mtobwa, Abdulla, Katallambula, Simbamwene, Musiba na Levi kudhihirisha tofauti zao kimuundo na kimtindo.

Kando na uandishi na uchapishaji, tahakiki zilizopo kuhusiana na riwaya ya kiupelelezi pia si nyingi ikilinganishwa na tahakiki zilizopo katika kipera cha riwaya dhati (kulingana na usomaji wetu). Baadhi ya wahakiki waliowahi kutoa kauli zao kuhusiana na riwaya ya kiupelelezi ni Hussein (1971), Kezilahabi (1975), Mgeni (1983), Arnold (1984), Madumulla (1988), Kimura (1992), Lindfors (1994), Mlacha na Madumulla (1995), Anyango (2016) na Mbatiah (2020) miongoni mwa wengine. Tahakiki hizi pia ziliegemea mno upande wa kimaudhui na kupuuza fani. Fani iliwekwa pembeni badala ya kuhakikiwa ili kuonyesha mchango wake katika kuibua umbuji wa riwaya hizo. Kuhusu upembezwaji wa riwaya za kiupelelezi na fasihi pendwa kijumla, Madumulla anatuambia:

> Fasihi pendwa imekuwa ikipuuzwa kwa kiasi kikubwa na siyo mashirika makubwa tu ya uchapishaji, bali na wahakiki pia. Mashirika makubwa yamekuwa yakiipuuza kwa kuchelea kukosa soko…Katika miaka ya sabini uhakiki wa maudhui uliiziba nafasi ya fani, fani haikujadiliwa na kutazamwa kwa ndani.(1988:13)

Huku kutengwa na kuwekwa pembeni kwa riwaya za kiupelelezi kunatuchochea kujiuliza maswali kadhaa. Je, upembezwaji huu umetokana na sera za kimakusudi kutoka kwa makampuni ya uchapishaji? Je fasihi ya aina hii ni duni na kama ndivyo, mwelekeo huu umechangiwa na nini? Kulingana na nukuu la hapo juu, Madumulla anaona kwamba mashirika makubwa hayakupendelea riwaya pendwa kwa sababu ya kuchelea kukosa soko. Hii ni kwa sababu mashirika mengi ya kiserikali yaliiona fasihi kama inayokiuka maadili ya kijamii. Jambo hili liliwalazimu baadhi ya watunzi kujiundia vituo vyao vya uchapishaji.

Riwaya ya kiupelelezi ni kipera cha Fasihi Pendwa (Swaleh, 2011:73). Kando na hiki, fasihi pendwa pia hujumuisha vipera vingine kama vile riwaya ya kiuhalifu, riwaya ya kimapenzi na riwaya ya kijasira. Riwaya ya kiuhalifu kwa mfano, huhusu msururu wa uhalifu hasa wa jinai ambapo wahusika wakuu huwa ni majambazi wakipambana na asasi za kidola. Riwaya ya kiupelelezi kwa upande wake nayo huhusisha uhalifu hasa mauaji na uchunguzi wa uhalifu huo na mwishowe kuadhibiwa kwa mhalifu.Todorov akinukuliwa na Malmgren (2001:116) anaeleza kwamba riwaya ya kiupelelezi inahusu hadithi mbili; hadithi ya uhalifu na hadithi ya upelelezi. Anamithilisha hali hii na sifa za hadithi za kifasihi simulizi za ‘fabula’ na ‘sujet’, yaani hadithi na msuko. Ingawa kauli hii ni ya kijumla, kuna vighairi vichache ambapo riwaya yaweza kuhusu upelelezi pasi na kuwa na uhalifu (Kwa mfano, katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* (1984), upelelezi uliopo hauhusu uhalifu bali ni udanganyifu wa kindoa ambapo mume, kwa kutumia jina tofouti, anamuoa mke wa pili na kumweka mjini, bila mke wa kwanza kufahamu). Hata hivyo katika Kiswahili tuna riwaya nyingi za kiupelelezi zenye motifu ya uhalifu.

Kulingana na Wamitila (2003:120), riwaya ya kiupelelezi huwa na dhamira ya kuburudisha wala si kuelimisha, sifa yake kuu ikiwa ni kupendwa na watu wengi. Kando na maoni ya Wamitila, kama tukakavyoonyesha baadaye kupitia utanzu wa riwaya ya kiupelelezi, kuna riwaya nyingine za kiupelelezi ambazo huburudisha na kuelimisha wakati huo huo. Kwa mfano, baadhi ya riwaya za Mtobwa na zile za Musiba, kando na upelelezi huangazia masuala ya kihistoria na utawala kama vile ukombozi wa Afrika Kusini, uhusiano wa kimataifa nyakati za vita baridi, hila za vyama

nyakati za uchaguzi na ukoloni mamboleo. Vipengele vya kifani vya muundo na usimulizi vilivyochaguliwa vitahakikiwa kuonyesha ikiwa vinafanikisha dhima hizi za burudani na kuelimisha. Kupendwa kwa fasihi hii hakutokani na maudhui yake tu bali pia matumizi ya mbinu sahili za uwasilishaji wa maudhui hayo. Kwa mfano, riwaya nyingi za kiupelelezi huwa na lugha nyepesi, visa vya ajabu na msuko unaozingatika kwa urahisi. Uchunguzi huu umebainisha kuwa vipengele vya kifani vya msuko, uhusika na usimulizi huchangia katika kupendwa kwa riwaya ya kiupelelezi. Vipengele hivi vya kifani vimehakikiwa kwa kuchunguza riwaya za Abdulla, Mtobwa, Katalambulla, Musiba, Simbamwene na Levi.

Riwaya ya kiupelelezi inapata mvuto pia kutokana na matumizi ya mada anuwai zinazolenga kuburudisha kama vile zile zinazosawiri mapambano baina ya polisi na magenge ya kiuhalifu, mbinu za uchunguzi zitumiwazo na mpelelezi na matumizi ya muundo wa kitaharuki. Kimura (1992:162) anasema kwamba waandishi wengi wa riwaya ya kiupelelezi kando na kuwa na dhamira ya kupeleleza, hujihusisha na mada anuwai zikiwemo mapenzi na uozo wa kijamii wa aina mbalimbali kama vile ulevi, ukahaba pamoja na aina mbalimbali za uhalifu kama vile wizi, biashara za magendo na ulanguzi. Hii ndio sababu riwaya hizi zimeshutumiwa na baadhi ya wahakiki kuwa zinaweza kuchochea ongezeko la upotofu wa maadili katika jamii (Kezilahabi, 1975, Lukacs, 1972). Kezilahabi, kwa mfano, anaona kuwa kuenea na kupendwa kwa riwaya hizi kunaweza kuwazuia watu wengi wasipokee vyema fasihi dhati. Naye Lukacs, anachukua mkabala wa kijamii na kuona kwamba fasihi kijumla inapaswa kuchangia katika ujenzi wa jamii mpya au kuleta mapinduzi ya kijamii. Kulingana naye, riwaya za kiupelelezi zinaishia tu katika kulijibu swali la kesi ya mauaji itatatuliwa vipi na ni nani muuaji. Kando na maoni ya waandishi hawa, tunaamini kwamba, kupendwa na kusambaa kwa riwaya hizi pia kunatokana na kweli kuwa zinasawiri maisha ya watu wa kawaida wakipimbana na hali ngumu za kimaisha kama vile ukosefu wa kazi na kuwepo kwa umaskini mwingi. Hali hizi zinachochea ongezeko la uhalifu hasa wizi na ukahaba kama njia za kujikimu. Hali hii inabidi kuwepo kwa polisi ili kudumisha usalama na kulinda mali ya tabaka la juu.

Kando na shutuma zilizopo dhidi ya riwaya ya kiupelelezi (Kezilahabi, 1975 na Madumulla, 1988), kuna waandishi na wahakiki ambao wanaitetea nafasi ya riwaya ya kiupelelezi kwa kusisitiza kuwa kama ilivyo fasihi dhati, riwaya ya kiupelelezi nayo imesheheni mafunzo mengi kwa jamii. Kimura (1992:13) anatuambia kuwa katika mkutano wa UWAVITA (Umoja wa

Waandishi wa Vitabu Tanzania) uliofanyika tarehe 26 hadi 29 Oktoba, 1987, mtunzi wa riwaya za kiupelelezi Hammie Rajab, kwa mfano, alizitetea riwaya hizi dhidi ya pingamizi zake kwa kusema kwamba zinawafunza wanajamii kutojihusisha na uhalifu, kuwa kwa vyo vyote vile uhalifu haulipi. Baadhi ya wahakiki pia wanachukua mkabala wa kimtindo kuitetea riwaya ya kiupelelezi kwa kudai kuwa baadhi ya waandishi wa riwaya dhati huzifanya kazi zao kuwa ngumu kwa kutumia mitindo inayowatatiza wasomaji. Kwa hivyo, kinyume na riwaya dhati, riwaya ya kiupelelezi ina mvuto kwa wasomaji wengi unaotokana na umbuji wa kifani na usahili wa kimtindo. Tunavyoona ni kwamba riwaya hizi ni mbinu bora ya kushawishi na kutia hamu ya usomaji kwa wasomaji wachanga haswa wanaoona ugumu katika kusoma riwaya dhati.

Katika muktadha wa Tanzania, Mabala (1989) anasema kuwa riwaya ya kiupelelezi inafaulu kufichua hali halisi ya kisiasa na kiuchumi na kwa sababu hiyo zinachochea mabadiliko katika jamii. Anakubali kuwa baadhi ya kazi hizo zinajihusisha na suala la ukombozi wa Kiafrika. Riwaya za kiupelelezi za Mtobwa, kwa mfano, hutoa taswira ya namna Tanzania ilivyoyasaidia mataifa ya Kusini mwa Afrika katika kupigania uhuru wao. Kwa kuzingatia maoni ya wataalam hawa, inadhihirika kuwa riwaya hii haina dhima ya kuburudisha tu kama ilivyodhaniwa hapo awali, bali pia inamulika masuala mazito katika jamii. Mandel (1984:152) alikuwa ametoa kauli kama hii, akionyesha kwamba riwaya ya kiupelelezi inamulika uhalisia wa kijamii. Anaona kuwa kazi hizi zimeambatana na mabadiliko ya kijamii. Anasema kuwa jamii ilipobadilika kutoka mfumo wa kiuchumi wa ukabaila hadi wa ubepari, fasihi nayo ilibadilika. Kwa mfano, ubepari ulisababisha kuwepo kwa mfumo wa polisi kufuatia ongezeko la uhalifu. Kwa hivyo, basi riwaya ya kiupelelezi ilichipuka kufuatia mabadiliko haya. Hii ni kwa sababu kulikuwa na haja ya kuchunguza visa vya uhalifu, kuwatia mbaroni wahalifu na kuwaadhibu ili kulihakikishia tabaka la mabepari usalama wa mali na viwanda vyao.

Kwa kurejelea umuhimu wa fani, Madumula anasema kuwa riwaya za kiupelelezi zina ujumi mkubwa ambao bila shaka unatokana na matumizi ya kiufundi ya fani. Kuwepo kwa baadhi ya vipengele vya kigeni vya kifani kumeboresha ujumi huo. Tumedhihirisha namna muundo na usimulizi huchangia katika kuumba ujumi huo katika utafiti huu. Kuhusu ubora wa fani katika riwaya ya kiupelelezi, anasema:

> Wahakiki waliisoza pembeni kama kitu kisichofaa pasipo hata na kuisoma.
> Lakini hivyo si sahihi kwa mhakiki wa ukweli. Riwaya hii si tupu kabisa. Kwanza

> inasisimua kwa sababu wasanii wake wanaipatia ujumi wa kisasa ambao umeletwa na utamaduni wa kigeni. Pili, kwa kiasi chake, maandishi haya hayafichui tu uozo wa kijamii (ya Kitanzania) ulioletwa na hali ya uchumi wa kibepari bali maandishi haya ni zao halisi la uozo huo. (Madumulla,1988:13).

Madumulla anashikilia kuwa mkabala unaofaa kufuatwa katika uhakiki ni ule unaozingatia maudhui na fani. Yaani kujali maswali ya ‘nini’ na ‘namna gani’. Anaona kwamba kupuuzilia mbali namna ya uwasilishaji maudhui ni sawa na kupuuzia usanifu wenyewe ilhali ndio unaoifanya kazi iwe ya kisanaa. Kwa misingi ya maoni ya wataalam hawa, fani ni muhimu kama ulivyo muhimu uchunguzi wa maudhui. Tasnifu hii imechunguza wajibu wa muundo na usmulizi katika kufanikisha maudhui mbalimbali katika riwaya ya kiupelelezi. Imebainishwa kuwa watunzi wa riwaya za kiupelelezi wanatumia ufundi mkubwa katika ujenzi wa msuko, usimulizi na uhusika.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Utafiti huu umehusu uhakiki wa muundo na usimulizi katika riwaya ya kiupelelezi kwa kujikita katika riwaya za Mohammed Said Abdulla, Ben Mtobwa, Faraj Katallambula, John Simbamwene, Elvis Musiba na Godfrey Levi. Riwaya ya kiupelelezi pamoja na vijitanzu vingine vya fasihi pendwa vimekuwa kimbilio la watu wengi, wazee kwa vijana kutokana na mvuto wake na uwezo wake wa kuburudisha na kuliwaza. Kabla ya majilio ya teknolojia ya filamu, runinga na simu, watu wengi wa Afrika Mashariki (waliosoma) walikuwa wapenzi wakubwa wa fasihi pendwa na hasa riwaya ya kiupelelezi. Hata hivyo, utanzu huu muhimu wa riwaya umekuwa ukipuuzwa na waandishi, wahakiki na hata mashirika ya uchapishaji (Madumulla, 1988). Madumulla anatueleza kwamba, kupuuzwa huku kumepelekea kijitanzu hiki cha riwaya kubatizwa majina mbalimbali kama vile “fasihi duni” au fasihi ya watu waliokosa elimu. Msimamo huu unaashiria kwamba, ingawa kazi hizi ni maarufu miongoni mwa wasomaji, umaarufu huo haujitokezi waziwazi miongoni mwa wahakiki. Hata hivyo, hakuna utafiti uliofanywa kubainisha ikiwa kupendwa kwa riwaya hizi kumetokana na muundo au usimulizi wake. Utafiti huu hivyo basi unakusudia kuliziba pengo hili. Umaarufu wa aina hii ya riwaya miongoni mwa wasomaji ulimwenguni na hasa katika Afrika Mashariki umetupatia kichocheo na hamu ya kuchunguza muundo na usimulizi ili kudhihirisha ikiwa vipengele hivi ndivyo vyanzo vya umaarufu huo.

Kuna tafiti nyingi ambazo zimefanywa kuhusu riwaya ya Kiswahili, hasa kuhusiana na maudhui na fani katika riwaya dhati. Hata hivyo, kuna tafiti chache mno kuhusu riwaya ya kiupelelezi na fasihi pendwa kijumla hasa kuhusiana na suala la muundo na usimulizi (Hussein 1971, Kezilahabi 1975, Madumulla 1988 na Gromov 2008). Kazi chache zilizopo kuhusu fasihi pendwa zimejitokeza katika majarida ya kiusomi na tahakiki za uzamili. Utafiti huu umekusudia kuliziba pengo hili kwa kuchunguza kwa kina zaidi mchango wa muundo na usimulizi katika kufanikisha dhamira kuu za watunzi.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

a) Je, ni mbinu zipi za kisimulizi zinazoutambulisha utanzu wa riwaya ya kiupelelezi?
b) Je, usawiri wa uhusika unachangia vipi katika ubunifu wa kimuundo wa riwaya ya kiupelelezi?
c) Je, msuko wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili huhusishwa na mbinu zozote maalum?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

a) Kubainisha namna usimulizi unavyotekelezwa katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.
b) Kutathmini usawiri wa uhusika kama sifa ya kimuundo ya riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.
c) Kuainisha mbinu za ujenzi wa msuko zipatikanazo katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Riwaya ya kiupelelezi na fasihi pendwa kwa ujumla hupendwa na watu wengi katika jamii na kwa sababu hii, riwaya ya aina hii imeenea miongoni mwa matabaka mbalimbali ya wanajamii. Kwa sababu hii, Mlacha na Madumulla (1995:56) wanasema kuwa kutokana na mvuto huu wa riwaya ya kiupelelezi, kuna baadhi ya wanajamii ambao wamefanya riwaya hii kibadala cha filamu. Hali hii inatuonyesha kuwa riwaya hii ina dhima kubwa katika jamii kando na ile ya burudani. Tumechukulia kuwa kupendwa kwa kazi hizi hakutokani tu na dhamira ya kuburudisha bali lazima kuwe na sifa nyinginezo za kifani zinazowavutia wasomaji. Hii ndio maana tasnifu hii

imechunguza muundo wa kisimulizi, uhusika na msuko ili kubainisha jinsi usanii huo unazua mvuto katika riwaya tulizoteua.

Kwa kuwa mwandishi wa kazi ya kifasihi haizalishi kazi yake kutoka kwa ombwe tupu, ni rahisi kwake kuathiriwa na kazi za watunzi wengine. Baadhi ya wahakiki (Madumulla 1988:12, Lindfors 1998:109, Hussein 1971:48) wanasema kuwa maandishi ya kiupelelezi katika Afrika Mashariki ni mwigo au mwendelezo wa maandishi ya Kimagharibi ya kina Conan Doyle, Agatha Christie, Ian Fleming, Hadley Chase na wengineo. Pia wanasema kwamba athari ya filamu za Kimagharibi zinazohusu uhalifu na upelelezi imechochea utunzi wa riwaya hizi katika mazingira ya Afrika Mashariki. Kwa sababu hii, riwaya chache za kiupelelezi zilizopo katika Afrika Mashariki zimeathiriwa na mitindo ya Kimagharibi. Utafiti huu, kwa hivyo umeonyesha namna athari hizo zimevyojitokeza kupitia muundo na usimulizi wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

Ingawa kuna tafiti na tahakiki nyingi kuhusu riwaya ya Kiswahili, kijitanzu cha riwaya za kiupelelezi hakijafanyiwa uhakiki wa kutosha ikilinganishwa na riwaya dhati hasa kuhusiana na uhakiki wa kifani. Kwa hakika kuna tahakiki chache mno zililzopo kuhusu riwaya pendwa hasa za kiupelelezi katika Afrika Mashariki.Wanjala (1980:67-68) anasema kwamba sababu kuu ya kukosekana kwa tahakiki zinazohusu riwaya za kiupelelezi ni kwamba zilikiuka mipaka ya maudhui ya kikawaida. Kwa mfano, baadhi zilihusu mauaji, wizi, harakati za kuwasaka wahalifu na mapenzi. Naye Madumulla (1988:13) anasema kuwa katika nchi ya Tanzania, sera ya elimu haikupendelea riwaya pendwa kutumika shuleni hasa ikiwa ilihusu mapenzi na uhalifu wa kisasa. Wanadai kuwa baadhi ya riwaya hizo ziliakisi mitindo ya kimaisha ya Kimagharibi kama vile kuwepo kwa mauaji yanayoendelezwa kwa kutumia ala za kigeni kama vile bunduki na hata matumizi ya kemikali mbalimbali. Kwa hivyo, kazi hii itakuwa nyongeza kubwa katika idadi ya tahakiki zilizopo katika kijitanzu cha riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

Kwa kuwa fasihi inakua kadri jamii inavyokua, utafiti huu umeonyesha baadhi ya mabadiliko ambayo yametokea katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi. Kwa kufanya hivi pia tumedhihirisha jinsi riwaya ya kiupelelezi imeanza kuchukua baadhi ya vipengele ambavyo kwa kawaida huhusishwa na riwaya dhati. Riwaya za Mtobwa kwa mfano, zinadhihirisha uhalisia wa kijamii kupitia usawiri wa maudhui ya ubaguzi wa rangi, siasa za mfumo wa vyama vingi na ukoloni mamboleo.Vilevile, kazi za Abdulla zinahusisha ubunifu na utamaduni wa jamii yake na kwa kufanya hivyo zinaangazia masuala muhimu katika jamii kama vile urithi, utabaka na dini.

Mulokozi (1996:58) pia anausifia uandishi wa Ben Mtobwa akimtaja kama mwandishi kama anayelenga kufunza adili fulani katika jamii. Hii ina maana kuwa riwaya za kiupelelezi, sawa na riwaya dhati zinaiakisi jamii.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Fasihi pendwa yaweza kujitokeza katika tanzu zote za fasihi zikiwemo hadithi fupi, riwaya na tamthilia. Vilevile, riwaya pendwa ni utanzu mpana unaohusu riwaya ya kihalifu, riwaya ya kiupelelezi, riwaya ya kimapenzi na riwaya ya kijasira. Utafiti huu umejihusisha tu na utanzu wa riwaya ya kiupelelezi pekee. Ingawa kuna vipengele kadhaa vya kifani vinavyoweza kuchunguzwa, tasnifu hii imejihusisha na suala la muundo na usimulizi katika riwaya ya kiupelelezi. Vipengele vya kimuundo ambavyo vimechunguzwa ni uhusika na msuko.

Kwa kuwa riwaya za kiupelelezi katika Afrika Mashariki zina waandishi wengi, utafiti huu umejikita katika riwaya za Mohammed Said Abdulla, Ben Mtobwa, John Simbamwene, Faraj Katalambulla, Godfrey Levi na Elvis Musiba kama wawakilishi wa waandishi wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Riwaya za Abdulla zitakazohakikiwa ni *Kisima cha Giningi* (1968) na *Duniani kuna Watu* (1973). Kando na hizi pia tutazihakiki kazi nyinginezo zinazokaribiana nazo kimtindo na kimaudhui za Mtobwa ambazo ni *Tutarudi na Roho Zetu?* (1984), na *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), riwaya mbili za Godfrey Levi ambazo ni *Fedheha ya Fedha* (1981) na *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975), riwaya moja ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo* (1965), riwaya za Musiba za *Njama* (1984) na *Uchu* (2000) na riwaya moja ya Simbamwene ya *Kwa sababu ya Pesa* (1971). Tumeonyesha pia ikiwa waandishi wa riwaya za kiupelelezi wa Afrika Mashariki wameathiriwa na watunzi wa Kimagharibi kama vile Arthur Conan Doyle, Agatha Christie na Edgar Allan Poe. Ingawa utafiti huu ulikusudia kuchunguza riwaya kutoka Afrika Mashariki, Kazi nyingi zilizoteuliwa ni za waandishi wa kutoka Tanzania (riwaya saba kati ya kumi) kwa sababu mataifa mengine ya Afrika Mashariki hayana waandishi wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Fasihi Pendwa na Riwaya ya Kiupelelezi

Katika sehemu hii tunafanya mapitio ya maandishi mbalimbali yanayohusu riwaya ya kiupelelezi, fasihi pendwa kijumla na vipengele vya kifani vya msuko, uhusika na usimulizi. Maandishi haya ni kama vile majarida, tasnifu za uzamili na uzamifu na machapisho mengine. Mapitio haya yatatubainishia mapengo ya utafiti kando na kutusaidia kuweka mipaka ya kazi hii.

Hapana shaka kwamba suala la uhakiki na uchanganuzi wa fani katika tungo za kinathari, kitamthilia na kishairi katika fasihi ya Kiswahili limewahi kujitokeza katika tafiti za aina mbalimbali, na limewahi kujadiliwa kwa njia anuwai katika fasihi ya Kiswahili na pia katika fasihi nyingi za kilimwengu. Tumeigawa sehemu hii kuwili tukifanya mapitio kuhusu kwanza, masuala ya kijumla yanayoihusu riwaya ya kiupelelezi na pili, mapitio yanayohusu fani.

### 1.7.1 Masuala ya Kijumla Kuhusu Fasihi Pendwa na Riwaya ya Kiupelelezi

Fasihi pendwa ya Afrika Mashariki imeshutumiwa kwa kukosa uhalisia wa kijamii na kuegemea zaidi kwenye ufantasia. Arnold (1984:63) anakosoa uandishi wa riwaya pendwa nchini Kenya akidai kuwa kazi hizo ni za kifantasia na zinazoepuka uhalisia wa kijamii. Anasema kuwa zimejaa dhamira za ulipishaji kisasi, mahusiano ya kingono, ukatili na uendelezezaji wa tabia za kiubepari za ushindani, ubinafsi na uabudu wa pesa. Kwa misingi hii anamkashfu Maillu, mwandishi wa riwaya pendwa kwa Kiingereza, kwa kwandika kazi za kiponografia. Mhakiki huyu anaamini kuwa Maillu ameathiriwa na mitindo ya filamu za Kimagharibi. Hata hivyo anamsifu kwa kwandika kazi nyingi zaidi katika eneo la Afrika Mashariki kwa Kiingereza. Anachukulia kazi za Msuya zikiwa kinyume na za Maillu kwa kusema kuwa Msuya huzalisha kazi zake kutoka kwa mazingira halisi ya kijamii. Hii ndiyo misingi anayotumia kukosoa waandishi wanaoandikia wasomi pekee, akiwafananisha waandishi hao na mjenzi anayeanza kujenga katika ghorofa ya kumi na kumalizia na msingi badala ya kuanzia na msingi. Mawazo haya yanatupatia taswira ya hali ya fasihi pendwa ilivyo nchini Kenya na hasa riwaya ya kiupelelezi. Tunakubaliana na maoni haya kuwa kwa kweli kuna ukame mkubwa nchini Kenya wa fasihi pendwa ya Kiswahili na hasa riwaya ya kiupelelezi. Jambo muhimu analozua Arnold ni kuwa kuna haja ya kuitathmini riwaya pendwa ya Kiswahili kwa misingi ya mazingira ya Afrika Mashariki badala ya kutumia vigezo vya Kimagharibi.

Kando na kuwa riwaya ya kiupelelezi inakuwa na dhamira kuu ya kuburudisha, inaweza pia kuangazia uhalisia wa kijamii kama zifanyavyo riwaya dhati. Mandel (1984) alihakiki riwaya za kiupelelezi kwa misingi ya Kimaksi na kutetea dai kwamba ni kazi zinazoakisi mabadiliko katika jamii. Yeye haoni hadithi za kiuhalifu zinazopatikana katika riwaya ya kiupelelezi kama fasihi tu bali kama tatizo la kijamii ambalo limeletwa na ubepari. Kwake riwaya hizi ni zao la ubepari kwani badala ya ushindani wa kisoko unaohusu ununuzi na uuzaji, katika riwaya hizi, badala yake huwa kuna ushindani wa kiakili na kimaarifa baina ya mpelelezi na mhalifu. Anasema kuwa ushindani

huu pia haujitokezi tu baina ya mpelelezi na mhalifu tu bali pia baina ya msomaji na mwandishi. Kinyume ni kwamba huku mpelelezi akifanikiwa kumshinda mhalifu, msomaji kwa upande wake huwa hafanikiwi kumshinda mwandishi. Kama jambo hili lingefanyika basi hadithi nayo ingepoteza taharuki, mshtukizo, uajabu au mtakasohisia ilhali mbinu hizo ndizo msingi wa riwaya ya kiupelelezi. Maoni haya ya Mandel yanatufaa katika kuhakiki matumizi ya mbinu hizi katika vitabu tulivyoteua pamoja na vipengele vingine vya kifani. Baadhi ya sifa nyinginezo anazodokeza ni kuwa mpelelezi hapaswi kumlaghai msomaji kwa kutumia njia za kimiujiza au kimafumbo katika uchunguzi wake. Bali awe na mbinu ya kumshtukiza msomaji bila kutumia siri fulani au uongo wowote. Anasema kuwa kutimiza haya ni kudhihirisha umahiri mkubwa katika utunzi wa riwaya ya kiupelelezi. Sifa za kimuundo anazoangazia Mandel zitakuwa msingi bora kwetu katika kuhakiki msuko na usimulizi.

Riwaya ya kiupelelezi imekuwa ikibadilika kadri jamii zinavyozidi kukumbwa na mabadiliko. Kimura (1992) alitafiti kuhusu mabadiliko ya kijamii na riwaya ya upelelezi katika mazingira ya Kitanzania ambapo alichambua sababu mbalimbali zilizochangia kuzuka kwa fasihi pendwa kijumla na riwaya ya kiupelelezi nchini Tanzania. Baadhi ya sababu anazotaja ni kupanuka kwa shughuli za kiuchumi na huduma za kijamii, kukua kwa miji, ongezeko la watu na ukosefu wa vyanzo vingi vya burudani kwa wanajamii na athari ya fasihi ya kigeni. Tasnifu yake ni kwamba mabadiliko ya kijamiii, kiuchumi na kisiasa yaliathiri utamaduni pakubwa na hasa fasihi. Katika upande wa elimu, kwa mfano, uandishi, uchapishaji na usambasaji wa fasihi uliimarishwa. Nayo maisha ya kimji, kufuatia ongezeko la watu yalizua uhalifu, ukahaba, ulofa na uhuni. Mambo haya nayo yalirutubisha na kuipa maudhui riwaya ya kiupelelezi. Anatambua sifa mahsusi za kimaudhui katika riwaya ya kiupelelezi kwa kudhihirisha kwamba kazi za Abdulla kimsingi huangazia maudhui ya urithi, dhuluma na uzazi haramu huku zile za Mtobwa zikihusu tamaa, mapenzi na uzalendo.Utafiti wetu unatofautiana na kazi hii kwa njia kadhaa: kwanza msisitizo wa Kimura upo kwenye mchango wa kijamii wa riwaya ya kiupelelezi huku kazi yetu ikihusu namna umbuji wa kazi hizo unavyodhihirishwa kupitia fani na pili, yeye anahakiki vitabu vya waandishi Abdulla, Mtobwa na Simbamwene huku nasi tukihakiki kazi za Abdulla, Mtobwa, Musiba, Simbamwene, Levi na Katalambulla. Tumefaidika na kazi hii kwani ametudokezea baadhi ya vipengele vya kimuundo vinavyobainika katika baadhi ya riwaya hizo kupitia vipengele vya fani kama vile msuko na uhusika.

Riwaya pendwa inaweza kuwekwa katika viwango mbalimbali kutegemea dhamira za watunzi wake. Kwa mfano, kuna zile zinazohusu mapenzi, uhalifu, jasira na upelelezi. Madumulla na Mlacha (1995) nao wanaainisha riwaya pendwa katika makundi matatu kwa kutumia vigezo vya kidhamira na kimtindo: aina ya kwanza wanasema ni riwaya ya kiupelelezi inayohusishwa na mtindo wa Abdulla. Sifa yake kuu ni upelelezi na uchanganuzi wa kadhia kwa kutumia mantiki, kwa mfano, *Kisima cha Giningi* (1968). Aina ya pili inahusu mtindo wa Musiba na sifa yake kuu ni upelelezi na kupambana na majambazi na majasusi kwa kutumia nguvu. Mfano wa riwaya hizi ni *Njama* (1984) *Uchu* (2000) za Elvis Musiba na baadhi ya riwaya za Ben Mtobwa kama vile *Tutarudi na Roho Zetu?* (1984). Aina ya tatu ni riwaya izingatiayo mtindo wa Msokile. Ni riwaya inayoegemea zaidi kwenye riwaya dhati, hususan kuwepo kwa uwiano kati ya wahusika na uhalisia. Hata hivyo, riwaya za Msokile zinalenga kuburudisha na wakati huo huo zikimulika masuala mazito ya kijamii. Ingawa hazitumii upelelezi kwa kina katika msuko wake, polisi na njia nyingine za kisheria hutumika kutatua uhalifu. Mfano mzuri wa kazi hizo ni, *Nitakuja kwa Siri* (1981). Mawazo haya ya Madumulla yametufaa katika kuzihakiki riwaya za Abdulla na Musiba na Mtobwa ambazo huhusu upelelezi unaotekelezwa kwa kuchambua kimantiki kadhia mbalimbali. Tutazihakiki ili kuthibitisha ikiwa sifa anazotambua Madumulla zipo au la.

Kuna mjadala unaohusu kuwepo au kutokuwepo kwa fasihi pendwa ya Kiswahili. Baadhi ya wahakiki wanaona kwamba fasihi pendwa kwa Kiingereza imekua kwa kasi zaidi kuliko ile ya Kiswahili hasa nchini Kenya. Gromov, (2008) anajihusisha na swali la ikiwa kuna fasihi pendwa katika lugha ya Kiswahili. Anabainisha kuwa fasihi pendwa ya Kiswahili ilianza katika miongo mitatu ya mwisho wa karne ya ishirini ambapo maudhui ya mapenzi na anasa yalishamiri. Waasisi wa kazi hizi anaowataja (katika muktadha huu) ni Faraj Katalambula, John Simbamwene, Eddie Ganzel, Hammie Rajab na wengine. Anaongeza kuwa katika kipindi cha baina ya 1960-1970 fasihi pendwa na fasihi dhati zilikuwa katika miaka yake changa na kwa sababu hiyo ilikuwa vigumu kuzitofautisha. Anasema kuwa nchini Kenya fasihi pendwa ya Kiswahili haijawahi kuvuma kama ilivyofanyika nchini Tanzania kutokana na matumizi mapana ya lugha ya Kiingereza nchini Kenya ambapo Kiswahili kilipewa hadhi ya chini. Pili, anadai kuwa fasihi pendwa ya Kiingereza ndizo zilizoshamiri nchini Kenya. Aidha anatueleza kwamba fasihi pendwa zilianza mapema nchini Tanzania ambapo zililenga wasomaji wa matabaka ya kati na chini yaliyokuwa na viwango vya chini vya elimu. Anasema kuwa riwaya hizo zilikuwa na uhusika mpevu na wa kuvutia na uliokuzwa vyema. Tumefaidika kutokana na maoni haya hasa kuhusu uhakiki wa uhusika. Sifa

kuu za riwaya pendwa anazozitaja ambazo ni kuwepo kwa mhusika bapa pamoja na mabadiliko makuu kuhusu ploti. Haya ni baadhi ya mambo tuakayochunguza kuhusiana na ujenzi wa ploti na uhusika. Kazi hii inatofautiana na yetu kwa kuwa Gromov analinganisha ukuaji wa fasihi pendwa nchini Kenya na Tanzania nasi tukichunguza fani katika riwaya ya kiupelelezi fasihi.

Fasihi Pendwa katika Afrika inatofautiana kiulingana na maeneo ya kijiografia inakotokea na vile vile mitindo ya waandishi. Newell (2002) alichunguza aina ya fasihi pendwa ya Afrika Kusini, Magharibi na Mashariki. Kuhusu Afrika Magharibi, anaisifu fasihi pendwa ya Soko la Onisha kwa kutoa nakala nyingi zaidi za fasihi pendwa katika Afrika. Sifa za kimtindo zilizowavutia wasomaji wa riwaya hizo anazotambua ni kwamba zilikuwa na lugha sahili iliyoeleweka na watu wa kawaida pamoja na matumizi ya picha kwenye blabu zake. Sifa nyingine anayozungumzia na ambayo inahusu utamaduni pendwa wote, ikiwemo filamu ni kwamba kazi hizi hazidumu sokoni kwa muda mrefu. Kazi hizo hupotea baada ya matumizi ya miaka michache. Sifa hii tunaiona pia katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili tunazozichunguza. Riwaya zilizoandikwa miaka ya sitini na sabini kwa mfano, ni vigumu kuzipata madukani. Kuhusu fasihi pendwa ya Afrika Kusini, anasema kuwa wandishi wengi waliandika kuhusu maisha ya mijini hasa mitaa ya mabanda wakimulika masuala ya uhalifu na umaskini. Anaonyesha kwamba kulikuwa na hadithi za kiupelelezi katika Afrika kusini, ambazo zilijitokeza katika jarida la *The Drum* ambalo pia lilikuwa na visa kuhusu maisha ya vikundi vya kiuhalifu na muziki pendwa. Katika Afrika Mashariki anatambua uandishi wa David Maillu na Ben Mtobwa kama waandishi walioangazia maisha ya wananchi wa kawaida hasa walioishi mijini.

Strinati (2004), akizungumzia utamaduni pendwa anachanganua vichocheo vya ukuaji wa utamaduni huo na kuhitimisha kuwa mapinduzi ya viwanda na ukuaji wa teknolojia ya Magharibi ni masiala makuu yaliyochangia katika maenezi ya utamaduni pendwa katika miaka ya 1920 na 1930. Anasema kuwa uvumbuzi wa radio na filamu ulichochea utoaji na upokeaji wa utamaduni pendwa kutoka jamii za Kimagharibi hadi kwingineko. Anasema kuwa vyombo vya mawasilano vilivyowafikia watu wengi vilifanikisha uchapishaji na usambazaji wa fasihi pendwa. Hii ni kwa sababu, vyombo kama radio na maonyesho ya sinema kando na kupendwa na watu wengi, pia vilitumiwa na serikali. Hata hivyo anaona kuwa serikali za kiimla zilitumia vibaya vyombo hivi kueneza propaganda na itikadi za Kifasisti. Mtafiti huyu anaikosoa fasihi pendwa akisema kuwa inatolewa na wachapishaji kwa lengo la kijilimbikizia faida tu, kwamba haimfikirishi msomaji

kando na kuinyima hadhira nafasi ya kutatua matatizo yao ya kimaisha. Anasema kuwa fasihi hii inapojaribu kusuluhisha matatizo ya kijamii inafanya hivyo kijuujuu kwa kuwa msisitizo wake uko kwenye biashara, utumiaji na faida.

Suala la historia na ukuaji wa riwaya ya kiupelelezi pia limezungumziwa kwa kina na waandishi mbalimbali kama vile Scaggs (2005), Romero (2015) na Philips (2016). Scaggs anachunguza chimbuko na maendeleo ya aina hii ya riwaya na kugundua kuwa iliasisiwa na Edgar Allan Poe ambaye anamtaja kuwa baba wa utanzu huu. Kulingana na Romero riwaya ya kiupelelezi huhusu aina mbili za hadithi: Hadithi ya maisha ya mpelelezi mwenyewe na hadithi kuhusu uhalifu. Kando na sifa hii, anatambua sifa nyingine nne za riwaya hii. Kwanza, anasema kuwa zinakitwa katika mazingira ya miji mikubwa na miji  mingine ya kisasa, tatu, husomeka kwa urahisi na nne, mpelelezi mkuu hawi na haraka ya kufichua malengo yake kwa wahusika wengine na mwisho mpelelezi mkuu hutumia vigezo vya kisheria na kisayansi kufichua namna uhalifu ulivyotendwa pamoja na kumfichua mhalifu. Maoni ya Philips ni kwamba maudhui ya riwaya hii huonyesha hamu ya wanajamii ya kupata haki na katika kutafuta haki, mara nyingine zinanishia kuendeleza propaganda za kidini au kisiasa. Pia anamtaja mhusika mkuu wa kazi za Edgar Allan Poe, Augustine Dupin, kama kielelezo kilichoigwa na waandishi wengine katika ubunaji wa wahusika wao. Mifano ya wahusika hao wa baadaye ni kama vile Sherlock Holmes katika kazi za Conan Doyle na Hercule Poirot katika kazi za Agatha Christie. Wote wana sifa zinazofanana kama vile kushirikiana na polisi katika kutatua vyanzo vya uhalifu. Historia hii inatufaa katika kuhakiki masalio ya sifa za awali katika riwaya za kiupelelezi za kisasa, hasa kutambua athari za Kimagharibi katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

Kuhusiana na maendeleo ya riwaya ya Kiswahili, Mbatiah (2016) alichunguza historia ya riwaya ya Kiswahili kwa kufafanua mchango wa waandishi mbalimbali katika ukuaji wa riwaya hiyo. Anatambua kuwa Mohamed Said Abdulla ndiye mtunzi wa kwanza kabisa wa riwaya za kiupelelezi katika fasihi ya Kiswahili. Anasema kuwa riwaya za Abdulla huchunguza uhalifu, chanzo cha uhalifu huo na athari zake. Anaeleza pia kwamba riwaya hizo huonyesha namna vyombo vya dola vinavyokabiliana na uhalifu huo. Hata hivyo, kama anavyokiri mwandishi huyu, riwaya hizi pia zinamulika masuala mengine ya kijamii kando na uhalifu na upelelezi. Anaonyesha ukuaji wa riwaya hizi katika miaka ya sabini kwa kuzingatia usawiri wa wahusika na uhusika.

Maelezo yake kuhusu uhusika yalitufaa kwani tunahakiki uhusika kama sifa moja ya kimuundo ya riwaya za Abdulla na waandishi wengine wa riwaya ya kiupelelezi.

Yenjela (2017) pia alichunguza historia kama hii lakini akijibana tu katika historia ya Kenya kama inavyojitokeza katika riwaya za Kiingereza na za Kiswahili zilizoandikwa katika kipindi cha miaka hamsini ya uhuru, yaani 1963-2013. Kuhusu riwaya pendwa, anaangazia maisha ya mijini kwa kuwasawiri wahusika wanaotamaushwa na maisha ya mijini na kukimbilia ulevi, uhawara na wizi. Kazi hizo anazohakiki ni *Son of Woman* (1971), *Going Down River Road* (1976), *Son of Woman in Mombasa* (1986) na *Anasa* (1996). Kando na kuonyesha uovu wa mijini, kazi hizi pia zinasawiri uhalisia wa kiuchumi wa wakati huo, hasa ukosefu wa kazi na ongezeko la umaskini.

Utamaduni pendwa katika Afrika unaweza kujitokeza kupitia sanaa za maonyesho, nyimbo, uandishi wa kibunilizi na ughanaji wa mashairi. Berber Karin (2018) anachunguza historia ya utamaduni pendwa katika Afrika kuanzia karne ya kumi na saba hadi sasa (2018) na kubaini kuwa utamaduni huo ulikuwa katika hali ya fasihi simulizi kabla ya karne ya kumi na nane. Anatumia idhibati ya kimaandishi na ile ya kifasihi simulizi katika kuchunguza chimbuko la utamaduni huo. Kulingana na mtafiti huyu, kabla ya karne ya kumi na nane, maandishi yahusuyo utamaduni pendwa ni yale yaliyoandikwa na wageni waliofanya safari zao Afrika. Kabla ya karne hii, tabaka la watawala ndilo lililouendeleza utamaduni pendwa kwani lilikuwa na uwezo wa kuwaajiri watunzi wa mashairi na nyimbo waliowaimbia nyimbo za sifa na za kishujaa kando na maonyesho ya utajiri wao. Fasihi pendwa ya tabaka la juu ndiyo iliyorekodiwa na wageni hawa katika maandishi. Berber anasisitiza kuwa ikiwa watu wa tabaka la chini kama vile watumwa na wakulima walikuwa na fasihi pendwa, basi fasihi yao haikuhifadhiwa kimaandishi. Historia hii inatuonyeha kwamba riwaya ya kiupelelezi kama sehemu ya fasihi pendwa imechimbuka kutokana na fasihi simulizi.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa kuhusu Fani Katika Riwaya za Kiupelelezi

Athari za Kimagharibi katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi zimejitokeza katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Hussein (1971) akihakiki ufundi wa Mohamed Said Abdulla, anausifu utumizi wa taswira mbalimbali katika riwaya ya *Mzimu wa watu wa Kale* (1960) kama vile taswira zinazofafanua mandhari ya chumba cha Msa na kuonyesha kuwa taswira hizi zinafanikisha ufundi wa Abdulla. Kando na sifa hii, Hussein analalamika kuhusu upenyezi wa mwandishi unaojitokeza katika usimulizi wa riwaya hii. Lalamiko la pili analotoa linahusu hadithi kujengwa juu ya mithili

ya wahusika waliotumiwa na Conan Doyle, Sherlock Holmes na Watson ambao ni vivuli vya Msa na Najum. Anaona mfananisho huu kama uigaji mbaya. Kwa mfano, anasema kuwa ni vigumu kuamini kwamba mtu kama Msa angeweza kupatikana katika Unguja (Msa anaonekana kwa njia zote kuwa Mwafrika lakini utamaduni wake na ustaarabu wake ni wa kigeni. Yeye ni Mzungu Mwafrika). Anaeleza pia kwamba habari za kiupelelezi zinazofanywa na mpelelezi wa kibinafsi miaka ya 1950 katika Unguja ni habari ngeni na ni vigumu kuzisadiki.

Hussein anaibua mambo muhimu kwa utafiti wetu kama vile suala la mwingilianomatini ambalo analiona kama uigaji usiofaa. Katika kazi hii, tutaonyesha kuwa Abdulla ameathiriwa na uandishi wa Kimagharibi na kwa hivyo akatumia baadhi ya vigezo vya Conan Doyle, Agatha Christie na Alla Poe. Pia tumefaidika na mtazamo wake kuhusu uhusika wa Msa haswa kutokana na maswali anayouliza kumhusu mhusika huyu. Suala la upenyezi wa mwandishi analoibua kama kasoro ya Abdulla litachunguzwa kwa kina katika riwaya teule chini ya usimulizi. Yeye amechunguza kipengele cha uhusika peke yake katika riwaya moja ya Abdulla. Sisi tmeachunguza vipengele vya kifani vya usimulizi, uhusika na msuko katika riwaya za waandishi kadhaa wa riwaya ya kiupelelezi.

Riwaya ya kiupelelezi kama kaida husawiri mandhari yenye uajabu. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya kwanza kuwahi kuainishwa kama ya kiupelelezi, *Murders in the Rue Morgue* (1841) ya Allan Poe. Mgeni (1983) anachunguza sifa za uajabu katika kazi za Mohammed Said Abdulla kwa kuzingatia vigezo vya uhusika na mandhari ya hadithi. Kiuhusika anamtaja mhusika Msa (anayepatikana katika kazi nyingi za Abdulla), Fundi Mangungu na Habussa (wote hawa wawili katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*) kama wahusika wa kiajabu. Kuhusu mandhari, anasema kuwa riwaya zote za Abdulla zinasimulia hadithi zinazogubikwa na uajabu fulani kama vile makaazi ya mapepo na mizuka, visima vya ajabu au mapango ya ajabu pamoja na harakati za uganga.Uhakiki huu wa Mgeni (keshatajwa) unatufaa kuelewa wasifu wa wahusika wakuu katika kazi za Abdulla na kwa hivyo kufanikisha uchambuzi wa wahusika, ploti na usimulizi. Pia kazi hii imegusia suala la mandhari hasa uajabu wa mandhari hayo. Vipengele hivi vya uhusika, mandhari na ploti tumevihakiki kwa kina katika kufafanua muundo wa riwaya tulizoteua. Kwa hivyo, kazi hii imetufaa kwani sisi tumehakiki muundo na usimulizi katika riwaya za kiupelelezi pasi na kujikita katika riwaya za Abdulla pekee kama anavyofanya Mgeni.

Suala la usambazaji wa mitindo ya Kimagharibi ya uandishi wa riwaya ya kiupelelezi katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili limeangaziwa na Lindfors (1994) katika makala iitwayo, 'Sherlock Holmes in Africa', ambapo anafafanua mshabaha uliopo baina ya vitabu vya Mohammed Said Abdulla na vile vya Conan Doyle haswa kuhusu wahusika, Sherlock Holmes na Msa kama wahusika wakuu na Watson na Najum kama wahusika wasaidizi. Kwa mfano, wote wawili Msa na Sherlock wanavuta tumbaku kwa kiko, wana uchunzaji makinifu, utumiaji mkubwa wa fikra na mantiki, ujasiri, utulivu na wasiofanya makosa (isipokuwa *Kosa la Bwana Msa*). Naye msaidizi wake, Najum, amesawiriwa akiwa na sifa sawia na zile za Watson; ukawaida, ukosefu wa msimamo thabiti na kushindwa kufikiria kimantiki na kwa haraka kama alivyo mhusika mkuu, Msa. Kando na kufanana huku, anakiri kuwa Abdulla anaandika kazi asilia na zenye ubunifu kwani mandhari yake ni ya Unguja, wahusika wake ni Waafrika, vitendo vyao, misemo yao na fikra zao zinafumbata uhalisia wa Afrika Mashariki. Lindfors (keshatajwa) anahitimisha kuwa ingawa kuna tofouti za kimsuko na kimandhari kati ya kazi za Abdulla na Conan, Abdulla ameathiriwa na kupata ilhamu yake kutoka kwa Conan Doyle. Kazi hii ingawa ni tofauti na yetu imetusaidia kuhakiki uhusika na ploti katika kazi za Abdulla. Pia mawazo yake ni muhimu katika kuchanganua athari za Conan Doyle katika uandishi wa Abdulla. Lindfors pia anaonyesha uhusiano uliopo baina ya riwaya ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo* (1965) na riwaya ya Abdulla ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960) kwa kusema kuwa ufanisi wa *Mzimu wa Watu wa Kale* ulipelekea uibukaji wa *Simu ya Kifo.* Anazua uhusiano wa kinasaba kwa kuonyesha kuwa kazi za Conan Doyle zilizaa kazi za Abdulla, nazo kazi za Abdulla zikazaa za Katalambulla.

Suala la msuko wa riwaya ya kiupelelezi kama sifa bainifu ya kitanzu hiki cha riwaya limechunguzwa na wahakiki kadhaa. Danyte (2011), kwa mfano, alichanganua sifa saba za fasihi ya kiupelelezi huku baadhi ya sifa hizo zikihusu muundo wa kimsuko: Kwanza, anataja kuwa uhalifu hasa mauaji hutendeka mwanzoni mwa usimulizi wa hadithi, pili, kunajitokeza washukiwa kadhaa ambapo kila mshukiwa anadhaniwa kwa sababu tofouti, tatu, mhusika mmoja mkuu anajitokeza kama mpelelezi wa kisa hicho, nne, mpelelezi anakusanya ushahidi wa kutosha kuhusu uhalifu huo na pia kuhusu waathiriwa wa uhalifu huo. Sifa ya tano anayotaja Danyte ni kuwa mpelelezi mkuu huwahoji washukiwa pamoja na watu walioshuhudia uhalifu huo, sita, mpelelezi hugundua mhalifu aliyehusika na kisha anasuluhisha kiini cha uajabu huo na mwishowe mhalifu sasa hutiwa mbaroni na kuadhibiwa. Kwa kutumia baadhi ya vigezo vilivyotajwa hapo juu alifafanua fasihi ya kiupelelezi kama ambayo kiini cha msuko wake ni kuwepo kwa uhalifu na

suluhisho lake. Sifa hizi zimetufaa katika kuhakiki msuko na uhusika katika riwaya zilizoteuliwa kwa lengo la kubainisha sifa maalum za utanzu huu wa riwaya.

Sifa za muundo wa msuko wa kazi za kiupelelezi pia zimedokezwa na Meintel (2012:131) ambaye alichunguza kaida za riwaya ya kiupelelezi katika kazi za kutoka nchi za Afrika Magharibi zinazozungumza Kifaransa. Akimnukuu Auden (1962), anaeleza kwamba msuko wa riwaya za kiupelelezi huwa na sehemu zifuatazo: (a) Kuwepo kwa amani na utulivu (b) Kuvurugwa kwa amani hiyo kupitia tendo la uhalifu (c) mwanzo wa uchunguzi ambao aghalabu hutatizwa kupitia uhalifu mpya au/na utolewaji wa ushahidi wa uongo. (d) Usuluhishaji wa mgogoro. (e) Kukamatwa kwa mhalifu. (f) Kurejea kwa amani na utulivu tena. Maelezo haya kuhusu msuko ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu moja ya malengo ya kazi hii ni kuchunguza ujenzi wa msuko katika riwaya za kupelelezi. Lengo hili limechunguzwa katika sura ya tano ya tasnifu hii.

Cawelti (1976) amechunguza sifa za kifomyula zitumiwazo katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi. Baadhi ya sifa hizo zinahusiana na vipengele tunavyochunguza vya uhusika, usimulizi na ujenzi wa msuko. Kuhusu uhusika Cawelti anatambua kwamba mhusika mpelelezi husawiriwa kwa njia spesheli kwani hujitokeza kama binadamu asiye wa kawaida. Kwa mfano anatumia mantiki na urazini kwa kiasi cha juu ikilinganishwa na wahusika wengine. Kuhusiana na ujenzi wa msuko na usimulizi Cawelti anaeleza kwamba taharuki ni kiungo kikuu katika msuko wa riwaya za kiupelelezi. Mawazo haya yamefaidi kazi hii kwa kuwa tumechunguza kwa undani uhusika, msuko na muundo wa kisimulizi.

Kipengele kingine cha kifani katika riwaya za kiupelelezi kinahusu kuwepo kwa miishio ya kifomyula. Segal (2020) anafafanua kwamba katika sura ya mwisho ya riwaya hizi, mpelelezi huwakusanya wahusika muhimu katika chumba ili kuwaelezea mchakato alioufuata katika kutatuamigogoro ya hadithini. Migogoro hii inahusu ni nani mhalifu, kwa nini anashiriki katika uhalifu huo na vipi tendo la uhalifu lilivyofanywa. Habari hizi huwekwa kama siri hadi mwishoni mwa hadithi kupitia taharuki na mfumo wa ishara kadhaa. Maelezo ya mpelelezi mwishoni huyajibu maswali ya hadhira huku yakiziba mianya ya kisimulizi iliyoweza kujitokeza na kumtatiza msomaji. Segal pia anafafanua kuwa riwaya za kiupelelezi huwa na msimulizi wa kifomyula ambaye huwa na maarifa mengi na anayewashinda polisi katika uchunguzi wao. Ingawa uhakiki wa Segal umejikita katika miishio ya riwaya za kiupelelezi, umetufaa katika kuelewa zaidi wasifu wa mhusika mpelelezi pamoja na kutudokezea mbinu za ujenzi wa msuko wa kazi za

kiupelelezi. Mbinu hizo za kimsuko ni kama vile mshtukizo na taharuki. Weiss (2014) naye pia akichunguza vipengele vya ishara, vidokezo na matumizi ya misimbo katika riwaya ya kiupelelezi anakubali kwamba usimulizi katika utanzu wa kiupelelezi hufanikishwa kwa kumpa msomaji vidokezo kadhaa mwanzoni mwa msuko ili aweze kuwa na usawa wa kushindana na mpelelezi katika utatuzi wa migogoro ya riwayani. Kazi ya Weiss ingawa inhusu uhakiki wa misimbo na ishara, imekuwa muhimu katika kuelewa muundo wa msuko wa riwaya za kiupelelezi.

Wahakiki wengine walioangazia viwango mbalimbali vya kifani katika riwaya ya kiupelelezi ni Gromov (2012), Khamis (2012) na Mbatiah (2020). Gromov alihakiki maendeleo ya riwaya ya kihalifu nchini Tanzania na kugundua kuwa waandishi wengi wa kazi hizo walifuata fomyula za Kimagharibi. Athari moja ya Kimagharibi inayojitokeza ni usawira wa mpelelezi wa kiserikali anayeshindwa na mpelelezi wa kibinafsi. Kulingana na Gromov, waandishi Ben Mtobwa na Elvis Musiba wameboresha viwango vya upelelezi katika kazi zao. Anaeleza kuwa wapelelezi wa kazi zao ni wa viwango vya kimataifa kwani wanapambana na maajenti wa kisiri na majasusi wa nchi nyingine. Mawazo ya Gromov yametufaa katika kupata misingi ya kuwakikia wahusika wa kiupelelezi katika riwaya teule. Kuhusu msuko, anadokeza kwamba taharuki ni kipengele muhimu katika kunasa makini ya msomaji. Anaeleza kuwa msuko hupitia mabadiliko makuu kabla ya kufika mwishoni pamoja na vitendo kufanyika kwa kasi ya juu kando na kuwa na miishio ya kushtukiza. Sifa nyingine inahusu utolewaji wa adili mwishoni mwa msuko. Khamis (2012:161-164) amehakiki wasifu wa Bwana Msa katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na kuonyesha kuwa ana sifa zinazoshabihiana sifa za Sherlock Holmes lakini wakati huo huo akidumisha uafrika wake. Anazitambua sifa za Msa kama vile kuwa jasiri, mwenye maarifa mengi na asiyeogopa kujiingiza katika hatari. Maoni haya yanatusaidia kuuelewa wasifu wa wahusika wa kipelelezi kijumla kando na kutuwezesha kutimiza lengo letu la pili. Mbatiah (2020) amehakiki sifa za fasihi pendwa katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea riwaya za *Mzimu wa Watu wa Kale, Simu ya Kifo*, *Mtaka Yote Hukosa Yote*, *Mwisho wa Mapenzi*, *Doa la Mauti* na *Najisikia Kuua Tena*. Amedhihirisha dhamira na motif zipatikanazo katika kazi hizo ambazo ni tama inayochochea uhalifu kama vile mauaji na vifo. Mauaji yanayoletwa na tama nayo yanachochea ulipishaji kisasi. Hizi ni sifa muhimu za kimsuko ambazo zitatufaa katika kujadili mbinu za ujenzi wa msuko wa riwaya teule. Sifa za kifani anazohakiki Mbatiah ni mandhari na uhusika. Kuhusu uhusika anaonyesha kuwa Abdulla amemuumba mhusika mpelelezi Bwana Msa kwa kielelezo cha Sherlock Holmes, ishara kuwa ameathiriwa na uandishi wa Conan Doyle huku naye Abdulla

akiwaathiri waandishi wa baadaye kama vile Faraj Katalambulla. Ingawa kazi yetu ni tofauti na hii, mkabala wake wa ufafanuzi wa wahusika umetufaa katika uhakiki wa uhusika hususan kuhusiana na uhusika wa kimwingilianomatini.

## 1.8 Msingi wa Kinadharia

Ili kuyaafiki vyema malengo ya utafiti huu, mtafiti ametumia nadharia tatu zinazokamilishana na kuingiliana. Kwanza, utafiti huu kwa kiasi kikubwa umetumia nadharia ya umitindo katika kuhakiki mbinu za ujenzi wa msuko za Sadfa, taharuki, mbinu rejeshi na kiona mbele miongoni mwa nyinginezo. Nadharia hii pia itatusaidia kuhakiki sajili za lugha, lahaja na lafudhi zinazojitokeza katika maongezi ya wahusika. Wamitila (2003) anaeleza kwamba nadharia hii iliwekewa misingi yake na Buffon (1930) ambaye alidai kwamba mtindo ni mtu mwenyewe, yaani jinsi mtu anavyotumia lugha kupitisha ujumbe wake. Mawazo haya yaliendelezwa na Coombes (1953) ambaye alifafanua kwamba ili kuchanganua mtindo katika kazi ya kifasihi ni lazima kuchanganua vipengele vinavyoifanya kazi hiyo ivutie. Vipengele hivyo ni kama vile uteuzi wa maneno, matumizi ya taswira, urari wa vina na mahadhi ya mashairi. Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa elimumitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi na uchanganuzi wa jinsi mbalimbali za kuelezea matukio katika kazi za kifasihi. Elimumitindo huhusisha uchunguzi wa sifa za kimtindo zinazojitokeza katika kazi za kifasihi na zinazomtambulisha mwandishi. Kwa kuzingatia maoni ya wataalam hawa, kazi hii imedhihirisha mitindo ya waandishi ambao kazi zao zinachunguzwa kwa kuzingatia uhakiki wa muundo na usimulizi katika riwaya ya kiupelelezi. Kwa kuzingatia mawazo ya Coombes, tumechunguza ikiwa usimulizi, msuko na uhusika kama vipengele vya kifani vimeendelezwa kwa njia inayoleta mvuto na kupendwa kwa riwaya ya kiupelelezi.

Wanamitindo husisitiza umuhimu wa lugha kama chombo kitekelezi kinachosaidia katika kuelewa maudhui yaliyokusudiwa. Wanasisitiza kuwa vipengele vya kiisimu hutumika kueleza jinsi lugha hutumika. Vipengele hivyo ni kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia na uteuzi wa maneno. Nadharia hii inachukulia kuwa tofauti za kimtindo huweza kutokana na mabadiliko yanayohusu kipengee kimoja kama vile kile cha uteuzi wa maneno au muundo wa sarufi. Kwa msingi huu tutachunguza namna wahusika wanavyotumia lugha kama vile kuwepo kwa sajili za aina mbalimbali katika riwaya za kiupelezi.

Leech (1969) anasema kuwa kazi ya fasihi hukusudia kuwasilisha hisi au tajriba fulani kwa wasomaji au wasikilizaji. Anadai pia kuwa, kazi za kisanaa huchambuliwa kwa kuangalia mitindo ya mwandishi. Alifafanua kwamba muundo wa kazi ya kifasihi ni muhimu katika kupitisha ujumbe. Kwa mfano, akirejelea mashairi, anasema kuwa ni vizuri kuchunguza jinsi msitari mmoja ulivyounganishwa na mwingine, ubeti na mwingine au wazo na lingine. Anaeleza kuwa lugha ya kifasihi nayo ina muundo wake uliosheheni vipengele kama vile usambamba, urudiaji, tanakali za sauti na ukiushi wa aina mbalimbali. Leech anatambua aina mbalimbali za ukiushi katika kazi za kifasihi. Aina hizo ni kama vile ukiushi wa kileksika, kifonolojia, kisemantiki kisintaksia na hata ukiushi wa kipindi cha kihistoria kiuandishi. Mawazo ya Leech yametufaa katika kuchunguza ikiwa ukiushi unaweza kujitokeza kupitia usimulizi, msuko na uhusika katika riwaya ya kiupelelezi.

Leech na Short (2007) wanamrejelea kazi yao ya mwaka wa 1981 ambayo ilijikita katika uhakiki wa kimtindo wa mashairi. Wanasema kwamba pamekuwa na maendeleo makubwa katika taaluma ya umitindo na kwa sababu hiyo, uhakiki wa kimtindo ni sharti uzingatie suala la usimulizi hasa mtazamo, uhusika, msuko na mandhari. Maoni haya yanatuhakikishia kuwa umitindo ni njia tosha ya kuchanganua masuala makuu ya utafiti huu ambayo ni usimulizi, msuko na uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Ifuatayo ni baadhi ya mihimili itakayofuatwa katika utafiti huu. Kwanza, dhana ya mtindo kuwa mtu mwenyewe ni mhimili tutakaotumia kuonyesha tofauti za kimtindo baina ya waandishi wa riwaya za kiupelelezi katika vipindi na maeneo mbalimbali. Kwa kuzingatia msingi huu, tutaonyesha namna mitindo ya Mohammed Said Abdulla, Elvis Musiba, Ben Mtobwa, Faraj Katalambulla na John Simbamwene inavyofanana, inavyotofautiana na kuathiriana. Pili, ukiushi hujitokeza katika viwango mbalimbali vya lugha. Kwa mfano, kuna ukiushi wa kifonolojia, kisemantiki, kileksika na kisarufi. Tutachunguza namna aina hizi za ukiushi zinavyojitokeza baina ya mazungumzo ya wahusika na sababu zinazochangia kuwepo kwa matumizi hayo. Kando na aina hizi, Leech (1969) anazungumzia pia ukiushi wa kipindi fulani cha kihistoria. Riwaya ya kiupelelezi ina mtindo maalum unaofuata kanuni zilizowekwa na waasisi wake. Utafiti huu utaonyesha ikiwa kanuni za kiutanzu zilizowekwa na waasisi wa utanzu wa kiupelelezi zimekiukwa au la. Tatu, muundo ni muhimu katika kuelewa ujumbe wa kazi ya kifasihi. Mwanaumitindo, Simpson (2004 na 2007) pia ametoa mawazo muhimu katika nadharia ya umitindo. Simpson (2004:26-34) anaeleza kwamba vigezo vya kisimulizi vya mtazamo na sawia mbalimbali za mtazamo zinaweza kuchunguzwa kupitia vipengele vya kiisimu. Kwa mfano,

uchunguzu wa sauti za kisimulizi huelezwa kupitia mabadiliko ya kisarufi. Vilevile, udhihirishaji wa mtazamo katika sawia za kiisimu, kimwanda-wakati na kisaikolojia hutegemea kategoria za kileksika. Mhimili huu ni muhimu katika kazi hii kwani umetufaa kuhakiki sawia za mtazamo. Simpson pia anafafanua (uk.85) mbinu mbalimbali za uwasilishaji wa usemi na fikira katika mazungumzo ya wahusika. Baadhi ya mbinu hizo zimetufaa katika kufafanua suala la uhusika na usimulizi.

Nadharia ya Utanzu imetumiwa pia ili kufafanua sifa bainifu zinazoipambanua aina hii ya riwaya na vipera vinginevyo vya riwaya. Kulingana na Chandler (1989), dhana ya utanzu hurejelea uwekaji wa makundi ya kifasihi katika kategoria na daraja. Robert (1989) akinukuliwa na Chandler anaeleza kwamba jukumu la nadharia ya utanzu ni kuugawa ulimwengu wa kifasihi katika kategoria maalum na kuzipa kategoria hizo majina maalum. Kwa hivyo, katika fasihi andishi, kuna tanzu za riwaya, tamthilia na ushairi. Utanzu wa riwaya nao una vijitanzu vya riwaya ya kiuhalifu, riwaya ya kijasira, riwaya ya kihistoria, riwaya ya kimapenzi miongoni mwa kategoria nyinginezo. Hata hivyo, uwekaji wa vipera vya kifasihi katika makundi haya si kazi rahisi kutokana na kuwepo kwa mwingiliano mkubwa baina ya tanzu. Chandler anajadili kuwa tanzu za kifasihi hazina mipaka bayana wala ramani dhabiti. Hii ni kutokana na kweli kwamba sifa zipatikanazo katika utanzu mmoja zinaweza kupatikana katika tanzu nyinginezo. Bordwel (1989:147) anaunga mkono wazo hili akisema kwamba ugawaji wa tanzu za kifasihi kwa misingi ya dhamira unaibua utata zaidi kwa kuwa dhamira zozote zinaweza kupatikana katika utanzu wowote ule. Mhakiki wa kifilamu, Stam (2000:14) anafafanua kuwa nadharia ya utanzu inahusu uwekaji wa vijipera vya kifasihi katika makundi yenye sifa zinazoshabihiana hivi kwamba kila kundi hujipambanua na kundi lingine kwa njia hiyo. Hata hivyo anakubali kwamba pana ugumu katika uainishaji wa fasihi kiutanzu. Anauliza, ‘Kuna mipaka bayana ya kiutanzu ama tanzu zipo tu kijumla? Je, tanzu zina mipaka ya kiwakati au la?, Je, tanzu zina mipaka ya kiutamaduni ama huwa sawa katika tamaduni zote?

Hata hivyo, ingawa kuna matatizo haya ya uainishaji wa fasihi kiutanzu, wahakiki na waasisi wa riwaya ya kiupelelezi wameweza kuibuka na sifa maalum zinazoipambanua riwaya ya kiupelelezi na aina nyinginezo. Baadhi ya sifa hizo maalum zinahusu masuala yanayochunguzwa na tasnifu hii ya uhusika, msuko na usimulizi. Sifa maalum zilizotangulizwa na waasisi wa utanzu wa kiupelelezi kama vile Edgar Allan Poe, Ronald Knox na S.S. Van Dine, ziliendelezwa baadaye na

watunzi waliofuata kama vile Conan Doyle. Kwa mfano, Allan Poe alipotanguliza utanzu huu (1841), alizua mfumo wa kutumia mpelelezi mkuu asiye afisa wa kipolisi lakini mwenye kipawa cha kutumia mantiki kuchunguza uhalifu na wahalifu. Pia alibuni mbinu ya kumtumia mhusika msaidizi lakini asiye na maarifa mengi kama alivyo mpelelezi mkuu. Kando na mbinu hizi, sheria za kuongoza utunzi wa kazi za kiupelelezi zimewekwa na wahakiki mbalimbali. Kwa mfano, William Huntington (1936) akiandika kwa jina la kimsimbo la Van Dine aliitunga sheria ishirini za utunzi wa riwaya ya kiupelelezi zilizojitokeza katika jarida la Kimarekani la mwaka wa 1936 kama nyongeza ya sheria kumi za utunzi huu zilizoanzishwa na Ronald Knox, 1929. Sheria na kanuni zilizowekwa na waandishi hawa zimekuwa msingi bora wa kuhakikia sifa bainifu za utanzu wa riwaya ya kiupelelezi. Nadharia hii ya utanzu kwa hivyo itatusaidia kuchunguza sifa za kiutanzu katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Sifa hizo zimechunguzwa kupitia vipengele vya msuko, usimulizi na uhusika.

Nadharia ya naratolojia pia imetumika katika utafiti huu ili kutuwezesha kuhakiki usimulizi katika riwaya teule. Genette (1983) anaeleza dhana ya simulizi kama mfuatano wa matukio halisi au ya kibunilizi, tendo lenyewe la usimuliaji au kauli ya kisimulizi inayonuiwa kuelezea tukio fulani. Mawazo ya kimsingi ya nadharia hii yalijitokeza mwanzo katika kitabu cha Plato, *The Republic* andiko la tatu. Katika kitabu hiki, Plato akizungumzia usimuliaji aliibuka na dhana za mimesia na daigesia. Katika mimesia mtunzi hajitokezi wazi wazi kama msemaji ilhali katika daigesia mtunzi, kupitia msimulizi hujitokeza na kutambulikana. Mtaalamu mwingine aliyechangia zaidi katika ukuaji wa nadharia hii ni Vladimir Propp alipochunguza miundo ya hurafa. Kuhusu msuko, alitambua matukio mbalimbali yanavyofutatana kiusababishi katika hurafa hizo. Mawazo yake yaliweka nguzo bora ya uchunguzi wowote wa kimsuko.

Mwananaratolojia mwingine ambaye maoni yake ni muhimu katika tasnifu hii ni Rimmon-Kenan (2002). Rimmon-Kenan alifafanua mbinu za kiusimulizi zipatikanazo katika kazi za kibunilizi, uainisho wa sauti za kisimulizi, udhihirikaji wa msimulizi na suala la mtazamo. Anaeleza kwamba ili kufafanua usimulizi vyema ni sharti mhakiki azingatie mpangilio wa matukio katika msuko, muda wa usimulizi na suala la mtazamo wa mwandishi au msimulizi. Anasisitiza pia suala la uhusika na wahusika sharti liangaziwe ili kuelezea vyema muundo wa usimulizi. Anaonyesha kuwa uhusika unaweza kudhihirika kupitia njia mbili kuu ambazo ni; uelezaji wa moja kwa moja unaofanywa na mwandishi kuhusu wahusika wake na pili, udhihirishaji wa wahusika kupitia

vitendo vyao. Kwa hivyo, maoni haya yametufaa katika kutimiza malengo ya kuhakiki usimulizi, uhusika na ujenzi wa msuko. Kando na kutufaa katika usimulizi, jambo hili litatufaa katika uhakiki wa uhusika. Bal (2017:83-90) pia anatoa mchango mkubwa katika uhakiki wa kinaratolojia. Maoni yake kuhusu mbinu za ujenzi wa msuko kama vile mbinu rejeshi, kiona mbele na usimulizi tegemezi yametufaa. Mawazo haya kijumla, yatakuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu yanalandana na malengo ya kazi hii ambayo ni kuchunguza uhusika, msuko na usimulizi katika riwaya za kiupelelezi.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti wowote ule hutegemea aina ya utafiti. Kwa hivyo, aina ya utafiti huathiri ukusanyaji wa data, uteuzi wa sampuli, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wake. Kwa mfano, utafiti kiasi huitaji data za kitakwimu ilhali utafiti stahilifu hutumia data ya kimaelezo. Utafiti huu hahuhusu data za kitakwimu bali za kimaelezo. Chini hapa tunaonyesha mbinu mbalimbali ambazo mtafiti alitumia katika ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

### 1.9.1 Ukusanyaji wa data

Kwa kiasi kikubwa utafiti wetu umefanywa katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Nairobi. Kwa sababu hii, sehemu kubwa ya utafiti huu imefanyika maktabani ambapo mtafiti atatumia maktaba ya chuo kikuu cha Nairobi pamoja na kuzuru vyuo vingine kutafuta na kusoma vitabu na makala mbalimbali. Data ya kimsingi ilihusu usomaji mpevu wa riwaya zilizoteuliwa kwa kuchambua vipengele vya vya uhusika, usimulizi na msuko pamoja na kudhihirisha dhima ya kila kipengele katika kuimarisha umbuji wa riwaya husika. Vifungu vimenukuliwa kutoka kwa riwaya hizo ili kuthibitisha kauli zitakazotolewa kuhusu uhusika, usimulizi na msuko.

Data ya ngazi ya pili ilipatikana kupitia usomaji wa tasnifu mbalimbali zinazohusu riwaya ya kiupelelezi na fasihi pendwa kijumla. Tulisoma vitabu mbalimbali vinavyozungumzia mada yetu, magazeti na majarida ya lugha na fasihi ili kupata data ya kiwango cha pili inayohusiana na mada yetu.Usomaji huu umetuwezesha kuona namna maswala ya muundo na usimulizi yanavyoangaziwa pamoja na uhakiki wa riwaya ya kiupelelezi kijumla. Usomaji huu pia umetupatia uelewa wa kina kuhusu nadharia za naratolojia, umitindo na ile ya utanzu ambazo zinaongoza utafiti huu pamoja na suala la utafiti. Pia tulifanya majadiliano na wasimamizi na wanafunzi wengine ili kupata maoni yao kuhusu hali ya riwaya ya kiupelelezi katika Afrika

Mashariki pamoja na maoni yao kuhusu muundo, usimulizi na nadharia. Zaidi ya hayo, tumerejelea mtandao pamoja na tovuti mbalimbali katika kutafuta vitabu na makala yanayohusiana na fani au riwaya za kiupelelezi.

### 1.9.2 Uteuzi wa Sampuli

Data ya utafiti huu imeteuliwa kimakusudi kwa kuzingatia vigezo kadhaa. Kwanza, tuliteua data ambayo ingewakilisha uandishi wa Afrika Mashariki. Kwa kuwa riwaya ya Kiswahili ina chimbuko lake katika Afrika Mashariki, riwaya zinazohakikiwa ziliteuliwa kwa misingi ya kimaeneo. Kwa hivyo, juhudi zilifanywa kuteua riwaya kutoka nchi za Afrika Mashariki. Hata hivyo, riwaya nyingi zilizoteuliwa zimeandikwa na waandishi wa Kitanzania (riwaya saba kati ya tisa zilizoteuliwa). Kuna kazi chache mno za kiupelelezi zilizoandikwa kwa Kiswahili kutoka kwa waandishi wa Kikenya. Kwa sababu hii, mtafiti alipata riwaya mbili tu za kiupelelezi kutoka nchini Kenya na hamna hata moja kutoka nchini Uganda. Inatarajiwa hata hivyo kwamba, sampuli hii imetosha kuwakilisha Afrika Mashariki.

Data ya kimsingi ilikusanywa kutoka kwa kazi za Mohammed Said Abdulla, Ben Mtobwa, Elvis Musiba, Godfrey Levi, Faraj Katalambulla na John Simbamwene. Uteuzi wa kimakusudi ulifanywa baada ya usomaji wa kina wa riwaya za watunzi hawa ili kuchagua kazi zilizo na fani pevu. Mtafiti aliteua riwaya za *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani kuna Watu* (1973), *Simu ya Kifo* (1965), *Tutarudi na Roho Zetu?* (1984), *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975), *Kwa Sababu ya Pesa* (1972), *Njama* (1984) na *Uchu* (2000). Vitabu hivi viliteuliwa kwa kuwa vina matumizi pevu ya kifani pamoja na kuangazia maswala muhimu ya kijamii. Pili, mhakiki aliziteua riwaya hizi kutegemea viwango vya upelelezi vinavyodhihirika katika kazi teule. Kuna riwaya zinazohusu upelelezi wa kimataifa na zile zihusuzo upelelezi wa kitaifa. Kwa msingi huu, riwaya za Mtobwa na zile za Musiba zimeteuliwa kuwakilisha upelelezi wa kimataifa.

### 1.9.3 Uchanganuzi wa Data na Uwasilishaji wa Matokeo

Data iliyopatikana maktabani ilichanganuliwa kiufafanuzi kwa kuongozwa na malengo ya utafiti huu pamoja na nadharia za naratolojia, umitindo na utanzu. Tulidondoa vifungu mbalimbali vilivyodhibitisha hoja zinazotokana na vipengele vya uhusika, msuko na usimulizi kutoka kwa

riwaya teule. Matokeo yametolewa kwa njia ya kimaelezo tukitumia mtindo wa kinadhari. Michoro michache kama vile majedwali, pia imetumika kuwasilisha baadhi ya data.

### 1.9.4 Mbeko Katika Utafiti.

Kwa kuwa kila taaluma huongozwa na maadili fulani, pia mtafiti sharti azingatie mbeko na maadili ili matokeo yake yaweze kuaminika. Kwa sababu hii, mtafiti hafai kutafiti kwa lengo la kujinufaisha au kuathiri jamii kwa njia hasi. Kwa kuwa utafiti wetu si wa nyanjani, maadili katika utafiti huu yameegemea zaidi upande wa mtafiti. Tumejiepusha na uigaji wa kazi za watafiti waliotutangulia na pale ilipotupobidi kunukuu wazo la mtafiti mwingine, kila juhudi zimefanywa kuhakikisha kwamba jina la mhakiki au mwandishi limetajwa pamoja na mwaka wa uchapishaji wa kazi hiyo. Uigaji wa kazi za kiakademia ni kinyume na sheria kando na kuwa ishara ya ukosefu wa uaminifu (Mugenda na Mugenda, 2003:190).

Ili kutimiza maadili katika utafiti huu, tutahakikisha kwamba matokeo ya uchunguzi wetu yamewekwa wazi kwa ajili ya kuinufaisha jamii. Ni ukosefu wa maadili kwa mtafiti kuficha matokeo ya utafiti wake. Kando na kuwa ni ukosefu wa maadili, pia ni upotezaji wa muda na rasilimali. Kwa sababu hii, matokeo ya utafiti huu yameanza kuchapishwa katika baadhi ya majarida ya kifasihi ili kuinufaisha jamii.

## 1.10 Hitimisho

Sura hii imeweka msingi wa utafiti kwa kufafanua swali la utafiti na usuli wake, kubainisha malengo pamoja na maswali ya utafiti. Nadharia zinazoongoza utafiti huu pia zimeelezwa pamoja na kufanya mapitio ya tafiti za awali zinazohusiana na fasihi pendwa, riwaya ya kiupelelezi na masuala ya kifani. Sehemu ya mwisho ya sura hii imeshughulikia mbinu za utafiti na masuala ya maadili katika utafiti.

# SURA YA PILI

# UKUAJI NA MAENDELEO YA RIWAYA YA KIUPELELEZI

## **2**.1 Utangulizi

Riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili imejitokeza katika miaka ya hamsini (Mlacha na Madumulla, 1995: 13, Swaleh, 2005: 72, Mbatiah 2016: 122) kutokana na maandishi ya Mohammed Said Abdulla. Hata hivyo, uchipukaji wa utanzu huo una historia ndefu. Kwa mfano, baadhi ya wahakiki wanaihusisha riwaya ya kiupelelezi na maendeleo ya kiteknolojia ya filamu za Kimagharibi (Madumulla, 1988: 13), huku nayo riwaya ya Kimagharibi ikihusishwa na uibukaji wa asasi za kipolisi huko Ulaya hasa katika mataifa ya Uingereza na Ufaransa. Sura hii inajaribu kufafanua vyanzo mbalimbali vya riwaya ya kiupelelezi ulimwenguni kabla ya kufika eneo la Afrika Mashariki. Tunachunguza vyanzo vya riwaya ya kiupelelezi katika fasihi simulizi, uibukaji wa riwaya hiyo Ulaya na Marekani, hasa kipindi cha urasmi cha miaka ya 1920-1930, uibukaji wa riwaya hizo Afrika Kusini na Magharibi na kisha kuzaliwa na kuendelea kwa riwaya hiyo katika maeneo ya Afrika Mashariki ili kuuelewa muktadha wa kihistoria uliosababisha ukuaji na maenezi yake.

Kuna mwingiliano mkubwa baina ya vipera mbalimbali vya fasihi pendwa kutokana na ukweli kwamba kuna sifa bia zipatikanazo katika vipera vyote vya riwaya pendwa. Kwa mfano, katika riwaya ya uhalifu, riwaya ya kimapenzi, riwaya ya kijasira na riwaya ya kiupelelezi kuna dhamira ya burudani katika tanzu zote. Pili, kazi nyingi za fasihi pendwa huandikwa kwa kutumia lugha sahili ili kurahisisha usomekaji wa kazi hizo. Mambo haya huongeza mvuto kwa kazi hizo hivyo kusababisha kupendwa na watu wengi. Dhamira bia nyinginezo zipatikanazo katika riwaya pendwa ni uhalifu (haswa unaofanyika katika mazingira ya mijini kutokana na hali ngumu za kimaisha zinazoletwa na ukosefu wa kazi), ukahaba, mapenzi, upelelezi na jasira. Ingawa utafiti huu unajikita katika kijitanzu kimoja cha riwaya pendwa, cha upelelezi pekee, dhamira zilizotajwa hapo juu pia huweza kujitokeza kama vipengele vidogo vya ujenzi wa dhamira kuu ya upelelezi.

## 2.2 Vyanzo vya Riwaya ya Kiupelelezi katika Fasihi Simulizi na Maandishi ya Mapema

Fasihi simulizi ina athari kubwa katika fasihi andishi ya lugha nyingi za ulimwengu. Kwa hakika wahakiki wengi wameonyesha kuwa fasihi andishi ya Kiswahili ni zao la fasihi simulizi (Mbughuni 1978:123, Ohly 1981:4, Park 2004:26). Kwa mfano, Park alichunguza kuwepo kwa athari za fasihi simulizi katika fasihi andishi ya mapema ya Kiswahili. Anasema,

> Ingawa fasihi ya Kiswahili ina historia ndefu ya kimaandishi, kazi za kibunilizi za Kiswahili zilianza kujitokeza katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa. Kama ilivyo katika fasihi za lugha nyinginezo, kazi za kibunilizi za Kiswahili katika awamu ya kwanza zilikuwa na elementi nyingi za fasihi simulizi (2004:17).

Uchunguzi wa visa vya kiupelelezi vyenye mizizi yake katika fasihi simulizi unatubainishia uhusiano uliopo baina ya riwaya ya kiupelelezi kama tunavyoifahamu leo na fasihi simulizi. Jamii mbalimbali zina ngano zinazoonyesha kuwa riwaya ya kiupelelezi ilichipuka kutokana na mizizi ya fasihi simulizi. Sayers (1929) akinukuliwa na Scaggs (2015:7) anatambua vyanzo vinne vya riwaya ya kiupelelezi ambapo vyanzo viwili kati ya hivyo vinne ni visasili kutoka karne ya tano kabla ya kuzaliwa kwa Yesu. Anataja kisasili cha Herodoti na kile cha Herakili. Katika kisa cha Herakili, mwizi Kakasi anatoa ushahidi wa uongo anapopatikana na hatia ya wizi. Inajulikana kwamba, baada ya upelelezi, mwizi Kakasi alipokuwa anasakwa alighushi nyayo zake ili kumpotosha aliyekuwa akimsaka. Nayo hadithi ya Herodoti inahusu mfalme Rhampisinitu na mwizi mmoja ambapo pia mwizi huyo alikuwa ameharibu ushahidi ili kuepuka kukamatwa. Inaaminika kwamba hii ndio hadithi ya kwanza kuwahi kutumia mazingira ya chumba kilichofungwa ambako uhalifu unafanyikia. Hali kama hii inakuwa ngumu kubaini kilichofanyika kwani inakuwa vigumu kuingia wala kutoka chumbani humo.

Hadithi hizi zinaashiria dalili za mwanzo kabisa kuhusu upelelezi, ikiwa ishara kwamba upelelezi uliendeshwa katika jamii mbalimbali hata kabla ya kuibuka kwa fasihi andishi. Mtindo wa uchunguzi wa mambo kwa njia kama hii unachukua nafasi kubwa katika hadithi za upelelezi zilizofuata miaka mingi baadaye. Mhakiki, Julian Symons (1993) anachukulia kuwa maoni haya yana ukweli kwa kiasi fulani. Wazo lake ni kwamba hadithi hizi zinazochukuliwa kuwa za mwanzo katika fasihi ya upelelezi zilihusu uchanganuzi wa mafumbo tu bila kuonyesha itikadi yoyote. Hata hivyo, anakubali kuwa kuwepo kwa mafumbo ni sifa moja kuu ya hadithi zote za upelelezi. Pili, Symons anazikashfu hadithi hizi kwa kutotoa adhabu kwa mhalifu kama sehemu

ya msuko wa hadthi.Yaani, badala ya kumuonyesha mhalifu akiadhibiwa, zilimsawiri kama shujaa. Kwa mfano, katika hadithi ya Herodotus, Mfalme Rhampsinitus anamsifu na kumtuza mwizi kwa sababu ya ujasiri na ujanja wa kuficha ushahidi wa uhalifu wake. Kama zawadi, anampa huyo mwizi bintiye amuoe. Kitendo hiki kinapotosha maadili kwani kinadhihirisha kwamba uhalifu hulipa.

Katika Bibilia, kitabu cha Danieli (chapa ya Kigriki, sura ya kumi na tatu), kuna ngano mbili zihusuzo upelelezi. Kwanza, kuna kisa cha Susana na wazee wawili mahakimu. Hiki ni kisa chenye etimolojia ya Kiebrania lakini kipatikanacho katika kanisa la Katoliki huko Ugiriki na pia katika kanisa la Kiothodoksi. Wazee hao walimtamani Susana na alipokataa matamanio ya kuzini nao, walimwekea kesi ya uongo kuwa alipatikana akizini na kijana fulani. Kisadfa, wazee hawa ndio mahakimu wanoisikiliza kesi ya Susana na wanaamua auawe kulingana na sheria za Musa. Kupitia maombi ya Susana, Mungu anamtuma Danieli kuwa wakili wake. Anapowahoji wazee hawa wanatoa majina tofaouti ya mti ambapo tendo lilifanyikia. Inabainika kwamba wao ni waongo na wanahukumiwa kifo. Hadithi ya pili kutoka kitabu hiki hiki inahusu Danieli na makasisi wa Bel ambapo makasisi hawa wanawalaghai waumini wanapopeleka kafara zao hekaluni. Wanadai kuwa mungu wa Babel, aina ya joka, ndiye hula na kunywa kafara zote zitolewazo na waumini ilhali makasisi hawa, bibi zao na watoto wao ndio huingia hekaluni kupitia mwanya wa siri na kula matoleo hayo wenyewe. Danieli kama mpelelezi, anaingia hekaluni kwa siri na kumwaga jivu kwenye sakafu ya hekalu na kisha kufunga hekalu kama kulivyokuwa awali. Baadaye anapoingia na kukuta nyayo kadhaa katika sakafu hiyo, anawaita makasisi hao na kuzilinganisha nyayo zao na zilizo sakafuni. Upelelezi wake unakamilika anapogundua kuwa makasisi ndio waliokuwa wakila matoleo hayo. Makasisi hao na familia zao pia wanahukumiwa kifo.

Scaggs anasema kuwa hadithi ya Danieli na makasisi hawa kama ilivyo ile hadithi ya Mfalme Rhampisinitu na mwizi, ndizo vyanzo vya hadithi za upelelezi zenye uajabu wa uhalifu hasa mauaji kutendeka ndani ya chumba kilichofungwa. Kama tutakavyoona baadaye katika hadithi nyingi za kiupelelezi zilizotokea hasa Ulaya, motifu hii inayohusu mauaji kufanyika katika chumba kisicho na upenyu wa kuingilia ilitumika sana. Symons (1993) anazisifu sana hadithi hizi za mwanzo akisema kuwa ziliweza kubeba kipengele cha adhabu kama sifa muhimu ya upelelezi. Kwa wahakiki kama Symons, hadithi za kiupelelezi zinachukua sifa ya kifasihi simulizi ya kudumisha maadili kwa kuonyesha adhabu inayomkabili mhalifu mwishoni mwa hadithi. Jambo

hili limeendelezwa katika riwaya nyingi za kiupelelezi kama tutakavyoonyesha katika riwaya za kiupelelezi zinazochunguzwa katika tasnifu hii. Hii ni ishara tosha kwamba riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili pia ina mizizi yake katika fasihi simulizi. Knight (1980:2) alikuwa ametambua sifa ya kufunza maadili ipatikanayo katika hadithi za kiupelelezi kwa kutoa mfano wa hadithi ipatikanayo katika Bibilia ya Kaini na Abeli. Kaini anapomuua ndugu yake anapata adhabu maradufu. Jambo hili linatilia mkazo wazo kwamba utoaji wa adhabu ni kipengele muhimu katika kulinda haki na sheria. Symons anahitimisha kuwa sifa hii inajitokeza katika kazi za mwandishi wa Uingereza Allan Poe, kwani kazi zake pia zinatoa adhabu kwa mhalifu ili kutetea maadili.

Kisasili kingine kinachohusu upelelezi ni kile cha kutoka mji wa Thebe huko Ugiriki. Kinahusu namna Edipode alivyomuua babake na kisha kumuoa mamake. Mji wa Thebe unakumbwa na janga kubwa na wakaazi wanamuendea mfalme Edipode awaokoe kama alivyokuwa amefanya hapo awali. Mfalme naye anamtuma ndugu yake, Krioni kuenda kuzungumza na miungu ili kupata namna ya kuwasaidia wenyeji wa Thebe. Miungu inatoa ujumbe kwamba ili matatizo ya wakaazi yakome ni sharti aliyemuua mfalme wa awali (Laio) asakwe na kupewa adhabu itakayohusu kuondolewa mjini. Krioni katika upelelezi wake anaambiwa kuwa muuaji huyo yuaishi tu mjini wao Thebe. Mfalme Edipode anatumia kipawa chake na nguvu zake za kiutawala na kupata habari kutoka kwa mtabiri (Teresia) kwamba muuaji alikuwa ni Edipode mwenyewe. Anapogundua haya, Edipode anajipa adhabu mwenyewe kwa kujitoboa macho yake na kujitenga na wananchi. Janga lililokuwepo linamalizwa na hali ya kawaida inarejea iliyokuwa imeharibiwa na uhusiano wa kindoa baina ya Edipode na mamake. Hadithi hii inatuonyesha namna upelelezi ulivyokuwa ukiendeshwa katika jamii hii kwa kutumia njia za kiganga badala ya zile za kisayansi zinazotumika katika riwaya za kiupelelezi za kisasa. Hata hivyo, ni ishara kuwa dhana ya kupeleleza ina historia ndefu kando na kuzagaa katika jamii nyingi za ulimwengu.

Huko Uarabuni kuna hadithi ambayo inachukuliwa kuwa ya kwanza kabisa ipatikanayo katika mkusanyiko wa hadithi za *Alfu Lela U Lela.* Hadithi hii inajulikana kama ‘Tufaha Tatu’. Katika hadithi hii, mvuvi akiwa mtoni anapata kijisanduku kikielea majini na kukichukua ambapo anamuuzia mfalme Khalifa Haruni Al-Rashid. Khalifa anaamuru kisanduku kifunguliwe ambamo mnapatikana mwili wa mwanamke ukiwa umekatwakatwa. Anamwagiza Waziri Jaffari kuchunguza chanzo cha mauaji hayo na ikiwa angeshindwa kutatua hali hii katika kipindi cha siku tatu, basi angeuawa. Kisadfa, anapotangaza kuwa ameshindwa, watu wawili, kijana na mzee

(babake mwanamke aliyeuawa) wanakuja na kuripoti kila mmoja kuwa ndiye muuaji. Hali hii inaufanya msuko changamano zaidi na kuzua taharuki. Baada ya usaili inabainika kwamba yule kijana ndiye aliyekuwa muuaji na kwamba mzee alikuwa anasema uongo ili yeye afungwe kwa niaba ya kijana (shemeji wake).

Ingawa hadithi hii inachukuliwa kuwa miongoni mwa hadithi za mwanzo kabisa za kiupelelezi, mpelelezi wake, Waziri Jaffari, ana udhaifu mwingi kwani anashindwa kumpata mhalifu. Hata hivyo ina taharuki kuu pamoja na mabadiliko makubwa ya msuko. Hizi ni sifa maarufu zipatikanazo katika riwaya ya kisasa ya kiupelelezi. Upatikanaji wa sifa kama hizo katika riwaya za kiupelelezi ni ithibati kwamba riwaya hizi zina mizizi yake katika fasihi simulizi. Sifa ya kifasihi simulizi ya kutoa funzo la kimaadili mwishoni mwa hadithi pia inadhihirika; utoaji wa habari za uongo unakashfiwa ingawa kasoro katika maamuzi ya Khalifa ni wazi mno; kwa nini kwa mfano anatishia kumuua waziri mara mbili anaposhindwa kuchunguza visa mbalimbali ilhali anamsamehe kijana aliyemuua mkewe.

Katika fasihi simulizi za Kiafrika pia kuna vyanzo kadhaa vinavyoashiria kwamba upelelezi ulikuwepona uliendeshwa kwa njia tofautitofauti. Kimura (1992:46) anashikilia kwamba kwa kuwa vyombo vya kisasa vya upelelezi havikuwepo, upelelezi uliendeshwa kwa matumizi ya uchawi, ulaji kiapo, imani, uganga na mitazamo mingine ya kijadi. Kwa mfano, uapishaji ulitumiwa kuwapata wahalifu katika jamii ya Wameru, ambapo washukiwa kadhaa walikusanywa na kulazimishwa kula kiapo ili kuthibitisha au kukana kuhusika kwao katika kukataa uhalifu fulani. Katika jamii hii, mshukiwa alizamishwa kumdunga beberu kisu huku akiapa, ‘Kama mimi ndimi niliyehusika katika tendo hili, naomba nife kama mbuzi huyu’. Mshukiwa alipokataa kula kiapo hiki basi inaamuliwa kuwa ndiye mhalifu na kupewa adhabu. Asipoathirika kwa njia yoyote baada ya miaka kadhaa, inachukuliwa kwamba siye aliyekuwa mhalifu. Katika miviga hii adhabu ilitolewa na kundi la wanajamii hasa kundi la wazee kwani ilikuwa vigumu kwa mtu mmoja kuapisha na kutoa adhabu na kuwa shahidi wakati hio huo. Kimura anasema kwamba katika baadhi ya jamii za Kitanzania, uapishaji ulihusu watuhumiwa kupewa kipande kidogo cha mti kilichotumbukizwa kwenye chungu chenye maji. Kila mshukiwa alikitemea kipande chake mate akisema, ‘Kama ndimi mhalifu maji ya chungu hiki yanimwagikie’. Baada ya kusema hivyo hudondosha kipande hicho chunguni na kikielea, inachukuliwa kuwa siye mhalifu, lakini maji yakirukaruka basi inahitimishwa kuwa ndiye mhalifu.

Mapitio haya ya hadithi za kifasihi simulizi yanaonyesha kwamba suala la upelelezi lilikuwepo tangu jadi katika jamii mbalimbali za ulimwengu. Hali hii inatokana na ukweli kwamba uhalifu hasa mauaji ni aina ya uovu ulio na historia ndefu kama ilivyo historia ya binadamu (Anyango, 2016:51). Urejeleaji wa visa hivi hapa unatuwezesha kuweka muktadha bora wa kuchanganua riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

## 2.3 Chimbuko na Maendeleo ya Riwaya ya Kiupelelezi ya Kimagharibi

Tunatumia dhana‘riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi’ kumaanisha riwaya zilizoandikwa na waandishi wa kutoka Ulaya na Marekani. Tathmini ya riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi itatuonyesha ikiwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili jinsi ilivyo kwa sasa imeathiriwa kimuundo na riwaya hizo za Kimarekani na Ulaya au la. Bajaj (2015:4) anasema kwamba katika Ulaya, riwaya hizi zilijitokeza mara ya kwanza katika kazi za watunzi wa Ufaransa na Uingereza. Anasema kwamba hadithi ya kwanza ya kiupelelezi iliasisiwa na Allan Poe alipoandika hadithi ya ‘Murders in the Rue Morgue’ (1841). Inahusu mandhari ya Paris ya mwaka wa 1839 ambapo msimulizi (asiyetajwa) anakutana na Auguste Dupin, mtu mwenye maadili mema lakini aliye na umaskini. Wanakubaliana kuishi pamoja na katika maisha yao wanatumia muda wao mwingi kusoma na kutembea mjini. Ni katika matembezi hayo ambapo msimulizi anagundua kuwa Auguste Dupin ana talanta ya uchunzaji na kupeleleza mambo kutokana na uunganishaji wa vidokezo vidogo vidogo. Riwaya hii inahusu kisa cha mauaji ya mwanamke mmoja na bintiye katika chumba chao. Auguste Dupin, anapochunguza anabaini kuwa mwili wa mama yule ulikuwa umetupwa nje ya dirisha nao ule wa binti ukiwa umeshindiliwa kwenye chimni. Dupin anagundua kuwa alama za kipigo zinazoonekana kwenye miili hiyo hazikutokana na mikono ya binadamu bali mnyama wa familia ya tumbili. Mabaki ya nywele za mnyama huyo na mikwaruzo kwa maiti hizo pia ni ishara nyinginezo zilizomuongoza mpelelezi katika kutatua ni nini kilichokuwa kimewaua. Inathibitishwa baadaye kuwa kuna mtu mmoja aliyemnunua mnyama huyo kutoka mbali lakini akatoroka kwake na kuingia vyumbani akiwahangaisha wakaazi. Mnyama huyo alikuwa amepanda hadi ghorofa ya nne na kuwaua watu hao.

Hii kama hadithi ya kwanza ya kiupelelezi iliyoandikwa, ina umuhimu mkubwa katika utanzu huu kwa kuwa iliweka msingi wa waandishi wa baadaye. Mpelelezi katika hadithi hii, Auguste Dupin ni kielelezo cha wapelelezi wa baadaye kama vile Sherlock Holmes. Kando na kuathiri uhusika na masuala mengine ya kimtindo kama vile msuko, hadithi hii imekuwa nguzo ya dhamira

zilizoendelezwa na watunzi wengine. Dhamira kuu ilikuwa mauaji na uchunguzi wa namna mauaji hayo yalivyotendeka. Mandhari ya utokeaji wa uhalifu katika chumba kilichofungwa pia ni motifu iliyotumika mno katika kazi za watunzi wa Ulaya na Marekani.

Hadithi hii ilifuatwa na riwaya ya Charles Dickens, *The Bleak House* (1853) ambayo ingawa si ya kiupelelezi ina visa kadhaa vya kiupelelezi. Naye mwanafunzi wa Dickens, Wilkie Collins akafuatisha na riwaya mbili za *The Woman in White* (1859) na *The Moostone* (1868). Wilkie Collins anachukuliwa kuwa ndiye aliyeibuka na sheria za kwanza kabisa zilizoongoza katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi. Baadhi ya sheria hizo ni kama vile: Uhalifu kufanyika katika nyumba ya mashambani, matumizi ya vidokezo vya kupotosha, mtuhumiwa mwenye uhusiano wa karibu na mhasiriwa, kuwepo kwa mpelelezi maarufu, kuwepo kwa polisi wasio na maarifa mengi, kuhojiwa kwa mashahidi, mtuhumiwa wa uongo, kuhusishwa kwa visa mbalimbali na mabadiliko makubwa katika msuko.

Sayers (1992:75) anasema kuwa huenda Poe katika kubuni riwaya yake ya kwanza alichochewa na jambazi sugu wa Kifaransa aliyebadilika na kuwa afisa wa polisi na baadaye kuwa mpelelezi hodari. Badiliko hili kwanza lilimwathiri mwandishi wa Kifaransa, Eugene Francois Vidoq alipochapisha *Memoires* 1828, ambapo alionyesha badiliko llilohusu shujaa mwizi aliyebadilika na kuwa shujaa wa polisi. Hali hii ilitokana na maisha halisi ya mwizi maarufu aliyebadili hulka yake, kuwa askari wa polisi na baadaye akaanzisha taasisi ya kwanza ya uchunguzi huko Paris iitwayo, 'Surete' mwaka wa 1812. Shirika kama hilo lilianzishwa huko Marekani 1850 miaka 30 baadaye, nako Uingereza shirika la upelelezi likaanzishwa mwaka wa 1828 kama anavyosema Bajaj, kufuatia kubuniwa kwa sheria za kulinda jiji la London. Taasisi hii ya uchunguzi ya Uingereza ilibuniwa chini ya usimamizi wa Sir Robert Peel aliyekuwa mwanajeshi na wakili. Jambo hili linatokana na kweli kwamba nchi ya Uingereza haikiwa na taasisi ya polisi kabla ya hapo na kwa sababu hiyo wanajeshi ndio waliojaza nafasi ya kupambana na wahalifu. Kulingana na Sayers, uibukaji wa riwaya ya kiupelelezi huko Ulaya kulitokana na uzukaji wa taasisi za polisi hasa za kiupelelezi.

Mwaka wa 1887 mabadiliko makubwa yalijitokeza katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi huko Ulaya wakati Sir Conan Doyle alipoandika riwaya ya kwanza, *A Study in Scarlet*. Katika miaka ya baadaye, alifuatisha kwa riwaya nyingine tatu na hadithi fupi hamsini na sita ambako alimbuni mpelelezi Sherlock Holmes. Holmes alipewa sifa za aliyekuwa mwajiri wa Conan Doyle, Daktari

Joseph Bell aliyekuwa na kipawa cha uchunzaji. *A Study in the Scarlet* ilikuwa riwaya yake ya kwanza ambapo mhusika mkuu na mpelelezi Sherlock Holmes pamoja na msaidizi wake, Dkt. Watson walipojitokeza. Katika hadithi hii, Conan Doyle alifuata mtindo wa wahusika wa kifomyula uliokuwa umewekwa na mwasisi wa utanzu huo Allan Poe mwaka wa 1841. Akikubaliana na maoni haya, Phillips anasema kuwa:

> Kielelezo cha Poe kiliwaathiri watunzi wengi waliofuata, hasa Arthur Conan Doyle na Agatha Christie. Hadithi nyingi za Conan Doyle zilizomhusu mpelelezi Sherlock Holmes na za Christie zilizomhusu mpelelezi Hercule Poirot zina sifa nyingi mno za Poe. Kwa mfano, zote zinasimuliwa na mpelelezi msaidizi, uhalifu wote kusuluhishwa mwishoni mwa hadithi kando na idara ya polisi kusawiriwa kuwa dhaifu. (2016:7)

Kama tunavyoona katika nukuu hili, mtindo wa Allan Poe uliwaathiri watunzi wengi si tu katika ubunifu wa mhusika mpelelezi bali pia katika mtindo wa usimulizi. Kama tutakavyoonyesha baadaye, mtindo wa kumtumia msaidizi wa mpelelezi kama msimulizi ni mbinu iliyoendelezwa mno na watunzi wa Ulaya na wale wa Marekani.

Kando na hadithi fupi ya *Murders in the Rue Morgue* (1841), Poe alimtumia mhusika Auguste Dupin katika hadithi fupi nyinginezo mbili; *Mystery of Marie Roget*, (1841) na *The Purloined Letter* (1844) na tangu hapo athari zake zimeendelea kujitokeza katika kazi za waliomfuata na kusambaa nje ya bara la Ulaya hadi Marekani. Bajaj (2015:5) anasema kwamba kutokana na uandishi wa Allan Poe, sheria za uandishi wa utanzu huu zifuatazo zinaweza kudondolewa: (i) Mpelelezi mwerevu lakini asiye na utaalam. (ii) Mpelelezi msaidizi lakini asiye na maarifa ikilinganishwa na mpelelezi mkuu. (iii) Mtuhumiwa wa uongo (asiye). (iv) Uhalifu kufanyika katika chumba kilichofungwa madirisha na milango. (v) Suluhisho la kushtukiza hutolewa. (vi) Mpelelezi hutumia mbinu za uwazaji zitumiazo mantiki kwa upana. (vii) Kugunduliwa kwa mhalifu asiyetarajiwa.(viii) Uchunguzi wa kisaikolojia.

Mwongozo huu wa kuandika riwaya za kiupelelezi ulioletwa na Allan Poe, unajitokeza vilevile katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Riwaya za Mohammed Said Abdulla kwa mfano, zimezingatia sheria hizi katika kumbuni mpelelezi Bwana Msa. Huyu ni mhusika anayetumia urazini na mantiki katika uchunguzi wake huku msaidizi wake, Najum akidhihirika kama asiye na maarifa mengi.

Tangu sheria hizi ziibuke kutokana na kazi za Allan Poe, waandishi wa Ulaya na wa Marekani wameendelea kutumia baadhi ya sheria hizo katika riwaya zao.Waandishi maarufu wa riwaya ya kiupelelezi kutoka Marekani ni kama vile Dashiell Hammet (1894-1961), Mickey Spillane (1918-2006), Patricia Highsmith (1921-1995), Rox Stout (1886-1975), Raymond Chandler (1888-1959), Robert Rodlum, John Grisham, Frederic Dannay (1905-82), Manftred Bennington Lee (1905-71) na wengine. Umaarufu wao unajitokeza kutokana na namna walivyotunga hadithi ambazo zilizingatia uajabu zaidi ya vipengele vingine muhimu vya hadithi kama vile uhusika au maudhui. Hata hivyo mwandishi aliyeweka msingi muhimu katika uandishi wa riwaya za kiupelelezi na kuacha athari kubwa ni Huntington Wright (1888-1939), ambaye pia alibuni sheria ishirini za kuandika riwaya ya kiupelelezi. Wright aliandika kwa jina la kilakabu la S. S. Van Dine na kumbuni mpelelezi kwa jina maarufu, Philo Vance. Mpelelezi huyu alisawiriwa akiwa na maarifa mengi ajabu kwani alikuwa na ujuzi katika takribani kila utanzu wa kielimu kama vile sayansi, sheria na sanaa. Wright alichapisha sheria ishirini za uandishi wa hadithi za kiupelelezi katika jarida lililoitwa *The American Magazine* katika mwaka wa 1928. Baadhi ya kanuni hizo zilimlenga msomaji, mpelelezi na mhalifu. Sheria hizo ni kama zifuatazo:

(i) Ni lazima msomaji apewe uwezo sawa na mpelelezi katika kufumbua mhalifu.

(ii) Ujanja na udanganyifu usitumiwe dhidi ya msomaji. Mbinu za ujanja na udanganyifu zitumiwe tu baina ya mhalifu na mpelelezi.

(iii) Kusiwe na matamanio ya kimapenzi kutoka kwa mpelelezi hadi kwa mhalifu

(iv) Mpelelezi au msaidizi wake hapaswi kugunduliwa kuwa ndiye mhalifu kufikia mwishoni mwa hadithi

(v) Mtuhumiwa agunduliwe kwa kutumia njia za urazini na mantiki tu wala asigunduliwe kiajaliajali, kisadfa au kukiri jambo bila sababu.

(vi) Hadithi yoyote ya kiupelelezi lazima iwe na mhusika mshukiwa.

(vii) Tatizo la uhalifu ni sharti lisuluhishwe kwa njia za kiasilia

(viii) Ni lazima mpelelezi awe mmoja.

(ix) Mshukiwa ni lazima awe ametajwa na kuhusika pakubwa katika hadithi.

(x) Mfanyikazi wa nyumbani, ofisi au mahali pa uhalifu asionyeshwe hadithini kama mhalifu (muuaji)

(xi) Makundi ya kisiri yasipewe nafasi yoyote katika riwaya ya kiupelelezi, kwa mfano dini za kisiri kama vile dhehebu la'Free Masons'.

(xii) Mbinu zilizotumika katika mauaji na zile za uchunguzi wa mauaji hayo sharti ziwe razini na zielezeke kisayansi.

(xiii) Riwaya ya kiupelelezi isiwe na vifungu virefu vya kimaelezo. Kwa hivyo, mambo yaliyo nje ya hadithi yasiingizwe katika maelezo na mwandishi asimhakiki mhusika wake.

(xiv) Mhalifu mwenye tajriba nyingi au mtaalam asitumike wala kupewa wadhifa wa kuwa mshukiwa

(xv) Uhalifu hasa mauaji, haupaswi kugunduliwa kuwa ulifanyika kiajali. Huku ni kumsaliti msomaji.

(xvi) Vichocheo vya uhalifu wowote ni sharti viwe vya kibinafsi.

(xvii) Mwandishi wa riwaya ya kiupelelezi yeyote anayejiheshimu asitumie mbinu za kumlazimisha mshukiwa kukiri kuhusika katika uhalifu.

(xviii) Wahusika mapacha au wenye hulka zinazofanana wasitumiwe katika hadithi ( ili kuepuka kumkanganya msomaji).

(xix) Mwandishi asitumie maandishi yanayoeleweka tu na mpelelezi pekee wala asitumie ishara au misimbo inayoeleweka na mpelelezi tu ( ilichukuliwa kuwa hadithi hizi ni kama mchezo wa karata baina ya msomaji na mpelelezi. Kwa sababu hii, ilihitajika msomaji asishtukizwe kupitia kwa mpelelezi kuzuka na mbinu fiche).

(xx) Mpelelezi asifanye uchunguzi wake kwa kuyalinganisha mabaki ya sigara (yakipatikana katika eneo la uhalifu) na mvutaji wa aina hiyo ya sigara.

Kama tunavyoona, sheria hizi zilikuwa nyingi kusudi likiwa ni kujaribu kumdhibiti sana mtunzi ili kuhakikisha kuwa msomaji amepata haki ya kuburudika na kurithisha hamu yake ya usomaji. Hata hivyo ziliishia kumdhibiti mtunzi mno hivi kwamba baadhi ya mambo anayoonya yasitumike yameendelea kutumika bila kuharibu ubora wa utanzu. Kwa mfano, sheria ya mwisho inayoonya

dhidi ya kuchanganua mabaki ya sigara, imetumiwa na Mohammed Said Abdulla katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* ambapo Msa anafananisha mabaki ya sigara aina ya *Cent* na mtuhumiwa aliyekuwa na mazoea ya kuvuta aina hiyo ya sigara, Ali Makame. Bajaj (2015: 6-7) anataja kwamba uzingatiaji wa sheria hizi zote ulikuwa vigumu na kwa sababu hiyo, kila mwandishi aliteua zilizomfaa na kuacha nyinginezo.

Ukuaji na maendeleo makubwa ya riwaya ya kiupelelezi huko Ulaya na Marekani ulishuhudiwa katika kipindi cha baina ya mwisho wa vita vya kwanza vya ulimwengu na mwanzo mwa vita vya pili. Hiki ndicho kipindi ambacho riwaya nyingi zilichimbuka katika mabara haya. Utafiti huu unachukulia kwamba kipindi hiki ndicho cha urasimi katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi.

### 2.4 Riwaya ya kiupelelezi katika kipindi cha Urasimi (1920-1930)

Kama tulivyodokeza hapo juu, hiki ni kipindi cha ukuaji mkubwa wa utanzu wa riwaya ya kiupelelezi. Kando na uchapishaji wa nakala nyingi za aina hii ya riwaya huko Ulaya na Marekani, kipindi hiki pia kilishuhudia mabadiliko makubwa katika mitindo mbalimbali ya riwaya ya kiupelelezi. Huko Ulaya kipindi hiki kilijulikana kama *Golden Age Of Detective Fiction* ilhali kule Marekani, kipindi hiki kilishuhudia mtindo wa utunzi wa riwaya za kiupelelezi na zikaitwa, *Hard Boiled Fiction*.[1] Mhakiki Howard (1942:23) anasema kwamba wakati wa urasimi, vijitanzu vingi vilizuka kutokana na utanzu wa riwaya ya kiupelelezi. Baadhi ya vijitanzu hivyo ni kama vile riwaya ya kijazira, riwaya ya kiuhalifu na riwaya iliyozuka Marekani ya kijasusi. Kulingana na Scaggs (2005:26) fasihi ya kiupelelezi ilifanikiwa kupata sifa ya utanzu katika kipindi hiki kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza wakati wa urasimi. Mabadiliko hayo ni kama yafuatayo.

(i) Kwanza, urefu wa hadithi ya kiupelelezi ulibadilika ambapo hadithi fupi zilizoshamiri kwa kipindi cha karne moja zilibanduliwa na nafasi yake kutwaliwa na riwaya mpya ya kiupelelezi iliyojitokeza. Uibukaji wa riwaya ya kiupelelezi kutokana na hadithi fupi ya kiupelelezi ulitokana pia na mabadiliko ya kimsuko wa hadithi. Badilko lingine lililochangia ukuaji huu ni ongezeko la hamu ya usuluhishaji wa migogoro kupitia uteguaji wa vitendawili. Ukuaji huu wa riwaya ya

[1]Hard Boiled fiction ni kijitanzu cha riwaya ya kiupelelezi kilichozuka Marekani miaka ya 1930 zilizohusu mandhari ya mijini na kusheheni ghasia

kiupelelezi uliohusu mabadiliko ya muundo wa riwaya pia, ulisababisha ujenzi murua wa wahusika na mandhari.

(ii) Badiliko la pili lililochangia ukuaji wa riwaya ya aina hii katika kipindi hiki, lilihusu utokezaji wa jinsia ya kike katika uandishi wa riwaya ya kiupelelezi. Evans (2019: 5-6) anasema kwamba kipindi cha kwanza cha karne ya ishirini kilishuhudia si tu uzukaji wa waandishi wa kike bali pia mahusiko ya wahusika wapelelezi wa kike. Hali hii ilijitokeza si tu katika kazi zilizoandikwa na wanawake bali pia zile zilizoandkwa na wanaume. Hata hivyo, kulingana na mhakiki huyu, kuna baadhi ya mambo yaliyokwama katika ukale na kuendelea kushuhudiwa katika riwaya ya kiupelelezi hadi miaka ya 1970. Kwa mfano, riwaya nyingi zimeendelea kutolewa na watu weupe zaidi ikilinganishwa na idadi ya waandishi weusi. Mbinu za usambazaji wa vitabu zilipoimarishwa kupitia mbinu kadhaa kama vile ujenzi wa maktaba za umma, kulipelekea watu wengi kuwa na uwezo wa kusoma riwaya hizo. Vile vile, mabadiliko ya kimuundo hasa mageuzi ya kimsuko tuliyotaja hapo juu yalisaidia kuwavutia watu wengi kuipenda na kuanza kuisoma riwaya ya kiupelelezi, huku ongezeko hili la wasomaji likihusu pia wanawake wengi.

Mwanamke mwandishi aliyeibuka katika kipindi hiki ni Agatha Christie. Baadhi ya riwaya zake ni, *After the Funeral* (2001), *ABC Murders* (1993), *Appointment with Death* (1993) na nyinginezo nyingi. Mwanamke mtunzi mwingine aliyezuka katika kipindi huki ni Dorothy Sayers, Ngaio Marsh na Margery Allingham.

(iii) Badiliko lingine la kipindi hiki lilihusu mageuzi ya hulka na tabia ya mpelelezi. Mpelelezi aliyebuniwa na Conan Doyle na ambaye sifa na matendo yake yaliendelezwa na waandishi waliofuata, sasa alianza kuangaliwa upya. Kabla ya kipindi hiki, mhusika mpelelezi alikuwa bapa na aliyekosa baadhi ya sifa za binadamu wa kawaida. Kwa mfano, mpelelezi aliyebuniwa na Conan Doyle, Sherlock Holmes, alikuwa na kipawa kisicho cha kawaida cha uchanganuzi wa masuala kimantiki. Zaidi ya haya, hakuhusika katika mambo ya kifamilia kama vile ndoa, mapenzi wala kuwa na watoto. Pia alikuwa mpelelezi wa kujitolea kwa kuwa hatuoni akidai malipo kwa baadhi ya kazi za uchunguzi afanyazo. Ubapa wa sifa yake unajitokeza zaidi anaposawiriwa kama binadamu asiye na kosa lolote wala asiyeweza kufanya makosa katika maamuzi yake. Kama tutakavyoona baadaye kuhusu uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, mhusika Msa, katika riwaya za Abdulla ni mhusika bapa. Kinyume na hali ya awali, baadhi ya wapelelezi

walioanza kujitokeza wakati wa urasimi walikuwa na sifa za binadamu wa kawaida kama vile kuwa na familia.

(iv) Sifa nyingine iliyodumishwa wakati wa urasimi ni ile ya matumizi ya mhusika msaidizi wa mpelelezi ambaye aghalabu ndiye msimulizi wa hadithi. Katika nadharia ya naratolojia, Rimmo-Kenan (2002:36) anasema kuwa kuwepo kwa msimulizi wa aina hii ni muhimu katika riwaya hizi kwa sababu yeye husaidia kuzidisha uajabu wa visa pamoja na uajabu wa mpelelezi. Hii ni kupitia namna msimulizi huyu anavyorefusha masafa ya kisimulizi baina ya msomaji na mpelelezi. Kuwepo kwake pia kunawafanya wasomaji wasiubaini msimamo wa mpelelezi mapema, hivyo kuendeleza taharuki ambayo ni kipengele muhimu katika muundo wa utanzu huu. Kwa sababu hiyo, msimamo wa mpelelezi unapaswa kutojulikana mapema huku udhaifu wa mpelelezi msaidizi ukiendelea kudumishwa hadi mwisho. Mbinu hii pia inasaidia kuchimuza ubora wa mpelelezi mkuu kiulinganuzi. Waandishi wengi walifuatia mtindo wa kumtumia mpelelezi na msaidizi wake kwa kuzingatia kielelezo cha Allan Poe na Conan Doyle. Mtindo huu wa uhusika unaonyeshwa kwenye jedwali lifuatalo:

Kielelezo 2.1 Mifano ya wahusika wa kiupelelezi na wasaidizi wao.

| **Mwandishi** | **Mpelelezi mkuu** | **Mpelelezi msaidizi** |
|---|---|---|
| Allan Poe | Auguste Dupin | Yupo lakini bila jina |
| Arthur Conan Doyle | Sherlock Holmes | Dkt John Watson |
| Agatha Christie | Hercule Poirot | Captain Hastings |
| Rex Stout | Nero Wolfe | Archie Godwin |
| Raymond Chandler | Phillip Marlowe | Hayupo |
| G.K Chersterton | Father Brown | Hayupo |
| Dorothy Sayers | Lord Peter Whimsey | Hayupo |
| Ngaio Marsh | Roderick Alleyn | Hayupo |
| Margery Allingham | Albert Campion | Hayupo |
| Williard Huntington | Philo Mance | Hayupo |
| Satyajit Ray | Feluda | Topsha |

(v) Sifa nyingine inayohusishwa na kipindi hiki ni ujitokezaji wa mtindo mpya wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiulaya, maarufu kama, '*Whodunit'*. Kulingana na Scaggs (2015:70) msamiati huu ulibuniwa na mwanahabari Sime Silverman (1934) kama ufupisho wa *who did it.* Sifa yake kuu ilihusu mwandishi kutoa vidokezo vichache mwanzoni mwa riwaya ili vimsaidie msomaji katika kufumbua fumbo la ni nani alitekeleza mauaji hayo. Katika kijitanzu hiki, mageuzi yalifanyika kuhusu msimulizi ambapo mhusika mpelelezi msaidizi hakutumika tena kwani nafasi hiyo ilianza kuchukuliwa na mpelelezi mwenyewe. Riwaya zilizozingatia mtindo huu zilihusu watuhumiwa kadhaa, mauaji yaliyofanyika kwa njia za kiajabuajabu pamoja na mandhari ya miji.

(vi) Kuhusu lugha na mtindo, riwaya za kipindi hiki zilitumia usimulizi wa nafsi ya kwanza (hasa kazi za Kimarekani), matumizi ya lugha ya mitaani na mara nyingi lugha yenye ukali unaotokana na matusi na kejeli. Njeo ya kisimulizi iliyopendelewa ni ile ya wakati uliopo. Usimulizi wa aina hii ulimpa msomaji nafasi ya kufuata mpelelezi unyo kwa unyo tangu mwanzo wa riwaya hadi mwisho.

(vii) Maendeleo mengine yaliyozuka katika kipindi hiki yalihusu uzukaji wa mpelelezi wa kibinafsi ambaye mara nyingi alifanya kazi kwa kukodiwa. Mandhari ya uhusika wake ni katika miji mikuu na aghalabu alisawiriwa akifanya kazi pamoja na msaidizi wake. Hata hivyo, mpelelezi wa aina hii hakukodishwa kuchunguza uhalifu uliohusu umma kwani hii ilikuwani milki ya polisi bali alichunguza hali mbali mbali zilizowahusu watu binafsi au mashirika ya aina ainati.

Mpelelezi wa aina hii alisaidia katika kufidia udhaifu wa polisi kwani ufaafu wake ulitokana na kushindwa kwa polisi ama usiri wa kesi unaohitajika. Kwa sababu hii, wapelelezi wa kibinafsi walichunguza visa kwa kupewa jukumu hilo na mtu binafsi, kundi maalum au shirika na aghalabu matokeo ya uchunguzi wao hayakutolewa kwa umma. Mfano,wa riwaya iliyomhusu mpelelezi wa kibinafsi huko Marekani ni *Red Harvest* ya Dashiell Hammett (1929). Mpelelezi wa kibinafsi alisafiri miji kadhaa kuchunguza visa na mara nyingine akiwa na wasaidizi kadhaa. Akielezea uzukaji wa aina hii mpya ya mpelelezi wa kibinafsi, Bynion (2001) anatueleza:

> Mapema katika miaka ya 1920, aina mpya ya riwaya ya kiupelelezi ilizuka Marekani. Riwaya hii mpya iliitwa kwa jina maarufu, '*The Private Eye*'. Riwaya hii ni tokeo la uhalisi wa Marekani. Mara nyingine mpelelezi katika riwaya hii ni mfanyikazi wa taasisi za uchunguzi au mtu binafsi tu anayewatetea wanyonge na waliokandamizwa (2001:34).

(viii) Badiliko lingine lilikuwa ni uibukaji wa kijitanzu cha riwaya ya kihalifu kama utanzu unaojibainisha na riwaya ya kiupelelezi. Ingawa riwaya hii pia ilihusu upelelezi kwa kiasi fulani, upelelezi huo haukupewa kipaumbele. Msuko wake ulihusu uhalifu kama vile wizi wa kiwango kikubwa, ufichuzi wa siri za mashirika ya kimataifa au mataifa ya kigeni. Kama jina la utanzu linavyoashiria, riwaya hizi zilikusudia kuburudisha wasomaji kupitia matendo ya kijasiri ya mhalifu na kwa sababu hiyo, riwaya hizo zilitumia mbinu kadhaa ili kuboresha mvuto huo. Mbinu hizo ni kama vile taharuki inayokuzwa na matarajio makuu kutoka kwa wasomaji, mshtukizo, uibuaji wa hisia za hofu na furaha kadri msuko unavyozidi kukunjuka kufikia kwenye kilele.

(ix) Umaarufu wa riwaya ya kiupelelezi kufuatia ongezeko la waandishi na wasomaji wa aina hiyo ya riwaya katika kipindi cha urasimi ulisababisha kuundwa kwa chama cha waandishi kiitwacho, *The Crime Club* mwaka wa 1930, huku G.K Chersterton (mtunzi aliyembuni mpelelezi Father Brown) akichaguliwa kuwa rais wa kwanza wa chama.

Kufikia mwaka wa 1932 chama kilikuwa na wanachama 25000. Ongezeko la idadi hii ya watunzi kufikia mwaka huu linatuthibitishia kwamba ukuaji wa riwaya ya kiupelelezi huko Marekani na Ulaya ulikuwa umefika katika upeo wake. Chama hiki kiliweza kutunga baadhi ya sheria zilizowadhibiti watunzi kwa kuelekeza vipengele vya lazima vilivyopaswa kutumiwa na kila mtunzi. Kwa mfano, iliafikiwa kuwa ni sharti mwandishi atoe suluhisho kuhusu uhalifu unaosimuliwa katika riwaya yake kufikia mwishoni bila kumwacha msomaji na maswali.

(x) Maendeleo makubwa ya mwishoni mwa kipindi hiki yalitokana na juhudi za uchapishaji wa kitabu kilichotolewa na Ronald Knox (1888-1957) ambacho kilikuwa ni mkusanyiko wa hadithi nyingi kiitwacho, *The Best Detective Stories of 1928.* Katika kitabu hiki, kando na kubuni mpelelezi kwa jina, 'Miles Brendon', Knox alitoa maelezo kwenye dibaji akionyesha kanuni ambazo kila mwandishi wa riwaya ya kiupelelezi alistahili kuzingatia. Knox aliziita sheria hizo *Andiko la Sheria kumi' (The Detective Decalogue),* akizingatia mfano wa sheria kumi ambazo Mungu alimpa nabii Musa wa Bibiliani. Sheria hizo ni kama zifuatazo:

(i) Mhalifu sharti awe ametajwa mwanzoni mwa hadithi hiyo na asiwe mtu ambaye msomaji amefuatia fikira zake.

(ii) Katika mauaji yanayofanyika ndani ya nyumba, kusiwe na zaidi ya kiingilio kimoja au vyumba vya siri na ikiwa vipo visiwe zaidi ya kimoja.

(iii) Kusitumiwe kemikali ngeni kama vile sumu ambayo haijawahi kuonekana au kutumika kwingineko. Vile vile kifaa kigeni kisitumike kutendea uhalifu au kuchunguzia ili kuepuka maelezo maarefu ya kisayansi kuhusu namna kemikali ama vifaa hivyo hufanya kazi. Kuepuka mambo haya pia kunamsaidia msomaji kutumia urazini wake katika kupata suluhu la mgogoro.

(iv) Mpelelezi asimfiche msomaji kidokezo chochote anachokitumia kufikia baadhi ya maamuzi yake. Kutenda hivyo ni kumdanganya msomaji.

(v) Msaidizi wa mpelelezi ni sharti ayaseme mawazo yake. Pia asiwe na maarifa kufikia kiwango cha mpelelezi au kuwa na maarifa mengi kuzidi yale ya mpelelezi mkuu.

(vi) Mpelelezi asigundue lolote kiajali au kisadfa.

(vii) Mpelelezi kamwe asigunduliwe kuwa ndiye mhalifu kufikia mwishoni mwa hadithi.

(viii) Ndugu wawili mapacha wasitumike kama wahusika wala hali mbili zinazofanana kutumika katika hadithi ya kupelelezi ili kuepuka kumtatanisha msomaji.

(ix) Matokeo ya upelelezi yasipatikane kuwa ya kiutani tu au vitendo kufanyika ili kuleta ucheshi pekee.

(x) Nguvu za kiungu au zisizo za kiasilia hazifai kutumika katika usuluhishaji wa mgogoro wa kiuhalifu unaotawala msuko wa riwaya ya kiupelelezi.

Kufikia mwishoni mwa miaka ya 1930 maendeleo makubwa yaliyokuwa yakishuhudiwa katika ukuaji wa riwaya ya kiupelelezi yalianza kufifia. Sababu kuu kama anavyotuambia Kimura (1992) ni kwamba riwaya hizi zilikuwa kama mchezo wa sarantanji na kwa sababu hiyo, zilimaliza mbinu zake za kuwavutia wasomaji. Wasomaji sugu wa riwaya hizi walikuwa wamezoea mbinu zitumiwazo na wapelelezi na watunzi hivyo wakakinaishwa na usomaji wake. Badiliko hili nalo likalazimu uibukaji wa tanzu mpya zilizotumia mbinu mpya za kiutunzi. Kwa hivyo kufikia mwishoni mwa kipindi cha urasimi vijipera vingine kama vile riwaya ya kijasira, riwaya ya kijasusi na riwaya ya kihalifu vilianza kuvuma kwani waandishi wengi pia walianza kufuata mtindo huu. Katika riwaya za kihalifu, kwa mfano, mhusika mkuu hakuwa mpelelezi kama ilivyokuwa hapo awali, bali mhusika mkuu alikuwa ni mhalifu au mhasiriwa wa uhalifu huo. Aidha kwa kuwa hiki kilikuwa kipindi cha kumazilika kwa vita vya kwanza na matayarisho ya vita vya upili vya ulimwengu, mpelelezi alijiona akiwa katika njia panda; awali alikuwa

akichunguza na kumkomesha muuaji lakini wakati huu wa vita vikuu vya kwanza, mpelelezi alishuhudia mauaji ya halaiki yalitekelezwa na mataifa mbalimbali dhidi ya raia wa mataifa mengine bila yeye kufanya lolote.

Uwezo wake ukafifia kisaikolojia nao waandishi wakakosa kielelezo cha kuiga. Wakati wa vita vya pili vya ulimwengu na baada ya vita hivyo, kukawa na haja ya mataifa kuimarisha usalama na upelelezi nao ulilazimika kuchukua sura nyingine ambapo ujasusi ulijitokeza na kuendeshwa baina ya mataifa. Hali hizi zikazua kijitanzu cha riwaya ya kijasusi na upelelezi wa kimataifa ambapo uhalifu nao ulichukua sura ya kimataifa pia. Cawelti (1987) akifafanua mabadillio haya anasema kuwa uhalifu pia ulihusu matendo ya kisiri, uenezaji wa propaganda na mahusiano mabaya ya kimataifa yaliyotokana na vita baridi vilivyozuka baada ya vita vya ulimwengu vya pili. Tumeona kwamba katika kipindi hiki huko Marekani na Ulaya ukuaji mkubwa wa riwaya ya kiupelelezi ulifikiwa katika kipindi cha baina ya 1920-1930 huku mabadiliko anuwai yakijitokeza katika muundo wake. Itakuwa vyema pia kufafanua baadhi ya sababu zilizochangia maendeleo haya.

## 2.5 Sababu za Maendeleo Makuu ya riwaya ya Kiupelelezi Wakati wa Urasimi

Maendeleo makuu ya utanzu huu tuliyoyaeleza hapo juu wakati wa urasimu yaliwekewa msingi wake na mapinduzi ya kiviwanda yaliyoanza katika Ulaya na Marekani katika karne ya kumi na nane. Uvumbuaji wa mashine ulisababisha watu wengi kuachishwa kazi kwani nafasi zao sasa zilitwaliwa na mashine zilizofanya kazi kwa haraka. Hawa walihitaji kitulizo ambacho kingepatina katika usomaji wa hadithi za aina mbalimbali hasa zile za kiupelelezi. Hadithi hizi aghalabu zilijitokeza katika magazeti na majarida. Mapinduzi haya pia yalichochea matukio mapya ya uhamiaji na ruwaza za ukaazi ambapo watu walitoka mashambani na kwenda kuishi mijini. Hali hii ilisababisha uibukaji wa miji iliyokosa mipangilio bora kama anavyosema Kimura (1992:73). Mhakiki huyu anasema kwamba mapinduzi haya yalisababisha ukuaji wa ubepari na ongezeko kubwa la watu kando na ukosefu wa kazi. Ukosefu wa kazi nao ukazua wizi, ulofa, ukahaba na aina nyinginezo za uozo wa kijamii. Ongezeko la watu hasa mijini pamoja na uhaba wa kazi ndiyo mambo yaliyozusha uhalifu katika karne ya kumi na tisa. Uhalifu nao ulipoongezeka, watunzi wa riwaya wakapata kariha na msukumo mpya wa kuandika kuhusu uhalisia huu hivyo kupelelekea kuzaliwa kwa riwaya ya kiupelelezi na ile ya kihalifu. Hata hivyo, uhaba wa kazi kwa upande mwingine, uliwaacha watu wengi na muda mwingi ambao waliutumia katika usomajiwa riwaya pendwa zikiwemo riwaya za kiupelelezi.

Pili, mapinduzi ya viwanda yalipelekea uvumbuaji wa mashine nyingi zikiwemo zile za uchapishaji. Uimarishaji wa teknolojia uliotokana na mapinduzi haya uliibusha mbinu mpya za utoaji na usambazaji wa vitabu. Kwa mfano, kasi ya utoaji wa vitabu iliongezeka huku idadi na aina za riwaya pendwa ikiongezeka na kuwafikia watu wengi. Kwa upande wa usafiri, teknolojia mpya ilisababisha kuwepo kwa mbinu za usafiri wa haraka. Nayo maendeleo ya usafiri yakahakikisha kuwa vitabu vimeifikia kila sehemu ya ulimwengu. Matumizi ya usafiri wa ndege na meli yalisambaza riwaya hizi kutoka Ulaya hadi maeneo ya Asia na Afrika. Akisisitiza maoni haya. Hartman (2008) anasema kwamba:

> Upanuzi wa viwanda uliathiri utoaji wa mashine za uchapishaji ambazo zilitumia muda mfupi wa kutoa vitabu na hali hii ikafikisha vitabu kwa watu wa matabaka ya kati na chini. Uwezo wa kununua vitabu pia uliongezeka. Magazeti pia yalichapisha msururu wa vijisehemu kadhaa vya riwaya hizo ili kufikia watu wengi.(uk.4)

Usambazaji wa fasihi hizo zilizokuwa zimeandikwa kwa lugha za Kiulaya katika maeneo ya kigeni kuliongeza hamu ya utafsiri na ufasiri wa kazi hizo kwa lugha za kigeni. Hii ikawa ni njia bora ya kuzifikisha kazi hizo maeneo mengi. Romero (2015:55) anafafanua kwamba utafsiri wa riwaya za Kiingereza na zile za Kifaransa hadi Kispanyola ndiko kulikosaidia riwaya ya kiupelelezi kuifika Marekani Kusini hasa nchini Mexico na Argentina. Tatu, uimarikaji wa ubepari huko Ulaya. Kabla ya kuzuka kwa tabaka la mabepari, mfumo wa kiutawala ulikuwa wa kifalme na kikabaila. Fasihi nayo ililenga masilahi na maisha ya tabaka hili na hasa familia za nasaba bora. Tabaka la ubepari lilipozuka katika karne ya kumi na nane lilihitaji fasihi yenye uhalisia wa maisha yao. Hitaji hili lilizalisha fasihi pendwa iliyowalenga watu wa kawaida.

Tatu, ubepari na sifa yake ya ubidhaaishaji[2] ulisababisha ujitokezaji wa waandishi waliochapisha riwaya pendwa kwa ajili ya soko ili kujikuamua kutokana na matatizo ya kiuchumi (Madumulla, 1988). Kwa sababu hii, kundi jipya la waandishi lisilotegemea ufadhili wowote kutoka kwa makampuni ya uchapishaji lilijitokeza na kupelekea usambavu wa riwaya hizo kwingi. Ili kufanikisha mauzo mazuri, watunzi wengine hata walianza kuvitembeza vitabu vyao wakiviuza kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine. Tatu, teknolojia ya habari na mawasiliano ilipokomaa

[2]Ubidhaaishaji katika muktadha huu hurejelea hali ambapo waandishi walichapisha vitabu vingi kwa haraka wakilenga kujitajirisha kwa kuviuza madukani kama bidhaa nyinginezo

na kuvumbua filamu, ilisaidia uenezaji wa riwaya za kiupelelezi kwani baadhi ya riwaya hizo zilitumiwa kama msingi wa kuundia filamu.

Nne, ongezeko la idadi ya watu lilisababisha kuwepo kwa kiasi kikubwa cha watu waliosoma na ambao walipanua soko lililokuwepo la riwaya ya kiupelelezi. Hii ni pamoja na juhudi za kiserikali za kusambaza elimu kwa wananchi wengi si tu katika mabara ya Ulaya na Marekani bali pia kwingineko ulimwenguni.Tano, ukoloni ulikuwa nyenzo bora ya kueneza aina hii ya riwaya. Wakoloni kutoka Ulaya walihamisha vipengele vingi vya utamaduni wao hadi Marekani, Afrika, na Asia, ikiwemo fasihi. Mifumo ya kielimu iliyobuniwa na mataifa ya kikoloni ilitumiwa kama njia ya usambazaji wa utamaduni huo kwani sera za kielimu zililenga kuyadhibiti mataifa yaliyotawaliwa kwa njia nyingi kama vile elimu na uchumi. Wakoloni walitafsiri baadhi ya riwaya zilizokuwa zimeandikwa kwa lugha zao hadi lugha za mataifa mengine ya Ulaya, Marekani Kusini na Kaskazini ili kufanikisha malengo ya kielimu. Romero (keshatajwa) anaeleza kuwa kupitia tafsiri hizi, riwaya ya kiupelelezi iliweza kufika Mexico na maeneo mengine ya Marekani Kusini na Kati.Wakoloni walianzisha mashirika ya kiuchapishaji katika mataifa hayo mapya ili kusaidia utoaji wa nakala nyingi za vitabu. Kwa mfano, Macmillan, Longman na Oxford ni baadhi ya mashirika yaliyoanzisha matawi yake katika sehemu nyingi za Kiafrika. Kwa hivyo, kupitia harakati za kikoloni, riwaya za aina mbalimbali hasa riwaya pendwa zilitafsiriwa kwa lugha mbalimbali ili kufanikisha mipango ya kielimu.

Mwisho, kufikia mwishoni mwa karne ya kumi na tisa usomaji wa ushairi ulikuwa umeanza kupoteza umaarufu wake na kwa sababu hii, watunzi wengi walielekeza nguvu nyingi katika uandishi wa kazi za kinathari kama vile riwaya na hadithi fupi.  Vile vile, wasomaji nao hawakusazwa nyuma kwani nao walipendelea kazi za kinathari hususan riwaya kuliko ushairi.Wakati huu, kazi zilizouzwa zaidi huko Uingereza na Marekani ni zile za kinathari. Mageuzi haya yalipokelewa vyema na wasomaji waliokuwa wakipata ugumu katika usomaji wa mashairi na kuongeza kasi ya usambaaji wa riwaya za aina zote hasa riwaya za kiupelelezi.

### 2.6 Riwaya ya Kiupelelezi katika Nchi za Kimashariki

Kwa kuwa katika sehemu ya hapo juu tumeona namna riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi ilivyoendelezwa, katika sehemu hii, tunachunguza kwa kifupi ukuaji wake katika mataifa ya Kimashariki. Kusudi ni kutathmini ikiwa ilichimbuka kivyake au ilitokana na athari za Kimagharibi hasa Ulaya. Kupitia ukoloni, utamaduni wa Ulaya uliweza kusambazwa hadi maeneo

ya Mashariki kama vile Uchina na Japani. Sera ya Uingereza ya kuleta usasa katika makoloni yake ilipelekea uanzishaji wa taasisi za kudumisha usalama kama vile polisi, mahakama na jela. Romero (2015:55) anasema kwamba usambazaji wa usasa huu ndio ulioweka misingi ya riwaya ya kiupelelezi katika maeneo ya Kimashariki kama vile India na koloni nyinginezo za Uingereza huko Asia kama vile Malysia. Haya yalifanyika kupitia utafsri wa riwaya za Uingereza kama vile kazi za Conan Doyle na zile za Mfaransa Leblanc. Mhakiki huyu anasema kwamba katika Ujapani, uongozi wa Meui ulileta taasisi nyingi za kisasa ikiwemo taasisi ya polisi iliyoanzishwa mwaka 1871. Kupitia juhudi za taasisi ya polisi za kuanzisha kitengo cha upelelezi, walikumbatia riwaya ya kiupelelezi ya Uingereza hasa kazi za Conan Doyle. Kufikia mwaka 1880 mwanahabari Ruiko Kuroiwa (1862-1920) alifasiri hadithi za mwanzo mwanzo za Mfaransa Eugene Gaboriau na za Doyle na kufikia mwaka wa 1889, alichapisha riwaya yake ya kwanza ya Kijapani iitwayo *Cruelty* (1889). Wakati riwaya ya kiupelelezi ilipofika Ujapani ilisababisha kuibuka kwa utanzu huo huko kwa jina maarufu, *Tentei Shosetsu.* Uibukaji wa utanzu huu unahusishwa na mwandishi Hirai Taro aliyeandika kwa jina la kilakabu la Rampo Edogawa (1894-1965). Taro ndiye hutambulikana kama baba wa utanzu wa riwaya ya kiupelelezi huko Ujapani kwa kuwa aliitanguliza riwaya hiyo huko. Katika kazi zake alimtumia mpelelezi Kogoro Akechi. Kazi zake ni kama vile *The Black Lizard*, *Beast* na *Best in the Shadow*. Watunzi wengine wa kazi zakiupelelezi wa Japani ni kama vile Miyuki Miyabe, Kanae Minato, Akimitsu Takaji, Seishi Yokomizo, Tohru Miyoshi, Eitaro Ishizawa, Seicho Matsumoto na wengineo.

Riwaya ya kiupelelezi nchini India pia inahusishwa na msambao wa riwaya ya aina hii kutoka huko Ulaya hadi India kupitia ukoloni. Utawala wa Uingereza ulikuwa na makao makuu jijini Calcutta, Bengali hadi 1911. Kufikia mwaka wa 1947 lugha ya Kibengali ilikuwa imejirutubisha kutokana na athari ya fasihi ya Kingereza.. Mwandishi aliyetunga riwaya za kiupelelezi ni Chattopadhyay ambaye katika riwaya zake kama vile *Penumbra* na *Here Falls the Shadow* alibuni mpelelezi Jonatdhan Maity na msaidizi ambaye ni mwanahabari Prakash Ray. Mwandishi mwingine aliye na wafuasi wengi ni Nihar Ranjan Gupta aliyembuni mpelelezi Kiriti Roy ambaye hadithi zake zimefanywa kuwa filamu za kisanjari zikitumia lugha ya Kibengali. Hata hivyo, kwa kuwa wananchi wengi wa India walitanguliziwa usomaji wa riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi mapema, kazi za waandishi wa India hazijapendwa na kuwavutia watu wengi kama zile za waandishi wa Uingereza hasa za Conan Doyle.

Katika Uchina, kuna hadithi za kiupelelezi zinazopatikana katika vijitanzu viwili, *Gong'an* na *Wuxia*. Msamiati *Gong'an* unamaanisha aina ya meza inayotumiwa na hakimu. Kwa hivyo, kijitanzu hiki kilihusu hadithi zilizotolewa na mahakimu. Mahakimu waliofahamika zaidi katika maamuzi yenye maarifa mengi katika riwaya hizi za kiupelelezi ni hakimu Dee na Bao Zheng. Hakimu Dee kwa mfano, alijitokeza katika hadithi nyingi za kiupelelezi za Uchina kama vile *Judge Dee at Work*, *The Chinese Maze Murders*, *The emperor's Pearl*, *Murder in Canton*, *The Red Pavillion* na *The Haunted Monastery.*

Katika kijipera cha *Wuxia*, mhusika mpelelezi huwa ni mtetezi wa haki za kibinadamu lakini hutumia nguvu zake za kimwili badala ya nguvu za kiakili katika kuwasaka wahalifu. Yeye pia huwa shujaa wa kivita. Robert (1998) anadokeza kuwa kinyume na hadithi za kiupelelezi za Ulaya na Marekani, hadithi za *Wuxia* na *Gong'an*, zilitanguliza uhalifu na mhalifu mapema badala ya kuachwa kama fumbo. Aghalabu msuko wa hadithi hizi ulihusisha mambo ya kutoka nje ya hadithi ili kuruhusu mazungumzo ya kifalsafa au ukaguaji wa stakabadhi mbalimbali.

### 2.7 Riwaya za kiupelelezi Afrika

Kama tulivyodokeza awali, utamaduni wa Ulaya ulisambazwa katika sehemu nyingi za Ulimwengu kupitia ukoloni. Katika Afrika, wakoloni wa Uingereza na Ufaransa ndio waliotawala mataifa mengi na utawala wao ulidumu baina ya 1880-1960. Hata hivyo katika mataifa yaliyotawaliwa na Ureno, ukoloni huo ulikuwa umeanza mapema na kuchukua muda mwingi zaidi kumalizika. Katika enzi hii, utamaduni wa Kimagharibi ulikita mizizi Afrika na kuwaathiri wenyeji kwa njia kadhaa. Kimura (1992:86) anasema kwamba mifumo ya kikoloni ya lugha, fasihi na elimu ndiyo iliyosaidia kueneza utamaduni huo. Wasomi waliopitia katika shule za kikoloni walisoma fasihi za Kimagharibi na wao walipoanza kuandika wakaendeleza baadhi ya taathira hizo. Kwa hivyo, riwaya pendwa na hususan za kiupelelezi zipatikanazo Afrika zina athari za Ulaya. Katika sehemu ifuatayo, tunachunguza chimbuko la riwaya hizo katika maeneo matatu makuu ya bara la Afrika; yaani Afrika Kusini, Afrika Mashariki na Afrika Magharibi ili kuweka muktadha bora wa uchunguzi wa riwaya ya kiupelelezi ya Kidwahili.

#### 2.7.1 Riwaya ya Kiupelelezi Afrika Magharibi

Riwaya pendwa iliyofahamika zaidi katika Afrika Magharibi ni ile iliyojulikana kama 'Fasihi Pendwa ya Soko la Onitsha'. Onitsha ni mji ulioko karibu na mto Niger, Mashariki mwa Nigeria. Na ndio mji unaouunga Magharibi na Mashariki mwa nchi hiyo kibiashara. Mji huu ulifahamika

kwa biashara za aina aina lakini ile iliyovuma zaidi ni biashara ya uuzaji wa vitabu. Kulingana na utafiti uliofanywa na Obiechina (2008), fasihi hii ya Onitsha ilianza kujitokeza katika miaka ya 1940-1950. Awali soko hili lilihusu vitabu vilivyoletwa na wageni wa kutoka India na Marekani waliofika sokoni hili baadhi yao wakiwa watalii. Askari wa Kiafrika waliokuwa wanatoka kushiriki vita vya ulimwengu vya pili huko Mashariki ya mbali kama vile Burma, ndio walileta kwa wingi nakala za riwaya hizo pamoja na mitindo ya kuziandika. Watunzi waliozisoma riwaya hizo za kigeni waliiga mtindo huo katika uandishi wa kazi zao baadaye. Nakala ya kwanza ilijitokeza mwaka 1947 wakati Cyprian Ekwensi alipoandika *When Love Whispers*, akitumia mitindo ya kazi hizo za kigeni. Vijiriwaya vya Marekani na India vilivyotangulia vilitumia lugha sahili, picha nyingi kwenye jalada hasa za wanawake warembo, na kuwa na kurasa chache.

Baadhi ya sifa nyinginezo za riwaya ya Onitsha ni; matumizi ya lugha isiyo na urasimi mwingi ambayo aghalabu ilihisu matumizi ya pijini na ya kuvutia. Kwa sababu hii hata watu wasiokuwa na elimu ya sekondari waliweza kujisomea na kuelewa kwa urahisi. Pili, kwa kuwa vijiriwaya hivi havikujali sana mpangilio wa kurasa, ruwaza za rangi wala blabu, ziliishia kutolewa na watu wengi hata wasio na elimu ya juu na kuzungumzia mada za kuvutia kama vile mapenzi, urafiki na ulaghai wa kibiashara.Tatu, Kwa kuwa hukukuwa na sheria za kulinda hatimiliki za watunzi, kitabu kilichochapishwa na mtu fulani hapo awali, kiliweza kutolewa baadaye na mtu mwingine na kuuza nakala nyingi bila kuhofia mwenyewe wa asili kulalamika. Sifa hii ilisaidia mno ueneaji wa riwaya pendwa.

Matumizi ya mbinu za kijanja zilijitokeza pia miongoni mwa makampuni ya uchapishaji ambayo yalinunua miswada kutoka kwa watu mbalimbali kwa bei ya chini sana nayo yakachapisha miswada hiyo na kuwa riwaya ambazo ziliuzwa kwa bei ghali. Makampuni pia yaliweza kubadili majina ya watunzi kwenye miswada kwa kuliweka jina la mwandishi maarufu ili kuongeza ununuliwaji wa kazi hizo. Mbinu nyingine ya kijanja ilihusu kuzibadili anwani za vitabu ambapo mtunzi alilazimishwa kukipa kitabu jina linalovutia zaidi kulingana na matakwa ya kampuni ya uchapishaji. Mwisho, riwaya pendwa za Soko la Onitsha zilihusu zaidi maisha ya mijini kuliko yale ya vijijini. Kwa mfano, zilihusu kuwaelekeza wakaazi wa miji kuhusu namna ya kupata fedha kwa haraka, sifa za mchumba mzuri, namna ya kujifunza Kihausa, suala la mahari na mahusiano ya wanaume na wanawake. Newell (2002:44) anafafanua baadhi ya sababu zilizopelekea umaarufu wa riwaya hizo akisisitiza kuwa eneo la Onitsha ndilo lililokuwa na shule nyingi zaidi katika

Nigeria kando na kuwa mojawapo wa masoko makubwa zaidi barani Afrika. Kwa sababu hii, wanafunzi na wafanyibiashara ndio waliokuwa wateja wakuu katika soko la Onitsha.

Kando na riwaya za Soko la Onitsha, kulikuwa na waandishi wengine walijitosa katika utunzi wa riwaya pendwa hususan riwaya za kiuhalifu na zile za kiupelelezi. Cyprian Ekwensi alianza kwa kutunga riwaya ya kihalifu kabla ya kuingilia utanzu wa riwaya ya kiupelelezi. Kwa mfano, aliandika riwaya ya kihalifu iitwayo, *People of the City*. Riwaya ya kiupelelezi maarufu ya Ekwensi ni *Yaba Rand about Murder* (1962) ambayo inamhusu mpelelezi John Faoulu anayepeleleza kesi ya mauaji. Ili kufanikisha uchunguzi wake, Faolu anafanya uchumba na mkewe mshukiwa. Riwaya hii ina sifa nyingi za Kimagharibi kama vile kupigiwa simu na mtu asiyejulikana, kuwepo kwa vidokezo kadhaa, habari kuhusu uhalifu kuripotiwa magazetini, mpelelezi wa polisi asiye na maarifa mengi na kadhalika. Tofauti iliyopo ni kuwepo tu kwa mandhari ya Kiafrika. Mwandishi mwingine wa riwaya za kiupelelezi kutoka Nigeria ni Dan Fulani aliyeandika, *No Condition is Permanent* (1981), *Flight 800* (1983) na *The Power of Corruption* (1983) ambapo alimbuni mpelelezi Pius Shale 005.

Kando na mataifa ya Nigeria, nchi za Cameroon na Ghana pia zimekuwa na waandishi wa riwaya za kiupelelezi. Kutoka Ghana, Kwei Quartey aliandika riwaya kadhaa za upelelezi kama vile, *Wife of the Gods* (2009), *Children of the Street* (2011) na *Murder at Cape Three Points* (2014) ambapo alimtumia mpelelezi Dawson. Pia ameandika riwaya ya hivi karibuni ya *The Missing American* (2020) ambako amemtumia mpelelezi wa kike, Emma Djan, aliyekuwa akifanya kazi katika idara ya polisi kabla ya kuingilia upelelezi wa kibinafsi. Kutoka Cameroon, mwandishi Linus Asong aliandika *The Crown of Thorns* (1992), *The Akroma File* (1997) na *The Crabs of Bengui* (2008). Kazi nyingine za kiupelelezi kutoka Afrika Magharibi ni *Tail of the Blue Bird* ya Nii Ayikwei wa kutoka Ghana, *The Lazarus Effect* ya Hawa Jande Golakai kutoka Liberia na *Bound to Secrecy* ya Vumba Sheriff kutoka Liberia.

### 2.7.2 Riwaya ya Kiupelelezi Kusini mwa Afrika

Eneo la Kusini mwa Afrika lina lina mataifa yenye historia ndefu ya ukoloni, hali ambayo imeathiri fasihi ya kutoka eneo hili. Kwa mfano katika Afrika Kusini, fasihi ya Kimagharibi ililetwa na kuendelezwa na wakoloni walioselelea humo kwa miaka mingi. Kuwepo kwa wakoloni pamoja na sera ya ubaguzi wa rangi kama itikadi ya kikoloni katika taifa hili, kumesababisha uibukaji wa

makundi matatu ya waandishi; Wazungu waliokuwa wakoloni, Waafrika ambao ndio watu asili humo, na chotara waliozaliwa baina ya Waafrika na Wazungu. Kundi la Wazungu ndilo lililotanguliza uandishi wa riwaya ya kiupelelezi nchini humo na kwa sababu hii, riwaya ya kiupelelezi ikawa kama mwendelezo wa riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi. Baadhi ya watunzi wa Kizungu ni kama vile Deon Meyer, Margie Ortoford, Richard Kunzmann na Mike Nicol ambao walichapisha riwaya zao kiusanjari. Mtunzi Deon Mayer alikuwa mwanahabari aliyevuma sana Afrika Kusini kwa kuchapisha riwaya kumi na tatu pamoja na hadithi fupi mbili. Baadhi ya kazi zake ni *Dead before Dying* (1999) ambayo kwanza ilitolewa kwa lugha ya Kiafrikana katika mwaka wa 1994 na baadaye kutafsriwa katika Kiingereza. Kazi nyingine ni *Heart of the Hunter* (2003), *Devils Peak* (2008), *Blood Safari* (2009) na nyinginezo.

Mwandishi mwingine aliyeandika katika enzi ya ubaguzi wa rangi Afrika kusini ni Wessel Ebersohn ambaye katika riwaya zake alijitokeza na mpelelezi Yudel Gordon, ambaye pia alikuwa daktari wa kuwatibu wafungwa. Ni katika shughuli za kuwatibu wafungwa ndipo anakopata hari ya kupeleleza kuhusu uhalifu na kisha kuwa mwandishi wa masuala ya uhalifu na upelelezi. Kwa kuwa mfumo wa utawala haukuruhusu kukosolewa wakati mtunzi huyu alipoandika, mara kwa mara Ebersohn alijipata akitiwa mbaroni na polisi. Yeye alionekana kuwa ndiye anayetoa siri na njama za polisi kwa watu wa kawaida. Kwa sababu hii akachukuliwa kama adui. Alilazimika kwenda mafichoni huku vitabu vyake vikipigwa marufuku. Baadhi ya riwaya zake ni *Divide the Night* (1981), *October Killings* (2009) na *African Aftermath* (2019) miongoni mwa nyinginezo. Mtunzi mwingine wa riwaya ya kiupelelezi aliyevuma Afrika Kusini ni MacClure James ambaye aliibuka na sanjari ya riwaya za kiupelelezi. Baadhi ya riwaya zake ni kama vile *The Steam Pig* (1971), *The Sunday Hangman* (1977), *Cop World* (1984) miongoni mwa nyingine.

Waandishi weusi wa Africa Kusini walianza kujitokeza baada ya miaka ya 1950 na kuongezeka maradufu baada ya kuanguka kwa ukoloni 1994. Mtunzi Diale Tiholwe kwa mfano, aliandika riwaya mbili, *Counting Coffins* (2008) na *Ancient Rites* (2011) na kufuata mtindo uliowekwa awali wa kumtumia mpelelezi yule yule katika kazi zinazofuata. Mtunzi mwingine wa Kiafrika aliyevamia uga wa riwaya ya kiupelelezi baada ya kuanguka kwa utawala wa kikoloni ni Meshack Masondo ambaye aliandika hadithi zake kwa Kizulu na kabla ya kifo chake mwaka 2013, riwaya zake zilikuwa zimeuza zaidi ya nakala 400,000. Masondo aliwahi kuandika riwaya kumi na moja zilizohusu uhalifu uliokuwa ukifanyika katika vijiji vya mashambani katika mkoa wa KwaZulu-

Natal. Baadhi ya kazi hizo ni *Kanti Nawe?* (1994), *Ngaze Ngazenza* (1994), *Sixolele* (2004) na nyinginezo. Mchango wake mkubwa unatokana na juhudi zake za kuendeleza na kuhifadhi lugha za kiasili kwa kutunga fasihi kwa lugha hizo. Baadhi ya vitabu vyake pia viliteuliwa kufundishia katika shule za msingi hasa darasa la nane na tisa. Riwaya zake mbili za mwisho zilihusu biashara haramu ya dawa za kulevya, uhalifu na migogoro baina ya waendeshaji wa magari ya teksi. Kinaya ni kwamba kifo chake pia kilitokana na migogoro kama hii aliyoiangazia katika riwaya zake, kwani alipowekeza katika biashara ya usafiri wa teksi, aliuawa na dereva wa teksi.

Mataifa mengine ya Kusini mwa Afrika pia yamewahi kuwa na riwaya za kiupelelezi ingawa kwa kiasi kidogo ikilinganishwa na Afrika Kusini. Kwa mfano, kutoka Botswana mwandishi Unity Dow aliandika riwaya ya kiupelelezi, *The Screaming of the Innocent* (2002), *The Heavens May Fall* (2006), *Saturday is for Funerals* (2010) miongoni mwa nyinginezo. Kuhusu uandishi wa riwaya za kiupelelezi nchini Botswana Alexander McCall Smith anafahamika kwa kwandika riwaya nyingi za kiupelelezi zilizomhusu mpelelezi wa kike, Mma Precious Ramotswe. Ingawa mwandishi huyu ni mzaliwa wa Scotland, riwaya zake zinahusu mandhari ya nchi ya Botswana hasa Gaborone. Katika msururu wa riwaya ishirini zilizotolewa baina ya 1998-2019, Mma Ramotswe ndiye mhusika mkuu na pia mpelelezi. Riwaya yake ya kwanza, *The No.1 Ladies Detective Agency* (1998) imetumiwa kama jina la msururu mzima wa kazi zake huku riwaya nyingi zikitafsiriwa katika lugha nyingi za kimataifa na kuuzwa kwa wingi huko Ulaya na Marekani. Baadhi ya riwaya nyingine zake ni *The Full Cupbord of Life* (2003), *The Kalahari Typing School for Men* (2002), na *In the Company of Cheerful Ladies* (2004).

Mtunzi mwingine mtajika ni Margie Orford, ambaye alikuwa mwanahabari wa kiupelelezi. Kazi zake zilipendwa katika mataifa ya Kusini mwa Afrika kama vile Namibia, Malawi na Afrika Kusini.Yeye aliishi nchini Namibia, Afrika Kusini na baadaye kuhamia Ulaya. Alimbuni mpelelezi wa kike katika riwaya zake, Clare Hart. Baadhi ya riwaya zake ni *Blood Rose* (2007), *Daddy's Girl* (2009), *The Magic Fish* (2012), *Water Music* (2013) na nyinginezo.

Uandishi wa aina yoyote ya kifasihi kutoka Afrika Kusini waweza kuchunguzwa katika vipindi viwili vya kihistoria ambavyo ni kipindi cha utawala wa kikoloni na ubaguzi wa rangi na kipindi cha baada ya ubaguzi wa rangi na kuanguka kwa ukoloni. Katika kipindi cha kwanza riwaya nyingi zilitolewa na Wazungu na zilisheheni itikadi ya kikoloni zilizojitokeza kupitia ubaguzi wa rangi. Hii ina maana kuwa ingawa riwaya ya kiupelelezi hulenga kuburudisha aghalabu huishia kutoka

nje ya lengo hili la kimsingi na kuangazia masuala halisi yanayohusu jamii ya mwandishi ya wakati huo. Hali hii aghalabu haipatikani tu katika riwaya ya kiupelelezi ya Afrika Kusini, bali pia hupatikana katika fasihi pendwa za sehemu nyngi za ulimwengu, ikiwemo riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili.

Ubora wa riwaya ya kiupelelezi katika kuangazia masuala ya kijamii umeangaziwa pia na Mandel (1984), ambaye anasisitiza kwamba ukuaji wa riwaya hii umeenda sambamba na mabadiliko ya kijamii. Katika kazi za watunzi wa Afrika Kusini, kama vile Deon Mayer, Mergie Orford, Mike Nicol na wengineo, kando na kuangazia suala la upelelezi na uhalifu, wameyaangazia pia matatizo ya wakati wa ubaguzi wa rangi na baada ya utawala wa ubaguzi wa rangi. Masuala mengine yanayojitokeza katika kazi zao ni kama vile ufisadi katika serikali, umaskini, tatizo la ukimwi na uhalifu (ambao umeendelea hadi katika mitaa kama vile Soweto) na siasa za kikabila.

### 2.7.3 Riwaya ya Kiupelelezi ya Afrika Mashariki ( ya Kiswahili)

Riwaya pendwa katika Afrika Mashariki kama tulivyoona katika Afrika Magharibi imechipuka kutokana na athari za ukoloni. Athari hizo ziliwajia watu wa eneo hili kupitia mfumo wa kielimu ambapo wasomi waliweza kutagusana na riwaya za Kimagharibi za kiupelelezi, kijasira, za kimapenzi na za kiuhalifu. Kama wanavyoonyesha wahakiki Mlacha na Madumula (1995:22), athari za riwaya ya Kimagharibi pia ziliwafikia watu wa Afrika Mashariki kupitia utazamaji wa filamu za kuvutia kama vile zile za James Bond, Bruce Lee na waigizaji wengine wa Kimarekani na Ulaya. Kando na kutazama filamu hizi, pia usomaji wa visa vya kuzizimua kutoka kwa kazi za watunzi kama Ian Fleming[3] ulisaidia kusambaza athari hizi.

Nchini Kenya riwaya pendwa zilizojitokeza kwa wingi ni zile zilizohusu uhalifu, mapenzi na uozo wa mijini kama vile ulevi na ukahaba. Riwaya za kihalifu ziliendelezwa kwa kiwango kikubwa na John Kiriamiti zilizojitokeza kiusanjari. Baadhi ya kazi zake ni *My Life in Crime* (1984) na *My Life with a Criminal* (1984). Riwaya nyingine zilizohusu uhalifu ni *A Brief Assignment* (Ayub Ndii, 1976), *Shortcut To Hell* (Kitololo, 1983), *The Mystery Smugglers* (Mwangi Ruheni, 1975)

[3] Riwaya zilizoandikwa na Ian Flemming ndizo zilizoweka msingi wa *filamu za James Bond*.

miongoni mwa nyinginezo katika fasihi ya Kiingereza. Msuko wa riwaya hizi huhusisha magenge ya wezi aidha wakiwa katika jela, wakitoroka jela au uhusiano wao na polisi, lakini miishio yake hutoa adili kwamba uhalifu haulipi. Katika fasihi ya Kiswahili, riwaya zinazoweza kuwakilisha kipera cha uhalifu nchini Kenya ni zile za Levi kama vile, *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu*, *Fedheha ya Fedha*, na kazi za Omolo Odera kama vile *Mtaka Yote Hukosa Yote.* Nchini Tanzania riwaya za Simbamwenne kama vile *Mwisho wa Mapenzi* na *Kwa Sababu ya Pesa* na riwaya za Rajab kama vile *Ufunguo Bandia* na *Sanda la Jambazi* zimo katika kategoria hii.

Baadhi ya kazi za Mangua kama vile *Son of Woman* (1971) na *Son of Woman in Mombasa* (1984) zinahusu mandhari ya mijini hasa maisha ya kudunisha ya mitaa ya mabanda yanayowasukuma vijana katika uhalifu. Maillu ndiye aliyeupa utanzu wa riwaya pendwa nchini Kenya mizizi kwani alifanya utafiti kabla ya kuanza utunzi wake ambapo alibaini kuwa hamu za wasomaji zilihusu mada za siasa, mahusiano ya kingono, nafasi ya dini, vifo na pesa. Kwa kutumia matokeo ya uchunguzi wake, Maillu aliandika riwaya zilizohusu dhamira hizo ambazo zilijitokeza katika riwaya za *Unfit for Human Consumption* (1973), *My Dear Bottle* (1973), *After 4:30* (1974), *Trouble* (1974), *No* (1976). Kutokana na mada hizi, kazi za Maillu zimekosolewa na si tu baadhi ya wahakiki bali pia na viongozi wa kiserikali. Kwa mfano, Kurtz (1998:95) anaripoti kwamba kazi hizo zilipigwa marufuku nchini Tanzania kutokana na namna zilivyoyasawiri mahusiano ya kingono kwa uwazi. Kutokana na usawiri huu, mhakiki Wanjala (1978:135-6) alizielezea kazi hizo kama za kiponografia. Meja Mwangi naye aliandika riwaya tatu zilizohusu maovu ya maisha ya mijini kama vile ulevi na ukahaba, kwa usanjari. Kazi hizo ni *Kill Me Quick* (1973), *Going Down River Road* (1976) na *The Cockroach Dance* (1979).

Riwaya pendwa ilifikia upeo wa ukuaji wake katika kipindi cha miaka ya 1970-1980 kama wasemavyo Mlacha na Madumulla (1995:32) kutokana na sababu za kiuchumi. Wanasema kwamba katika kipindi hiki kulikuwa na matatizo mengi ya kiuchumi yaliyowalazamisha watunzi kuchapisha riwaya zao ili kujikuamua kutokana na matatizo ya kiuchumi. Matatizo hayo yaliletwa na ongezeko la bei ya mafuta, kuongezeka kwa bei ya mashine zilizokuwa zikiagizwa kutoka nje na ukame uliovikosesha viwanda vingi malighafi, hivyo kuvifanya kufunga na kuwafuta kazi waajiriwa wengi. Kwa sababu hii, wahakiki hawa wanasema kuwa vituo vya kuchapisha fasihi pendwa vilianzishwa kiholela na kuwalazimu baadhi ya watunzi kujiuzia vitabu vyao mitaani wenyewe.

Kando na matatizo haya ya kiuchumi, sababu nyingine zilizochangia kuibuka kwa vituo vya uchapishaji ni kuwepo kwa soko kubwa lililoletwa na vijana pamoja na uhaba wa aina nyingine za burudani. Hata hivyo, kulingana na wahakiki hawa, riwaya pendwa haitekelezi tu wajibu wa kuburudisha bali pia zinakuza maadili. Wanatoa sifa zifuatazo za riwaya pendwa: (a) Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha taharuki. (b) Mtiririko unaofuatika kirahisi. (c) Mhusika mkuu huwa mkwezwa. (d) Dhamira zake hupendwa na watu wengi. (e) Mandhari yake yameundwa kwa namna ya kipekee. (f) Matumizi ya lugha rahisi ya kila siku. (g) Jinsia ya kike hutumiwa kama chombo cha anasa. Sifa hizi hazijitokezi tu katika riwaya pendwa ya Kiswahili, bali pia katika riwaya pendwa ya Kimagharibi, ikiwa ni ishara ya msambao wa athari hizo kutoka Ulaya hadi janibu hizi za Afrika Mashariki. Hata hivyo, inaelekea kwamba katika kipindi hiki, jamii nzima ilikuwa na mitazamo duni dhidi ya mwanamke, jambo linalojitokeza pia katika tanzu nyinginezo za fasihi.

Riwaya ya kiupelelezi kwa Kiingereza na Kiswahili haikushika kasi nchini Kenya ingawa kuna watunzi wachache waliojaribu kubuni riwaya sahili kuhusiana na upelelezi. Katika Kiingereza, Marjorie Oludhe aliandika *Murder in Majengo* (1972) ambapo katika msuko wake hadithi inaanza na mauaji lakini baadaye anabadili mkondo wa vitushi na kuegemea maisha ya mijini ya jamii ya Wajaluo baada ya uhuru. Meja Mwangi pia alitunga riwaya iliyohusu upelelezi na ujazira, *Assassins on Safari* (1983), ambapo askari, Kanja, anapeleleza njama ya mamuluki wa kutoka Ujerumani wanaopanga kumuua waziri wa mambo ya nje wa Marekani pindi anapofika katika mbuga ya wanyama ya Amboseli. Kanja anaizambaratisha njama hii na kupitia ufanisi huu, anailetea idara ya polisi ya Kenya sifa kuu kwani kupitia vitendo vyake Kanja, polisi wanasawirika kuwa na uwezo wa kulinda sheria za nchi yao. Mukoma wa Ngugi pia ameandika riwaya ya kiupelelezi kwa Kiingereza, *Black Star Nairobi* (2007), yenye mandhari ya Nairobi wakati wa uchaguzi wa mwaka wa 2007. Mwandishi wa riwaya ya kiupelelezi kwa Kiswahili Godfrey Levi alitoa riwaya sahili mbili, *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975 na *Fedheha ya Fedha* (1981). Ingawa riwaya hizi hazilipi suala la upelelezi uzito unaostahili katika utanzu huu, zinahusu polisi wakichunguza visa vya kiuhalifu na ukusanyaji habari kutoka kwa wafungwa.

Mlacha na Madumulla, wanaiweka riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili katika makundi matatu kutegemea mitindo ya waandishi mbalimbali: Kwanza, wanazungumzia mtindo wa Mohamed Said Abdulla ambapo sifa kuu ni upelelezi wa kadhia kupitia uchanganuzi wa kimantiki wa hali fulani. Kunakuwa na uhalifu, ambapo aghalabu polisi wanauchunguza uhalifu huo na

wanaposhindwa wanamtafuta mpelelezi wa kibinafsi kuwasaidia. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, Bwana Msa anapoalikwa na Inspekta Seif kumsaidia kuchunguza wizi wa mali ya Mwana wa Giningi. Pili, wahakiki hawa wanazungumzia mtindo wa Musiba ambao sifa yake kuu ni mhusika mkuu kufanya uchunguzi kuhusu uhalifu kwa kutumia nguvu za kimwili kupambana na wahalifu. Hali hii inadhihirika katika kazi za Elvis Musiba kama vile *Uchu* (2001) ambapo mpelelezi Willy Gamba anapambana na wachochezi wa mzozo wa kisiasa nchini Rwanda kwa kutumia zana mbalimbali za kivita pamoja na kusafiri kutoka Tanzania hadi Rwanda na Kongo kuharibu mipango ya adui. Vilevile katika riwaya ya Kassam iitwayo *Mpango* (1982) mtunzi anatumia mtindo sawa na Musiba[4]. Huu ndio mtindo autumiao Ben Mtobwa pia kwani mpelelezi wa kazi zake, Joram Kiango anatumia mbinu kadhaa za upiganaji zikiwemo vifaa vya teknolojia ya kisasa vya kivita kando na kupeleleza. Katika mtindo huu wa riwaya ya kiupelelezi, mpelelezi huwa situ bingwa wa kufikiri, kama ilivyo katika kazi za Abdulla, bali ana uwezo wa kutumia silaha na viungo vyake vya mwili katika kupambana na wahalifu. Hata hivyo mara nyingine hufanya makosa madogo madogo ambayo humwingiza katika mitanziko na mahasidi wake lakini hujinasua mwishowe.

Utafiti huu umebaini kwamba sifa hii inayojitokeza katika kazi za Kiswahili imetokana na athari za Kimagharibi ambapo riwaya zilizobuniwa kati ya miaka ya 1920-1930 zilizingatia mkondo huu. Athari hizi zilijidhihirisha kupitia mavazi, vijitabia fulani vya wahusika kama vile matumizi ya lugha ya mitaani, uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe. Fauka ya hayo, aghalabu suala la mapenzi na upelelezi huandamana kwani wapelelezi katika mtindo huu husawiriwa wakitembea na wanawake warembo. Mtindo wa tatu ni ule wa Mbunda Msokile ambapo kando na uhalifu na upelelezi, riwaya hii pia huhusisha uhalisia wa kimaisha upatikanao pia katika riwaya dhati hasa kwa kutilia mkazo kwenye suala la maadili. Badala ya upelelezi kinachopewa kipau mbele ni uhalifu na mara tu unapotokea polisi na njia nyingine za kisheria hutumika.Baadhi ya riwaya nyingine zinazofuata mtindo huu ni zile Godfrey Levi wa Kenya kama vile *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975 na *Fedheha ya Fedha* (1981) pamoja na kazi za John Simbamwenne kama vile *Kwa Sababu ya Pesa* (1972).

[4] Mtindo wa Kassam na Musiba unahusu mhusika mkuu kupeleleza pamoja na kutumia mbinu kadhaa za upiganaji na maadui zikiwemo matumizi ya silaha kali na pia viungo vyake vya mwili.

Utafiti huu umebaini kwamba kuna mtindo mwingine unaohusu ujasusi wa kimataifa ambapo uhalifu unayahusu mataifa kadhaa na kumbidi mpelelezi kuzuru nchi na miji mbalimbali kupeleleza hali hizo. Katika kiwango hiki, mwenye hatia ni taifa au ajenti anayetumwa na taifa, kundi la mataifa ama shirika fulani la kijasusi. Hii ndiyo hali iliyoshuhudiwa huko Ulaya na Marekani katika riwaya za kiupelelezi zilizojitokeza katika kipindi cha urasimu. Upelelezi wa kiwango cha kimataifa unajitokeza tena wakati wa vita baridi ambapo mataifa yalifanya upelelezi wa kisiri dhidi ya mataifa mengine ili kusambaratisha itikadi za kisiasa za adui. Kwa mfano, wakati wa vita hivi, kulikuwa na uenezaji wa itikadi za ubepari na usosholisti uliosababisha ushindani mkali kuibuka baina ya taifa la Marekani na Muungano wa Sovieti. Katika ushindani huu, ujasusi ulichukua nafasi kubwa katika siasa ya dunia na mashirika ya kijasusi yaliweza kujipenyeza kisiri katika mataifa yaliyoegemea siasa za mrengo wa adui ili kukusanya habari kuhusu mipango ya adui zao. Hii ndio sababu riwaya za kiupelelezi zilizotungwa baada ya kipindi hiki cha vita baridi zilihusu upelelezi wa aina hii. Baadhi ya riwaya za Ben Mtobwa kwa mfano, zilihusu upelelezi uliofanywa na makaburu wa Afrika Kusini dhidi ya mataifa jirani yaliyounga mkono vita vya uhuru na kupinga ubaguzi wa rangi nchini humo.

Mahusiko ya Tanzania katika ukombozi wa Afrika Kusini yanadhihirika katika riwaya za Mtobwa za *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984) na *Tutarudi na Roho Zetu?* (1984). Dhamira kama hii pia inadumishwa katika kazi za watunzi wengine. Kwa mfano, katika riwaya ya Hammie Rajab ya *Roho Mkononi* (1984), na ile ya Kassim Kassam ya *Mpango* (1992).

Kama tulivyoona hapo awali ni kwamba mabadilko mengi yalijitokeza katika riwaya ya kiupelelezi wakati wa urasimu huko Marekani. Mabadiliko kadhaa pia yameshuhudiwa katika ukuaji wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili kutokana na mpito wa muda. Badiliko mojawapo lilihusu uibukaji wa wapelelezi wa kike. Kama anavyosema Knight (2003: 166-182) uibukaji wa wapelelezi wa kike huko Ulaya na Marekani ulianza kujitokeza baada ya vita vikuu vya pili vya dunia. Huu ndio wakati Agatha Christie alipombuni mpelelezi wa kike aliyevutia wasomaji mno, Jessica Fletcher. Katika fasihii ya Kiswahili, mpelelezi wa kike amejitokeza mara ya kwanza katika kazi ya Jumaa Mkabarah iitwayo, *Mbio za Kipofu* (1985). Mpelelezi huyo, Mainda Jumaa alikuwa msichana mrembo na kama anavyosawiriwa urembo wake pia unaongeza mvuto katika riwaya hii. Pia anazifanya kazi za mtunzi huyu zioane na uhalisia wa wakati huo, miaka ya 1980, ambapo tetezi kuhusu usawa wa kijinsia zilikuwa zimeanza kushika kasi. Ukosefu wa wapelelezi

wengi wa kike katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili na za Kimagharibi huenda umetokana na mtazamo wa jamii nyingi kwamba mwanaume ndiye mwenye nguvu za kustahimili hatari kinyume na wanawake ambao huchukuliwa kama wanyonge. Hata hivyo, katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, waandishi wa kike hawajajitokeza kama tulivyoona katika Ulaya na Marekani miaka ya 1920-1930 ambapo watunzi wa kike wengi walijitokeza kama vile Dorothy Sayers, Anna Katharina Green, Agatha Christie na wengine.

#### 2.7.3.1 Sifa za Riwaya ya Kiupelelezi ya Kiswahili

Katika sehemu hii, tunaonyesha sifa za kifani na na za kimaudhui zinazoibainisha riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Riwaya hizi ni zile zilizoandikwa na waandishi wa Afrika Mashariki hususan, Kenya na Tanzania.

Kwanza, sifa muhimu inayozibainisha riwaya za kiupelelezi za Kiswahili na kuzitofautisha na zile za nchi za Kimagharibi ni namna imani na itikadi za kitamaduni zinavyotumika kuongeza utata kwenye upelelezi. Kuna imani zinazohusu matumizi ya uchawi kama chanzo cha mauaji ambapo mtu anauawa ili viungo vya mwili wake vitumike katika uchawi au hali ambapo uhalifu unapofanywa, wachawi wanasingiziwa kuwa ndio waliohusika ili mhalifu aepuke kutiwa mbaroni. Katika riwaya za Mohamed Said Abdulla, baadhi ya visa vya kiuhalifu vinahusishwa na miviga ya kichawi. Riwaya zake ni kama vile; *Mzimu wa Watu wa Kale* (1958), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mke Mmoja Waume Watatu* (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) *Kosa la Bwana Msa* (1984). Kezilahabi (1980:79) anatueleza kuwa matumizi ya uchawi katika jamii za Kiafrika ni ishara ya tofauti za kitabaka baina ya matajiri na maskini. Maskini anamkimbilia mganga ili aelezwe kiini cha ufukara wake na namna ya kuumaliza, naye tajiri anamwendea mganga ili ajikinge dhidi ya laana za watu wa tabaka la chini na pia ili ajiepushe na wivu wa wenzake wa tabaka la juu. Katika riwaya za Abdulla, za *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957) na *Kisima cha Giningi* (1968) imani za kichawi zinadhihirika lakini kufikia mwishoni mwa hadithi hizo, mwandishi anadhihirisha kuwa uchawi unatumika kama kisingizio cha uhalifu. Mtunzi huyu anadhihirisha pia kuwa uhalifu unatekelezwa kwa sababu kadhaa zikiwemo za kiuchumi hususan urithi wa mashamba. Kama tulivyoona hapo awali, imani za

kichawi pia zinajidhihirisha katika riwaya ya kiupelelezi ya Afrika Kimagharibi hususan katika riwaya za Kwei Quartey kama vile *Wife of the Gods.*

Sifa nyingine muhimu ya riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili ni kuwa usambazaji wake uliambatana na uchapishaji wa hadithi za kiupelelezi katika magazeti mbalimbali. Hii ni kwa sababu wengi waliochapisha riwaya zao pia walikuwa wanahabari katika magazeti hayo. Kwa kuwa walifahamu mahitaji ya soko, waliweza hata kutangaza vitabu vyao katika magazeti hayo pamoja na kuandika hadithi fupi katika magazeti pia. Kwa mfano, Katalambulla alikuwa mhariri katika gazeti la *Tanzania Films,* Hammie Rajab naye alikuwa mhariri katika gazeti la *Busara*, Kassim Kassam ni mchapishaji wa riwaya za kiupelelezi na mhariri mkuu wa gazeti la *Cheka* naye Ben Mtobwa alikuwa mhariri wa gazeti la *Heko.*

Tatu, ufisadi wa polisi na maofisa wa mahakama ni sifa ya kidhamira inayoibuka katika riwaya kadhaa za kiupelelezi za Kiswahili. Kuna udhaifu wa polisi katika utenda kazi wao ambao unalazimisha kuwepo kwa mpelelezi wa kibinafsi kuitwa ili kufanikisha uchunguzi. Kando na udhaifu huu, kuna hali ambapo polisi wanapotosha ushahidi ili kuwaondolea baadhi ya washukiwa lawama. Reuster-Jahn (2012:173-184) anaeleza kwamba kumekuwa na ongezeko la visa vya utoaji hongo na kuathiri mwelekeo wa uchunguzi wa polisi na maofisa wa mahakama. Anafafanua kuwa mtindo huu umeshusha viwango vya uaminikaji kutoka kwa umma. Anatoa mfano wa riwaya za kiupelelezi zinazomulika suala la ufisadi wa polisi kama vile *Simanzi* ya Abdul Ntandu ambapo kesi inageuzwa na kumfanya aliyeripoti uhalifu kuwa ndiye mhalifu. Pia katika riwaya ya *Bora Ujiuwe* ya Amos Izengo, maofisa wa polisi wanaghushi ushahidi. Kulingana na Reuster-Jahn, kuwepo kwa riwaya zinazozungumzia mahusiko ya polisi katika ufisadi ni dhihirisho la uhalisia wa mabadiliko ya kijamii yaliyofika Tanzania baada ya kuanguka kwa Ujamaa.

Nne, sifa nyingine inayobainika inahusu riwaya za kiupelelezi zilizojitokeza katika miaka ya themanini ambapo kazi nyingi zilihusu suala la mahusiano ya kimataifa hususan baina ya mataifa ya Kimagharibi na yale ya Kiafrika kwa upande mmoja na baina ya nchi za Kiafrika zenyewe. Baadhi ya riwaya za Mtobwa kama vile *Tutarudi na Roho Zetu* na *Najisikia Kuua Tena* zinaangazia uhusiano baina ya Tanzania na mataifa ya Kusini mwa Afrika kama vile Afrika Kusini. Zinaonyesha mchango wa Tanzania katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika kama vile Angola na Msumbiji. Baadhi ya kazi za Musiba pia kama vile *Uchu* na *Njama* zinahusu dhamira ya uhusiano wa kimataifa. Kwa mfano, riwaya ya *Uchu* inahusu mauaji ya halaiki nchini

Rwanda huku ile ya *Njama* ikihusu njama za makaburu wa Afrika Kusini za kuchelewesha uhuru wa watu weusi. Kutokana na hali hii, riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili imefumbata uhalisia wa wakati huo ambapo juhudi za kupigania ukombozi wa mataifa ya Afrika Kusini zilikiuwa zimepamba moto.

Tano, katika riwaya zenye mandhari ya miji, kuna uangazaji wa maisha ya mijini hususan changamoto zinazochangia kuwepo kwa uhalifu. Baadhi ya riwaya zinaonyesha matatizo ya wakaazi wa mijini kama vile ukosefu wa kazi, vyakula na makaazi. Mambo haya yanachochea ongezeko la aina mbalimbali za uhalifu kama vile wizi, uuzwaji wa mihadarati na mauaji. Riwaya za Simbamwenne kwa mfano zinayamulika maisha ya vijana wakiwa mijini na jinsi wanavyojiingiza katika uhalifu ili kukidhi mahitaji ya anasa. Vilevile, katika baadhi ya riwaya za Mtobwa, matendo mengi yanamhusu mpelelezi akipambana na wahalifu katika miji ya Dodoma, Nairobi, Arusha na hata katika miji ya Ulaya.

Kuhusu mtindo, karibu riwaya zote za kiupelelezi zina matumizi makubwa ya mbinu ya taharuki ambayo inasababisha mvuto kwa wasomaji na kuzidisha uburudishaji wa riwaya hizi. Kwa kuwa suluhu la migogoro inayohusu ni nani mhalifu na sababu za uhalifu huo inatolewa mwishoni mwa riwaya, hamu ya msomaji ya kuendelea kusoma inadumishwa hadi mwishoni mwa riwaya.

Sifa nyingine muhimu kuhusu mtindo, inahusiana na uhusika, usimulizi na msuko. Kuhusu uhusika, mhusika mpelelezi katika riwaya za Abdulla, Musiba na Mtobwa amesawiriwa kama binadamu mwenye uwezo unaozidi binadamu wa kawaida kiujuzi na matendo yake. Kwa njia hii, wahusika wapelelezi katika kazi hizi wameumbwa kwa misingi ya Sherlock Holmes, mpelelezi katika kazi za Conan Doyle. Hii ndio sababu baadhi ya wahakiki (Madumulla 1988:14, Kezilahabi, 1975:8) wanasema kuwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili imeathiriwa na mitindo ya waandishi wa Kimagharibi kama vile Conan Doyle na Agatha Christie. Kushadidia wazo hili, Gromov (2012:152), anasema kuwa katika kazi za Mtobwa, mpelelezi Joram Kiango anashabihiana na Philip Marlowe, mhusika mpelelezi katika kazi za Raymond Chandler. Kuna mtindo pia katika riwaya za Kiswahili za kiupelelezi, kama ilivyo katika riwaya za Kimagharibi, wa kumtumia mpelelezi yuleyule katika riwaya nyingi za mwandishi mmoja.

### 2.7.3.2 Sababu za Kuzuka na Kukua Kwa Riwaya ya Kiupelelezi ya Kiswahili

Kuna baadhi ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yaliyochochea uibukaji wa riwaya ya kiupelelezi katika mazingira ya Afrika Mashariki. Kwanza, kuna baadhi ya waandishi walioanza kubuni na kuchapisha riwaya zao kwa sababu za kiuchumi tu. Madumulla (1988:11) anasema kwamba kati ya miaka ya 1970-1980 eneo la Afrika Mashariki lilikumbwa na matatizo ya kiuchumi yaliyoletwa na ukame, mgogoro wa mafuta mwaka wa 1973 na katika taifa la Tanzania kulikuwa na vita vya Kagera vya 1979-1980. Hali iliharibika zaidi kufuatia misukosuko ya kiuchumi ya ulimwengu mzima wakati huu. Athari hizi ziliathiri uibukaji wa fasihi pendwa hususan riwaya ya kiupelelezi katika Tanzania. Waandishi wengi walianza uchapishaji wa vitabu kama njia ya kuijikuamua kutokana na matatizo ya kiuchumi. Hii ndio maana kipindi cha miaka ya themanini kilishuhudia utolewaji wa riwaya pendwa nyingi zikiwemo za kiupelelezi pamoja na vyumba vingi vya uchapishaji. Ili kukumbana na matatizo haya, baadhi ya watunzi walianza kuuza riwaya zao kwa reja reja mitaani pamoja na kuanzisha maduka yao. Pili, kulikuwa na ongezeko la idadi ya watu katika kipindi cha baada ya uhuru hadi kufikia miaka ya themanini. Jambo hili lilipanua soko la si tu vitabu vya kiupelelezi bali pia vya aina nyinginezo. Waandishi na wachapishaji nao walipoligundua soko hili hasa miongoni mwa vijana, walizidisha juhudi zao katika utoaji wa vitabu vya fasihi pendwa, hivyo riwaya pendwa ikapata nguvu.

Tatu, mfumo wa kielimu ulichangia pakubwa katika uibukaji na ueneaji wa riwaya pendwa ikiwemo riwaya ya kiupelelezi katika maeneo ya Afrika Mashariki. Ili kuongeza idadi ya wananchi wasio na elimu, serikali za mataifa ya Afrika Mashariki zilianzisha juhudi za kimakusudi za kuwavutia wasomaji kupitia wizara za elimu. Kutokana na kusudi hili, riwaya pendwa za Kimagharibi za watunzi kama vile James Hadley Chase, Harold Robbins na wengineo zilipatikana nchini Kenya na Tanzania pamoja na fasihi dhati za kikoloni zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi kwa Kiswahili ili kuifikia elimu kwa watu wengi. Kimura (1992:55) anasema kwamba Watanzania waliosoma tafsiri hizo waliathirika nazo hivi kwamba, riwaya walizotunga zilikuwa kama nakala za riwaya hizo za kigeni kimuundo, kimsuko, tabia za wahusika na silaha watumiazo.

Kupitia mfumo huu wa shule wanafunzi waliweza kutagusana na fasihi pendwa na fasihi dhati za kigeni. Ni kupitia juhudi hizi, riwaya za *Kisiwa Chenye Hazina*, *Elisi katika Nchi ya Ajabu* na *Mashimo ya Mfalme Suleiman* ziliweza kutumiwa shuleni nchini Kenya kama vitabu vya ziada.

Baada ya uhuru, mfumo wa elimu pia ulichangia kuieneza riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili kupitia uteuzi wa baadhi ya riwaya hizo kutumika kama vitabu vya kiada katika shule za upili. Nchini Kenya kwa mfano, riwaya ya *Simu ya Kifo* na *Mzimu wa Watu wa Kale* ziliteuliwa kutahiniwa shuleni miaka ya sabini, kisha baadaye miaka ya themanini, riwaya ya *Siri ya Sifuri, Mwana wa Yungi Hulewa* na ile ya *Kisima cha Giningi* ziliteuliwa kutahiniwa shuleni. Katika miaka ya tisini, riwaya ya *Kisima cha Giningi* iliteuliwa tena kusomwa na kutahiniwa shuleni. Nchini Tanzania baadhi ya riwaya za kiupelelezi zilizotumika shuleni ni *Mfadhili* ya Hussein Issa Tuwa, *Zawadi ya Ushindi*, *Hofu* ya Elvis Musiba na nyinginezo.

Nne, juhudi za kamati ya usanifishaji wa lugha ya Kiswahili iliyoanzishwa katika miaka ya 1930 zilifanikisha uwekaji wa chembechembe za kwanza katika uibukaji wa riwaya ya kiupelelezi. Chini ya usimamizi wa kamati hii, kamusi na majarida kadhaa yalianzishwa. Kadhalika, kamati hii iliandaa mashindano ya uandishi mara kwa mara. Kwa njia hii kamati hii ilopokea miswada mbali mbali kutoka kwa waandishi chipukizi.Wazo hili linaungwa mkono na mhakiki, Mbatiah (2016) ambaye anasema kwamba ni kupitia juhudi za kamati hii, mswada wa Abdulla wa *Mzimu wa Watu wa Kale* uliweza kuchapishwa mara ya kwanza 1948. Kamati hii pia ilianzisha Shirika la Uchapishaji la Afrika Mashariki (EALB) ambalo lilichangia katika uchapishaji wa aina mbalimbali za riwaya zikiwemo riwaya za kiupelelezi kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale* ya Mohammed Said Abdulla na *Simu ya Kifo* yake Faraj Katalambulla.

Sababu nyingine inayoweza kuhusishwa na uibukaji wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili ni usomaji wa riwaya za Kimagharibi hasa za Kiingereza za watunzi kama vile Agatha Christie, Ian Fleming, James Hadley Chase na wengineo. Usomaji wa kazi hizi uliwachochea watunzi wa Kiswahili kubuni kazi zao kwa misingi iliyowekwa na waasisi wa utanzu huu. Kwa mfano, Gromov (2008) katika mahojiano na Mtobwa, mwandishi Mtobwa anakiri kwamba ameathiriwa na riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi katika utunzi wake. Kando na athari za Kimagharibi, kuna athari za filamu za kutoka mataifa ya Kimashariki kama vile Japan na Uchina. Katika baadhi ya riwaya za Musiba kama vile *Njama*, Musiba anamsawiri mpelelezi, Willy Gamba akitumia mitindo ya upiganaji ya Kininja ya Japan na mtindo wa Kung Fu ya Uchina. Hii ni ishara kwamba, ubunifu wake katika kumuumba mhusika mkuu umeathiriwa na utazamaji wa filamu hizi.

Mwisho, riwaya hii iliibuka kama njia ya kuongeza huduma za burudani hasa kwa wakaazi wa mijini. Hii ni kwa sababu ongezeko la wakaazi wa mijini halikuambatana na ukuaji wa huduma za

burudani kwa umma kama vile majumba ya sinema, viwanja vya michezo na mabustani ya mapumziko. Utafiti uliofanywa na Kimura (1992) katika Tanzania ulionyesha kwamba huduma za burudani zilizokuwepo kabla ya uhuru zilipungua baada ya uhuru. Kwa mfano,anasema kwamba majumba ya sinema yaliyokuwa 41 mwaka wa 1966 yalipungua hadi majumba 36 kufikia 1976. Huenda upungufu huu ulitokana na sera ya kisiasa ya Ujamaa iliyoshinikiza wananchi wengi kuhamia vijijini kushiriki kilimo.Upungufu huu ndio uliotoa nafasi ya mjo wa riwaya pendwa ili kuliziba pengo hilo. Vile vile kulizuka makundi ya maonyesho ya sanaa yaliyozuru mabaa kati ya 1970-1980 ili kuwaburudisha watu. Kundi la waandishi wa riwaya za kiupelelezi lilizuka na mtindo wa kwandika hadithi fupi katika magazeti kando na riwaya ili kukidhi mahitaji ya burudani kwa umma. Tangu wakati huo, riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili imekua zaidi nchini Tanzania kwa kasi ilikilinganishwa na mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

#### 2.7.3.3 Wasifu wa Waandishi na Muhtasari wa riwaya zinazohakikiwa

Kufahamu wasifu wa mwandishi kunaweza kumsaidia mhakiki kuelewa uhusiano uliopo baina ya kazi za mtunzi fulani na kazi hizo. Bajaj (2015:27) anaeleza kwamba mtindo wa kuihusisha kazi ya kifasihi na historia ya maisha ya mwandishi ulianza wakati wa mapinduzi ya maarifa kati ya karne za 14-17. Uchunguzi wa usuli wa mwandishi pamoja na uhakiki wa kihistoria ulimfaa mhakiki kuifasiri kazi ya kifasihi kwa kuzihusisha na mazingira ya kihistoria ya mtunzi huyo. Uhusiano huu unajitokeza kwa njia mbili; kwanza, kuelewa maisha na wasifu wa mwandishi kunaweza kumfaa mhakiki katika kuzielewa zaidi kazi za mwandishi huyo. Pili, kuzielewa kazi za mwandishi kunaweza kuwa njia bora ya kumuelekeza mhakiki kwenye wasifu wa mwandishi huyo. Katika sehemu hii tunatoa taarifa fupi kuhusu watunzi ambao kazi zao zinahakikiwa pamoja na muhtasari kuhusu riwaya zao.

**Mohammed Said Abdulla**

Mtunzi huyu anatambulika kama baba wa riwaya ya kiupelelezi katika Afrika Mashariki ( Ohly 1981, Syambo 1992, Madumulla 1988 na  Mbatiah 2016 ), kwa kuwa ndiye wa kwanza kutanguliza kipera hiki katika maeneo ya Afrika Mashariki. Kulingana na maelezo ya Syambo 1992 na Mbatiah 2016, Abdulla alizaliwa mwaka wa 1918 katika eneo la Makunduchi, Unguja Mashariki. Alilelewa katika utamaduni wa Waswahili na kusomea katika shule za kimishonari chini ya mfumo wa kikoloni. Ni kupitia elimu hii ya kikoloni alikopata athari za hadithi za Kimagharibi katika masomo ya shule ya msingi na ya upili. Alipomaliza masomo ya shule ya upili, aliajiriwa na

serikali ya kikoloni katika idara ya masuala ya Kiafrika. Taasisi za kikoloni ndizo pia zilizomsaidia kuandika na kuchapisha kazi zake za mwanzo. Kwa mfano, kamati ya usanifishaji wa lugha iliyoasisiwa miaka ya 1930 ilianzisha mashindano ya uandishi ambapo watunzi chipukizi wa Kiafrika walituma miswada yao kutathminiwa na kuchapishwa. Kufuatia juhudi za kamati hii, aliandika mswada wa *Mzimu wa Watu wa Kale* ulioshinda tuzo la kwanza. Mswada huu ulichapishwa mwaka wa 1958 kama riwaya yake ya kwanza ya kiupelelezi. Baadaye Abdulla alitunga riwaya zake sita ambazo zilisawiri migogoro mbalimbali kama vile masuala ya urithi, uanaharamu, dhuluma na utabaka. Katika utunzi wa kazi zake, inadhihirika kwamba ameathiriwa na watunzi wa Kimagharibi kama vile Arthur Conan Doyle. Mpelelezi wake, Bwana Msa kwa mfano, ana sifa nyingi za mpelelezi wa Conan Doyle, Sherlock Holmes. Tofauti kuu ikiwa mandhari ya kijiografia kwani riwaya za Doyle zinahusu mazingira ya Ulaya huku za Abdulla zikihusu mazingira ya Unguja. Pia alikuwa mhariri msaidizi wa majarida na magazeti kadhaa. Mohammed Said Abdulla alifariki mwaka wa 1991.

**Faraj Hassan Hussein Katalambulla**

Mwandishi huyu alizaliwa mwaka wa 1942 huko Igalula karibu na Tabora, Tanzania. Ni mtunzi aliyeibuka katika miaka ya 1960 alipoichapisha riwaya yake ya kwanza ya kiupelelezi, *Simu ya Kifo* ambayo aliandika bado akiwa mwanafunzi. Baada ya riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965), alichapisha hadithi nyinginezo ikiwemo riwaya ya *Pili PiliPili* (1976). Baadaye alianzisha gazeti liitwalo *Film Tanzania* alilotumia kuwasilisha tungo zake kwa wasomaji kwa njia rahisi zaidi. Riwaya zake zilisawiri hali halisi ya maisha baada ya uhuru hususan namna vyombo vya dola vilivyoshughulikia uhalifu. Kinyume na riwaya za Abdulla ambapo upelelezi unafanywa na mtu binafsi, katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, upelelezi unafanywa na polisi. Inspekta Far Katy Wingo anachunguza msururu wa vifo katika familia ya Mzee Jacob. Hata hivyo, mpelelezi wa kibinafsi, Bwana Tojo, anajitokeza baadaye na kuwasaidia polisi. Kupitia ushirikiano huu, upelelezi unakamilika na inabainika kwamba mhalifu alikuwa Agness akiwa analipiza kisasi cha wazazi wake waliouawa. Faraj Katalambulla alifariki dunia mwaka 2012.

**Elvis Aristablus Musiba**

Musiba alizaliwa katika kijiji cha Kiagata, Musoma mkoa wa Mara mwaka wa 1950 na kupata elimu ya msingi kuanzia 1957 na kujiunga na shule ya upili 1964-1968. Baadaye alihitimu elimu

ya juu kutoka vyuo mbalimbali na kupata shahada katika fani za uhasibu, utawala na biashara. Alifanya kazi katika mashirika mabalimbali ya kiserikali kama vile Baraza la Biashara la Afrika Mashariki. Aliandika riwaya za *Kufa na Kupona* (1974) *Kikosi cha Kisasi* (1979), *Njama* (1981), Kikomo 1980, *Hujuma* (1991) *Uchu* (2000) na *Hofu* (2002) ambapo aliibuka na mpelelezi, Willy Gamba. Riwaya ya *Hofu* inahusu njama za jeshi la Afrika Kusini ambapo jeshi hili lina kitengo maarufu kinachowasaka wanaopigania uhuru wa Afrika Kusini pamoja na mataifa mengine ya Kusini. Mwa Afrika. Willy Gamba pamoja na majasusi kutoka Zimbabwe na Kenya wanaungana kusimamisha njama hizo. Riwaya yake ya *Uchu* pia inaangazia upelelezi katika nchi ya Rwanda ambapo Willy Gamba anagundua njama za baadhi ya viongozi wa kiserikali wa mataifa jirani katika kuchochea vita baina ya Wahutu na Watutsi nchini Rwanda. Usomaji wa kimakinifu wa kazi za Musiba unaonyesha athari kubwa ya Kimagharibi hususan athari ya filamu za Kimarekani za James Bond katika ubunifu wa riwaya zake. Kulingana na gazeti la Arusha Times la tarehe 13/11/2010, Musiba aliaga dunia tarehe 31/10/2010.

**Ben Mtobwa**

Mtobwa alizaliwa mnamo tarehe 28, Agosti 1958 katika kijiji cha Ujiji, mkoa wa Kigoma, Magharibi mwa Tanzania. Mtobwa alianza kuandika akiwa katika kidato cha tatu katika shule ya upili ya Dodoma. Baadaye, alijiunga na chuo kikuu cha Dar es Salaam. Alifanya kazi katika kiwanda cha nguo na baadaye pamoja na rafikiye mmoja wakaanzisha gazeti la *MwanaHabari* ambapo waliendelea kuchapisha hadithi za watoto. Aliandika riwaya kadhaa, ya kwanza ikiwa ni *Lazima Ufe Joram* (1983) na riwaya ya mwisho ikiwa ni *Mtambo wa Mauti* (2004). Alihusika pia katika utayarishaji wa filamu kupitia kampuni ya *Heko* aliyoisimamia. Mtobwa ni mwandishi anayeitumia riwaya ya kiupelelezi kufichua njama za maadui wa Tanzania hasa makaburu wa Afrika Kusini. Kazi zake zinahusu mpelelezi Joram Kiango ambaye mara kwa mara husaidia polisi na kufanikiwa kuchunguza masuala yanayowashinda polisi, wakiwakilishwa na Inspekta Kombora. Mpelelezi wake, Joram Kiango, aghalabu anazuru mataifa mbalimbali katika kazi yake ya ujasusi pamoja na miji kama vile Nairobi na London. Hii ndio maana tumedokeza hapo awali kwamba riwaya nyingi za Mtobwa zinahusu upelelezi katika kiwango cha kimataifa.

**John Msimbe Simon Simbamwene**

Simbamwene ni mzaliwa wa Morogoro Tanzania mwaka wa 1949. Alifanya kazi kama msaidizi wa Maktaba ya Tanganyika Library Service, ambako aliweza kutumia nafasi hiyo kuandika riwaya zake.Ni mtunzi aliyeandama utunzi wa riwaya za kiuhalifu ambapo mpelelezi wa kibinafsi hajitokezi bali kazi ya uchunguzi inafanywa na polisi. Kazi zake zinahusu uhalifu unaotekelezwa ndani ya nchi kwa kutumia mabavu au mbinu nyinginezo kama vile njama baina ya wafanya kazi wa benki hasa makarani na walinda usalama. Lengo la uhalifu huo ni kujitajirisha haraka na kuishi katika maisha ya anasa. Katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa* (1972) kwa mfano, Rashid anamshawishi mpenzi wake, Salima, anayefanya kazi katika benki aibe kitita cha pesa ili watorokee mbali. Naye anafanikiwa kutoka nazo lakini polisi wanapofanya uchunguzi wao anajulikana kuwa ndiye aliyeziiba na wote Salima na Rashid wanatiwa mbaroni.

**Godfrey Levi Shimanyula**

Ni mtunzi wa riwaya za kiuhalifu na kiupelelezi kutoka nchini Kenya. Aliwahi kutunga vitabu vya watoto wa shule za msingi vingi kati yavyo vikitumiwa na wanafunzi wa darasa la saba na nane. Baadhi ya kazi zake ni *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975), *Fedheha ya Fedha* (1981) na *Mbegu za Chuki* (1981). Riwaya yake ya kwanza ilivuma sana miaka ya themanini kutokana na namna mtunzi alivyomsawiri nguli wa riwaya hii akipambana na genge la wahalifu wanaowahangaisha wakaazi. Suala la wizi wa benki unaofanywa na makarani wa benki wakishirikiana na wahalifu wa nje pia linaangaziwa. Riwaya zake zinahusu afisa wa polisi, Inspekta Kombo, ambaye pia ndiye mpelelezi akichunguza uhalifu mara tu unapofanyika. Katika msuko wa riwaya hii, mchakato wa upelelezi unachukua muda kidogo mno huku masuala ya kuwasaka wahalifu na kuwafikisha mahakamani yakipewa kipau mbele. Kimuundo kazi zake ni sahili mno kimsuko zikiwa na kurasa mia moja au chini ya mia moja, sifa zinazozifanya kusomeka kwa urahisi hasa na wasomaji wachanga. Levi anazihakiki riwaya zake katika dibaji kwa kuwa anatanguliza kwa kutoa adili kwa njia ya misemo. Kwa mfano, mwanzoni wazo anataja misemo ianayoakisi adili mbalimbali kama; uhalifu haulipi chochote na kikulacho ki nguoni mwako.

**2.8 Hitimisho**

Katika sura hii tumeonyesha kwamba riwaya ya kiupelelezi ina historia ndefu ya ukuaji kwa kutathmini vipindi mbalimbali vya kihistoria pamoja na maeneo tofautitofauti yanayohusishwa na

historia hiyo. Tumeonyesha kwamba kama zilivyo riwaya za aina nyinginezo, riwaya ya kiupelelezi ina mizizi yake katika fasihi simulizi. Tumetumia visa na vijihadithi kutoka maeneo kadhaa ya ulimwengu kuthibitisha vyanzo vya upelelezi katika fasihi simulizi. Ili kufanikisha maelezo ya kina kuhusu kuzaliwa na kusambaa kwa riwaya ya kiupelelezi katika maeneo mengi ya ulimwengu, utafiti huu umetalii ukuaji wa riwaya ya kiupelelezi katika Ulaya, Marekani, sehemu za Mashariki (India, Japani na Uchina), Afrika Kusini, Magharibi na Mashariki na kuonyesha hali ilivyo kwa sasa. Kwa kufanya mapitio haya, tumejaribu kuweka wazi ukweli kwamba riwaya ya kiupelelezi ni aina ya bunilizi ipatikanayo katika ulimwengu mzima na kwamba sifa za kimuundo zitakzochunguzwa katika sura zijazo, hazipatikani tu katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili bali pia katika riwaya za kwingineko ulimwenguni.

Tumeona kwamba ukuaji wa utanzu huu umepitia mabadiliko anuwai yakiwemo kutungiwa sheria za kuongoza utunzi wake katika kipindi cha urasimi, yaani miaka ya 1920-1930. Sheria na kanuni hizo zimekubalika na kutumiwa kama kiunzi muhimu cha nadharia ya riwaya ya kiupelelezi. Baadhi ya mabadiliko mengine yalihusu uibukaji wa waandishi wa kike pamoja na matumizi ya wapelelezi wa kike kinyume na hali ilivyokuwa kabla ya vita vikuu vya dunia ambapo jinsia ya waandishi wa kiume ilitawala. Hata vivyo, tumeonyesha kwamba riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, tangu kuchimbuka kwake miaka ya 1960 haijapitia mabadiliko mengi kama ilivyofanya riwaya ya kiupelelezi ya Ulaya na Marekani. Mageuzi mengine yalihusu kuchunguza uhalifu katika kiwango cha kimataifa ambapo watunzi waliwasawiri wapelelezi wao wakipambana na hali za ukiukaji wa sheria unaofanywa na nchi moja dhidi ya nyingine. Huu ni ujasusi wa kimataifa uliojitokeza mno katika kazi za Musiba na Mtobwa.

Utafiti huu pia umebaini kwamba riwaya ya kiupelelezi inatumiwa na watunzi kuendeleza baadhi ya itikadi zao kando na kutoa burudani kwa wasomaji. Waandishi wanazitumia kumulika maovu ya kijamii hasa mambo ya ukweli na ya siri yasiyozungumziwa na riwaya dhati. Kwa mfano, tumeona kwamba katika kazi za waandishi wa Afrika Kusini, suala la mabaki ya ubaguzi wa rangi limechukuliwa kwa uzito kuliko linavyooangaziwa kwingineko. Vivyo hivyo, riwaya za kiupelelezi kutoka India zinagusia mno suala la mgawanyiko wa kimpaka baina ya India na Pakistani pamoja na tofauti za kidini (Uislamu na Uhindu) kati ya mataifa hayo ambayo yalikuwa taifa moja awali. Katika Afrika Mashariki, riwaya za kiupelelezi hasa za Mtobwa na Musiba

zimeangazia uhusiano wa kimataifa baina ya Tanzania na Mataifa ya kusini mwa Afrika hususan kuhusiana na ukombozi wa kikoloni.

Kimuundo, imebainika kwamba waandishi wengi wamewatumia wahusika wale wale hususani mhusika mpelelezi, katika kazi zao ambazo aghalabu hujitokeza kiusanjari (series). Wengi wao wamewatumia wahusika wa kijozi ambapo wameandamanisha mpelelezi na msaidizi wake. Usimulizi unaendeshwa mara nyingi na msaidizi wa mpelelezi ambaye huifasiria hadhira vitendo na hulka za mpelelezi. Sifa bia zinazoonekana katika kazi za maeneo haya yote ni kuwa msuko wa riwaya za kiupelelezi huwa na taharuki, sadfa, misukumo pofu na taswira wazi za kimandhari miongoni mwa nyinginezo zinazoboresha sifa kuu ya kuvutia. Katika sura zijazo, tutachunguza mdhihiriko wa sifa hizo zaidi katika riwaya teule za Kiswahili.

# SURA YA TATU

## USIMULIZI KATIKA RIWAYA YA KIUPELELEZI YA KISWAHILI

### 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza suala la usimulizi katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili huku tukijibana katika vipengele vya sauti za kisimulizi na mtazamo. Kwa kuwa suala la mtazamo ni pana mno, tutachunguza pia sawia mbalimbali za mitazamo zipatikanazo katika riwaya teule. Hizi ni sawia za kiitikadi, kisaikolojia, kiisimu na sawia ya mwanda-wakati. Tunachunguza aina za sauti za kisimulizi, udhihirikaji wa msimulizi na dhima ya msimulizi. Mwisho, sura hii inachunguza dhana ya simulizi tegemezi na ujitokezaji wake katika riwaya za kiupelelezi. Ili kufanikisha utimizwaji wa lengo hili, tunatumia misingi ya kinadharia ya naratolojia na umitindo huku tukijikita katika mawazo ya wananadharia Rimmon-Kenan (2002), Leech na Short (1981), Simpson (1993, 2004) na Bal (2017). Urejeleaji wa kazi tofautitofauti za kinaratolojia unatufaa katika kutambua mabadiliko ya kiukuaji katika nadharia hii.

### 3.2 Sauti za Kisimulizi

Genette (1980:212) anaeleza kwamba mwandishi hawi msimulizi wa kazi yake bali huteua wakala wa kuisimulia hadithi. Ajenti huyo ndiye sauti ya kisimulizi. Sauti hiyo pia yaweza kuwa ya mmoja wa wahusika anayejulikana au wakala asiyejulikana. Wamitila (2002:38-38) anatambua aina tatu za sauti za kisimulizi ambazo ni: (a) Usimulizi wa nafsi ya kwanza ambao huwakilishwa na neno, ‘mimi’ au kiambishi ‘ni’ katika umoja au ‘tu’ katika wingi. Anafafanua kuwa msimulizi anayetumia sauti ya aina hii pia anaweza kuwa mshiriki katika masuala anayosimulia au akawa anayashuhudia tu. Tusomapo riwaya ya *Kufa Kupona* (2018) tunapata aina ya msimulizi anayeshiriki ambapo mhusika mpelelezi, Willy Gamba ndiye msimulizi. (b) Usimulizi wa nafsi ya pili unatambulishwa kwa matumizi ya kiwakilishi ‘wewe’ au ‘nyinyi’ ama viambishi ‘u’ na ‘m’. Hata hivyo huu ni mtindo wa kisimulizi ambao haujazoeleka sana na waandishi. (c) Usimulizi wa nafsi ya tatu ambao unaashiriwa kwa viwakilishi ‘Yeye’ au ‘Wao’ ama kwa kutumia viambishi ‘a’ na ‘wa’. Katika usimulizi wa aina hii, msimulizi anaonyesha umaizi wa kila kitu na kwa sababu hii anaweza kusimulia hata fikira za wahusika. Simpson (2004:77-78) anasema kwamba msimulizi wa nafsi ya tatu huwa nje ya hadithi (heterodaijesia) na kwa sababu hii anajitenga kiumbali na

msomaji kinyume na msimulizi wa nafsi ya kwanza (homodaijesia) ambaye ana uhusiano wa karibu na msomaji.

### 3.3 Udhihirikaji wa Msimulizi

Simulizi hudhihirisha kuwepo kwa msimulizi kwa viwango mbalimbali. Baadhi ya simulizi hudhihirisha uwepo wa msimulizi waziwazi ilhali uwazi huo unafifia katika baadhi ya simulizi nyingine. Chatman (1978:220) anaeleza kwamba kuwepo kwa msimulizi kunaweza kujitokeza kwanzia kiwango cha udhihirikaji waziwazi hadi kiwango cha kugubikwa kabisa. Rimmon-Kenan (2002:99) anasema kwamba kila simulizi ina ishara za kuwepo kwa msimulizi zikiwemo zile simulizi ambazo mazungumzo yametumika kwa kina hivi kwamba nafasi ya msimulizi inaonekana kugubikwa. Chatman anafafanua mbinu sita mbalimbali za kutambua uwepo wa msimulizi katika kazi za kifasihi na kuzipanga kulingana na viwango vya uwazi. Anazipanga kwa kwanzia kwa zile zisizo na uwazi hadi zile zenye uwazi zaidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

#### 3.3.1 Maelezo ya Kimandhari

Ufafanuzi wa mandhari huchukua nafasi kubwa katika kazi nyingi za kinathari. Kwa kawaida katika tamthilia, mandhari hutangulizwa mwanzoni mwa sehemu au onyesho na katika filamu mandhari huonyeshwa kupitia picha. Katika riwaya na hadithi fupi, maelezo kuhusu mandhari hutotelewa kupitia sauti ya msimulizi. Kuwepo kwa maelezo haya ni ishara ya kuwepo kwa msimulizi. Wamitila (2002:34) anaeleza kuwa mandhari ni sifa ya kiutanzu katika baadhi ya riwaya kama vile riwaya za kiupelelezi tunazohakiki katika tasnifu hii. Katika utanzu huu, mandhari huelezwa kwa sifa zisizokuwa za kawaida ili kuzidisha taharuki. Hii ni kwa sababu taharuki ni mbinu ya kiutanzu na kimtindo pia katika riwaya za kiupelelezi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mandhari ya shamba la Hakimu Marjani lililoko eneo la Kazole ambako mzee huyu alikuwa ameficha pesa zake yanaelezwa kwa njia inayodhihirisha uajabu wa eneo hilo. Mali hiyo ilikuwa imefichwa karibu na mto katika pango lililofunikwa kwa jabali. Pango hili nalo lilikuwa karibu na mti wa Mzeituni. Maelezo ya mandhari ni ishara ya kuwepo sauti ya kisimulizi inayofafanua mazingira yalivyokuwa huko shambani Kazole. Kuwepo kwa maelezo ya mandhari ni ushahidi wa kuwepo kwa msimulizi.

### 3.3.2 Utambulishaji wa mhusika

Msimulizi ndiye humpa msomaji maarifa fulani kumhusu mhusika fulani na kwa njia hiyo kuathiri namna msomaji anavyomwelewa mhusika huyo. Kwa hivyo, msimulizi anapotoa taarifa za kitambo anazozijua kumhusu mhusika, anasaidia kumtambulisha mhusika huyo kwa msomaji. Kwa kawaida habari hizo hutolewa mwanzoni mwa simulizi kabla ya msimulizi kuzigundua mwenyewe. Katika riwaya ya *Uchu* (2000:1) msimulizi anaanza kwa kumtambulisha mwenye nyumba ambapo wageni wa Umoja wa Wanaharakati wa Afrika (PAM) walikuwa wanakutana ili amuelewe vyema mhusika huyo. Msimulizi anaeleza hivi, 'Christopher Temu, ambaye Jumapili hii nyumbani kwake Arusha, alikuwa amefikiwa na ugeni kutoka sehemu mbalimbali za Afrika, alikuwa mwanachama wa chama hicho'. Katika dondoo hili, msomaji anapata habari kwamba Temu ni mwanaharakati, kwake ni Arusha na kuwa ni mwanachama cha PAM. Kwa njia hii, taarifa muhimu zinamfikia msimuliwa kupitia uwepo wa msimulizi. Utambulishaji wa mhusika pia unahusu ufichuzi wa historia yake ili kumsaidia msomaji kuelewa chanzo cha hali aliyoko mhusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*? msimulizi anampasha msomaji historia ya mhusika Von Iron hivi, 'Alihitaji kujua siri iliyoko katika ngozi hii nyeusi. Siri ambayo ilimfanya amkose mamake na babake.' Uk.125. Sinekidoki 'ngozi nyeusi' inaashiria itikadi ya ubaguzi wa rangi kutoka kwa Von Iron kwa msemewa.

Rimmon-Kenan anaeleza kwamba utolewaji wa habari hizi mwanzoni mwa hadithi hutokana na chukulizi kwamba msimuliwa hana habari hizo. Kwa sabahu hiyo, linakuwa jukumu la msimulizi kumjuza msomaji kile asichokijua. Katika mfano wa hapo juu, msimulizi anamfahamisha msimuliwa usuli wa Von Iron hususan kuhusiana na chuki yake dhidi ya watu weusi.

### 3.3.3 Maelezo ya Mpito wa Wakati

Kwa kuwa hadithi inaweza kuanza mwanzo, kati au mwishoni mwa ploti yake, uwepo wa maelezo ya namna hadithi hiyo inavyokwenda kiwakati ni ishara ya kuwepo kwa msimulizi. Maelezo haya huyajibu maswali yaliyomo akilini mwa msimuliwa kuhusu mianya ya kisimulizi iliyopo (Chatman, 1978:223). Katika riwaya dhati, msimulizi ndiye huamua ni kipi kisemwe kimuhtasari na ni suala lipi linafaa kuangaziwa kwa kina ili kueleza kuwepo kwa mianya mbalimbali ya wakati ambapo mambo fulani yalifanyika. Hata hivyo, katika riwaya za kiupelelezi, kama sheria ya kiutanzu, msimulizi analazimika kuficha baadhi ya mambo hadi mwishoni mwa riwaya ambapo mpelelezi hufafanua maswala tata yote. Maelezo ya ni nini kilifanyika, lini, na mhusika ni yupi

yanasaidia kuipunguza taharuki ya msomaji. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, kuna mwanda wa wakati mkubwa kati ya wakati Joram alipolipuliwa kwa bomu na wakati inapokuja kugunduliwa kwamba hakufa. Inaaminika kwamba alikuwa amekufa kwa kuwa viungo vya mwili vilionekana vikitawanyika katika vifusi vya jengo hilo. Pia vitu vingine kama vile fimbo yake pamoja na madevu yake bandia vilikuwa vimeokotwa lakini Joram mwenyewe hakuwa ameonekana. Ili kukidhi hamu ya msomaji kuhusu kupotea kwa Joram wakati huu, msimulizi anafichua kuwa kwa kipindi hicho, Joram alikuwa amejificha nyumbani kwa msichana aliyemwokota, Unono. Hii ni baada ya kumuokota kutoka kwa vifusi vya nyumba iliyobomolewa. Maelezo haya ya mianya ya wakati katika usimulizi ni thibitisho kwamba kuna msimulizi katika hadithi.

3.3.4 Tathmini ya kisimulizi

Msimulizi anaweza kuutathmini usimuliaji wake unavyotekelezwa ama kuyatathmini masuala anayosimulia. Katika baadhi ya kazi, msimulizi huanza kwa kuonyesha udhaifu wake katika usimuliaji hasa ukosefu wake wa tajriba ya usimuliaji. Hali hii hupatikana mno katika baadhi ya tenzi za Kiswahili. Katika riwaya, msimulizi hutumia mbinu tofauti kutathmini usimulizi na masuala mengine. Chatman (keshatajwa) anasema kwamba kuna mbinu tatu zinazoonyesha utathmini wa msimulizi. Kwanza, tathmini inaweza kudhihirika kupitia ufasiri wa suala fulani. Kulingana na Chatman ufasiri nao unaweza kutoa habari kuhusu mfasiri huyo au tukio linalofasiriwa. Kuwepo kwa mfasiri basi ni ishara kwamba kuna msimulizi. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* msimulizi analifasiri suala la uagizaji wa nguo kutoka nje ya Afrika Mashariki baada ya kulitathmini vazi la Neema. Msimulizi anasema, ‘Lilikuwa gauni la kitambaa chepesi ambacho ni dhahiri kilitokea nje ya Afrika Mashariki’. (Uk. 15)

Pili, kuwepo pia kwa hukumu tofautitofauti kuhusu tabia au hali fulani ni ishara nyingine kwamba kuna msimulizi. Maamuzi haya aghalabu huonyesha msimamo wa kimaadili wa msimulizi. Katika *Salamu Kutoka Kuzimu,* msimulizi anatoa uamuzi unaoonyesha kupendezwa kwake na mavazi ya Neema. Anamlimbikizia sifa anazozifahamu yeye kama msimulizi badala ya kumpa msomaji nafasi ya kuzigundua mwenyewe, jambo linalovuruga utobinafsi wake. Msimulizi anasema, ‘Macho ya mwanadada huyu yalikuwa na uzuri wa kipekee, uzuri wa kubembelezebembeleza, uzuri wa kishujaa’.uk.15 Hiki ni kinyume cha jinsi msimulizi huyu anavyomweleza Unono, msichana aliyemwokoa Joram kotoka kwa kifusi cha nyumba iliyolipuliwa. Msimulizi anasema,

‘Kimaumbile, Unono hakuwa na umbo la kuridhisha wala hakujidanganya kuwa ana sura nzuri. Vijana wa kiume walimwepuka kama jinni na kumtazama kama jinamizi’. Utolewaji wa hukumu kama hii ni ithibati kwamba kuna msimulizi anayewaona wahusika akiwa mbali na kumfafanulia msomaji sifa zao.

Mbinu ya tatu ni ujumlishaji. Hii ni aina ya tathmini isiyojikita katika mhusika, hali au jambo moja maalum, bali katika vikundi au jamii pana ya kibinadamu. Kuhusu tathmini ya kiujumlishaji, msimulizi, kama sauti ya mwandishi anatoa kauli za kijumla kuhusu hali fulani ya kimaisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, msimulizi anatoa baadhi ya kauli zinazoonyesha tathmini ya ujumla wa maisha na ambao ni ukweli unaoaminika na watu wengi. Mojawapo wa kauli hizi ni hii, ‘Duniani kuna vilima na mabonde, kuna kupanda na kushuka, kuna mashaka na raha’ uk.37. Kauli hizi zinaonyesha utathmini wa kijumla unaofanywa na msimulizi. Kauli kama hii pia inaashiria itikadi ya mwandishi kwamba hakuna hali inayodumu maishani. Maisha ni mabadiliko.

### 3.3.5 Ripoti Kuhusu kile ambacho hakikusemwa wala kufikiriwa

Hizi huwa ni habari ambazo mhusika hazitoi kwa msomaji kwa kuwa anazificha habari hizo ama yeye mwenyewe hazijui. Msimulizi mwenye uwezo wa kufichua habari kama hizi ni maizi ambaye ana uwezo wa kuzifikia fikira, majuto na hata matamanio ya mhusika fulani. Habari hizo zingebaki fiche kama msimulizi maizi asingalikuwepo. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965), hisia za ndani za Agnes kuhusiana na chuki yake dhidi ya mpelelezi Wingo, zinatolewa kupitia sauti ya kisimulizi hivi: ‘Agnes alikubali shingo upande. Daktari naye akawa amechukizwa kabisa na jambo hilo. Agnes hakupendelea kabisa mambo ya Inspekta’.Uk.86. Utolewaji wa maelezo yaashiriayo hisia na mitanziko ya kindani kama hii, ni ithibati ya kuwepo kwa msimulizi.

### 3.3.6 Tafsili ya Mhusika

Kinyume na utambulishaji wa mhusika ambapo msimulizi anatoa taarifa za awali anazozifahamu kumhusu mhusika, tafsili ya uhusika, inatoa maoni ya kijumla kumhusu mhusika ili kutilia mkazo zaidi wasifu wake. Tafsili ya mhusika hudhihirika zaidi ikiwa imetolewa na msimulizi mwenye mtazamo wa nje. Hii ni kwa sababu msimulizi wa aina hii si mshirika katika matendo ayasimuliayo na kwa sababu hii, anaweza kuaminika zaidi. Maelezo yatolewayo kwa njia hii, humwacha msimuliwa bila kuwa na nafasi ya kumtathmini tena kwa kuwa tayari tathmini imetolewa na

msimulizi kupitia mtazamo wa nje. Kuwepo kwa tafsili horomo ni ishara ya kuwepo kwa msimulizi. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, msimulizi anatoa sifa za kijumla kumhusu Waridi hivi, ‘Yu msichana mwenye sura nzuri, umbo zuri, mwendo mzuri na kila kitu kizuri’. Uk.4. Katika uelezaji huu, msomaji analazimika kwamini sifa hizi za Waridi bila kuzivumbua mwenyewe. Utoaji wa tafsili kama hii ni ishara kwamba kuna msimulizi katika hadithi hii. Udhihirikaji wa tafsili kama hii pia unaonekana kuhusiana na jinsi msimulizi anavyoieleza sura ya Unono. Msimulizi anasema, ‘Joram alitamani kumwachia kofi kali ambalo lingetua katika sura hiyo mbaya na kuirejeshea akili’. (uk.79). Katika dondoo hili, tunaona kwamba msimulizi anamjuza msomaji kijumla kuwa Unono ana sura mbaya na akili kidogo bila kumwacha msomaji atambue mwenyewe. Msomaji naye hana budi kwamini yasemwayo kwa kuwa hasa yanatolewa na msimulizi anayefahamu kila kitu. Kulingana na Chatman (1978:222-224), njia hizi sita ndizo hudhihirisha kuwepo kwa msimulizi, ambaye hujitokeza katika viwango mbalimbali vya uwazi. Kwa hivyo, njia hii ya tafsili ya mhusika ndio yenye uwazi zaidi katika udhihirishaji wa kuwepo kwa msimulizi huku ile ya kwanza ya maelezo ya mandhari ikidhihirisha ufiche zaidi. Katika sehemu ifuatayo, tunafafanua majukumu mbalimbali ya msimulizi ingawa kwa kiasi kikubwa, majukumu hayo yanaingiliana na mbinu tulizojadili hapo juu za udhihirishaji wa uwepo wa msimulizi.

### 3.4 Dhima ya Msimulizi

Jukumu la kimsingi la kuwepo kwa msimulizi katika hadithi ni kusimulia visa vya hadithi hiyo. Hata hivyo, uchunguzi wa mchakato mzima wa usimuliaji unaashiria kuwepo kwa majukumu mengine yanayotekelezwa na msimulizi. Genette (1988:255) anatambua dhima tano za msimulizi kulingana na mahusiano mbalimbali baina ya msimulizi huyo na hadithi yenyewe, mpangilio wa hadithi, mwelemeo wa mwandishi na mchakato wa usimuliaji wenyewe. Baadhi ya majukumu hayo ni:

#### 3.4.1 Dhima ya Usimuliaji

Hili ndilo jukumu kuu la msimulizi kwa kuwa pasipo na usimuliaji, pia msimulizi hawezi kupatikana. Ni kupitia kwake ndipo kazi ya kifasihi huweza kupangika na kupitishwa kutoka kwa mwandishi hadi kwa msimuliwa (msomaji). Katika jukumu hili la usimuliaji, msimulizi ndiye huamua ni visa vipi vipewe uzito zaidi na vipi visivyohitaji uzito sana. Ndiye anayeamua pia

namna visa hivyo vitakavyofuatana katika hadithi nzima. Katika riwaya tunazohakiki, usimulizi unafanywa kwa mtazamo wa nje ambapo msimulizi anaripoti mambo anayoyajua bila kushiriki. Hata hivyo aghalabu anajitenga kando na kuwapa wahusika kuuendeleza usimulizi kupitia mazungumzo yao.

### 3.4.2 Dhima ya Uelekezaji

Msimulizi ndiye huelekeza mawasiliano katika muktadha wa usimuliaji. Ndiye anayeyaelekeza mawazo ya msomaji kwenye suala husika, hali au mhusika fulani. Kwa mfano, katika mazungumzo, msimulizi ndiye anayemwelekeza msomaji kuhusu ni jambo lipi linalosemwa na mhusika yupi au kumwelekeza kutofautisha fikra na kauli za wahusika mbalimbali. Kwa mfano, kauli kama ‘alisema’, ‘alidai’, na ‘alifikiri’ aghalabu hutanguliwa na jina la aliyesema, aliyedai au aliyefikiri. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa*, kuna kauli hii, ‘Nilijua wazi kuwa utaniamsha, nami nilikuwa nikingoja ufanye hivyo,’ Salima alisema. Katika kauli hii, maneno ‘Salima alisema’ yana dhima ya kumuelekeza msomaji kwenye msemaji. Vilevile, ikiwa kuna visa ambavyo msomaji hakuvielewa vyema, msimulizi anamwelekeza msomaji kwavyo. Jukumu hili huwa wazi zaidi katika mashairi ya kiutenzi ambapo sauti ya msimulizi aghalabu husikika ikimrai msimuliwa kumfuata msimulizi kutoka mwanzo hadi mwisho. Hii ni kwa sababu tungo hizi huwa na msimuliwa bayana. Pia panapotokea mabadiliko katika msuko, mbinu kadhaa hutumika ili kumwezesha msomaji kumfuata vyema msimulizi. Kwa mfano, msimulizi mwingine anapoanza kusimulia, msomaji anatangulizwa kwake hasa kwa kutumia mbinu rejeshi. Fauka ya hayo, mabadiliko ya kimandhari yatokeapo, linakuwa ni jukumu la msimulizi kumwelekeza msomaji kwenye mabadiliko hayo. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa mfano, msimulizi anamwelekeza msomaji kuhusu mwendo wa Msa na Najum walipokaribia eneo la mzimu lenye mazingira ya kuogofya. Msimulizi anaanza kueleza namna walivyotembea njiani na mabadiliko ya mwendo wao pindi mazingira ya eneo hilo yanapobadilika. Msimulizi anaeleza:

> Walitembea kimya kimya kwa kitambo kidogo. Sasa wamefika katikati ya mzimu na hapo hapakuwa na miti kabisa. Najum alitazama inapata hatua mia kulikokuwa na makaburi marefu saba, yanapata futi kumi na tano kila moja. (Uk.37)

Katika mfano huu, msimulizi anaelekeza kuhusu hali ya mandhari ya kuogofya pamoja na jinsi wahusika walivyoathiriwa na mazingira hayo ili msimuliwa aipate taswira ya eneo la mzimuni. Kwa mfano anafafanua umbali wa makaburi kutoka pale wahusika walipokuwa (hatua mia moja)

kando na kumwelekeza msimuliwa kuhusu ukubwa wa makaburi yapatikayo hapo. Uelekezaji huu unaashiria kuwepo kwa kani fulani inayodhibiti mwendo wa simulizi. Kani hiyo ni msimulizi akitekeleza wajibu wa kuelekeza.

### 3.4.3 Jukumu la Kumshirikisha msomaji

Kwa mujibu wa Genette (1980:256), msimulizi huboresha hali ya mchakato wa usimuliaji kwa kujenga uhusiano baina yake mwenyewe na msomaji ambaye huweza kudhihirika wazi ama akawa hayupo. Kwa hivyo, jukumu hili hurejelea mwegemeo wa msimulizi kwa msimuliwa hususan kupitia namna anavyodumisha uhusiano wa kimazungumzo na msimuliwa. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* kwa mfano, msimulizi anamshirikisha msomaji kwenye kitendo cha usimuliaji kwa kumfafanulia mahali wapo (msimulizi na msomaji) na anapoenda mbali na msomaji, anamweleza msomaji kuhusu umbali huo ili wadumishe uhusiano bora. Katika riwaya hii, msimulizi anamuonyesha msomaji sehemu mbalimbali za mji pamoja na majumba yanayoendeleza biashara tofautitofauti. Anasema, '**Tu**ko Mburahati, mbele ya moja kati ya majumba ya aina hii. Ni majuzi tu Waridi alipotokea **hapa** Mburahati na kujipatia chumba'.uk.4. Katika nukuu hili, msimulizi anajileta karibu na msimuliwa ili amshirikishe kwa ukaribu kwa kutumia njia kadhaa. Kwa mfano, anatumia kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi '**Tu'** pamoja na kivumishi 'hapa' ili kuonyesha uhusiano wao wa karibu. Katika riwaya ya *Njama*, msimulizi anamshirikisha msomaji kwa kumzungumzia moja kwa moja hivi, '**U**naposafiri **u**sikae na watu ovyoovyo tu kwani wengine wana mikosi. Kama **wewe** hujui namna ya kuwatambua watu wenye mikosi basi nitafute siku moja nita**ku**nong'oneza'. uk.8. Kiashiria 'wewe' na viambishi vilivyokolezwa rangi vinaonyesha namna msimulizi anavyojileta karibu na msomaji ili kumshawishi zaidi.

### 3.4.4 Jukumu la Kutoa Ushuhuda

Jukumu hili hurejelea namna msimulizi hujenga uhusiano baina yake na hadithi yenyewe. Genette anafafanua kuwa dhima hii inahusu uwajibikaji wa msimulizi kimaadili na kiakademia. Hii ni kwa kuwa msimulizi anajukumika kukiri chanzo cha habari anazosimulia ili habari hizo ziweze kuaminika na msomaji. Katika kutekeleza jukumu hili msimulizi anaonyesha usahihi wa kumbukizi zake pamoja na hisia na matukio aliyoyashuhudia. Msimulizi anadhihirisha kuwa hatoi taarifa za uongo. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* msimulizi anatoa ithibati kuhusu hofu aliyo nayo

mpelelezi Far Katy Wingo. Msimulizi anaeleza kwamba mpelelezi aliposoma barua zilizoachwa na Marehemu Mzee Jacob, alipatwa na mshangao na mashaka mengi kwa kuwa upelelezi wake sasa ulianza kupatwa na utata. Msimulizi anasema kwamba, 'Baada ya kuisoma barua hii, Inspekta alikunja uso wake kwa chuki. Alikuwa na shaka kuwa barua ilimwongezea matatizo. Hakuielewa vizuri. Akaanza kufikiri'. Uk.44. Ni wazi kwamba katika muktadha huu, msimulizi anathibitisha chanzo cha habari ya kutatizika kwa mpelelezi kulikotokana na kufichuliwa kwa barua hizo kutoka nyumbani kwa Mzee Jacob. Katika riwaya ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* msimulizi anatumia ushuhuda uliotolewa na mkuu wa mashtaka kuonyesha chanzo cha habari za uhalifu anazotoa. Anaeleza kwamba wahalifu walikuwa wameshiriki katika wizi, mauaji na kupatikana na silaha kinyume cha sheria lakini anakiri kuwa ukweli huu unatokana na mahojiano (uk.62) ya kiongozi wa mashtaka kwa wahalifu, Dali, Rono, Karikenye na Mita.

### 3.4.5 Jukumu la Kuendeleza Itikadi ya mwandishi

Mahusiano ya msimulizi na hadithi anayoisimulia yanaweza kutuelekeza kwenye itikadi ya mwandishi kupitia tathmini anazotoa. Rimmo-Kenan (2003:84) anaeleza kwamba katika matini kunaweza kuwa na maelezo yanayoashiria kwenye itikadi fulani inayoungwa mkono ama kupingwa na mwandishi. Itikadi inayojitokeza katika riwaya za kiupelelezi inajikia katika misingi ya Kimaksi hususan kuhusiana na masuala ya dhuluma na utabaka. Rimmo-Kenan vilevile anaeleza kwamba katika matini kunaweza kuwa na itikadi kuu moja pamoja na nyinginezo ndogo ndogo. Itikadi hii kuu ndiyo hutumiwa kama msingi wa kutathminia itikadi zile nyinginezo ndogondogo zinazoweza kupatikana katika hadithi. Itikadi hizi ndogondogo huwa zimetegemezwa kwenye ile kuu. Katika riwaya za Mtobwa, msimulizi anatuelekeza kwenye itikadi ya mwandishi, kwamba anapinga dhuluma za kimataifa ambapo mataifa yenye nguvu za kiuchumi yananyanyasa mataifa dhaifu kiuchumi. Msimulizi anaichimuza itikadi hii kupitia dhamira za ubaguzi wa rangi, utegemezi wa misaada kutoka nchi za Ulaya. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, msimulizi anatuelekeza kuona jinsi mwandishi anavyopinga utegemezi wa misaada miongoni mwa mataifa huru ya Kiafrika. Anasema:

> Baada ya kuzitawala na kuzinyonya sana nchi zetu nyingi za Kiafrika, na baada ya 'kutoa' uhuru shingo upande, Uingereza iliendelea kujifanya baba na mama wa makoloni yake ya awali. Falsafa hii ndiyo chanzo cha visaada kadha wa kadha.(uk. 73)

Katika nukuu hilo hapo juu, toni ya kauli ya msimulizi inafichua kwamba msimulizi anawaelekeza wasimuliwa kwenye itikadi ya mwandishi kwamba mataifa yaliyotawala mataifa ya Afrika wakati wa ukoloni yangali yanaendeleza ukoloni mamboleo kupitia utoaji wa misaada ili mataifa hayo yaendelee kizitawala nchi hizo. Msimamo wake ni kuwa mataifa ya Kiafrika yanafaa kukatiza utegemezi wa kiuchumi ili yapate uhuru kamili. Suala hili la itikadi limefafanuliwa zaidi katika sehemu ya mtazamo katika sura hii.

Majukumu haya yana mwingiliano mkubwa kwa kuwa msimulizi huyaendeleza kwa pamoja. Pia hakuna jukumu linaloweza kutupiliwa mbali kwa kuwa yote ni muhimu. Hata hivyo, Genette (uk.256) anashikilia kuwa jukumu la kwanza la usimuliaji ndilo kuu na muhimu zaidi kwa kuwa pasi na usimuliaji ni vigumu msimulizi kuwepo. Tofouti katika udhihirishaji wa majukumu haya huweza kujitokeza tu kuhusiana na kiwango cha msisitizo kutoka kwa msimulizi. Kwa hivyo, katika riwaya za kijamii kwa mfano, msimulizi anaweza kusisitiza itikadi zaidi kuliko uelekezaji.

## 3.5 Mtazamo katika Usimulizi

Suala la mtazamo limefafanuliwa kwa njia tofautitofauti na wahakiki mbalimbali (Rimmon-Kenan, 2002, Simpson, 2004, Leech na Short, 2007, Bal, 2017). Kwa mfano, Rimmon-Kenan (2002:43) anaeleza kwamba mtazamo ni msimamo wa sauti ya kisimulizi kuhusu kinachosimuliwa. Anafafanua kuwa sauti hiyo huchukua nafasi kubwa kuhusu namna masuala yaliyomo katika hadithi yanavyopokelewa na wasomaji kwa kuwa msimamo wa msimulizi unaweza kuhawilisha maarifa, hisia na itikadi za msimulizi kwa msomaji. Rimmo-Kenan anafafanua kwamba mtazamo unaweza kujitokeza katika viwango kadhaa kama vile katka sawia ya kiitikadi na ile ya kisaikolojia. Hata hivyo, tutachunguza aina nyinginezo za mianda ya mtazamo kando na hizi mbili. Roberts (1995:73) anafafanua mtazamo kama msimamo wa msimulizi wa hadithi kuhusu falsafa ya mtunzi. Yaani, kwake mtazamo ni jinsi msimulizi anavyomwelekeza msomaji kwenye itikadi ya mwandishi. Tukitathmini maoni ya wahakiki hawa tunaona kwamba suala la mtazamo kuwa ni msimamo wa mtazamaji au msimulizi kuhusu yale yanayosimuliwa likisisitizwa. Pia Roberts anagusia suala la itikadi kama kijenzi cha mtazamo jambo ambalo pia Rimmo-Kenan analizungumzia. Genette (1980) pia, anatueleza kwamba kutathmini sauti ya usimulizi ni njia moja ya kutuelekeza kwenye suala la mtazamo. Njia ya pili ya kutathmini suala la mtazamo anayoizungumzia ni kuchunguza mwelekeo ambao hadithi inasimuliwa nao, msisitizo wake ukiwa katika umbali wa kimasafa baina ya msimulizi na

msimuliwa. Kwa hivyo, matukio yanaweza kuwa mbali au karibu na msimulizi. Kwa kutegemea umbali huu wa kimasafa, Genette anaeleza kwamba kuna aina mbili za mtazamo; mtazamo wa nje na mtazamo wa ndani. Kwa kuwa tumelishughulikia suala la sauti ya kisimulizi, katika sehemu iliyotangulia, tutazingatia zaidi dhana ya mtazamo katika sehemu hii. Yaani kuuchunguza mtazamo kwa kurejelea uhusiano wa kimasafa baina ya msimulizi na kisimuliwacho. Hii ni kwa sababu mtindo wa kurejelea sauti ya kisimulizi pekee una ufinyu unaotokana na ukweli kwamba riwaya za kiupelelezi tunazohakiki zote zinasimuliwa kwa nafsi ya tatu. Kwa hivyo, uchanganuzi wa mtazamo kwa kufuata uhusiano baina ya msimulizi na matukio ayasimuliayo unatupatia upana wa kuyachunguza masuala mengi yanayohusiana na mtazamo. Kwa kuyarejelea maoni ya Genette, hapa chini tunafafanua aina za mitazamo miwili:

### 3.5.1 Mtazamo wa Ndani

Aina hii ya mtazamo inahusishwa na usimulizi unaotumia nafsi ya kwanza. Msimulizi wa nafsi ya kwanza anaweza kuwa mmoja wa wahusika anayeshiriki katika matendo kama wahusika wengine ama akawa ni mtazamaji tu asiyeshiriki katika matendo hayo, kazi yake ikiwa ni kuripoti tu yale anayoyaona (Genette, 1980:189). Msimulizi huyu huwa na upungufu wa kutoweza kuyaona mengi kama vile fikira na hisia za mhusika. Hii ni kwa sababu anayoyaripoti hutegemea uwezo wa kuyasikia maoni ya wahusika wengine au kushuhudia vitendo vyao. Mtazamo huu wa ndani unaweza kukuzwa na msimulizi-mhusika mkuu au hata msaidizi wa mhusika mkuu. Hii ndio hali tunayoiona katika riwaya za kiupelelezi za Conan Doyle, ambapo msaidizi wa mhusika mkuu, Dkt.Watson ndiye msimulizi mshiriki. Katika riwaya ya kiupelelezi ya *Njama*, mpelelezi na mhusika mkuu, Willy Gamba ndiye msimulizi, na kwa hivyo msomaji anayaelewa maswala mengi kupitia mtazamo wa mhusika huyu. Kwa vyovyote vile, msimulizi mshiriki anaposimulia matendo ya mhusika mmoja hadi mwingine, ndivyo mtazamo wake kuwahusu au kuhusu hali nyingine unavyoendelea kujitokeza. Wamitila (2002:46) anataja ubora wa mtazamo wa ndani akisema kuwa ni rahisi kwa msomaji kujitambulisha na msimulizi wa nafsi ya kwanza kuliko msimulizi wa nafsi ya tatu. Anasema kwamba hii ni kwa sababu masafa ujumi baina ya msomaji na msimulizi ni mafupi kuliko yale yaliyomo baina ya msimulizi wa nafsi ya tatu na msomaji. Leech na Short (2007:213) pia wanasema kwamba usimulizi unaotumia mtazamo wa ndani unajenga uhusiano wa kibinafsi baina msimulizi na msomaji na kwa sababu hii, humshawishi zaidi msomaji kukubaliana na mtazamo wa msimulizi.

Katika riwaya ya *Njama* kwa mfano, msimulizi mshiriki, Willy Gamba anafanikiwa kumshawishi msomaji mara kadhaa ili aafikiane na mtazamo wake. Anafanya hivyo kwa kumwelezea baadhi ya mambo moja kwa moja. Kwa mfano, kuhusiana na talanta yake ya kuwavutia wasichana warembo, Willy anaongea na msomaji kana kwamba wako pamoja hivi, 'Na**ku**ambia mimi nilizaliwa na bahati ya kuelewana na hawa watoto wa kike, maana ni mara chache sana kunichenga; sijui **wewe mwenzangu** vipi?'. Uk.9. Maneno yaliyokolezwa wino na kiambishi 'Ku' yanaonyesha jinsi mtazamo ndani kupitia msimulizi wa nafsi ya kwanza unavyofanikiwa kumleta msimulizi na msomaji karibu.Kauli hii ya mpelelezi Gamba ni ishara kuwa mwandishi wa riwaya ya *Njam*a ameathiriwa na mtindo wa Kimarekani wa 'Hard-boiled detective fiction' ambapo mpelelezi katika kazi hizo husawiriwa akiwa na wasichana wengi warembo.

3.5.2 Mtazamo wa Nje

Simpson (2004:22) anafafanua kwamba mtazamo huu ujitokeza katika hadithi zinazosimuliwa kupitia msimulizi wa nafsi ya tatu. Kwa njia hii, msimulizi si mmoja wa wahusika bali yuko nje ya matukio. Yeye hutazama na kutoa maoni akiwa nje. Viwakilishi 'Yeye' au 'Wao' husheheni katika simulizi za aina hiyo. Pia viambishi 'a' au 'wa' hutumika mno kwenye vitenzi. Simpson anafafanua kwamba kuna aina tatu za mtazamo wa nje; Kwanza, kuna msimulizi maizi, ambaye hujua kila kitu, huwa kila mahali na mwenye nguvu za Kiungu kwa kuwa yeye anaweza kuripoti chochote wakati wowote. Umaizi wa msimulizi wa nafsi ya tatu pia hudhihirika kutokana na uwezo wake wa kuingia katika fikira za mhusika na kufichua hisia na matamanio yake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, uwezo huu wa kiajabu wa msimulizi maizi unajitokeza kupitia ufichuzi wa fikira unaotuelekeza kwenye hali ya kisaikolojia ya mhusika. Msimulizi anasema:

> Lakini akilini hakuwa na utulivu wowote. Kichwa chake kilikuwa kazini kikitafakari matukio yote yaliyopita na yajayo. Aliukumbuka kwa uchungu mpango wake madhubuti ambao aliuandaa kwa gharama kubwa na muda mrefu. (uk.88)

Katika kifungu hiki, uwezo wa mtazamo nje unadhihirishwa kupitia namna msimulizi anavyoyaeleza mawazo yanayomsumbua mhusika akilini. Haya ni mawazo ya Proper akiwaza kuhusu mpango wake wa kuyaharibu mataifa mengi ya Kiafrika kwa kuwaua marais kadhaa.

Msimulizi anaonyesha mambo ya kitambo na yajayo yanayomsumbua Proper. Kupitia mbinu rejeshi, ni wazi kwamba mhusika huyu alikuwa amepanga jambo ambalo lilimwachia uchungu.

Aina ya pili ya usimulizi wa nafsi ya tatu ni msimulizi maizi kihusika. Huyu pia ni msimulizi wa nafsi ya tatu na mwenye kiwango kikubwa cha ujuzi na maarifa lakini ujuzi huo huelekezwa kwa mhusika mmoja tu. Yeye hukita utazamaji na maelezo yake kwenye matendo, hisia na fikira za mhusika mmoja, aghalabu mhusika mkuu. Wakati huo huo, msimulizi huyu hueleza machache mno kuwahusu wahusika wengine. Kwa mfano, katika riwaya ya *Uchu*, msimulizi anatoa maelezo mengi kumhusu mpelelezi Willy Gamba, ikiwemo asili ya familia yake, na kutoa taarifa chache kuwahusu wahusika wengine. Tatu, kuna msimulizi maizi horomo. Katika mtindo huu, msimulizi haingizi maoni yake kumhusu mhusika au hali fulani bali hueleza ukweli ulivyo na kuwapa wasomaji nafasi ya kutathmini sifa za wahusika na hali mbalimbali wenyewe. Msimulizi maizi horomo hafanyi jaribio lolote la kufafanua wala kufasiri fikira za mhusika bali hujibana kwenye sifa za kuonekana au kusikika za mhusika au hali fulani. Kisurulia (2012:39) anasema kwamba mtindo kama huu ni bora katika hali ambapo maoni ya msemaji hajahitajiki kama vile katika kortini au katika utangazaji.

Ndani ya mitazamo hii miwili, kuna sawia mbalimbali za mitazamo. Simpson (2004) na Rimmon-Kenan (2002) wanazungumzia aina nne za mtazamo kama walivyofanya Uspensky (1973) na Fowler (1986). Hata hivyo, uchanganuzi wa Simpson unaegemea kwenye isimu zaidi kuliko fasihi. Hivi ni viwango ambavyo kwavyo suala la mtazamo huweza kudhihirika. Sawia hizo ni; (a) Mtazamo katika sawia ya kiitikadi.(b) Mtazamo katika sawia ya kiwakati.(c) Mtazamo katika sawia ya kimwanda na (d) Mtazamo katika sawia ya kisaikolojia. Leech na Short (2007) wanakubaliana na uainisho wa mtazamo katika viwango hivi vinne lakini wanaongeza aina ya tano ya sawia ya kijamii, ambayo hurejelea uhusiano wa kijamii baina ya mhusika ambaye mtazamo wake unaelezwa, na wahusika wengine.

#### 3.5.2.1 Mtazamo Katika Sawia ya Kiisimu

Kulingana na kielelezo cha Uspensky (1973:17), mtazamo hudhihirika katika kiwango cha lugha wakati ambapo msimulizi anapotumia usemi usiokuwa wa moja kwa moja au anapotumia njia nyinginezo kadhaa kufafanua sifa mbalimbali za wahusika. Kwa mfano, mhusika anaweza kuelezwa kupitia mtazamo wa mhusika mwingine, kupitia mtazamo wa msomaji au kutokana na

nafsi nyingine ya tatu. Anafafanua kwamba njia maarufu ya kuudhihirisha mtazamo ni majina ya wahusika. Majina kando na kuwa nembo ya ujitambulishaji wa wahusika, yanaweza pia kutumiwa kuonyesha mtazamo wa msimulizi au hata mtazamo wa mhusika kumhusu mhusika mwingine. Kwa mfano, katika kazi za kinathari, mhusika mmoja anaweza kuelezwa kwa njia mbalimbali na wahusika tofouti, kila njia ikionyesha mtazamo wa msemaji kwa msemewa. Wahusika wanaweza kuliumba jina kwa kulifinyanga kwa njia kadhaa kama vile kulirefusha, kulifupisha au hata kwa kutumia herufi kulisimamia jina zima. Pia jina halisi linaweza likabadilishanwa na lile la kilakabu kulingana na mahusiano ya wahusika. Kwa mfano, katika *Duniani Kuna Watu*, mhusika Kasim anarejelewa mara kadhaa na dadake kama Kaka K. Urejeleaji huu unatuashiria uhusiano wa kindugu baina yao na hasa namna Selume anavyomjali ndugu yake wa kiume. Kwa mfano, Kasim anapomuomba Selume ampe pesa za kuchezea kamari, Selume anakiri kwamba kila wakati Mungu anapomjaalia kuwa na pesa atakuwa anampa Kasim. Selume anasema, 'Nasikia Kaka K. Tuombe Mungu niwe ninazo tu, na wakati ukija kutaka, nikupe. Ahsante sana.'uk.15. Hata Kasim anapokuwa mkali na kumkemea Selume kwa kutembea mjini na kuzuru majumba ya sinema, Selume hakasiriki bali anamjibu tu kiupole, 'Sasa Kaka K, unapenda nitawe nyumbani tu, nisitoke nje?'uk.16. Katika mazungumzo yao inabainika kwamba Selume anamdhamini Kasim na kumpenda ndio maana anamwita Kaka K kinyume na jinsi Kasim anavyomchukulia dadake huyo. Kwa hivyo, kupitia namna Selume anavyolitumia jina la ndugu yake, msimuliwa anaweza kutambua mtazamo wake Selume kwa Kasim.

Ufupishaji wa jina la mhusika ni njia nyingine inayoweza kutuelekeza kwenye mtazamo wa msemaji. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, ufupishaji wa jina la mhusika pia unafanyika ikiwa ishara kuwa watu wanaolitumia jina hilo fupi wanavutiwa naye au wana uhusiano wa karibu. Kwa mfano, Juma Jeuri anamwita Sichana kwa kifupi, Sicha (uk.27). Naye Sichana pia analifupisha jina Juma Jeuri na kuwa Jeejee. Hili ni dhihirisho la uhusiano wa kindoa baina yao. Katika riwaya hii pia, majina ya Amanullah na Mwanatenga yanafupishwa na kuwa Manu na Tenga mtawalia kuonyesha uhusiano wao wa kimapenzi hasa baada ya kuoana. Msa pia anawaita hivyo kuonyesha kwamba anawatakia mema katika maisha yao ya ndoa. Hitimisho hili linatokana na kweli kwamba mtazamo hutegemea na kusudi la mhusika alitumialo jina kwa njia hii. Kisurulia (2012:56) anasema kwamba utumiaji wa majina yaliyofupishwa ni njia ya kuonyesha uhusiano wa karibu baina ya makundi ya watu kama vile watu wa rika moja au baina ya wapenzi. Mkakati huu pia hutumiwa kudumisha uhusiano mwema baina ya mahirimu. Hii ndio hali tunayoiona katika

mfano tuliotoa hapo juu wa jina Juma Jeuri kufupishwa na maharimu wake na kuwa Jeejee au Mwanatenga kuwa Tenga.

Kando na ufupishaji wa majina ili kuonyesha mtazamo, jina pia linaweza kurefushwa au kubadilishwa hata kimatamshi. Katika *Duniani Kuna Watu*, Kasim analibadilisha jina la babake na kulitamka kwa njia inayoonyesha ukosefu wa heshima na mtazamo hasi kumhusu. Anamwita Baa Mkubwa badala ya Baba. Ili kuthibitisha kwamba hili ni jina la kuchukiza, Selume anamuuliza Kasim, 'Ndo adabu gani hizo za mtoto kumwita mzee wake baa? Uk.13. Kwa kuwa Kasim hana heshima kwa babake, anaendelea kulitumia jina hilo huku akifahamu kuwa linamuudhi dadake, Selume. Anapolitumia tena katika muktadha mwingine, Selume anamkosoa vikali akimkumbusha Kasim kwamba mtoto hafai kumwita babake hivyo. Selume anapomwambia aende kwa baba akamwombe pesa, Kasim anamjibu, 'Ah Baa Mkubwa yule!'Uk.35. Kuonyesha kuwa Kasim amefanya uteuzi mbaya wa maneno ya kumrejelea babake, Selume anashangaa, 'Kaka K, unamwita baba Baa Mkubwa? uk.35. Baada ya muda kidogo Kasim anafafanua sababu za kumwita hivyo kuwa ni kutoachiwa mali kama msimamizi na mtawala, akiwa na nia ya kuyapora mali hiyo katika kamari na pombe. Kasim anafichua waziwazi baadaye kuwa hampendi babake, anaposema, 'Huyo si baba tena, amekuwa baa mkubwa'.uk.16. Kwa hivyo, Kasim anaposisitiza tofauti baina ya 'baba' na 'baa mkubwa' anaonyesha mabadiliko ya mtazamo wake kwa babake; kuwa awali babake alipokuwa na nguvu na afya nzuri, Kasim alimheshimu lakini sasa kwa kuwa amezeeka hastahiki heshima.

Majina ya kilakabu pia huweza kutumika kuashiria mtazamo wa msemaji. Kwa kuwa haya ni majina ambayo mtu anapewa na wengine, wanaompa jina ndio huamua maana za lakabu hiyo na kwa njia hiyo kudhihirisha mtazamo wao kumhusu anayeitwa. Hata hivyo, mtu anaweza pia kujipa jina la kilakabu ili kusisitiza sifa fulani anazopenda. Kisurulia (keshatajwa) akikubaliana na hali hii anaposema kwamba jina la kilakabu huweza kutumika kuonyesha maamuzi wahusika waliyo nayo kuhusu tabia za mrejelewa. Lakabu inaweza kuashiria sifa hasi au chanya za mrejelewa, hivyo kuthibitisha ikiwa wanaompa jina hilo wanachukizwa au kupendezwa naye. Katika *Duniani Kuna Watu,* tunaona Selume akimwita Saleh, mfanyikazi wa nyumbani kwao kwa jina, 'Bwana Mfanyikazi' badala ya jina 'boi' ambalo Saleh anajiita, ishara kwamba anavutiwa na juhudi zake kazini. Katika maongezi baina ya Saleh na Selume, msimamo wa mwandishi kuhusu kazi unajitokeza. Nao ni kwamba mtu ni kazi na kwamba yule anayefaa kujidharau ni yule ambaye

hafanyi kazi. Selume anasema, 'Vipi wewe mtu mfanyakazi ujidharau nafsi yako kuwa wewe unafanya kazi? Mtu wa kudharauliwa ni yule mtembezi, mtukufu asiyefanya kazi'. Uk.28.

Kama tulivyodokeza hapo juu, lakabu pia inaweza kuelekeza kwenye mtazamo hasi wa mtumiaji wa jina hilo kwa anayepewa. Kwa mfano katika *Kisima cha Giningi* (uk.22), babake Mwana wa Giningi anapompa Mwana wa Giningi wosia kuhusu namna ya kuishi na Ali Makame, anamuonya kujihadhari naye kwa kuwa ni mtu mwenye tamaa kubwa ya mali. Anamwita Ali Makame, 'Sumu Baridi'. Kupitia urejeleaji wa aina hii, babake Mwana wa Giningi anadhihirisha kwamba hampendi ndugu yake kwa sababu ni mwovu.

Njia nyingine idhihirishayo mtazamo wa msimulizi au mhusika katika ngazi ya kiisimu ni mwingiliano wa kauli za wahusika au kuchanganyika kwa kauli za msimulizi na zile za mhusika. Hali hii hufanyika pale ambapo, katika maandishi na pia katika usemi, mhusika anatumia kauli zilizosemwa na mhusika mwingine awali katika hadithi hiyo au katika kazi nyinginezo za kisanaa. Kauli hizo zitokazo kwingineko huweza kuingilia usemi wa mhusika na kujitokeza kama maneno yake. Kwa njia hiyo, kauli hizo zinaashiria mabadiliko ya mtazamo wa msemaji kuhusu jambo au hali fulani. Kwa mfano, kauli za kidini zitokazo katika Kurani au Bibliani zinaweza kutamkwa na mhusika kana kwamba ni maneno yake mwenyewe. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, msimulizi anafafanua namna mzee Hakimu Marjani alivyokuwa mtu karimu kwa watu wote, lakini watu hao wakautumia wema huo wake kumlaghai. Msimulizi anasema:

> Mkono wake ulikuwa wazi. Hamwendei mtu mwenye haja akamwambia **'Njoo Kesho'**…Kwa tabia hii yake kuna watu waliokuwa wakimkaramkia bwana huyo kwa kumlaghai na kumghilibu ili wapate wao, na yeye hayatii moyoni hayo wala habari hapati. Leo hii kaondoka; '**Kwa Mungu ndiko tutokako na ndiko turejeako'**. (Uk.39)

Katika nukuu hili, maneno yaliyo katika herufi nzito,si ya msimulizi bali yametokana na kauli zitokako kwingine. Kauli, 'Njoo Kesho' kulingana na mtazamo wa msimulizi ni usemi unaotumiwa katika diskosi pana ya wanajamii, hasa watu wasiotaka kuwakopesha wengine ilhali kauli ya pili, ina asili katika dini ambayo msimulizi anatumia kuhitimisha hali ya maisha ya mzee Hakimu Marjani. Kauli ya kwanza pia inaonyesha mtazamo wa msimulizi kwamba anachukizwa na watu wenye mkono birika huku akionyesha kupendezwa na ukarimu wa Hakimu. Mwingiliano wa kauli za msimulizi, kauli ya watu wanaokataa kukopesha na kauli ya kidini, zinaashiria

mabadiliko ya mtazamo wa kiitikadi wa msimulizi. Katika muktadha huu, kuna kuingiliana pia kati ya mtazamo wa kiisimu na ule wa kiitikadi. Itikadi inayojitokeza hapa inahusu asili ya maisha kwamba Mungu ndiye asili ya maisha na ndiye hatima ya maisha.

Vilevile katika mazungumzo, hasa katika tamthilia ni rahisi kwa mhusika 'kuyakopa' maneno ya mhusika mengine na kuyatumia kama yake. Kwa njia hii, anaishia kuonyesha kukubaliana au kuathiriwa na mtazamo wa msemaji wa awali. Hali hii pia inaweza kudhihirika katika mazungumzo baina ya wahusika katika riwaya za kiupelelezi tunazozichunguza. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, Selume anaathirika na maneno ayatumiayo Saleh kujieleza na kuanza kuyatumia mwenyewe kama yake. Kwa mfano, wakati Saleh anapojiita 'boi', 'kabwela' (uk.29) na mfanyikazi wa nyumbani asiyestahiki kumuoa msichana wa kitajiri, Selume anayatumia maneno yayo hayo kuonyesha kuwa Saleh, ingawa ni mwajiriwa ana haki ya kuoa na kumpenda binti ya tajiri, bila kuchukuliwa kwamba anasukumwa na tamaa ya pesa. Salume anamwambia, 'Sasa basi **Bwana Mfanyakazi,** Bwana **Kabwela** kweli kweli unapenda kuoa **binti wa kitajiri?**'. Uk.29. Maneno yaliyokolezwa wino si ya msemaji bali ameyatumia maneno yaliyozungumzwa hapo awali na Saleh mwenyewe akionyesha kujidharau kwa kuwa yeye ni mfanyikazi wa nyumbani. Alijiita kabwela na mfanyikazi asiyestahili kumuoa binti wa kitajiri kama Selume. Selume anapotumia maneno haya, mtazamo wake na ule wa Saleh unaingiliana lakini (Selume) anamkosoa akifafanua kwamba tofauti hizo za kitabaka hazifai kuwazuia yeye na Saleh kuoana.

Mwingiliano wa kauli za wahusika unapatikana pia katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*. Amanullah alikuwa ameota ndoto ambamo aliona mtu akimjia na kumwambia, 'Nenda Darsalama mafanikio yako yako Darsalama'. Baadaye, mwishoni mwa hadithi, Msa anayatumia maneno yaya haya kumpa Amanullah wosia kwamba anapoota ndoto na ikamshughulisha sana asimusimulie yeyote bali apeleleze ajue ni nini kinaweza kutokea. Msa anamwambia hivi:

> Umeona ukweli wa ndoto yako uliyoota Emmanuel? Unaambiwa, '**Nenda Darsalama, mafanikio yako, yako Darsalama**.' Umekwenda Darsalama, umerudishwa mbio mbio, uje huku uwe mwana kindakindaki, baba yako anakutaka, na mamako anakutaka. Ukiota ndoto ikakushughulisha kwa kuiona kuwa ina maana sana, usipendelee kuisimulia; ukisimulia, unaiharibu… (uk.123-124)

Katika dondoo hili, Msa anatumia maneno, 'Nenda Darsalama, mafanikio yako, yako Darsalama' yaliyosemwa na Amanullah mwanzoni mwa hadithi kuhusu ndoto aliyoota na ambayo ilimpa msukumo wa kusafiri hadi Dar es Salaam ili kumtafuta babake, yanatuonyesha mtazamo wa Msa kuhusu umuhimu wa kuhifadhi siri. Pia maneno haya yanaashiria kuwa Msa anakubaliana na mtazamo wa Amanullah kuhusu ufasiri wa ndoto na safari hiyo iliyotokana na ndoto hiyo; kwamba ilifaa. Msa anaelekea kuhitimisha kwamba adui za mtu wanaweza kuyatumia maono yake kujitajirisha wao pekee. Kama vile Amanullah alivyonyimwa haki yake na walezi wake, Twajuana Binti Abdalla na Sikudhani Binti Abdalla, waliopewa jukumu la kuhifadhi urithi wake ili kumpa atakapokuwa mtu mzima.

Baadhi ya wageni wa kutoka bara Asia na Ulaya waliomo katika miji ya Afrika Mashariki wanatumia lugha zao badala ya kujifunza lugha ya wenyeji. Wanapojaribu kukitumia Kiswahili, wanapachika maneno ya kigeni pamoja na lafudhi zao. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, tunashuhudia hali kama hii pale Mwarab Ali Abri anapoenda kwa polisi kuripoti mauaji ya Mwana wa Giningi. Mwanzo anaeleza kwa Kiingereza lakini baadaye anapolazimishwa kueleza kwa kina anafafanua mwanzo hadi mwisho wa matukio kwa Kiswahili fasaha. Hii ni ishara kwamba, alikuwa na uwezo wa kuwasiliana kwa Kiswahili. Anasema,

> Well Spekta,..hata sijui nisemeje. Nimekuja hapa kumleta misesi yule pale kutazama kile well yenu maarufu, kumbe imekuwa safari yetu imekill two birds…Too bad. Too bad! (uk.63)

Katika dondoo hili, Ali Abri anafahamu hata misemo na nahau za Kiingereza lakini misamiati na sarufi yake ya Kiswahili inaashiria mtazamo wake hasi kuhusu Kiswahili. Ikiwa ameishi katika Unguja kwa miaka mingi vipi ashindwe kuwasiliana kwa lugha ya eneo hilo? Kwa hivyo, kando na kutuelekeza kwenye mtazamo wa msimulizi kuwahusu wageni, pia mtazamo wa wageni kuwahusu wenyeji na lugha zao unajitokeza kupitia kauli hizi za wageni hawa.

3.5.2.2 Mtazamo Katika Sawia ya Mwanda-Wakati

Mtazamo huu unahusu namna uhusiano baina ya msimulizi, msomaji na simulizi inavyohisika kutegemea wakati na mahali alipo msimulizi (Rimmon-Kenan, 2002:77). Rimmon-Kenan anafafanua kwamba vipengele vya wakati na mahali vinaweza kuathiri namna habari zinazosimuliwa huweza kufasiriwa. Simpson (1993:12) anaeleza kwamba mtazamo wa kimahali

hurejelea alipo msimulizi anapoisimulia hadithi. Anaeleza kuwa uhusiano baina ya alipo msimulizi kama mtazamaji na masuala ayasimuliayo ni sawa na uhusiano wa anavyosimama mpigaji picha na kamera yake. Kwa hivyo, msomaji anaweza kuwasilishiwa matukio, wahusika na visimuliwa viingine kwa njia inayompa taswira ya umbali au ukaribu kama zilivyo picha za filamu.

Kulingana na Simpson (1993:10), msimulizi anaweza kuwa nje ya hadithi hivyo kumwezesha kutoa utazamaji wa kijumla au akawa mtazamaji aliyewekewa mipaka. Aina ya kwanza inamhusu msimulizi mwenye uwezo mpana wa kutazama kila kitu. Hii ndio maana Uspensky (1973:63) anauita usimulizi huu, 'Usimulizi wa jicho la ndege.' Uspensky anaendelea kufafanua kwamba aina hii ya usimulizi aghalabu hupatikana mwanzoni na mwishoni mwa hadithi. Naye Rimmon-Kenan anauita usimulizi wa aina hii, 'Usimulizi wa kipanorama'. Anaeleza kuwa usimulizi kama huu umuwezesha msimulizi kuyaeleza mambo yanayotendeka kila mahali. Yaani msimulizi anaweza kutazama na kuyaeleza yatendekayo yakiwa mbali au ya karibu. Nayo aina ya pili, ambayo ni utazamaji wenye mipaka, kulingana na Uspensky hujitokeza wakati usimulizi unapofanywa na mhusika mmoja katika hadithi. Uspensky anasema kwamba huyu ni mhusika anayembeba msimulizi na kwa sababu hii, msimulizi humfuata mhusika huyo kila mahali aendapo.

Wamitila (2002:47) anaeleza kwamba kuna vielekezi vya kilugha vinavyotumiwa kudhihirisha mwanda-wakati. Kuna viashiria na vielezi vya kimahali vinavyoelekeza kwenye uhusiano uliopo baina ya mahali alipo msimulizi na kile anachokisimulia. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, mwandishi anaonyesha mtazamo huu kupitia viashiria hivi:

> Kukawa kumekucha vizuri siku ya pili yake baada ya kifo cha Mzee Jacob. Inspekta Wingo hakuchelewa kufika kufanya upelelezi zaidi **kule Rufita Street**. Akawakuta watu wengine wamejazana **pale.** Inspekta Wingo akaingia **mle ndani. (**uk.11)

Viashiria vilivyokolezwa wino katika dondoo hilo hapo juu, vinatuelekeza kwenye mwendo wa msimulizi akimfuata mhusika katika hatua mbalimbali azifuatazo. Anamfuata Inspekta Wingo katika upelelezi wa mauaji ya Mzee Jacob kiwakati na kimahali. Kwanza, kiashiria 'Kule' kinatuonyesha umbali wa msimulizi na mahali ambako mpelelezi yuko, kisha umbali huu unafupishwa na kuwa karibu kiasi, ishara kwamba msimulizi anamfuata mpelelezi. Msimulizi anaashiria mwendo huu anapotumia kiashiria 'Pale'. Masafa ya kimahali yanafupishwa hata zaidi msimulizi anapotumia kiashiria 'Mle ndani'. Hii ni ishara kwamba msimulizi amekuwa akimfuata

msimulizi kwa hatua kutoka mbali hadi anapokaribia kuingia katika nyumba ya Mzee Jacob. Kwa hivyo, mtazamo wa msimulizi umekuwa ukibadilika kutoka utazamaji wa mbali hadi wa karibu, unaoashiriwa na kiashiria 'mle ndani'. Kiashiria hiki kinaonyesha uhusiano wa karibu baina ya msimulizi na kinachosimuliwa kwa kuwa tayari msimulizi amempeleka msomaji katika eneo halisi la mauaji na ambalo pia linafanyiwa upelelezi. Baada ya mpelelezi inspekta Far Katy Wingo kuingia ndani ya nyumba ya Mzee Jacob, msimulizi pia anaonyesha kumfuata mhusika huyu zaidi kwani anazidi kuyaeleza yaliyotokea mle ndani. Katika maelezo hayo, anatumia viambishi vinavyoonyesha msururu wa vitendo na viashiria vya ukaribu zaidi. Msimulizi anaeleza hivi:

> A**ka**andikandika ushahidi wake **mle,** a**ka**maliza. Hakuendelea kuwaulizauliza **wale** wanawake watatu juu ya mambo ya jana, wakati ule. Basi Inspekta a**ka**amua kuwachukua mpaka ofisini kwake. Wanawake **hawa** wakawa wanaingizwa ofisini kwa zamu. (Uk.11).

Kiashiria 'hawa' kinatudokezea kwamba msimulizi hasimami mahali pamoja bali anabadilisha mahali anapotazamia masuala anayosimulia. Anamfuata msimulizi kutoka mbali, wote wawili wanafika Rufita Street, wanaenda nyumbani kwa Mzee Jacob na kisha katika ofisi ya mpelelezi ambapo anawahoji wanawake washukiwa. Pale kwa ofisi, msimulizi anakaribia zaidi mahali alipo mpelelezi na kuwaonyesha wasimuliwa vitendo vya mpelelezi kama vile kuwaingiza wanawake hao kwa zamu na kuandika ushahidi wao. Kiambishi 'ka' kinaonyesha mfululizo wa vitendo vilivyofanyika katika ofisi ya mpelelezi nacho kiashiria 'Hawa' kinaonyesha kuwa msimulizi sasa amewakaribia wahusika waliomo ndani, mpelelezi Wingo na wanawake washukiwa.

Kwa kawaida msimulizi anaweza kusimulia visa akiwa amesimama pahali pamoja au akawa anasonga kihatua. Huu ndio mtindo wa kisimulizi tunaona katika kisa hicho hapo juu, ambapo msimulizi si tuli bali anasonga kadri mhusika anavyosonga. Kuhusu mtindo ambapo msimulizi husonga, Simpson (1993:15) anasema kuwa msimulizi anaweza kutoka kwa mhusika mmoja na kuanza kumwandama mwingine au kutoka katika tukio moja hadi lingine huku msomaji akipewa jukumu la kuunganisha maelezo hayo ya kandokando ili kuunda picha pana. Usimulizi huu unaweza kufananishwa na ule mwendo wa kamera unaokita katika tendo au onyesho moja hatua kwa hatua. Kanuni hii ya ubadilikaji na usongaji wa mtazamo au ufokasi unajitokeza pia katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, msimulizi anapoeleza namna sebuleni kwa Spekta Seif kulivyojaa watu walioitwa na Msa ili awafafanulie matokeo ya uchunguzi wake. Kuna matumizi ya viashiria

vya mbali na vya karibu vinavyoelekeza kuhusu namna msimulizi alivyokuwa akiangaza kila mtu na kila tukio lililofanyika katika chumba hicho. Msimulizi anaeleza hivi:

> **Tu**kiwatazama wanaume, **tu**naona **yule pale** Bwana Haji Isa, Sheha wa Kazole…Yule pale Bwana Saleh Abdulla, dereva wa Bwana Hakimu Marjani na suti yake aipendayo…**Tu**sistaajabu kuona watu wote **hawa**, tunaowajua sote namna zao na makazi yao. Wote wa**me**hudhuria pale kwa wito maalum. (Uk.76)

Katika dondoo hili hapo juu, viambishi vilivyokolezwa wino pamoja na vivumishi vionyeshi 'Yule Pale' na 'Hawa' vinatuonyesha mitazamo mbalimbali ya msimulizi. Kwanza, kiashiria 'pale' kinaonyesha umbali kati ya msimulizi na wahusika ambao wanatangulizwa kwa wasimuliwa. Baada ya utangulizi huo, msimulizi sasa anasonga karibu na wasomaji. Kiashiria 'hawa' kinatuelekeza kwenye mwendo wa msimulizi kuwakaribia wahusika. Kando na kutumia viashiria kuonyesha uhusiano wa kimahali baina ya msimulizi na msimuliwa, kuna viambishi vya nafsi ya kwanza vinavyoonyesha namna msimulizi anavyomkaribia msimuliwa. Kwa kutumia viambishi hivi, msimulizi anajiweka karibu na msomaji ili aweze kumshawishi zaidi. Kiambishi cha nafsi ya umoja wingi **Tu** katika maneno 'Tukiwatazama', 'Tunaona' na 'Tusistaajabu' kinadhihirisha mwendo huu. Kando na hili, kiambishi hiki kinafifiza utengano baina ya msimulizi na msimuliwa hivyo basi kumpa msimuliwa nafasi ya kujitazamia masuala mwenyewe. Hivyo basi mtazamo wa msimulizi na ule wa msimuliwa unaungana. Kivumishi **Sote** kinaashiria kukubaliana na kuungana kwa mitazamo hii.

Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* kuna matumizi ya viambishi vya nafsi ya umoja ili kuashiria ufupishaji wa masafa ya kisimulizi baina ya msimuliwa na msimulizi. Kupitia mkakati huu, usimulizi unageuzwa kutoka mtazamo wa nje na kuwasilishwa kwa mtazamo wa ndani ili kuyafupisha masafa kwa lengo la kumkaribia msimuliwa. Msimulizi anasema hivi, '**Tu**ko Mburahati, mbele ya moja kati ya nyumba za aina hii. Ni majuzi tu Waridi alipokuja **hapa** Mburahati na kujipatia chumba'. Kwa kutumia kiambishi 'Tu' msimulizi anajiweka pamoja na msimuliwa ili waone matukio kwa pamoja. Zaidi, anapotumia kiwakilishi kionyeshi 'hapa' anayafupisha masafa hayo zaidi.

Mtazamo unaweza pia kujidhihirisha kupitia mahusiano ya kiwakati baina ya msimulizi na kinachosimuliwa. Vipengele vya kisarufi pia vinaweza kutumika kuonyesha mahusiano haya.

Viashiria vya wakati pia hutumika kuonyesha umbali na ukaribu uliopo kati ya matukio yanayosimuliwa na wakati masuala hayo yanaposimuliwa (Wamitila, 2002:48). Simpson (1993:16) anafafanua kuwa viashiria vya wakati vinaweza kuwa vya kuonyesha dira au vinavyotaja mahali kunakohusishwa na msemaji. Anaeleza kwamba kando na viashiria, kuna vitenzi vinavyoonyesha mwendo wa kuelekea au kutoka kwa msemaji ambavyo huashiria mtazamo wa kiwakati. Baadhi ya vitenzi hivyo ni kama vile 'Chukua', 'Leta', 'enda', 'Kuja' pamoja na vihusishi vinavyoonyesha alipo msemaji. Baadhi ya vihusishi hivyo ni kama vile, 'karibu na,' 'nyuma ya', 'mkabala wa', 'chini ya' na mengineyo. Katika usimulizi wa hadithi, viashiria vya wakati vinavyotumika zaidi ni 'sasa', 'wakati huo', 'leo', 'wakati huu', 'jana', 'juzi' miongoni mwa maneno mengine. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* mwandishi anaeleza habari za utokezaji wa Waridi katika maisha ya mjini na namna alivyolazimishwa na Proper kutumika kumuua mpelelezi Joram Kiango hivi, 'Ni **majuzi tu** Waridi alipotokea hapa Mburahati na kujipatia chumba.' Matumizi ya kielezi cha wakati 'majuzi tu' na kiashiria 'hapa' kunasaidia kuyafupisha masafa ya kiwakati baina ya msimulizi na msimuliwa, hivyo kuonyesha mtazamo wa msimulizi; kwamba anayoyasema ni ya ukweli kwa kuwa msimulizi aliyashuhudia kimahali (hapa) na kiwakati (majuzi tu).

Kirai kinachotumika aghalabu katika simulizi kujenga uhusiano huu wa kiwakati ni 'Leo hii'. Katika riwaya hii, msimulizi anasema, '**Leo hii** Waridi alikuwa katika hali yake ya kawaida'.uk.4. Hali hii inaonyesha ukaribu wa msimulizi na kisimuliwa. Tunaona matumizi ya kirai hiki pia katika riwaya hii tena wakati msimulizi anapoeleza wasifu wa Proper wa kujigeuza sura ili kuwalaghai watu mbalimbali wakiwemo wasichana. Kuhusu hila hizi, msimulizi anasema, 'Mfano ni **leo hii** alipokuwa akitoka na msichana **huyu** aliyechanganyikiwa, Waridi'. Uk.7. Matumizi ya kirai 'Leo hii' yanasaidia kumleta msomaji karibu na msimulizi na kuuboresha uhalisi wa kiubunifu. Kwa kuyafupisha masafa hayo, msimulizi anafanikiwa kumshawishi zaidi msimuliwa na kuathiri mtazamo wa msimuliwa. Kama tulivyoona kuhusiana na mtazamo wa kimahali, pia katika mtazamo wa kiwakati msimulizi hatulii pahali pamoja bali husonga mbali au karibu na msimuliwa. Wamitila (2002:37) anaeleza kwamba matumizi ya viashiria vya wakati kama 'Sasa', 'Leo' katika simulizi vinatuonyesha wakati uliopo kihistoria na ambao ni sifa moja muhimu inayotofautisha kazi za kifasihi na zile ambazo si za kifasihi. Anaendelea kufafanua kwamba matumizi ya mbinu hii ya wakati uliopo kihistoria huonyesha kuwa kazi za kifasihi zina sifa ya kutofungika katika wakati maalum.

Kando na viashiria na virai hivi pia kuna viambishi mbalimbali vinavyotumika kuonyesha mabadiliko ya mtazamo wa msimulizi au msomaji. Viambishi vya nyakati na hali kama vile 'me', 'ka', 'li', 'na', 'ta' huweza kutumika kuashiria mwendo wa msimulizi kiwakati. Kwa mfano, msimulizi anaweza kuanza kusimulia masuala katika wakati uliopita na kisha kuyaeleza ya sasa. Mwendo huo unaweza kuonyeshwa kwa kutumia viambishi **Li** na kuelekea kwa kiambishi **na**. Kiambishi **Ka** nacho huweza kutumika katika simulizi kuashiria mfuatano wa vitendo kwa msururu ambapo kando na kuashiria kasi ya vitendo, kiambishi hiki pia huweza kudokeza hali ya kisaikolojia ya mhusika. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* mpelelezi Far Katy Wingo, akisumbuliwa na vifo vingi anavyopasa kuchunguza, anajawa na mawazo mengi. Msimulizi anaeleza vitendo vilivyofuatana na mawazo yake hivi:

> A**li**kuwa na mawazo mengi juu ya vifo vile. A**ka**jitahidi kufikiri namna ya kupata vidokezi ambavyo vingalimwezesha kupata muuaji. **Saa moja unusu** akawa a**me**fika ofisini. A**ka**toa kiko chake na mkebe wa tumbaku, a**ka**anza kuishindilia. A**ka**kiweka kiko mdomoni, kisha a**ka**angalia akifikiri kwa makini.(uk.74)

Katika kisa hiki, msimulizi anamwonyesha msomaji hali ya kiakili ya awali ya mpelelezi Wingo kwa kutumia kiambishi cha wakati uliopita 'li', na kumleta karibu kiwakati, kumuonyesha wakati alipofika ofisini. Anapomfikisha msomaji hapo kwa ofisi, msimulizi pia anaharakisha mtindo wa usimulizi kwa kutumia kiambishi 'Ka'. Mwendo huu kiwakati unasaidia kuusawazisha mtazamo wa msimulizi na ule wa msomaji na kufanikisha ushawishi wa msimulizi kwa msomaji. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, kiambishi 'Me' kimetumika kufanikisha lengo kama hili. Baada ya Msa kukusanya mashahidi mbalimbali ili kithibitisha kesi inayohusiana na urithi kwa watoto wa Hakimu Marjani, viambishi vya wakati na vielezi mbalimbali vinatumiwa na msimulizi ili kuashiria uhusiano wa karibu baina ya kinachosimuliwa, wasomaji na msimulizi. Msimulizi anasema, 'Wote wamehudhuria pale kwa wito maalum ambao vilevile, ni muhimu kwa wote. Hadhara hii aliiunda Bwana Msa tangu juzi'.uk.78. Katika nukuu hili, virai 'Wa**me**hudhuria' na 'Aliunda tangu juzi' vinaonyesha mabadiliko ya umbali wa kiwakati kutoka kale hadi sasa. Kiambishi 'me' kinaashiria kuwa tayari msimulizi amemnasa msomaji kiwakati, kusudi amwathiri kimtazamo wawe na mtazamo mmoja.

Wamitila (2002:48) anasema kuwa umbali mkubwa zaidi kiwakati huathiriwa na matumizi ya fomyula za kifasihi simulizi kama vile 'Hapo zamani za kale,' 'Zama za zama' miongoni mwa

fomyula nyinginezo. Tusomapo riwaya ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu,* hii ndio hali tuipatapo katika mwanzo mwa hadithi. Usimulizi wake unaanza hivi, 'Hapo zamani za kale palikuwa na inspekta mmoja wa polisi aliyejulikana kama Mzee Kombo'. Fomyula ya kifasihi simulizi hapa inampeleka msomaji katika kipindi kirefu cha wakati uliopita na kwa njia hii kumuondoa karibu na msimulizi. Utengano huu unaathiri hali ya uaminifu wa msimulizi kuhusu masuala anayosimulia hivyo kuathiri mtazamo wa msomaji.

Kuna baadhi ya mbinu nyinginezo ambazo huweza kutumika kuonyesha namna kipindi kirefu cha wakati uliopita kinavyoweza kuathiri mtazamo. Kwa mfano, mbinu rejeshi inaweza kuwa na jukumu la kufafanua muktadha wa kihistoria wa tukio fulani (Matumizi ya mbinu hii yatafafanuliwa kwa kina katika sura ya tano). Katika *Salamu Kutoka Kuzimu*, asili ya mhusika Waridi inaelezwa kwa mbinu rejeshi hivi, 'Ni **miezi kadhaa** tu **iliyopita**. **Wakati huo** Waridi a**li**kuwa waridi hasa. Ua maridhawa ambalo kila nyuki a**li**litamani. Kila kipepeo ki**li**limezea mate' uk.9 Kupitia maelezo haya, msimulizi anadhihirisha namna mhusika alivyobadilika kisura na kiwakati. Kirai cha wakati, 'wakati huo' kinaashiria kuwa Waridi amebadilika mno kisura. Yaani, mara ya kwanza alipoonekana mjini alikuwa anavutia lakini sasa amebadilika. Mpito huo wa wakati unaonyesha jinsi alivyochukuliwa na watu wengine, hasa wanaume alipojitokeza mara ya kwanza jijini. Msimulizi anadhihirisha kuvutiwa naye wakati huo, na ndio maana anatumia chuku kueleza sifa zake nzuri kama vile kuhusu urembo wake.

3.5.2.3 Mtazamo katika Sawia ya Kiitikadi

Rimmo-Kenan (1983:83) anasema kwamba itikadi ni kanuni za kijumla kuhusu mwonoulimwengu. Mwonoulimwengu huo unaweza kuwasilishwa kupitia msimamo wa msimulizi maizi au kupitia wahusika. Hata hivyo, anakiri kwamba itikadi inayoishia kuwa na nguvu zaidi ni ile inayopitishwa kupitia msimulizi maizi (wa nafsi ya tatu). Hii ni kwa sababu itikadi inayopitishwa na mhusika aghalabu huwakilisha msimamo finyu kwa kuwa hisia zake zinaweza kuutawala mtazamo huo. Mhusika anaweza kusema waziwazi itikadi yake kuhusu dhana fulani ulimwenguni au kupitia tabia na matendo yake. Kwa upande wake, Simpson (2004:78) anasema kwamba itikadi ni kusanyiko la imani ambazo hutuelekeza kuuelewa ulimwengu pamoja na nduni zinazodhibiti namna tunavyoishi katika jamii. Kwa hivyo, usimulizi unaogemea mtazamo wa kiitikadi huhusu namna matini inavyochimuza imani hizo aidha kupitia mwandishi, simulizi

au mhusika. Anasema kuwa kupitia wahusika, matini hudhihirisha itikadi ambazo zinaweza kushabihiana ama zisishabihiane na itikadi ya mwandishi.

Uspensky (1973:13-19) anachunguza mbinu na michakato mbalimbali ya udhihirishaji wa itikadi. Anaeleza kuwa mbinu hizo zinaweza kujitokeza kupitia msimulizi, mwandishi au mhusika. Baadhi ya mbinu hizo ni kama vile:

Kwanza, maelezo yanayotolewa na mhusika au msimulizi kwa njia ya moja kwa moja kumhusu mhusika mwingine au hali fulani, yanaweza kutumiwa kubaini mtazamo wa mwandishi au msimulizi. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* kwa mfano, msimulizi anaueleza wasifu wa Selume kwa njia inayoonyesha kuvutiwa kwake na wasifu huo. Anasema, 'Selume alikuwa msichana apataye miaka ishirini na tano, mzuri wa sura na tabia, hana makuu na mtu yeyote, watu wote kwake ni sawa'. Njia nyingine inayokaribiana na uelezaji wa moja kwa moja na inayoonyesha mtazamo wa mwandishi ni matumizi ya majina ya kimajazi ya wahusika. Baadhi ya waandishi huwatumia wahusika wenye majina ya kimajazi ili kupitisha itikadi fulani kwa wanajamii. Kwa mfano, Shabaan Robert huwatumia wahusika wa kimajazi kama vile Utubora na Adili ili kupitisha itikadi ya utu. Mohamed Said Abdulla pia huwatumia wahusika wa kmajazi katika baadhi ya riwaya zake za kiupelelezi ingawa majina hayo hayaichimuzi itikadi yake waziwazi.

Pili, kwa kutumia maelezo kinzani. Uspensky anaeleza kwamba katika kazi ambapo mwandishi ameathiriwa na itikadi ya Umaksi, kama vile kazi zinazodhihirisha utabaka, dhana kinzani kama vile wema na uovu hujitokeza. Katika miktadha kama hii, tabaka tawala huonyeshwa likitenda uovu dhidi ya tabaka linalotawaliwa. Mifano mingine ya maelezo kinzani na ambayo huenda yakadokeza itikadi ya mwandishi ni mahusiano baina ya maskini na tajiri, mwajiriwa na mwajiri, wahalifu na walinda usalama, wapiga kura na wapigiwa kura miongoni mwa mahusiano mengine. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, dhana kinzani zinazojitokeza zaidi ni mahusiano baina ya mhalifu na mlinda usalama. Mpelelezi anawasaidia polisi kuwasaka wavunja sheria ili kudumisha usalama wa jamii na kufikia mwishoni mwa hadithi nyingi za kiupelelezi walinda usalama, wakiwemo polisi na wapelelezi hushinda wavunja sheria. Fomyula hii nayo inatuelekeza kwenye itikadi nyingine yenye dhana kinzani ya wema na uovu. Katika riwaya ya *Uchu* (2000), dhana kinzani ya tabaka la chini na tabaka la juu inaangaziwa. Kwa mfano, msimulizi anaziweka wazi tofauti baina ya tabaka tawala na tabaka linalotawaliwa. Watawala wanasawiriwa wakiwa

watu wasiojali masilahi ya watawaliwa. Hii ni kupitia namna huduma za kimsingi zinavyotolewa kwa misingi ya kitabaka. Kwa mfano, watu wa tabaka la chini wanapewa elimu duni huku watu wa tabaka la juu wakisawiriwa kama wanaofaidika na elimu bora. Kwa sababu hii, watawala hawatii juhudi zozote kuboresha elimu ya umma kwa kuwa wao huwapeleka watoto wao ng'ambo kusomea huko. Msimulizi anaeleza:

> Kwa vile **watoto wa wafanyakazi na wakulima** ambao ndio wengi katika nchi hii, watapata **elimu duni**, basi hawa **watoto wa viongozi na matajiri** ambao ni kama asilimia mbili ya idadi ya watoto wote wa nchi hii, watarudi na **elimu nzuri** na hivyo ndio watakaoshika madaraka hapo baadaye maana wao watakuwa wamesoma vizuri.(uk.18)

Dhana zilizokolezwa wino hapo juu zinaonyesha ukinzani wa kimaisha baina ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Msimulizi anadhihirisha kuchukizwa kwake na hali ambapo watu wachache wenye utajiri ndio wanaopata elimu bora na kuishia kuwa viongozi baadaye. Kwa hivyo dhana kinzani za 'elimu duni', 'elimu bora', 'watoto wa maskini na watoto wa tajiri' zinatumika katika muktadha huu kuchimuza itikadi ya Umaksi kuhusu ukosefu wa usawa katika jamii. Uwekaji sambamba wa dhana hizi unatusaidia kufasiri mtazamo wa mwandishi kuhusu suala linalosimuliwa la ukosefu wa usawa katika utoaji wa huduma za kijamii za elimu. Mtazamo huu wa msimulizi unaafikiana na maoni ya Althusser (1971:132-133) kwamba elimu ni taasisi moja ya kiserikali inayotumika kuendeleza itikadi ya kiutawala. Althuser anazigawa taasisi hizi kuwili; Kwanza, taasisi za kijamii kama vile dini, utamaduni, shule na familia na pili, taasisi za kisheria kama vile mahakama, polisi na jela.

Katika riwaya za Mohammed Said Abdulla tunazohakiki, dini imeathiri pakubwa itikadi yake kuhusu masuala kadhaa yahusuyo maisha. Kwa mfano, mwandishi anaamini kwamba dini ndicho chanzo cha maisha. Anakiri kwamba maisha huanza na kuishia kwa Mungu, kuwa Mungu ndiye humpa kiumbe maisha na ndiye huyachukua. Kwa mfano katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, kuhusiana na kifo cha Hakimu Marjani msimulizi anaeleza hivi, 'Kwa siku ya pili, Mungu alimhitari, akachukua roho yake iliyokuwa ni amana kumpa kiumbe chake.' uk.37. Ili kuisisitiza itikadi hii, sauti ya kisimulizi pia inabadilika kutoka nafsi ya tatu na kuwa msimulizi mshiriki ili kuyafupisha masafa ya usimulizi. Mwandishi anafanya hivi hili kumshawishi msomaji zaidi. Kiambishi cha nafsi ya kwanza 'tu' kinatumika. 'Kwa Mungu ndiko **tu**tokako na ndiko **tu**rejeako'.

Uk.39. Kauli hii haihusu tu mabadiliko ya sauti ya kisimulizi bali pia inaweza kuchukuliwa kama upenyezi wa mwandishi. Kauli hii inatuashiria imani ya mwandishi kuhusu chanzo cha maisha kuwa ni Mungu. Kwa kuwa msimulizi anajileta karibu na msomaji anapobadili nafsi kwa kuchukua nafsi ya kwanza wingi, anafanikiwa kumshawishi msomaji ili kumwaminisha zaidi. Baadaye (uk.103) anahitimisha kuwa Kurani ni kiongozi cha Waislamu wote ili kutuonyesha kwamba maoni yake kuhusu dini yanatoka kwenye kitabu hicho.

Katika baadhi ya riwaya za Musiba pia itikadi yake kuhusu maisha inajitokeza. Katika Njama, imani ya dini inaonekana kuathiri mtazamo wa mwandishi pakubwa kuhusiana na dhana za kuishi na kufa. Katika mazungumzo baina ya Veronika Amadu, Sherriff na Willy Gamba, Veronika anasema:

> Unajua Willy dakika ile mtu anapozaliwa pale pale anapewa hukumu ya Kifo. Nina maana  kuwa binadamu hata haishi vipi kufa lazima atakufa. Kule kuishi baada ya kuzliwa ina maana kuwa ile hukumu ya kifo imeahirishwa. Wengine huaihirishwa kwa mwezi mmoja…wengine huishi hata miaka mia moja. Hivyo kila mtu ana sehemu yake ya kuishi. Kwa hivyo kuogopa kufa ni ujinga. (uk.58)

Itikadi kuhusu uovu wa ubepari pia inajitokeza katika baadhi ya riwaya za Mohamed Said Abdulla. Katika riwaya zake kadhaa, anaweka sambamba maisha na taasisi za matajiri na kuzilinganisha na maisha ya wanyonge kwa kuonyesha namna wanavyodhulumiwa nao. Katika *Duniani Kuna Watu*, tunaona namna mabepari wanavyowakopesha pesa watu wasiojiweza kwa lengo la kunyakua mali yao. Mwandishi anachukizwa na unyanyasaji huu. Kuhusiana na hali ya uhitaji ya Kasim, msimulizi anasema

> Sasa ulikuwa ni wakati wake wa kupata fedha azitakazo kwa mabepar ambao lazima watamkopesha maadamu wanajua kuwa yeye ndiye mrithi pekee wa mali adhimu aliyohalifu babake.(uk.39)

Katika riwaya hii pia, Abdulla anaonyesha kutoridhishwa na vizingiti vya kitabaka vinavyojitokeza katika mahusiano ya kindoa. Tofauti za kiutabaka zinakuwa vikwazo kwa vijana wanapotaka kuoa au kuolewa. Saleh, mwajiriwa wa Hakimu Marjani anahisi kwamba ingawa anampenda binti ya mwajiri wake, tofauti za kiutabaka zitamzuia kumuoa binti huyo, Selume. Mazungumzo baina ya Saleh na Selume yanaonyesha mtafaruku huu:

> Sipendi kuoa **bibi wa kitajiri**, ilivyokuwa **mimi ni maskini**. Alijibu Saleh kwa kuzingatia, bali nampenda bibi huyu ghaya ya kumpenda lakini sidanganyi nafsi yangu kwa kuwa nathubutu kutaka kumuoa. Na ikitokea bahati ya kumuoa, hapana shaka watu watasema kwamba nimemwoa kwa sababu ya kutaka kumlia pesa zake.(uk.29)

Nukuu hili linaashiria mtazamo wa msimulizi kuhusu mtanziko wa ndoa baina ya matabaka katika jamii, kwamba mtoto wa tabaka la maskini anapotaka kuoa katika tabaka la matajiri, wanajamii hufikiri kuwa msukumo wa kutaka kujitajirisha ndio unaochukua kipaumbele badala ya mapenzi. Hata hivyo, mtoto wa tajiri anapompenda mtoto wa maskini mtazamo wa kujitajirisha hauzingatiwi. Katika siku za hivi majuzi, uhalisia huu umejitokeza ambapo mwanamke Mwafrika anapoolewa na Mzungu au mwanaume Mwafrika kumuoa mwanamke Mhindi, suala la kujiinua kiuchumi linachukuliwa na baadhi ya wanajamii kuwa msingi wa ndoa hizo.

Njia nyingine inayodhihirisha mtazamo wa kiitikadi ni kuwepo kwa kaida na nduni za kijamii pamoja na chukulizi zinazoonyesha mwelekeo wa jamii hiyo. Kaida hizo kwa mfano huwaaminisha wanajamii kwamba jambo au hali fulani ni baya na nyingine ni bora. Lye akinukuliwa na Kisurulia (2012:87) anasema kuwa kila jamii huwa na kanuni zinazoweka mipaka baina ya uovu na wema na kwamba kanuni hizo huweza kujitokeza katika simulizi. Chukulizi na kaida hizi ni ishara ya itikadi za kundi fulani la watu katika jamii. Kaida hizi ndizo huwabainishia sifa pendwa na zile hasi ambazo wanajamii hawapendi zipitishwe miongoni mwa vizazi vyao. Katika riwaya za Abdulla kwa mfano, itikadi kuu ni ile inayopinga uendelezaji wa maovu kama vile ufisadi, mauaji, uchawi na ulaghai unaohusishwa na urithi. Katika *Kisima Cha Giningi*, kwa mfano, mwandishi anapinga itikadi ya wanajamii kuhusu nguvu za uchawi na ulaghai katika urithi. Ali Makame anatumia uramali kumtenganisha Mwana wa Giningi na mumewe, Vuai, ili iwe rahisi kwake kumlaghai shamba lake aliloachiwa na babake. Njama hizi zinaposhindwa anaamua kumuua ili achukue urithi huo. Mpelelezi Msa anamkabili mganga Fundi Mangungu na kuonyesha kwamba anatumia uongo akijidai anawapa tiba za masuala mbalimbali.

Katika *Duniani Kuna Watu*, mwandishi anaonyesha itikadi kwamba ufisadi ni uovu unaofaa kupingwa kwa dhati. Katika riwaya hii, wenye nguvu za kiuchumi wanawahonga wagawaji urithi ili kurithi kisicho chao. Kasim anataka kuuchukua urithi wa Selume kwa kuwahonga wagawaji urithi. Kasim anahisi kuwa wanawake hawafai kurithi mali ya baba zao. Msimulizi anasema hivi:

> Selume? Selume nini? Atatengeneza mipango na wagawaji urithi kwa ‘kuzunguka mbuyu’, Selume arushwe hapa, anyang’anywe pale, adokolewe hiki, afililishwe kile, hata kama atabaki na kitu, hakitakuwa kitu cha kuitwa ‘kitu’ ila ni kitu kidogo cha uzembe tu.(uk.39)

Nukuu hili linatuashiria mtazamo wa mwandishi kuhusu upotokaji wa kimaadili unaoletwa na tamaa ya ulimbikizaji wa mali kwa njia za mkato. Kupitia maelezo haya, inabainika kwamba wanyonge kama vile wanawake wanadhulumiwa na wenye nguvu hasa wanaume kuhusiana na umilikaji wa mashamba.

Uspensky anaangazia njia nyingine ionyeshayo mtazamo wa kiitikadi ambayo ni upenyezi wa mwandishi. Msimulizi anaweza kujitenga na masuala anayosimulia na kumpa mwandishi nafasi ya kuwahutubia wasomaji moja kwa moja. Kwa njia hii, mwandishi anaweza kudhihirisha mtazamo wake wa kiitikadi. Kama tulivyoonyesha awali, upenyezi si sawa na tathmini ya kisimulizi ambapo msimulizi hutathmini usimulizi wake unavyoendeshwa ama akatathmini masuala anayosimulia. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* sauti ya mwandishi inajitokeza na kutoa wosia kuhusu matatizo na fanaka za maisha. Mwandishi anatoa wosia huu kuhusiana na tabia ya Kasim ya kuandama anasa kila wakati bila kufikiri mustakabali wa kesho. Mwandishi anasema:

> Kusema haya na haya, duniani kuna vilima na mabonde; kuna mashaka na raha. Yote hayo, hayaendelei, ikawa moja tu hilo hilo kila siku. Unapanda kilima kwa mashaka, taabu, kuchoka na jasho kukutoka lakini kilima kina mwisho wake; haiwi utakipanda tu moja kwa moja; mwisho wa kilima utateremka bonde kwa raha na wepesi, na hata ukilimaliza bonde hilo, kaa ukijua kuwa mbele yako kuna kilima kingine kinakungoja. Hivi ndivyo dunia inavyokwenda; baada ya dhiki faraja na baada ya faraja dhiki. (uk.37)

Kupitia upenyezi huu, mwandishi anaidhihirisha imani yake kuhusu maisha yalivyo ulimwenguni; kwamba ni raha na karaha au dhiki na faraja na kuwaonya wanajamii kutotaraji yote mawili. Upenyezi huu unafanikiwa kutoa wosia kwa msukumo wenye nguvu zaidi ya ikiwa wosia huo ungewasilishwa kupitia mtazamo wa nje. Anapotumia virai kama vile, ‘kaa ukijua’, mwandishi anafanikiwa kumleta msimuliwa karibu naye na kumzungumzia kana kwamba anatumia usemi wa moja kwa moja.

Njia nyingine ionyeshayo mtazamo wa kiitikadi ni kupitia matumizi ya lugha yaonyeshayo kejeli, matusi au ubaguzi wa rangi. Kauli zinazotumia kejeli, matusi na misemo ionyeshayo ubaguzi (wa rangi au kijinsia) huashiria mtazamo hasi wa msemaji kwa msemewa. Katika riwaya ya *Simu Ya Kifo,* msimulizi anaonyesha kuchukizwa kwake na lugha itumiwayo na mhusika Agnes ya kumtusi na kumtesa mpelelezi Far Katy Wingo. Msimamo wake ni wazi anapomwita Agnes katili. Hivi ndivyo msimulizi anavyosema, ‘‘Yule **mwanamke mkatili** akamwambia inspekta, ‘Haya we mbwa, ukiangusha kikombe hata komoja tu, ujue ndio mauti yako. Leo nakuapia kabisa sitaki mzaha’’. Kisha katika muktadha mwingine, msimulizi huyu anasema, ‘‘**Malkia wa ukatili** akaanza kumuuliza inspekta, ‘Sasa we inspekta hebu sasa nieleze kisa cha kuingilia mambo yasiyokuhusu’’. Katika visa hivi viwili, inaonekana kwamba msisitizo wa msimulizi ni kuwa Agnes hakupaswa kumteka na kumtishia Inspekta Far Katy Wingo kwa kiasi alichofanya. Anatoa hukumu inayodhihirisha mtazamo wa kutopendezwa na vitendo vya Agnes unaoashiriwa na maeneo, ‘katili’ na ‘malkia wa ukatili’. Kauli hii ya msimulizi pia inaakisi kwa kiasi kikubwa saguzi za kitamaduni miongoni mwa wanajamii wengi kumhusu mwanamke. Hata hivyo, baadaye msimulizi anafichua sababu za Agnes kufanya hivyo. Wakati huo huo, lugha ya Agnes yenye matusi na vitisho vingi kwa Inspekta Wingo, ni thibitisho kwamba Agnes anachukizwa na uchunguzi wa Wingo kuhusu mauaji ya Mzee Jacob pamoja na watu wengine wa familia yake.

Katika riwaya za Mtobwa kama vile *Salamu Kutoka Kuzimu*, mhusika mpinzani anaelezwa kwa njia inayoashiria mtazamo wa msimulizi kuhusu vitendo viovu vya mhusika huyu, Proper. Inaonekana kuwa msimulizi anaupinga uovu. Mhusika Proper anaendeleza uovu kupitia wizi, mauaji na upangaji wa njama za kupindua serikali. Waridi anashuhudia uovu wa Proper wakati mhusika huyu alipobadili jina na kujiita Bomba Kimara. Anajibadili sura pia kwa kujivisha nguo za Kiarabu ili kumtishia Waridi zaidi akisema kwamba angemuua. Msimulizi anasema kuhusiana na namna Waridi alivyochukizwa na Proper, ‘Ghafla alijikuta kamchukulia Bomba kama shetani. Hata sura yake sasa aliiona mbaya kama dhambi’. Uk.11. Mtazamo wa Waridi kwa Bomba (Proper) ni hasi mno kulingana na maoni ya msimulizi, kiasi cha kumfananisha na shetani au dhambi.

Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu,* msimulizi anaonyesha mtazamo wake kuhusu itikadi zinazoweka msingi wa ubaguzi wa rangi. Msimulizi anaelekea kutetea usawa wa watu wa rangi zote. Anafanya hivi kwa kuzishambulia fikira za Wazungu wanaowaona Waafrika kama watu wa

ngazi za chini. Baadhi ya Waafrika wanaofanya kazi ya kuchimba migodi wanalipwa misharahara midogo kuliko wenzao wa Kizungu katika chimbo la babake Von Iron. Wakati mgodi huu unapoporomoka, wachimbaji weusi wanasakwa, wanatiwa mbaroni na wengine kuuawa. Msimulizi anaeleza matatizo yanayowakumba watu weusi hivi:

> Ilikuwa siku ngumu mno kwa watumishi weusi. Wengi wao waliambulia kuishia katika vituo vya polisi ambako waliteswa kwa kosa ambalo hawakulifahamu. (uk.129)

Kisa hiki kinaashiria wazi kwamba msimulizi anachukizwa na hali ya ubaguzi wa rangi katika Afrika Kusini inayosababisha mateso kwa watu weusi. Kwa hivyo, itikadi ya mwandishi ni kwamba ubaguzi wa rangi unafaa kukomeshwa na hali ya usawa ikipendekezwa. Anakosoa pia mfumo wa kisheria unaoendeleza ukandamizwaji wa watu weusi huku ukiwapendelea watu weupe. Kwa kuwa riwaya za Mtobwa zinalimulika suala la upelelezi katika kiwango cha kimataifa, msimulizi wa baadhi ya riwaya zake anafanikiwa pia kuusawiri uhusiano uliopo baina ya mataifa ya kikoloni na nchi zilizokuwa chini ya himaya ya wakoloni. Itikadi inayojitokeza ni kwamba mataifa hayo ya kikoloni yana mtazamo hasi dhidi ya nchi zilizotawaliwa za Kiafrika. Msimulizi anasema kuwa Uingereza iliendelea kujifanya baba na mama wa makoloni yake ya awali na hii ikawa ndio falsafa iliyotumiwa na mataifa hayo kuendelea kuchapisha taarifa za habari zilizoonyesha ubora wa Ulaya na udhaifu wa Afrika. Itikadi kama hii inajitokeza pia katika kazi za wasomi wengine waliowahi kuutetea ubora wa Afrika huku wakishambulia Ulaya. Kwa mfano, Said (1993:xiv) katika *Orientalism* anasema kuwa Ulaya iliendelea kusambaza mitazamo hasi dhidi ya Waafrika na watu wengine kote ulimwenguni waliotawaliwa. Watu hawa walionyeshwa kama wenye udhaifu wa kiakili, kitabia, kiuchumi na wazembe huku Wazungu wakijieleza kama wenye nguvu za kifikra, wenye ustaarabu na maendeleo makuu. Msimulizi (uk.73) anatueleza kwamba vyombo vya habari vya Uingereza viliendeleza habari kama hizi na kuepuka kutaja zile nzuri. Uteuzi wa habari kama hizi ni ishara ya mtazamo wa kiitikadi wa taifa hilo dhidi ya mataifa ya Kiafrika.

Uspensky (1973:42) anaeleza kwamba njia nyingine iwezayo kumuelekeza msomaji kwenye mtazamo wa kiitikadi ni namna msimulizi anavyoyaeleza mahusiano baina ya jinsia mbalimbali. Katika baadhi ya riwaya tunazohakiki, kuna mahusiano ya kijinsia yanayoashiria itikadi ya ukosefu wa usawa wa kijinsia. Katika baadhi ya tamaduni, mwanaume huwa na nguvu nyingi za

kiuchumi, kijamii na kisiasa katika jamii kuliko mwanamke. Ili kudumisha hali hii, baadhi ya wanaume wanapinga juhudi zozote za kuleta usawa wa kijinsia. Abdulla katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, anaikuza itikadi ya usawa wa kijinsia, akionyesha kuwa masuala ya elimu na urithi ni misingi inayoweza kutumika kukuza usawa wa kijinsia. Hii ni kupitia kuwaelimisha watoto wa kike na wa kiume na kugawa urithi kwa njia isiyowabagua watu kwa misingi ya kijinsia. Katika riwaya hii, Hakimu Marjani anahakikisha kuwa bintiye, Selume anapata elimu bora kwa kumpeleka katika chuo cha Cambridge. (Uk.75). Baada ya kupata elimu hii, Selume hana hisia za ubaguzi wa kitabaka kama ndugu yake Kasim ambaye hakusoma hadi kiwango hiki. Kwa hivyo ni imani ya mwandishi kwamba, elimu ni nguzo bora ya kuumaliza ubaguzi wa kitabaka na kuleta usawa wa kijinsia. Msimulizi akitilia mkazo mwonoulimwengu huu mpya wa Selume anasema, ‘Selume ni mzuri wa sura na tabia. Hana makuu na mtu yeyote, watu wote kwake ni sawa na katika masomo, yeye kasoma mpaka masomo ya juu kwa daraja na ujuzi mkubwa’. Uk.7. Kama anavyosema Althusser (132-133), elimu ni taasisi moja itumiwayo na serikali kuendeleza itikadi zake.

Kuhusu urithi, Abdulla anaonyesha kuwa ni vyema kwa watoto wa kiume na wa kike warithishwe mali ya wazazi wao bila ubaguzi. Katika hati yake ya urithi, Hakimu Marjani alimrithisha bintiye Selume na mtoto wake wa kiume, Saleh, mali yake yote. Hata hivyo, Kasim, mtoto wake wa kupanga, anapinga mtoto wa kike kurithi. Anauliza babake, ‘ Unamweka mtoto wa kike mbele?.. Atakufaa nini mtoto wa kike. Nitakufaa mimi nitakayekuchukulia jeneza nikupeleke kaburini kwako, nikuzike.’uk.35. Kasim katika muktadha huu anajitokeza kama kiwakilishi cha vikwazo vinayolemaza juhudi za kukuza usawa wa kijinsia. Pia anawakosoa wanaume wasiotaka juhudi za usawa kufikiwa. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* hali kama hii inajitokeza pia. Mpelelezi Far Katy Wingo anapotekwa nyara na kutishiwa na Agnes, anashangaa ni vipi mwanamke anavyoweza kumhangaisha kwa kiasi hicho. Anasema, ‘Huyu ni mwanamke tu, naye anataka kunitesa mimi’.uk.99. Kauli hii inaonyesha mtazamo wa baadhi ya wanajamii kuwa wanawake ni dhaifu hivyo ni aibu kwa mwanaume kuteswa naye.

#### 3.5.2.4 Mtazamo Katika Sawia ya Kisaikolojia

Sawia hii huangazia hali ya kiakili ya msimulizi pamoja na hisia zake ama hisia za mhusika kuhusiana na kile kinachosimuliwa. Kwa misingi hii basi hisia na mawazo ya msimulizi au mhusika ndio nguzo inayoashiria mtazamo wao kuhusu kinachosimuliwa**.** Hii ni kwa sababu fikira

za mhusika na matamanio yake yanaweza kutuelekeza kuhitimisha ikiwa kinachosimuliwa kinamvutia au kumchukiza msimulizi ama msomaji. Kama zilivyo sawia nyinginezo, sawia ya kisaikolojia inaweza kujitokeza kupitia mtazamo wa nje au wa ndani. Simpson (1993:30) anaeleza kuwa ingawa sawia ya kisaikolojia inaweza kujitokeza kupitia mitazamo yote miwili, mtazamo nje ndio hudhihirisha sawia ya kisaikolojia zaidi kwa kuwa ndio humpa msimulizi uwezo wa kufikia hisia na fikira za wahusika.

Fowler (1986:127-147) anatumia kielelezo chenye vipengele vinne katika kuifafanua sawia ya kisaikolojia. Kwanza anaugawa mtazamo ndani kuwili na kupata mtazamo ndani ‘A’ na ‘B’ na mtazamo nje katika ‘C’ na ‘D’. Aina ya ‘A’, anasema hutawaliwa na usimulizi wa nafsi ya kwanza unaodhihirika kupitia sauti ya msimulizi-mhusika. Usimulizi wa aina hii unachimuzwa kupitia tathmini ya mwandishi pamoja na matumizi ya vitenzi vionyeshavyo hisia na fikira (Verba Sentiendi). Fowler anashikilia kuwa usimulizi huu huwa na ubinafsi mwingi kwa kuwa umejaa maoni ya msimulizi na namna anavyowahukumu wahusika wengine. Pia msimulizi wa aina hii anatoa maoni na hukumu kuhusu masuala mengine ya hadithini. Aina ya pili (B) inahusu hali ambapo msimulizi anajikita katika mhusika mmoja tu. Ingawa msimulizi ana mtazamo wa ndani, anapewa uwezo kama ule wa msimulizi wa nafsi ya tatu kwa kuwa ana uwezo wa kuyafafanua mawazo ya mhusika huyo. Aina ya tatu, (C), kulingana na Fowler, ni usimulizi unaohusu mtazamo wa nje usioegemea upande wowote. Katika usimulizi huu, msimulizi anajiepusha na utathmini wowote wa wahusika na masuala yanayosimuliwa. Pia anajiepusha na hisia na mawazo ya mhusika. Kwa hivyo, msimulizi huyu, hatumii ‘Verba Sentiendi’ (vitenzi vionyeshavyo hisia na fikira). Msimulizi anachukua mtindo wa kati ambao ni aminifu na wenye utobinafsi. Aina ya nne (D), ni changamano zaidi kwa kuwa inahusu mtazamo nje lakini wenye ishara za mtazamo ndani zinazowakilishwa na kuwepo kwa viambishi vya nafsi ya kwanza. Msimulizi huyu hudhibiti usimuliaji na wakati huo huo hutoa tathmini za wahusika na matukio isipokuwa mawazo na hisia zao. Kwa hivyo, uchangamano wake unatokana na uhusishwaji wa mitazamo yote miwili lakini katika viwango tofauti.

Maelezo haya ya Fowler, ingawa yana utata kwa kiasi kuhusiana na aina ‘B’ na ‘D’ yametupatia msingi wa kuchanganulia viashiria vya mtazamo katika ngazi ya kisaikolojia. Kwa mfano, dhana yake ya Verba Sentiendi itakuwa muhimu zaidi. Anavyoeleza ni kweli kuwa lugha kama chombo cha mawasiliano hubeba hisia mbalimbali zinazofanikisha mahusiano ya kijamii. Hisia hizi huhusu

maoni, furaha, uchungu, woga, matamanio na misimamo ya watu. Hapa chini tunachunguza namna udhihirikaji wa hisia unavyoweza kudokeza mtazamo wa kisaikolojia.

3.5.2.4.1Matumizi ya Maneno ya Mkabala (Verba Sentiendi)

Haya ni maneno hususan vitenzi yanayoonyesha hisia na fikira. Kwa kuwa riwaya tunazohakiki ni za kiupelelezi ambazo muundo wake unahusu uhalifu na uchunguzi wa uhalifu huo, aghalabu kuna matumizi ya maneno ya kejeli, kukashfu, vicheko, vilio na hata vitisho. Lugha inayotumia kejeli, vicheko na mbinu nyinginezo zinazoibua hisia za msemaji, zinaweza kutuelekeza kwenye mtazamo wa kisaikolojia wa msemaji. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, Waridi alipomuua Bomba, alipatwa na usumbufu mkubwa kufuatia kitendo hicho. Msimulizi anaieleza hali yake ya kisaikolojia hivi:

> Siku zote **aliteswa na huzuni** kwa kukumbuka damu isiyo na hatia aliyoimwaga, **hofu** kwa kudhani kuwa wakati wowote polisi wangekuja kutaka kumchukua na zaidi, **maumivu makali moyoni** kwa **kuhisi** ile sauti ya Bomba **alipolia** kwa **uchungu** na picha ya macho yake **yanayosihi.** (uk.12)

Katika kifungu hiki maneno yaliyoandikwa kwa herufi nzito, yanaashiria hisia za aina mbalimbali zinazotokana na kitendo kimoja cha mauaji aliyoyafanya Waridi; kuteseka kutokana na huzuni, kuwa na hofu ya polisi, kukumbuka sauti ya Bomba na hata sura yake kunamtia kiwewe Waridi. Kwa hivyo, msimulizi kupitia maelezo haya anadhihirisha mtazamo wake wa kuchukizwa na kitendo cha mauaji. Vilevile, mhusika Waridi pia haonekani kupenda alichofanya kwani ana majuto mengi.  Usawiri wa Waridi katika hali hii pia unaelekea kuonyesha itikadi ya mwandishi kwamba uovu haufai.

Mdhihiriko wa hisia kama hizi pia unashuhudiwa katika riwaya ya *Simu ya Kifo.* Kutokana na kitendo cha Agness cha kulipiza kizazi kuhusu mauaji ya wazazi wake, anapoona kuwa sasa anachunguzwa na polisi anapatwa na hisia zenye uchungu na kuanza kulia. Yeye Agnes hakupenda kuchunguzwa kutokana na mauaji aliyofanya ya Mzee Jacob na mkewe. Hali hii inaelezwa hivi, ‘Agnes alikubali shingo upande. Daktari naye akawa **amechukizwa kabisa** na jambo hilo. Agnes **hakupendelea** kabisa mambo ya Inspekta. Agnes akaondoka pale **kwa kinyongo sana**. Alipoona kwamba Inspekta anakichukua kitabu cha kuandika habari za kila siku, alianza **kulia kwa uchungu mwingi’**. Uk.86-87. Katika kifungu hiki, kando na kutumia verba Sentiendi kama vile ‘Amechukizwa,’ ‘Kulia’ na ‘Hakupendelea’, pia msimulizi ametumia vielezi kadhaa kuashiria

kiwango cha hisia zake. Kwa mfano, katika 'Amechukizwa **kabisa',** tunaona kiwango cha juu cha kitendo cha kuchukia. Kuna vielezi vya namna vinavyoelekeza kuhusu jinsi matendo yalivyofanyika ambavyo ni '**kulia kwa uchungu'** na 'kuondoka **kwa kinyongo'**. Matumizi ya vitenzi vya hisia pamoja na vielezi vya namna na kiasi, yanaongeza uzito wa hisia hivyo kumuathiri msimuliwa zaidi. Kwa kufanya hivi, msimulizi anafanikiwa kudhihirisha mtazamo wa kisaikolojia wa Agnes kuhusu tukio la kuchunguzwa linalofanywa na Inspekta Wingo. Pili, maelezo haya yanafichua kuwa Agnes ana msimamo hasi dhidi ya mpelelezi.

Kuna sentensi ambazo pia humwezesha msimuliwa kuzifahamu hisia za mhusika na hali yake ya kiakili kana kwamba ameambiwa moja kwa moja kuhusu hali hizo. Katika riwaya ya *Kisima Cha Giningi*, tunaona usumbufu wa kisaikolojia unampitikia Mwana wa Giningi anapokumbuka asili yake hususan namna alivyolelewa na mwanamke asiyekuwa mamake. Kupitia mtazamo wa nje msimulizi anasema:

> Mwana wa Giningi ilimjia kufikiri kuwa, juu ya kuwa yeye hivi sasa kamchukua huyo bibi **aliyemlea kwa vizuri namna hiyo** na akamweka kwake lakini **yote atakayomfanyia hayafidii mashaka** na taabu aliyokuta bibi yule mikononi mwake alipokuwa mtoto…Ilimjia tena kudhukuru siku zake za utotoni.(uk.21)

Katika kifungu hiki, kando na msimulizi kuangazia usuli wa Mwana wa Giningi, pia anatuonyesha hisia zinazoelekeza kwenye mtazamo wake kumhusu mama aliyemlea. Hisia zake ni kwamba mama huyo alimlea vyema na sasa Mwana wa Giningi naye haoni ikiwa angeweza kulipa wema huo. Msimulizi pia ana mtazamo sawa na ule wa Mwana wa Giningi kuwa, malezi bora yaliyotolewa na bibi huyo. Usimulizi wa aina hii unamwaminisha msomaji kwa kuwa unawasilishwa na sauti isiyo ya mhusika. Msimulizi wa aina hii ana uwezo wa kuingia akilini na kuwaonyesha wasimuliwa yaliyomo katika akili ya mhusika. Uwezo kama huu pia unajitokeza katika riwaya za Mtobwa. Katika riwaya yake ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, sentensi zinazoonyesha hisia za aina aina, zimetumika kuonyesha mtazamo wa kisaikolojia. Wakati Proper alipolitega bomu katika nyumba Joram Kiango alipokuwa anaishi, alifurahi mno alipoenda kushuhudia uharibifu aliousababisha. Hivi ndivyo asemavyo msimulizi:

> Mtu huyo alipoondoka, Proper aliendelea kutazama ajali huku akijitia **kunung'unika.** Lakini **rohoni alikuwa akisherehekea** na kushangilia sana, 'Kifo

> kinachostahili kabisa'. **Aliwaza kwa furaha**. 'Mnofu mmoja mmoja! Na ajiunge basi tuone ulipo huo ushujaa wake. (Uk.38)

Haya ni mawazo na hisia za Proper zinazoonyesha jinsi alivyofurahishwa na mlipuko uliotawanya nyumba hiyo na waliokuwemo hasa adui yake, Joram Kiango. Msimulizi anafichua hisia zake za ndani kwamba alifurahi na kushangilia rohoni. Maneno yaliyoandikwa kwa herufi nzito yanatuonyesha uwezo wa msimulizi wa kuangaza mawazo na hisia zilizo katika roho ya mtu. Tabia yake ya ukatili inaashirika kupitia namna alivyosherehekea matokeo hayo. Proper hakugundua kuwa alichoona kilikuwa ni mavazi na madevu bandia ya Joram Kiango na kuwa Joram hakuwa ameumizwa. Kuhusu mtu mwingine aliyeshuhudia mlipuko huo, Unono, msimulizi anatuonyesha hali ya ukinzani wa kisaikolojia katika fikira za Unono. Unono alikuwa ameenda kuzuru eneo hilo akitafuta mwanaume kwa sababu mbili; kwanza, sababu za kiuchumi na pili, hakuwa anapata nafasi ya kupendwa kwa kuwa sura yake haikuwavutia wanaume kutokana na umbo lake lisiloridhisha. Msimulizi anasema:

> **Kichwani**, Unono alikuwa na **mawazo tofauti**, nje kabisa na msiba huo uliotokea. Alikuwa na **mawazo yenye mchanganyiko** baina ya matatizo ya kiuchuni na kimapenzi. **Alihisi** kuwa sehemu hiyo ingeweza kumfanya apate ufunguzi wa tatizo moja au yote mawili. Sura yake haikumtendea wema katika biashara yake. Alipata mwanaume wa kumfariji kwa bahati tu, na alipopata ilikuwa muhali mwanaume huyo kurudi.(uk.39)

Katika kifungu cha hapo awali tuliona uwezo wa msimulizi wa kufichua yaliyomo rohoni ya mhusika na katika kifungu hiki nacho, tunaona uwezo wake wa kufichua yaliyomo akilini. Unono alifikiri kwamba kutembelea eneo la mahame ambapo wahalifu hujificha, angepata bahati ya kumpata mwanaume. Huu ndio usumbufu wa kisaikolojia anaopitia. Msimulizi anatumia sentensi ionyeshayo hisia za wanaume kumhusu Unono, 'Sura yake haikumtendea wema katika biashara yake.' Sentensi hii inamtathmini Unono kama mhusika mwenye kasoro fulani ya kimaumbile inayomkosesha bahati miongoni mwa wanaume. Katika sentensi na virai vya hapo juu, inadhihirika kwamba hisia na fikira zinawasilishwa kwa sababu ya kuwepo kwa vitenzi vionyeshavyo hisia kama vile 'alihisi', 'aliwaza' na mengineyo ili kuchimuza hali za kisaikolojia za wahusika.

Kuna vitenzi halisi ambavyo pia huweka wazi hisia za aina mbalimbali. Baadhi ya vitenzi hivyo ni 'Cheka', 'Lia', 'Kasirika', 'Ogopa' miongoni mwa viingenevyo. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, msimulizi anaeleza namna Von Iron alivyokuwa akiogopwa na maofisa aliowasimamia. Alikuwa akiwazungumzia kwa sauti ya kutisha na kuwatazama kwa macho ya kuogofya. Hivi ndivyo asemavyo msimulizi, 'Akawageukia wenzake na kuwatazama kwa lile jicho la kutisha, jicho ambalo lilikuwa msingi uliowafanya waendelee **kumuogopa** na kutomkosoa'.uk.128. Dondoo hili linatuelekeza kwenye msimamo wa wafanyikazi kumhusu kiongozi wao, Von Iron, kwamba wafanyakazi wana mtazamo hasi kwake unaosababishwa na jinsi anavyowatisha. Kwa hivyo wanaishi katika hali ya hofu na kutojiamini mbele yake.

Kando na vitenzi vya hisia, kuna vitenzi na maneno mengine ambayo huonyesha maoni ya mhusika ama msimulizi kuhusu jambo fulani. Mifano ya vitenzi hivyo ni kama vile 'Yaelekea', 'alionekana'. Wakati msimulizi anapotumia vitenzi vya aina hii, haonyeshi hali za kisaikolojia za ukweli za msemewa bali hutoa maoni yake ambayo huenda yakawa ya ukweli ama yasiwe ya ukweli kuhusu msemewa. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* msimulizi anatoa maoni yake kuhusiana na sababu zilizomfanya Mwana Wa Giningi kumpa Ali Makame shamba lake alisimamie. Msimulizi anasema, 'Kufanya hivyo labda ndio njia nzuri ya kutafuta amani, salama na mapatano baina yake na huyo babake mdogo, Ali Makame'.uk 23. Katika nukuu hili, inaonekana kwamba aidha msimulizi hana hakika kuhusu sababu zake kufanya kitendo hicho, kwa hivyo anakisia tu ama hataki kuegemea upande wowote. Kwa njia hii anachukua mtazamo wa kati kuhusu suala hilo la shamba.

3.5.2.4.2 Matumizi ya Vitenzi Visaidizi vya Uwezekano, Idhini na Masharti

Kwa mujibu wa Simpson (1993:46) vitenzi hivi huonyesha upendeleo, uwezekano ama umasharti katika lugha. Anasema kwamba maneno haya yanaweza kutumika kuonyesha mtazamo wa kisaikokojia wa msemaji kuhusu tukio, hali ama mhusika fulani. Mwelekeo huu, unatofautiana na ule wa Fowler (keshatajwa) kuhusu viashiria vya mtazamo katika sawia ya kisaikolojia. Huku Fowler akisisitiza matumizi ya 'Verba Sentiendi', Simpson anatilia mkazo kwenye vitenzi visaidizi vya uwezekano, idhini na Masharti. Misamiati inayoonyeha matamanio au kupendezwa na hali fulani huweza kutumika kuashiria mitazamo ya kisaikokolojia. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, misamiati kama 'Tamani' na 'Tumaini' imetumika kuonyesha kuvutiwa na kupendelea jambo au hali fulani hivyo kuathiri mtazamo wa kisaikolojia wa msemaji. Katika

riwaya hii, Nuru anapotazama runinga akiwa chumbani alikofungiwa huko Afrika Kusini, anavutiwa mno alipoona majumba makubwa yakiangushwa na mabomu waliyoyatega yeye na Joram Kiango. Hivi ndivyo asemavyo msimulizi kuhusiana na matamanio yake, '**Alitamani** apige ukelele wa furaha. Tangu alipoanza harakati hizo hakuwa na hakika kama walikuwa wakifanya kitu chenye uhakika'. (uk.158). Kitenzi 'alitamani', hapa ni ishara ya hisia za furaha pamoja na uzalendo wake katika kupigana na adui wa taifa lake. Vitenzi vingine vyenye jukumu sawa na hili ni 'kutumaini', 'kutaraji', 'kutaka' na viinginevyo.

Vitenzi visaidizi vya kushurutisha pia vinaweza kutumika kuonyesha mtazamo wa msemaji kwa msemewa au msemewa kwa msemaji. Maneno haya huonyesha viwango mbalimbali vya uwajibikaji baina ya wasemaji. Mifano ya maneno hayo ni, 'lazima', 'sharti', 'pasa', 'labda' na mengineyo. Katika riwaya ya *Kisima Cha Giningi,* kwa mfano, kuna maongezi baina ya Msa na Fundi Mangungu ambapo Msa anamtania na kumkejeli Fundi Mangungu kwa kuzitenganisha ndoa za watu kadhaa kwa kutumia ujanja wake. Mangungu naye kwa upande wake hatishiki na anamlazimisha Msa kuzingatia sheria za uganga na kuwacha kupinga sheria za kiganga. Mangungu anamwambia Msa, 'We kijana acha ujuba wako wa kimji huo, haukufai hapa. **Sharti** ukumbuke kuwa hapa ni Giningi**, sharti ufuate** mwendo wa watu wa hapa'. Uk.47. Fundi Mangungu anapotumia kitenzi kisaidizi cha masharti hapo juu mara mbili ni ishara kuwa anachukizwa na namna Msa anavyomkosea heshima hasa kwa kukataa kuheshimu kazi yake. Hisia za kukasirishwa na Msa zinadhihirika, Mangungu anaposema, 'Ala! We kijana acha ujuba wako wa kimji'. Anamkumbusha Msa kwamba watu wa mashambani huheshimu kazi yake kinyume na walivyo watu wa mjini kama Msa. Kwa njia hii mwandishi anawasawiri watu wa mashambani kama wanaoamini sana itikadi za kichawi.

Kauli kama hizi za ushurutishaji pia zinapatikana katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu* wakati mhusika Von Iron anapowafokea maofisa waliokuwa wakilinda chumba ambacho Nuru na Joram walikuwa wamefungiwa. Von Iron aliwaamuru namna hivi, '**Mtafuteni** haraka, aletwe akiwa hai, atakufa pole pole kama mbwa wenzake'.(uk.128). Kauli kama hii iliyojaa vitisho na matusi haidhihirishi tu mtazamo wake wa kisaikolojia kuwahusu askari hao, bali pia inaashiria mtazamo wake kuhusu ubaguzi wa rangi, ambapo Von Iron anawaona Waafrika kama mbwa. Hali ya kisaikolojia inayomsumbua ni kuwa amekasirishwa na jinsi Joram alivyotoroka jela bila walinda jumba hilo kutambua.

Simpson (1993:48) anaeleza kwamba kuna maneno mengine yanayotumiwa kuonyesha viwango mbalimbali vya ukweli katika kauli au sentensi. Anasema kuwa kuna viwango vya chini na vile vya juu zaidi kuhusu hali za ukweli kulingana na kiwango cha ushuhuda kinachobebwa na kauli hizo. Kauli zenye viwango vya juu vya ukweli zinaaminika zaidi. Viwango vya chini vya ukweli huashiriwa na maneno kama 'dai', 'pengine' na mengineyo. Kiwango cha kati cha ukweli kinaashiriwa na maneno kama vile 'Labda'. Kiwango cha juu nacho huashiriwa na maneno kama vile 'hakika', 'bila shaka', 'kwa kweli' na mengineyo. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* mpelelezi Far Katy Wingo akisumbuliwa na mawazo chungu nzima kuhusu ni nani mhusika katika mauaji ya watu wa familia ya Mzee Jacob, anazuru maeneo mbalimbali ya mjini na mashambani kufanya uchunguzi wake. Linalomshangaza zaidi ni kuwa kila wakati mtu anapouawa anapigiwa simu na mtu anayejiita, Fambo. Msimulizi anasema, 'Alielewa kuwa kama angempata yule anayejiita Fambo, **bila shida** yoyote angempata muuaji. **Labda** alikuwa yeye mwenyewe Fambo'.uk.71. Neno 'Labda' katika nukuu hili linatuonyesha kiwango cha kati cha ukweli kuhusu uwezekano wa Fambo kuwa ndiye muuaji. Msimulizi anaona huenda ikawa Fambo ndiye muuaji au ikawa si yeye. Msimulizi hamwambii msimuliwa moja kwa moja ukweli wa mauaji haya, bali anajitenga na kuiacha taharuki itande. Hata hivyo, anaonyesha kiwango cha juu cha uaminikaji anaposema kwamba ikiwa angempata Fambo, basi kazi yake ingekuwa rahisi. Usumbufu wake wa kisaikolojia unajitokeza tena wakati anapopigiwa simu. Anajiuliza, 'Sasa huyo muuaji ni nani? **Labda** ndiye Fambo mwenyewe. Lakini ikiwa ndiye, kwa nini apige simu kunieleza? Huwa anataka nini kwangu?. Uk.32

Katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa,* Salima anatamani kwenda dansini ili ashuhudie bendi ya Azimio Jazz lakini ana shaka ikiwa angemwona mwimbaji mashuhuri ampendaye au la. Kupitia usimulizi wa mtazamo wa nje, msimulizi anasema, 'Salima alifikiri **labda** yule mwimbaji wa zamani alijiuzulu kwenye bendi ile au siku hiyo alikuwa akijipumzisha akimpa nafasi mwenzake'. Uk.21. Kutokuwa na hakika kumhusu mwimbaji huyu kunamtatiza Salima kiakili na baada ya muda mfupi, hakuweza kuendelea kukaa katika jumba hilo la mziki. Kwa hivyo, ukosefu wa mwimbaji mmoja unaathiri mtazamo wa Salima kuhusu bendi nzima ya Azimio Jazz. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu***,** msimulizi ametumia maneno, 'bila shaka' kuonyesha hali ya juu ya ukweli kuhusu akisemacho. Akishangazwa na kitendo cha Joram Kiango cha kulipiza kisasi kwa kulipua majumba kadhaa jijini Johanesburg, Von Iron aliwaza kuhusu ni nini dhamira ya Joram. Kwanza, Von alichukulia kwamba ulikuwa wazimu tu wa Joram lakini baadaye akagundua

kuwa ni ulipizaji wa kisasi dhidi ya maafa yaliyokuwa yakipangwa na makaburu dhidi ya baadhi ya nchi za Kiafrika. Von anasema, **Bila shaka** alikuwa akijifariji kwa kumwaga damu zisizokuwa na hatia'. Uk. 129. Katika kauli hii, kuna kiwango cha juu cha uaminikaji kwa kuwa msimulizi anatoa hakikisho la ukweli huo. Hakikisho hilo linamwepushia msimuliwa jukumu la kufasiri msukumo wa Joram wa kuyachoma majumba ya jiji hilo, Afrika Kusini.

Tunapata matumizi ya kirai 'Bila shaka' pia mara kadhaa katika riwaya ya *Simu ya Kifo*. Huku Inspekta Wingo akitathmini wahusika wanaoweza kushukiwa kwa mauaji ya Mzee Jacob, anafikiri uwezekano wa mwanawe, Geva, kuhusika katika mauaji hayo. Hata hivyo, anamwondoa lawamani Geva kwa kufahamu kwamba Geva alikuwa anampenda babake, hivyo hawezi kuwa ndiye aliyemuua. Wingo anasema, 'Na kama hakumuua babake basi alikuwa anampenda. Geva **bila shaka** alichukizwa na mtu aliyemuua babake'. Uk.67. Kirai 'Bila shaka' kinatumika kumhakikishia msimuliwa kwamba kuna mhusika mwingine aliyemuua babake Geva na hivyo kumzidishia hamu ya kuisoma hadithi yote hadi mwisho ili amjue huyo mhalifu. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* Proper anapokutana na washirika wake ili kupanga mikakati ya kuwaua viongozi wengi wa Kiafrika na kupindua serikali za nchi nyingine, anawahakikishia wajumbe wake kwamba ni lazima Joram auawe kabla ya mpango huo wao kuendelea. Anasema kwamba wanafaa kutumia mbinu za kisayansi ili isijulikane Joram alikufa vipi. Proper anasema, 'Daktari ataupima mwili wake na kuona kuwa kafa kutokana na kansa ya moyo. Atauawa kitaalamu na kufa kistaarabu. **Msiwe na shaka'**.uk.3. Kirai 'msiwe na shaka' kinatuonyesha kwamba msemaji anatoa kauli ya kweli na kuwa mtazamo wake kuhusu mipango yake ni wa kupendeza. Yaani Proper anapendezwa na mauaji anayoyapanga na mapinduzi ya kiserikali. Kwa kutumia kirai hicho, anaaminika zaidi na wenzake na kwa njia hiyo kujenga uhusiano bora baina yao.

Kiwango cha chini cha uaminifu na ukweli kama tulivyodokeza hapo awali kinaashiriwa na misamiati kama vile 'dai', 'onekana' na matumizi ya vikanushi vya hali za ukweli kama vile 'kuna shaka', 'lililotiliwa shaka' miongoni mwa maneno mengine. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* tunaona hali hii ya shaka kutoka kwa wanajeshi wakizungumza na mkuu wao. Kikosi cha ulinzi wa anga kinampigia simu mkuu wa jeshi kumwarifu kuhusu ndege iliyombeba Joram Kiango na mpenzi wake Nuru. Askari hao katika simu wanasema:

> Rubani wa ndege hiyo anaomba kutua **akidai** kuwa ametekwa nyara na abiria hao ambao wamejitambulisha kama Joram Kiango na mpenzi wake Nuru. Tunauliza kama tuwaruhusu kutua ama tuwalipue. (uk.103).

Afisa wa kijeshi anayetoa ripoti hii, anaonyesha kuwa haamini maneno ya rubani kuwa alikuwa ametekwa nyara. Angetaka mkuu wa jeshi naye achukue mtazamo kama huu ili awaruhusu kuwalipua walioko ndani ya ndege hiyo. Hii ni kwa sababu neno 'dai' linamwelekeza msimuliwa kwenye ukosefu wa ushuhuda na ukweli. Kwa hivyo, matumizi ya vitenzi visaidizi kama hivi yana uwezo wa kuubadili mtazamo wa anayezungumziwa ili akubaliane na mtazamo wa msemaji.

Katika sehemu hii, tumeangazia suala la mtazamo kwa upana kwa kujikita katika sawia nne za mtazamo. Sawia hizo ni mtazamo wa kiitikadi, kiisimu, wakati na mahali na mwishowe sawia ya kisaikolojia. Tumeona kuwa baadhi ya masuala yanayojitokeza katika sawia moja pia yanaweza kudhihirika katika sawia nyingine. Kwa hivyo tofauti baina ya viwango hivi si bayana sana kwa kuwa kuna mwingiliano wa viwango vya mtazamo. Kwa mfano baadhi ya masuala ya sawia ya kiisimu, ndiyo pia yanayodhihirisha mtazamo katika sawia ya kisaikolojia na mwanda-wakati.

### 3.6 Simulizi Tegemezi


Rimmon-Kenan (2002:91) anaeleza kwamba mhusika ambaye vitendo vyake vinasimuliwa katika hadithi, naye pia anaweza kusimulia visa vingine ama matendo ya wengine. Katika kisa akisimuliacho mhusika huyu, panaweza pia kuwa na mhusika mwingine anayesimulia kisa kingine. Upangiliaji huo wa visa mbalimbali unasababisha hali ambapo kuna ngazi au viwango vya simulizi. Viwango hivi vya simulizi hujitokeza kidaraja ambapo kila kisa kinachojitokeza huwa kiko katika ngazi ndogo kuliko kisa kilichokitangulia. Kwa hivyo, hadithi inaweza kuwa katika daraja ya kwanza, ya pili, ya tatu na kadhalika.

Bal (2017:53) akifafanua uhusiano uliopo baina ya hadithi kuu na hadithi tegemezi anasema kwamba uhusiano huo ni sawa na ule wa kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi changamano. Anaeleza kwamba hadithi ya msingi na hadithi tegemezi zinaweza kuwa na uhusiano wa karibu sana hivi kwamba zinakosa kutofautika kibayana ama zikawa tofouti kabisa huku tofouti zao zikijitokeza wazi. Bal anajadili kuwa ikiwa msuko wa hadithi tegemezi umekuzwa sana ni rahisi kwa msomaji kuisahau hadithi msingi. Hali hii inatokana na kweli kwamba hadithi tegemezi inabuniwa katika ulimwengu mpya na kuwahusisha hata wahusika wapya. Anaeleza kwamba katika baadhi ya vipera vya simulizi kama vile hadithi za kutahadharisha, hadithi tegemezi inaweza


kuwa ndio ndefu kuliko hadithi msingi (uk.53). Katika mfano kama huu, hadithi tegemezi huwa tu na jukumu la kuifafanua hadithi msingi.

Genette (1980:85) alieleza kuwa hadithi msingi inaweza kubeba vijihadithi vingine ambavyo huwa katika daraja mbalimbali kama vile daraja ya kwanza, pili na tatu. Bal anatoa mfano wa *The Arabian Nights,* anafafanua kwamba visa vingi vifupi vinaweza kupangiliwa kidaraja kwenye simulizi msingi hadi daraja ya nane. Hata hivyo anakubali kuwa mara nyingine hadithi tegemezi inaweza kuchukua nafasi kubwa kuliko hadithi msingi. Genette alitumia kielelezo kifuatacho kuonyesha uhusiano kati ya hadithi msingi na hadithi tegemezi.

**Kielelezo 3.1 Kielelezo cha hadithi msingi na hadithi tegemezi**




**Kielelezo 3.2 Kielelezo cha hadithi tegemezi za daraja tofauti**





Katika kielelezo 1, hadithi msingi ni ‘A’ huku hadithi tegemezi ikiwa ‘B’. Katika kielelezo 2 hadithi msingi ni ‘A’ huku hadithi B na $B^1$ zikiwa za daraja ya pili, nayo hadithi C ikiwa ya daraja ya tatu. Hadithi msingi huwekwa katika daraja la kwanza huku nazo hadithi tegemezi ukiwekwa katika daraja la pili. Ikiwa kuna hadithi tegemezi ndani ya hadithi tegemezi nyingine, nayo inachukua darala la tatu na kuendelea. Hata hivyo, ikiwa kuna hadithi tegemezi kadhaa ambamo hamna iliyo ndani ya nyingine, basi zote zipo katika daraja moja, kama inavyoonyeshwa katika kielelezo 3 hapa chini. Wamitila (2008:138) pia ana maoni sawa na ya wahakiki hawa kuhusu

uhusiano baina ya hadithi msingi na hadithi tegemezi. Anaeleza kwamba hadithi tegemezi inaweza kukuzwa na kuchukua nafasi kubwa kuliko simulizi msingi.

Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, uhusiano baina ya simulizi msingi na simulizi tegemezi unajitokeza zaidi katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*. Riwaya hii inaonyesha uhusiano wa utegemezaji katika viwango vitatu. Yaani hadithi kuu na hadithi tegemezi za daraja ya kwanza na pili. Hadithi kuu inahusu wizi wa mali ya Mwana wa Giningi na uchunguzi kuhusu ni nani aliyeiba mali hayo. Hata hivyo, kuna hadithi kadhaa zilizotegemezwa katika hadithi hii. Kwa mfano, kuna hadithi kuhusu usuli wa Mwana wa Giningi na jinsi alivyokuja kuishi katika eneo la Giningi na hadithi kuhusu utapeli wa Fundi Mangungu. Pia kuna kijihadithi kuhusu uajabu wa Kisima cha Giningi na zote zipo katika daraja ya pili. Katika daraja ya tatu kuna hadithi ya Habusa na vyumba saba. Kijihadithi cha Habusa na vyumba saba kipo ndani ya hadithi inayohusu usuli wa Kisima cha Giningi. Habusa ni msichana anayepatikana majini na ambaye inaaminika kwamba akitupiwa vyakula anuwai kama vile mayai huweza kuvuta Baraka. Inaaminika kwamba kumpa zawadi Habusa kunasaidia kujibika kwa maombi kwani lolote liombwalo kwa jina lake hutendeka. Kisa hiki ni kama kisasili katika fasihi simulizi kwani kinasaidia kuajabisha Kisima cha Giningi kando na kueleza asili ya uajabu huo. Kwa kuirejelea riwaya hii, tunaweza kutumia kielelezo kifuatacho kuonyesha uhusiano baina ya hadithi msingi na hadithi tegemezi:

**Kielelezo 3.3 Kielelezo cha Genette kinachoonyesha hadithi kadhaa tegemezi ambazo ziko kivyake**



### 3.6.1 Dhima ya Hadithi Tegemezi

Kulingana na Bal (2017:53-55) hadithi tegemezi inaweza kuwa tofauti kabisa na hadithi msingi, inaweza kuwa kifuatilizi chake, au hata ikawa sawa kabisa na hadithi msingi. Pia hadithi tegemezi inaweza kuwa inaipinga ile ya msingi. Kwa sababu hii, hadithi tegemezi inafaa kuchunguzwa kama elementi huru na pia kwa kuhihusisha na hadithi msingi ili kupata maana ya hadithi tegemezi na maana inayohusishwa na hadithi msingi. Mahusiano baina ya hadithi katika ngazi hizi mbili, msingi na tegemezi, yanafichua kuwa hadithi tegemezi ina majukumu kadhaa. Hadithi tegemezi hutekeleza majukumu yafuatayo katika simulizi:

#### 3.6.1.1 Dhima ya Kiufafanuzi

Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan, hadithi tegemezi hufafanua hadithi msingi kwa kurejelea masuala ya kitambo yaliyochangia kuibuka kwa muktadha wa sasa katika usimulizi. Hadithi hizo hujibu maswali kama vile ni nini kilichochangia hali ya sasa ya mhusika. Ujibiwaji wa swali kama hili, aghalabu hujitokeza kupitia hadithi tegemezi ambayo inaweza kufafanua usuli wa hali au mhusika kama vile maisha yake ya utotoni, alivyolelewa, elimu yake, ndoa yake na mengineyo na namna usuli huo unavyoathiri hali ya sasa ama tukio la sasa. Aghalabu matumizi ya analepsia huwezesha maelezo hayo kufanyika. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* kwa mfano, kuna kisa kinachofafanua usuli wa Mwana wa Giningi. Maelezo hayo yanasaidia kuelewa upweke anaoishi nao kwa kuwa yeye ni kama mgeni katika eneo analoishi. Kisa kinaeleza kwamba aliletwa katika eneo la Giningi na babake kutoka Saadani ambako alitenganishwa na mamake akiwa mchanga na kulelewa na ajuza. Ufafanuzi unaotolewa na kijihadithi hiki unamwezesha msimuliwa kuielewa saikoljia ya mhusika huyo pamoja na mahusiano yake na wahusika wengine wa karibu kamavile babake, Ajuza aliyemlea na mjombake, Ali Makame.

Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* kuna hadithi fupi inayofafanua asili ya uovu wa mhusika Proper. Hadithi hii tegemezi inasimulia kwamba Proper alizaliwa katika eneo fulani karibu na pwani ya Bahari ya Hindi. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili alitoroka nyumbani kwao kwa kudandia meli moja iliyotia nanga katika Bandari ya Tanga. Humo, alilakiwa na mabaharia wakatili waliomtendea maovu mengi lakini akayavumilia. Mwishowe akashika unyama wa mabaharia wale. Alimchukia kila mtu na hata kuichukia nafsi yake. Katika kisa hiki, mwandishi anatuonyesha jinsi mambo ya utotoni yanavyoishia kuwa msingi mkuu katika tabia ya utu uzima kama inavyoelezwa na wanasaikolojia Bandura Albert (1976:122) na Sigmund Freud (1905:123-

246). Hadithi hii imetumika kufafanua hali ya sasa ya Judor Proper ya kutaka kuwaua, kwa kuwapa sumu marais na mawaziri wanaokutana mjini Arusha. Proper alikuwa amefanya maovu mengine mengi kama vile kuwanajizi wanawake kadhaa na kisha kuwakata koo, kuwatupa watu baharini wanaodandia meli na mengine. Hadithi hii imetegemezwa kwenye hadithi msingi inayohusu jinsi wasaliti wa ndani ya nchi wanavyoshirikiana na adui wa nje katika kusambaratisha nchi za Afrika, hususan nchi zilizokuwa zikiyasaidia mataifa ya Kusini mwa Afrika kupigania uhuru wao. Yaani, mchango wa Tanzania katika kuyakomboa mataifa ya Namibia, Msumbiji, Zimbabwe Angola na Afrika Kusini.

3.6.1.2 Dhima ya Kidhamira

Hadithi tegemezi inaweza kutumika kuendeleza dhamira ambazo aidha zaweza kuhusiana na hadithi msingi ama zikawa tofouti nayo. Utekelezaji wa jukumu hili unaweza kutokea kupitia uhusiano wa moja kwa moja na hadithi msingi ama uhusiano wa kianalojia ambapo hadithi tegemezi inahusishwa kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja. Kwa kuwa riwaya za kiupelelezi kama kijipera cha fasihi pendwa aghalabu hutumia mtindo sahili ili ziburudishe kwa urahisi, hadithi tegemezi za kianalojia au kisitiari hazitumiki sana. Vijihadithi vinavyotumika ni vile vinavyojenga uhusiano wa moja kwa moja na hadithi msingi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* dhamira ya ubaguzi wa rangi inakuzwa kupitia hadithi tegemezi. Hadithi hii inahusu namna Mzungu mmoja, Von Iron, alivyomiliki mgodi ambapo aliwaajiri watu weusi aliowanyanyasa mno. Walilipwa hela kidogo na kufanyishwa kazi ngumu na hatari. Dhamira hii inahusiana na dhamira pana ya uhusiano wa kimataifa hususan suala la ukoloni na ukoloni mamboleo. Hadithi kuu inahusu jinsi utawala wa kikoloni Afrika Kusini ulivoyadhulumu mataifa jirani kama vile Angola na Namibia. Katika *Simu ya Kifo*, kuna kisa kinachotolewa na Agnes kwa mpelelezi Far Katy Wingo kuhusu namna Mzee Jacob alivyoidhulumu familia yao kwa kumuua mamake Agnes na kuchoma nyumba yao. Agnes anakiri kwamba yeye ndiye aliyewaua watu wa familia ya Jacob lili kulipiza kisasi cha mauaji ya mamake. Kisa hiki kinaendeleza dhamira ya ulipizaji kisasi ambayo inahusiana kuu ambayo ni mauaji ya Mzee Jacob na familia yake na uchunguzi wa mauaji hayo.

3.6.1.3 Dhima ya Kiutekelezaji (uwekaji msingi wa kimsuko)

Rimmon-Kenan (2002:95) anaeleza kwamba kando na kufafanua maudhui na kutekeleza jukumu la ufafanuzi, hadithi tegemezi pia hukuza msuko wa hadithi kuu. Baadhi ya vijihadithi tegemezi

husaidia kuboresha msuko wa hadithi kuu kwa kuuchelewesha usifikie kilele mapema. Katika utanzu wa riwaya za kiupelelzi, ucheleweshaji wa kilele cha msuko unaandamana na taharuki inayotokana na hadithi tegemezi. Kwa mfano katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, Msa na Amanullah wanapokutana katika meli, Amanullah anampa Msa hadithi kuhusu alivyoota mara tatu. Katika ndoto hiyo, alimwona mtu akimjia katika ndoto na kumwambia aende Darsalama ilia pate mafanikio yake huko. Hadithi hii ya Amanullah inakuwa msingi wa hadithi kuu kwa kuwa kuanzia hapo, msuko wa riwaya nzima unahusu maisha ya Amanullah na dadake, Sichana, walivyolelewa na wazazi wa kupanga waliowatenganisha na kuwapoka urithi wao. Hadithi ya ndotoni ni tegemezi huku ile kuu ikihusu namna Sichana na Amanullah walivyotenganishwa, wakapoteza urithi na uchunguzi wa walikoenda na kuhusu ni nani aliyechukua urithi wao.

Ingawa mtindo wa hadithi tegemezi unaotumika zaidi katika simulizi nyingi ni ule unaohusu wakati uliopita, kuna uwezekano wa kubuniwa kwa hadithi tegemezi inayojikita katika wakati ujao. Rimmon-Kenan (93) anasema kwamba ingawa mtindo huu hautumiki sana katika simulizi, aghalabu hutumika kiubashiri katika baadhi ya hadithi hasa zile za Bibilia. Anaongeza kwamba mtindo wa kutumia wakati ujao katika simulizi hupatikana katika hadithi ndani ya hadithi kama ubashiri, kulaani au kama ndoto za wahusika wa kibunilizi. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (uk.62-63), Proper anawasimulia kuhusu mkutano unaotarajiwa wa viongozi wa nchi za msitari wa mbele uliokuwa unapangwa ili kujadili ukombozi wa Namibia. Anawaambia kuwa angetaka siku hiyo ikifika viongozi hao wauawe wote ili liwe jambo lisilosahaulika katika historia. Anawaeleza hivi, ‘Safari hii nataka wafe wengi pamoja. Huenda wakaanguka wote pamoja juu ya meza zao. Kwa kweli litakuwa jambo la kufurahisha sana’.uk.62 Usimuliaji wa kisa hiki katika wakati ujao unasaidia kukuza taharuki ya hadithi nzima na kuzua mgogoro ambao ndio kiini cha mapambano yaliyoko katika hadithi kuu katika ya mpelelezi na mhalifu. Kwa hivyo, kisa hiki kinaweka msingi wa msuko wa hadithi nzima. Tukio la kihistoria la mvutano baina ya nchi zilizopinga uhuru wa mataifa ya Kusini mwa Afrika na zile zilizounga mkono juhudi hizo linatumika kisanii kuangazia suala la uhusino wa kimataifa

Katika riwaya ya *Uchu* (2000:70-73), mpelelezi Willy Gamba anasafiri hadi nchini Rwanda kuchunguza namna mauaji ya halaiki yalivyofanyika nchini Rwanda bila ya mataifa jirani kusaidia kukomesha hali hiyo. Anapofika anaelekezwa kwenye kituo cha Centre Christus ambapo anasimuliwa matukio ya historia ya ukoloni na mchango wa wakoloni katika kusababisha vita vya

kimbari nchini Rwanda. Anasimuliwa hadithi na Padri Sibomana na Padri Karangwa. Katika hadithi hiyo tegemezi, Padri Karangwa anamthibitishia Willy kwamba chuki za kikabila baina ya Wahutu na Watutsi zililetwa na mkoloni kupitia mbinu ya tenga utawale. Hadithi hii tegemezi inamwezesha mpelelezi Willy kuelewa asili ya mzozo wa Rwanda uliopelekea mauaji ya takribani watu laki nane. Hadithi hii inaboresha ujenzi wa msuko kwani inachelewesha kilele cha hadithi pamoja na kujenga taharuki.

### 3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumelishughulikia suala la usimulizi kwa kuchunguza sauti za kisimulizi na mtazamo katika riwaya teule za kiupelelezi. Imebainika kuwa riwaya tunazozichunguza zimesimuliwa kupitia mtazamo nje. Ubora wa mtazamo huu unajitokeza kupitia uwezo wake wa kutodhihirisha hisia za kibinafsi. Pia mtazamo huu, humwezesha msimulizi kutoa tathmini ya masuala anayosimulia. Hali hii inatokana na ukweli kwamba msimulizi si mmoja wa wahusika bali ni mtazamaji aliye kando na masuala ayasimuliayo hivyo kuibua utondoti. Hii ni kinyume na usimulizi ndani ambao huendelezwa na msimulizi mhusika. Hata hivyo, imeonyeshwa kwamba usimulizi ndani pia una ubora wa kuyafupisha masafa baina ya msimulizi na msimuliwa. Kwa hivyo, msimulizi anayetumia mtazamo ndani anakuwa na uhusiano wa karibu zaidi na masuala anayosimulia na msimuliwa.

Tumeona kwamba mtazamo hujitokeza katika viwango au sawia mbalimbali kama vile sawia ya kisaikolojia, mwanda-wakati, kiitikadi na sawia ya kiisimu. Sawia hizi zinaingiliana na kuchangizana. Kwa mfano, sawia ya kiisimu inakuwa msingi bora unaofanikisha ujitokezaji wa sawia za kisaikolojia, mwanda-wakati na itikadi. Imebainika kwa mfano kwamba msimulizi hutumia vipengele maalum vya lugha kama vile misamiati teule ili kumuelekeza msomaji kuhusu mwelemeo wake wa kiitikadi. Vile vile sawia ya kiisimu inakuwa msingi bora wa kuchunguzia sawia ya mwanda-wakati, kwa kuwa vipengele vya kisarufi kama vile vivumishi vionyeshi ‘hapa’, ‘kule’, ‘hapo’, miongoni mwa viinginevyo hutumika. Virai vinavyoonyesha wakati kama ‘leo’, ‘leo hii’, ‘siku hiyo’ hutumika kuonyesha mwanda wakati. Tumechunguza pia suala la usimulizi tegemezi ambapo imebainika kwamba hadithi tegemezi inaweza kujitokeza katika viwango mbalimbali na kutekeleza majukumu mbalimbali hususan kuifafanua hadithi msingi. Katika sura ijayo, tunachunguza suala la msuko na namna mbinu za kimtindo zinavyotumika kisanaa kufanikisha ukuzaji wa msuko.

# SURA YA NNE

# UHUSIKA KATIKA RIWAYA YA KIUPELELEZI YA KISWAHILI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza namna usawiri wa wahusika unavyotekelezwa kwa njia maalum inayobainisha utanzu huu wa riwaya ya kiupelelezi na kuutenga na tanzu nyinginezo za riwaya. Kwa kuchunguza mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya teule za kiupelelezi, tutakuwa tumetimiza lengo la pili la utafiti huu. Misingi ya kinadharia ya Utanzu itatumika katika kufafanua suala la uhusika kwa kuwa riwaya ya kiupelelezi ina sifa maalum za kihusika kama vile kuwepo kwa wahusika wa aina tatu: mpelelezi, mhalifu na mhaasiriwa, miongoni mwa kanuni nyingine. Baadhi ya mihimili ya nadharia ya umitindo kama vile miktadha ya lugha za wahusika na mchango wa kauli zao katika uhusika, itatumika.

Suala la uainishaji wa wahusika ni changamano na lenye utata mwingi. Hii ni kwa kuwa waandishi na wahakiki mbalimbali wamewaweka wahusika katika makundi tofautitofauti kwa misingi ya majukumu yao na hulka zao. Kwa mfano, baadhi ya wahakiki wanawainisha wahusika wao kwa misingi ya kijadi ilibuniwa na Forster (1921) ya ubadilikaji au kutobadilika kwa mhusika. Forster (1986:69) anatumia misingi ya mtazamo na ubadilikaji katika kuwaainisha wahusika. Anawaweka wahusika katika makundi makuu mawili ambayo ni; wahusika bapa na wahusika duara. Kulingana na Forster, mhusika duara ni yule mwenye uwezo wa kumshtukiza msomaji kwa njia ya kiushawishi. Naye husika bapa ni mhusika anayekosa sifa hiyo. Hata hivyo, uainishaji huu umekosolewa na wahakiki wengi kwa kuwa unakosa utondoti na pia vigezo vya kupimia ubapa ama uduara hutofautiana kutoka kwa msomaji mmoja hadi mwingine. Abbott (2002:127) kwa mfano, anaukosoa uainisho wa Ki-Forster akisema wahusika bapa wana kiasi fulani cha uduara na vilevile wahusika duara nao wana kiasi fulani cha ubapa. Anaendelea kusema,

> Kuwafinya wahusika katika kategoria ni kuwanyima nafasi ya kuonyesha utu wao. Ni kuwanyima wahusika uwezo wa kutushtukiza kupitia tabia zao zinazozidi zile tunazozijua. (uk.129).T.Y

Nukuu hili linaonyesha ugumu uliopo katika kuzungumzia aina za wahusika katika kazi za kifasihi. Maoni kama haya ya Abbott yametolewa pia na Rimmon-Kenan (2002) ambaye anakosoa dhana ya ubapa akisema kwamba inaashiria ukosefu wa uhai wa mhusika.Wamitila (2002:22) pia anahoji kuwa uainishaji huu unaishia kuwapuuza wahusika wapatikano katika kazi za kiupelelezi

na visasili, kwani wote huwekwa katika kundi moja la wahusika bapa. Hata hivyo, kando na shutuma zilizopo kuhusu uainishaji wa Ki-Forster, uainishaji huu umeendelezwa na wahakiki kama vile Mohamed (1985), Njogu na Chimerah (1999) na wengineo. Kwa misingi hii, Mohamed anapata wahusika wa aina tatu: (a) Mhusika Mviringo, (b) Mhusika bapa na (c) Mhusika kinyago. Nao Mlacha na Madumulla (1995:23-28), wanachunguza ukuaji na maendeleo ya mhusika mkuu katika riwaya ya Kiswahili na wanaainisha kategoria nne za wahusika wakuu wanaobainika katika riwaya ya Kiswahili kutoka enzi ya Shaaban Robert hadi miaka ya themanini. Wahusika hao ni:

Kwanza, mhusika mkwezwa- Huyu ni mhusika mwenye uwezo usio wa kawaida na huumbwa kama kielelezo cha kuigwa. Aghalabu hutumiwa na waandishi kama kiwakilishi cha itikadi zao hususan itikadi zinazohusu ujenzi wa jamii mpya. Huyu ni mhusika anayepatikana katika hadithi za fasihi simulizi na riwaya za mapema za Kiswahili kama vile riwaya za miaka ya 1950 hasa kazi za Shabaan Robert kama vile mhusika Adili katika *Adili na Nduguze* (1952). Aina hii ya mhusika pia hupatikana katika riwaya pendwa hasa zile za kiuhalifu na riwaya za kiupelelezi. Baadaye tutazichambua sifa hizi kwa kina katika riwaya teule tukizingatia mhusika mpelelezi kwa kuwa amesawiriwa kama mkwezwa. Udhaifu wa mhusika huyu ukiwa ni kushindwa kwake kuwakilisha binadamu halisi. Pili, kuna mhusika wa kimapinduzi-Huyu ni mhusika anayepigania mabadiliko mema kuzuka katika jamii yake, kiuchumi na ya kisiasa. Mlacha na Madumulla wanasema kwamba wahusika wa kimapinduzi walianza kujitokeza katika riwaya ya Kiswahili miaka ya sabini na themanini. Wasifu wao wa kiutu unajidhihirisha katika upiganiaji wao wa mageuzi. Wahakiki hawa wanaendelea kusema kwamba ujitokezaji wa wahusika wa kimapinduzi ulitokana na usambavu wa fikira za Kimaksi zilizoletwa na viongozi wa Afrika kama vile Julius Nyerere na Kwame Nkrumah. Ni katika kipindi hiki pia ambapo juhudi za ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika zilipamba moto (Angola, 1975, Msumbiji, 1975, Namibia 1990 na Afrika Kusini 1994) pamoja na vita dhidi ya ubaguzi wa rangi.

Aina ya tatu inahusu mhusika mkuu wa kisaikolojia. Huyu ni mhusika mkuu anayedhihirisha ukataji tamaa kutokana na masaibu yaliyomfika kutokana na mazingira yake. Ana unyonge wa kimwili na kiakili na ufahamu usio mpana. Mhusika wa kisaikolojia huwa na uwezo wa kuyaangaza mawazo ya ndani na kudhihirisha tafakari nzito. Pia husawiriwa kama aliyekosa malezi bora kutoka kwa jamii yake. Kwa hivyo, yuko katika hali ya ukiwa na kutojitegemea. Ingawa yuko katika hali hii duni, anaonyesha hali hafifu ya kujitetea dhidi ya wakandamizaji.

Mifano mizuri ni wahusika wakuu katika riwaya za *Kiu* na *Nyota ya Rehema*[5]. Pia katika riwaya za kiupelelezi za Mohammed Said Abdulla, Mhusika Bwana Msa huweza kuchukuliwa kuwa yuko katika hatua pevu ya kuwa mhusika wa kisaikolojia. Nne, mhusika jumuia-Huyu anaweza pia kuitwa mhusika mwakilishi kwa kuwa ni wahusika wengi katika umbo la mhusika mmoja. Yaani anakuwa na sifa za wahusika wengi na kwa sababu hiyo yeye ni kama kiwakilishi chao.

Njogu na Chimerah (1999:40) wanakubaliana na uainishaji uliofanywa na Mlacha na Madumulla hasa kuwepo kwa mhusika mkuu mkwezwa, wa kisaikolojia, kimapinduzi na mhusika jumuia lakini nao wanawaweka wahusika wao katika matapo matatu makuu ambayo ni wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Tofauti na uainisho wa Mlacha na Madumulla ambao walimchunguza mhusika mkuu peke yake, Njogu na Chimerah wanaainisha wahusika kijumla. Zaidi ya hayo, walichunguza aina nyingine za wahusika ambazo ni mhusika duara, mhusika bapa na mhusika shinda.

4.2 Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Katika sehemu hii tunachunguza mikakati inayotumiwa na waandishi katika ujenzi wa wahusika na maendelezo yao. Tumekwishatambua kuwa kijumla wahusika huweza kuainishika katika makundi manne au matatu kulingana na mawazo ya wahakiki Mohamed (1995), Mlacha na Madumula (1995) na Njogu na Chimerah (1999). Tunazingatia mikakati ya usawiri wa wahusika iliyowekwa na mwananadharia Rimmon-Kenan (2002:61-72) pamoja na mawazo ya Wamitila (2002:23-26) katika kujadili mbinu za usaawiri wa wahusika katika riwaya ya kiupelelezi. Shlomith anasisitiza kwamba kipengele chochote cha riwaya kinaweza kutumiwa kama kiashiria cha uhusika ingawa vile vile kinaweza kuwa na majukumu mengine riwayani. Kulingana na mhakiki huyu, kuna njia mbili kuu za usawiri wa wahusika: (a) Uwasilisho wa moja kwa moja na (b) Uwasilisho usiokuwa wa moja kwa moja. Katika uwasilishaji wa uhusika wa moja kwa moja vivumishi mbali mbali hutumiwa kuelezea sifa za mhusika kama vile; ‘alikuwa mtu mkarimu’, ‘wema wake haukuwa na mipaka’ na kadhalika. Uwasilishaji usiokuwa wa moja kwa moja nao hautaji sifa kwa kutumia vivumishi kama hivi bali hutumia njia kadhaa za kumuelekeza msomaji

[5] Katika riwaya hii, mhusika Rehema anapitia hali ngumu inayoashiria matatizo ya kihistoria katika jamii ya Unguja wakati wa umwinyi na ubepari wa baadaye.

ili azitambue sifa hizo mwenyewe. Tunachambua namna aina hizi mbili za usawiri zilivyotumika katika riwaya za kiupelelezi tulizoteua**.**

4.2.1 Uwasilishaji wa Moja kwa Moja

Uwasilishaji huu ni sawa na usawiri wa wahusika kwa njia ya kimaelezo au ya kimajazi. Uwasilishaji wa wahusika kwa njia ya majazi pia huweza kuonekana kama wa moja kwa moja kwa sababu majina yao yanaweza kulinganishwa na maelezo. Maelezo kuwahusu wahusika yanaweza kutekelezwa kwa njia mbili kuu: (a) Maelezo ya msimulizi kumhusu mhusika fulani na (b) maelezo yatolewayo na mhusika mmoja kumhusu mhusika mwingine. Mbinu ya kumtegemea msimulizi kudhihirisha wasifu wa mhusika inapendelewa kwa sababu kadhaa. Kwanza, Wamitila (2002:23) anasema kwamba mwandishi anapotumia njia hii anapata fursa ya kuonyesha chuki au mapenzi yake kumhusu mhusika huyo. Pili, anasema kwamba hii inakuwa njia rahisi ya kueleza wasifu wa mhusika ambao ungechukua muda mrefu ikiwa mbinu nyinginezo zingetumika. Naye Arege (2012:156) anatuambia kwamba kutumia njia hii kunamnyima msomaji uhuru wa kumtathmini mhusika mwenyewe. Kufanya hivi kunamlazimisha msomaji kuridhika na msimamo wa mwandishi.

Maelezo ya mhusika kumhusu mhusika mwingine nayo ingawa yanaweza kutupa wasifu au tabia za wahusika hao, mara nyingine hukumbwa na mwingilio wa hisia za kibinafsi ambazo huvuruga ukweli kuhusu sifa hizo. Kwa sababu hii, maelezo ya mhusika kumhusu mhusika mwingine yanahitaji kutolewa ithibati nyinginezo kwa kutumia vigezo vya aina nyingine vya usawiri. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, tunaona usawiri kwa njia ya moja kwa moja kutokana na mifano ifuatayo: Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* Mhusika Kasim anaelezwa na msimulizi hivi:

> Taa zilimmulika Kasim Hakimu Marjani na kutuonyesha kuwa yeye ni kijana kiasi, si chini ya miaka thelathini, mwembamba tena mrefu, hadharani wa rangi, kavaa koti na suruali namna moja na kichwa chake ki wazi kutuonyesha nywele zilizochanwa na kupasuliwa katikati.(1973:3)

Kwa njia hii ya maelezo ya mwandishi/msimulizi tunaona wasifu wa nje wa Kasim, mtoto wa Hakimu Marjani na kwa hivyo kufanikiwa kutupatia taswira ya umbo lake. Ingawa maelezo haya hayatuonyeshi sifa zake, maelezo ya kitabia yanaletwa baadaye ili msomaji aelewe umbo la ndani

baada ya kumuelewa kwa nje na kwa njia hii, amuelewe kikamilifu. Katika kurasa za baadaye wasifu wake sasa unatokeza hivi:

> Kasim hakusimama ila kamarini kwa Rehani. Ilivyokuwa kwake ni lazima alewe ijapokuwa kidogo kabla hajababahatisha kucheza.(uk.14.)

Katika mwendeleo huu wa usawiri wa wahusika, inadhihirika kwamba wasifu wa kindani ndio unafuata ule wa nje. Kwa mfano, sasa mwandishi anatufichulia kuwa Kasim ni mpenda kucheza kamari na ili kufanikisha tabia hii ya uchezaji kamari, yeye hupenda kulewa kwanza. Kwa hivyo, Kasim hupenda vileo. Kama tulivyodokeza hapo juu, mhusika mwingine anaweza kuwa ajenti wa kufafanua sifa za mhusika mwingine. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), mhusika Inspekta Kombora anatufichulia uajabu wa mpelelezi, Joram Kiango. Mshangao na uajabu vinatokana na kweli kwamba Joram alidhaniwa kuwa alikuwa amekufa kwani chumba alimokuwa anajificha kilikuwa kimelipuliwa na viungo vya mwili wake kuonekana vikitawanyika. Kombora anasema:

> Kabla sijaanza jukumu lolote la muhimu nadhani unao wajibu wa kufafanua vipi uko hai baada ya lile bomu ambalo lilitapanya maungo yako. Sipendi kuamini kwamba ulikufa na ukafufuka (uk.77)

Sifa moja maarufu ya Joram Kiango kama inavyokuwa kawaida ya mhusika mpelelezi yeyote, ni uajabu unaohusishwa na nguvu zake za kimwili na kiakili. Waandishi wengi wa utanzu huu wa riwaya huwasawiri wahusika wapelelezi wanaokiuka uhalisia wa kibinadamu wa kawaida kwa kuwapa nguvu za ajabu kama vile kutenda mambo yaliyoko nje ya uwezo wa binadamu. Kwa mfano, uajabu wa Joram unahusu namna alivyoweza kuokoka kutokana na kulipuliwa na bomu. Kutawanyika kwa viungo vyake kuliwawathibitishia wapinzani wake kwamba alikuwa amekufa. Kitendo hiki kinaelekea kumuashiria Joram Kiango kama mhusika wa kihalisiajabu. Hii ni sifa inayojitkeza pia katika riwaya za Musiba kuhusiana na usawiri wa Willy Gamba. Sifa hii ya uajabu pia inajitokeza katika kazi za Abdulla hususani kuhusiana na usawiri wa mhusika Msa. Mgeni (1983) alihakiki uajabu katika kazi za Abdulla na kubaini kwamba kuna njia kadhaa ambazo mhusika Msa anadhihirisha uajabu. Kwanza, nyumbani kwake ana kitabu maalum kiitwacho ‘Kinyume cha Mambo’ kinachompa maarifa mengi kuhusu upelelezi. Kwa mfano, usomaji wa kitabu hiki ulimpa uwezo wa kufasiri mambo yaliyosemwa na mgonjwa, Kipwerere katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1958). Katika hali ya ugonjwa Kipwerere alitamka maneno

yasiyoweza kueleweka lakini Msa kwa uajabu wake akawaeleza wahusika wengine maanake. Maneneo hayo yalikuwa, ‘Nimeona. Nimeona Kiza!A. a a a. Hapana kitu…Safi kabisa…Nyekundu’.(uk.12)

Fasiri ya Msa kuhusu maneno haya ni kwamba, maneno ‘kiza na nyekundu’ ni damu iliyomwagwa. Kwa hivyo bwanake Kipwerere, Bwana Ali, ameuawa. Ufasiri wa Msa wa kisa hiki unazidisha uajabu wake. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* Msa anadhihirisha uajabu tena kupitia namna alivyochunguza kesi ya kupotea kwa mali ya Mzee Hakimu Marjani. Anajifungia chumbani kwa siku nyingi, bila kuzungumza na yeyote, bila kuoga wala kula akichunguza msahafu ambao Saleh, dereva wa Hakimu Marjani, alikuwa amepewa na mamake. Baada ya siku hizo Msa alipata ufunuo kuhusu ni vipi pesa za Hakimu Marjani zilikuwa zimepotea. Anagundua kwamba pesa hazikuibiwa bali mwenyewe Hakimu alikuwa amezificha kando na mto sehemu ya Kazole maili kumi na mbili kutoka nyumbani kwa Hakimu Marjani.

Kuhitimisha sehemu hii, tunatoa kauli kwamba maelezo yatolewayo na msimulizi, hasa msimulizi wa nafsi ya tatu kumhusu mhusika yanaelekea kuwa ya kwaminika zaidi kuliko maelezo ya mhusika kumhusu mhusika mwingine. Hii ni kwa sababu maelezo ya msimulizi, hayaingizi hisia za kibinafsi. Zaidi ya hayo, msimulizi ana uwezo wa kumpa msomaji taswira kamili kwa kuwa anamwona mhusika kutoka mitazamo mbalimbali.

4.2.2 Usawiri wa Kiishara (Usio wa Moja kwa Moja)

Kwa kutumia mkakati huu, msomaji huelekezwa kwenye sifa za mhusika kwa njia mbalimbali kama vile kupitia vitendo na usemi wa mhusika huyo ili msomaji akisie na kutambua sifa alizoashiriwa. Kupitia njia hii, kinyume na ile ya uwasilshaji wa moja kwa moja, angalau msomaji ana uhuru wa kufasiri ishara tofautitofauti kivyake na kuielewa hadithi kwa namna yake binafsi. Arege (2012:161) anasema kwamba mkakati huu huwezesha sifa na tabia mbalimbali kuibuliwa kutokana na kitendo kimoja cha mhusika. Kwa hivyo, ufasiri wa sifa na hulka za wahusika huathiriwa na mitazamo na itikadi zinazokinzana za wasomaji tofautitofauti. Udhihirishaji wa wahusika kwa njia ya uashiriaji unaweza kutekelezwa kwa njia zifuatazo:

4.2.2.1 Vitendo vya wahusika

Wahakiki kadhaa wanashikilia kwamba uhakiki wa vitendo vya wahusika ni njia murua zaidi ya kuzifahanu hulka zao. Kwa mfano, Abbot (2002) anatilia mkazo umuhimu wa vitendo vya wahusika akisema hivi:

Wahusika ndio ajenti wanaosababisha matendo. Kupitia matendo yao wanatufichulia kuwa wao ni nani kihulka, kimalengo, kupitia nguvu zao,

> uaminifu wao, uwezo wao wa kupenda na kuchukia na udhaifu wao. Kupitia vitendo vyao tunawajua. (uk.124.) T.Y

Rimmon-Kenan anaainisha vitendo vya wahusika kwa njia mbili kuu; Yaani vitendo vya mara kwa mara au mazoea na vitendo vya mara moja. Anasisitiza kwamba wasifu wa mhusika unaweza kujitokeza kupitia vitendo afanyavyo kimazoea au vile vya mara moja tu. Anasema kuwa vitendo vya mara moja ni muhimu kwa sababu vinaonyesha ukuaji wa mhusika huyo huku vitendo vya mazoea vikimsawiri mhusika kama aliyekwama katika jambo moja. Kwa hivyo, kitendo cha mara moja kinaweza kuwa na uzito mwingi kuhusu wasifu wa mhusika kuliko vitendo vya mazoea. Kwa mfano, ikiwa mhusika amesawiriwa kama anayependa kusoma sana kisha siku moja amuue mtu fulani, kitendo hiki cha mauaji ingawa cha mara moja kinaathiri wasifu wake zaidi na kuamua anavyochukuliwa na wengine kuliko mazoea yake ya kusoma. Vitendo vya mara moja pia huonyesha mhusika anayebadilika kinyume na vile vya mazoea ambavyo huweza kumsawiri mhusika kikejeli kwa kubakia katika mtindo mmoja tu huku wengine wakiwa wanabadilika.

Rimmon-Kenan anavigawa zaidi vitendo vya wahusika kwa njia tatu: (a) Mambo yaliyotendwa, (b) Vitendo achwa-Mambo ambayo mhusika alipaswa kufanya lakini hakufanya na (c) Vitendo vya Kufikirika-Mipango ya kutenda baadaye iliyomo akilini mwa mhusika lakini bado haijatekelezwa. Vitendo vya kufikirika huashiria matamanio ya mhusika yaliyofichika akilini mwake na yanaweza kujidhihirisha baadaye katika matendo halisi. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, vitendo mbalimbali kama vinavyoainishwa na Rimmon-Kenan vinachangia usawiri wa sifa za wahusika wa riwaya hizo. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* (1960), Mwana wa Giningi alipoachiwa shamba kubwa na babake ili ajikidhi kwalo, aliamua kumshirikisha babake mdogo, Ali Makame katika usimamizi wa shamba hilo. Makubaliano yalihusu Ali kulima

mikarafuu na mimea mingine na kuuza na kumgawia Mwana wa Giningi faida. Kuhusu kitendo hiki, msimulizi anasema;

> Alimpa babake mdogo shamba kulitazama na kulifanya atakavyo, yeye amletee safi yake tu iliyobakia, yaani aliweza kukodisha ghila, kuangusha nazi na kuchumisha karafuu na kuziuza kwa bei yoyote aitakayo, alipe kharji zote na kila kitu halafu tena kinachobakia amletee (uk.23)

Katika dondoo hili, tunaona kwamba kupitia matendo ya babake Mwana wa Giningi, mzee huyo anasawiriwa kama baba aliyemjali bintiye ndio maana akampa shamba alitumie kuendeshea maisha yake ya baadaye. Mwana wa Giningi naye anasawiriwa kama mhusika mpenda amani na asiye na tamaa. Hii ndio sababu anampa babake mdogo shamba alilorithi awe msimamizi ili kuepukana na bughudha zake na waishi kwa amani naye. Alifuatia wosia aliopewa na babake kwamba Bwana Ali Makame ni mtu mwenye tamaa nyingi ya mali. Kitendo cha kumpa Ali Makame shamba kulisimamia ni ishara ya werevu pia kwani Mwana wa Giningi alielewa kwamba tamaa na ubabedume wa Ali haungemruhusu kulitumia shamba hilo kwa utulivu. Fauka ya hayo, kitendo cha Mwana wa Giningi pia kinatuonyesha namna wanyonge hasa wanawake wajane walivyodhulumiwa na wenye nguvu katika jamii ya Kiunguja.

Tunaweza kuona kwamba vitendo vya wahusika vinaweza kuthibitisha hulka zao kwa uzito zaidi kuliko hata usemi wao. Kama anavyosema Wamitila (2002:24), mbinu ya kimatendo kama ilivyo katika tamthilia humwezesha msomaji au mhakiki kumjua mhusika bila kuathriwa na mtazamo wa mwandishi.

Tunaona matumizi ya mbinu ya vitendo vya kufikirika pia ikitumiwa na waandishi wa riwaya ya kiupelelezi kuwasawiri wahusika wao. Kwa kuwa hivi ni vitendo visivyoonekana, aghalabu huwa ni mipango na matamanio ya kutendwa baadaye. Kwa hivyo, mbinu hii hubainika kupitia mipango ya wahusika. Katika riwaya za Mtobwa, kwa mfano, tunaona namna mataifa adui wa Tanzania wanavyofikiria kuzua mizozo ili kuharibu utulivu wa nchi hiyo. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (1984), viongozi wa ngazi za juu serikalini wanakutana na mwakilishi wa taifa la Afrika Kusini, Kwame, ili kuwashawishi kuipindua serikali ili serikali mpya ikiundwa wapewe vyeo vya juu zaidi katika serikali mpya pamoja na kupewa pesa nyingi kutoka ng’ambo. Ingawa hiki ni kitendo cha kufikirika tu wala hakikufanyika, kinatufichulia sifa za viongozi hao wa juu serikalini

kama wenye tamaa na waliokosa uzalendo. Mwakilishi huyu, Kwame, akizungumza na viongozi hawa wa kiserikali anawaambia:

> Tusisahau kuwa mpango huu una utajiri mwingi ambao wengi wenu hamjawahi kuugusa na vyeo ambavyo msingeweza kuvifikiria. Wala msihofu kuwa utawala wenu wa kidikteta hata muwe kama maadui wa wananchi wenyewe. Mbinu zitatumika mara tu baada ya vifo vya wakubwa wachache ili majina yenu yazibe mapengo hayo.(uk.65)

Katika mpango huu, ni wazi kwamba njama za mapinduzi ya serikali aghalabu hushirikisha baadhi ya viongozi wachache katika serikali wenye tamaa ya uongozi pamoja na maadui wa kutoka nje wenye nia ya kuleta itikadi zao katika utawala wa nchi nyingine. Dhamira kama hii pia tunaiona katika riwaya ya Musiba ya *Uchu* (2000) ambapo Mfaransa, Jean na mwanasiasa maarufu katika serikali ya Tanzania, JKS, wanapanga namna watakavyoingilia siasa ya Rwanda na kuvuruga mikakati ya kupata amani nchini humo. Kwa upande wake, JKS anasaidiwa na Jean kuwakomesha wapinzani wake ili aweze kukifikia kiti cha urais wa Tanzania. Katika maongezi baina ya JKS na Jean, JKS anajitokeza kama mhusika msaliti na mwenye tamaa ya uongozi na mamlaka. Mpango huu unafichuliwa na mpelelezi Willy Gamba na kuusambaratisha kabla ya kutekelezwa. Mhusika Jean naye ni kiwakilishi cha mataifa ya Kimagharibi ambayo aghalabu huamua aina ya utawala utakaodumishwa katika mataifa machanga kwa kutumia nguvu za kiuchumi. Kwa mfano, Jean akiwa Ufaransa anaweza kutawala mfumo wa kiasiasa na kiuchumia wa Rwanda na Tanzania. Maongezi ya Jean na JKS kwa njia ya simu yanaenda hivi:

> Sasa mimi nitakusaidia vipi? JKS aliuliza. Utanisaidia mimi au utajisaidia vipi? Unasema kana kwamba wewe hauko kwenye huu mchezo. Mchezo huu ni hatari kwako kuliko ulivyo hatari kwangu maana huyu mtu akigundua kuwa wewe umekuwa mmoja wa wanaohujumu mwelekeo wa nchi yako kuhusu suala la Rwanda na maswala mengineyo, basi ujue umeisha na urais wa Tanzania utauangalia kwenye ndoto zako tu. Kwa hivyo, mtu huyu ni hatari kwako kuliko kwangu. Hivyo ni kwa faida yako auawe mara moja. Jean alimuaga JKS. (uk.65)

#### 4.2.2.2 Usemi wa Wahusika

Leech and Short (2007:296) walioweka msingi wa nadharia ya umitindo tunayotumia katika utafiti huu wanasema kuwa uhakiki wa wahusika unafaa kuzingatia namna wahusika wanavyotumia lugha kwa kutathmini matumizi yao ya lafudhi na lahaja. Wanaeleza kwamba mazungumzo ya

wahusika ni njia bora ya kufichua tabia fiche ya mhusika. Naye Rimmon-Kenan akiunga mkono wazo hili anasema kwamba lugha ya mhusika ikitumika kwa njia tofauti na ile ya msimulizi yaweza kuashiria sifa za kijumla kumhusu mhusika huyo kama vile asili yake, anapoishi, tabaka lake na hata taaluma yake. Kwa kutumia mifano michache kutoka kwa riwaya teule tunaonyesha namna matumizi ya lafudhi, lahaja na sajili mbalimbali yanavyoweza kuashiria asili, tabaka na hata taaluma ya wahusika. Lahaja ni namna mbalimbali za uzunguzaji lugha moja huku lafudhi ikiwa ni matumizi ya lugha kwa njia inayombainisha mtu binafsi. Katika riwaya za Abdulla, aghalabu tunashuhudia matumizi ya lahaja ya Kiunguja katika kazi zake. Lahaja hiyo inajitokeza kupitia misamiati na matamshi ya wahusika na kwa njia hiyo kudhihirisha mtindo wa Abdulla. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani kuna watu,* kuna misamiati kama vile ‘kutuzulu’ badala ya kutuzuru,(uk.50), ‘mia tani’ badala ya mia tano, (uk.45), ‘kunya chai’ badala ya kunywa chai, (uk. 43), na ‘ndo’ badala ya ndio, (uk.57) yote yakiashiria asili ya wazungumzaji kuwa ni wazawa wa Unguja, hivyo kuzifanya riwaya za Abdulla kuwa na uhalisia mwingi.

Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, mpelelezi wa polisi, Spekta Seif, mpelelezi wa kibinafsi Bwana Msa na msaidizi wake, Najum wakichunguza mauaji ya Mwana wa Giningi, wanazuru eneo la mauaji na kuwahoji watu kadhaa wakiwemo wachuuzi, Pandu, Bwana Machano na Shame. Pandu anapotoa taarifa kwao anaongea kwa lahaja ifuatavyo:

> Bwana Spekta siwezi kusema kwa yakini, lakini nadhani nisikii maneno kama yano, kumfisidi’sijui tena, rasilimali yakwe, sijui tena, lazima amfungishe’. Maneno kama yano. Kisha kamsikia Vuai yaujibu, Nini faida kupigizana kelele njiani? Akamwambia aende zake nyumbani na yeye katakwenda huko. Bibi kanakataa katakata hamtaki huyo Vuai.(uk.75)

Lahaja inayotumiwa na mhusika huyu, inatofoutiana na Kiswahili sanifu kimatamshi, kisarufi na kiuteuzi wa msamiati ikiwa ishara ya eneo maalum la kijiografia atokako mhusika. Leech na Short (2007) wanaeleza kwamba lahaja huweza kujitokeza kupitia viwango mbalimbali vya lugha kama vile fonolojia, sarufi na semantiki. Hii ndio maana kauli za msemaji hapo juu zinadhihirisha ukiushi mkubwa wa kimatamshi, kisarufi na wa kigrafolojia. Usemi wa mhusika huyu unaashiria asili yake kwamba ni mkaazi wa eneo la Unguja na kwa sababu yeye ni mwenyeji wa eneo lenye kisima hiki, ithibati yake kuhusu maongezi ya Mwana wa Giningi na Vuai hapo kisimani inaaminika. Kupitia ripoti yake ni wazi kwamba Vuai na mkewe hawakuwa na uhusiano mwema hivyo ni rahisi kuchukulia kwamba Vuai ndiye aliyemuua mkewe. Hii ndio ithibati Spekta Seif

anayoamini zaidi na kama si Msa asingekuwapo Vuai angekamatwa. Hata hivyo kauli zao ni makisio wala hawaonyeshi kutazama upande mwingine wa uchunguzi. Kwa kuwa lahaja huwa na majukumu kadhaa katika kuwapambanua wahusika, kando na kuashiria asili, yaweza pia kuwa ishara ya kiwango cha elimu cha msemaji, hali yake ya kiuchumi na tabaka lake. Katika dondoo hili, waliokuwa wakihojiwa wapo katika tabaka la chini na hali duni yao ya kiuchumi inadhihirika kupitia biashara yao ya kuuza miwa kando na kisima. Simpson (2004:102) anasisitiza kwamba lahaja katika maongezi ya wahusika huweza kuashiria tabaka au misimbo mingine ya kijamii kama vile viwango vya kielimu.

Lafudhi pia inaweza kutumika kama kitambulisho cha wahusika. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* kwa mfano, Msa, Spekta Seif na Najum wanapotembea mjini wanapata msongamano wa watu karibu na duka la Mmanga. Inabainika kuwa wanashuhudia wizi uliofanyika hapo. Mmanga huyo anawaambia kwamba alijiwa na mgeni Mwarab siku iliyopita na alipoondoka, huenda ndiye aliyeiba upanga wa mweneye duka, Mmanga. Anaporipoti, lafudhi yake inaashiria kuwa ana asili ya Uarabuni:

> Kafanya kher sbakta Seif, Mafanya kher makugya kwangu. Mimi mwenyewe nataka nakugya huku huku steeshin nariboti kwako. Yule mwarab mgeni bu nafika kwangu gyuzi, gyana maondoka haba wakti wa maghribi sinarudi tena l'aan. Leo natazama naona ufanga yangu hayuko mahl yake, la shaka nashukuwa yeye tu.(uk.51)

Lafudhi hii ya Kiarabu ni ithibati tosha kwamba jamii ya Unguja ilikuwa na wageni wengi wa kutoka Uarabuni waliokuwa wakija kufanya biashara. Kwa sababu ya maingiliano yao na wenyeji wanazungumza kwa kuswahilisha Kiarabu ili wawasiliane na hao wenyeji. Kwa hivyo, mbinu hii inaboresha uhusika kwa kuonyesha uhalisia unaoletwa na tofauti za kiasili za wahusika. Kwa kumalizia sehemu hii kuhusu umuhimu wa usemi wa wahusika kama kiashiria cha uhusika, suala la sajili pia ni muhimu. Huu ni msimbo wa kijamii unaobainisha miktadha mbali mbali ya matumizi ya lugha. Sajili yaweza kutumika kuashiria tofauti za kicheo baina ya wazungumzaji, viwango vyao vya kielimu na hali zao za kiuchumi. Katika riwaya ya Levi ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* (1975), kuna sajili ya mahakamani inayobainika kupitia mazungumzo baina ya wahalifu Rono, Mita, Deli na Karikenye wakihojiwa na hakimu:

> Kwa vile mmekiri mashtaka na nimewapata na hatia, nitawahukumu kulingana

> na sheria za nchi…Hakimu alimuuliza kiongozi wa Mashtaka, “Una la kusema kabla ya kuwahukumu washtakiwa? (uk.63).

Katika sajili hii, misamiati kama vile ‘hakimu’, ‘sheria’, ‘washtakiwa’, ‘hatia’ na ‘kiongozi wa mashtaka’ inabainisha matabaka ya wahusika mawili. Huku hakimu na kiongozi wa mashtaka wakiwa wahusika wa tabaka la walinda sheria nao washukiwa wakiwa katika tabaka la wahalifu.

Usemi wa wahusika unaweza kuashiria matamanio yao yaliyofichika kando na kufichua wasifu wa wahusika wengine. Culpeper (2002:41) anaonyesha namna mazungumzo ya wahusika yanavyoweza kudhihirisha saikolojia zao. Anasema kuwa mazungumzo hayo yanaweza kuhusu mhusika kujisemea mambo yanayomhusu na kufichua sifa zake mwenyewe ama kusema mambo yanayowahusu wahusika wengine na kuishia kufichua sifa zao kwa njia hiyo. Mtazamo wa mhakiki huyu unaashiria kwamba tunaweza kuzipata sifa hizo kwa njia mbili; ile ya dayalojia ama uzungumzi nafsia. Rimmon-Kenan naye ansema kwamba usemi wa wahusika unafaaa kutathminiwa kwa njia mbili kuu; kwanza kwa kuchambua maudhui ya usemi huo, yaani nini kinachosemwa na pili, kuzingatia fani, yaani namna jambo hilo lilivyosemwa. Mhakiki huyu pia anakubaliana na kauli ya Culpeper kwamba usemi wa mhusika unaweza kuwa kiashiria cha sifa yake au sifa ya msemewa. Wamitila (2002:26) ana maoni sawa na ya wahakiki hawa akisema kwamba maneno yasemwayo na mhusika ‘A’ kumhusu ‘B’ yanaweza kuangaliwa kwa njia mbili; kwanza maneneo hayo yanaweza kutusaidia kumuelewa ‘B’ au huenda kauli anazotoa ‘A’ kumhusu ‘B’ zikatuonyesha alivyo ‘A’ badala ya ‘B’. Kwa kuwa kaida hizi zote za usemi wa wahusika zinaweza kujitokeza katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, hapa chini tunatoa mifano ya usemi wa aina mbili, yaani dayalojia ya kinathari na uzungunzi nafsi na kuonyesha namna mbinu hizi ziwezavyo kufichua wasifu wa wahusika.

#### 4.2.2.2.1 Dayalojia ya Kinathari na Uhusika

Mazungumzo yana dhima kubwa katika kuendeleza uhusika kwa kuwu ni kupitia njia hii ambapo msomaji anaweza kuelewa motisha ya vitendo vya wahusika kwa undani. Zaidi ya haya, mazungumzo huweza kumchochea mhusika kufichua hali yake ya kisaikolojia na migogoro inayomhusu au imayowahusu wahusika wengine.

Mazungumzo ya wahusika katika kazi za kinathari kama vile riwaya na hadithi fupi kwa kawaida hayaendeshwi kwa njia ya kidrama kama ilivyo katika tamthilia. Hii ni kwa sababu huku usimulizi

ukiendeshwa kwa mazunguzo katika tamthilia, kwa upande wake, riwaya hutumia masimulizi zaidi ya maongezi. Hata hivyo, wakati mwingine msimulizi huwapa wahusika nafasi kujisemea mambo fulani wenyewe na kwa njia hizo hufichua hulka zao, mitazamo yao na ya wahusika wengine kwa wasomaji. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* Joram Kiango, ambaye ndiye mpelelezi katika kazi za Mtobwa, akizungumza na msichana msaidizi wake, Nuru, anamuonyesha namna magazeti ya kigeni yalivyoripoti wizi wa pesa katika benki ya Tanzania. Katika habari hizo, Mwingereza anamkejeli Mwafrika kwa kuibia nchi yake pesa za kigeni na kukimbilia London kuzifuja hela hizo huko. Kuhusu madai hayo, mhusika Joram anamwambia Nuru:

> Kinachochekesha ni kwamba Mwingereza anajifanya ana uchungu na nchi yetu kuliko sisi wenyewe. Utafiti alioufanya hautokani na moyo wake wa kuwajibika bali unatokana na nguvu alizo nazo za kiuchumi.Uwezo ambao ameuiba kutoka makoloni yao miaka nenda, miaka rudi. (uk.75)

Katika muktadha huu, inabainika kwamba Joram ni mzalendo kwani ingawa anashutumiwa kuiba pesa za kigeni kutoka benki moja nchini mwake, kusudi lake lilikuwa ni azitumie hela hizo katka juhudi zake za kupambana na adui wa kimataifa wanaotaka kupindua uongozi uliopo. Chuki yake dhidi ya mkoloni inajitokeza kupitia namna anavyomchukulia Mwingereza kama mwizi wa rasilimali. Kwa hivyo, kando na kutufichulia wasifu wake kama mzalendo na mwanamapinduzi, usemi wake unasawiri wasifu wa mataifa ya Kimagharibi kama walioleta uharibifu barani Afrika na pia kufichua mtazamo wa Wazungu kuhusu Afrika. Hapa tunaona kauli ya Wamitila (2002) kwamba usemi wa mhusika kuweza kuashiria wasifu wake ama wasifu wa mhusika mwingine ni kweli. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* (1973) majambazi wanalilivamia jumba la Hakimu Marjani na kumkaba koo mzee huyo na kujaribu kuiba pesa zake lakini kwa bahati nzuri dereva wake, Saleh, anaonyesha ujasiri wa ajabu katika kupambana na majambazi hao na kufanikiwa kumuokoa mzee huyo. Anapomaliza kutenda haya, anawaita polisi ambao pia wanapofika wanautambua ushujaa wa Saleh. Mmoja wa askari hao anasema:

> Bahati nzuri bwana huyu katokea kwa wakati kabla ya wao hawajaanza kazi yao mbaya. Bwana huyu kaonyesha ushujaa mkubwa sana. (uk.26)

Katika usemi huu ingawa hatuoni wasifu wa askari hawa ukidhihirika, kauli ya askari inatuashiria ushujaa wa Saleh. Katika riwaya ya Simbamwene ya *Kwa Sababu ya Pesa* (1972) mhusika Rashid anatengeneza mpango wa kumtumia mpenzi wake, Salima anayefanya kazi katika benki kuiba

pesa za benki hiyo ili yeye Rashid akazitumie pesa hizo na mpenzi mwingine, Rehema. Rashid anafanya hivi kwa kuwa ana mshahara mdogo wa utarishi lakini ana tamaa kubwa ya maisha ya anasa na starehe. Mwanzo Salima anasita kuukubali mpango wa Rashid lakini baadaye anakubali. Salima anamwambia Rashid:

> Mpenzi Rashid naona mpango huu wa kuziiba pesa za benki, tuuzike na kuusahau kabisa. Ukitaka unaweza kuendelea peke yako. Najitoa kabisa. Unataka kunitumia mimi ili uzipate fedha kwa urahisi.(uk.30)

Usemi wa Salima unatuashiria wasifu wa Rashid kama mtu mwenye tamaa ya utajiri, mpenda anasa na mjanja huku wakati huo huo usemi huu ukiashiria wasifu wa Salima kama mhusika mtambuzi, mwaminifu na mwajibikaji kazini. Hata hivyo, uthabiti wa baadhi ya sifa zake haudumu kwani baadaye anashawishika na maneneo ya Rashid na kukubali kuziiba pesa za benki na kumpa Rashid. Ingawa utanzu wa riwaya pendwa kijumla hulenga kuburudisha, tunona riwaya hizi aghalabu zikiakisi uhalisia wa kimaisha. Kwa mfano, katika riwaya hii, suala la tofauti za kitabaka zikibainika, ambapo watu wa tabaka la chini wanatamani hali ya maisha ya tabaka la matajiri. Kama wasemavyo Madumulla (1988:13) na Kimura (1992:41) sababu mojawapo iliyosababisha uibukaji wa riwaya pendwa katika Afrika Mashariki ni kushamiri kwa matatizo ya kiuchumi katika miaka ya sabini na themanini. Matendo ya baadhi ya wahusika katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa* yanatokana na uhalisia huu. Rashid kwa mfano, ni tarishi anayepata mshahara mdogo lakini anapotazama wafanyikazi wa viwango vya juu serikalini, anavutiwa na hali nzuri ya maisha yao. Pia suala la wizi wa benki ni uhalisia unaoshuhudiwa sana katika mataifa mengi ulimwenguni hasa ukiwahusu wafanyakazi wa benki wakishirikiana na watu wengine.

#### 4.2.2.2.2. Uzungumzi Nafsiya na Mkondo wa Ung'amuzi

Kando na kuzungumziana, wahusika pia wanaweza kutufichulia wasifu wao kupitia uzungumzi nafsia. Hii ni hali ambapo mhusika hujisemea peke yake bila kuelekeza kauli zake kwa mhusika mwingine yeyote. Ingawa kwa kawaida hii huwa ni mbinu ya kijukwaa, inaweza vile vile kupatikana katika kazi za kinathari kama vile riwaya. Mkondo wa ung'amuzi ni matumizi ya maelezo marefu yanayomulika mawazo yanayompitikia mhusika akilini (Wamitila, 2002:25). Njia hizi mbili ni maarufu katika kuonyesha hisia, mitazamo, matamanio fiche au matatizo ya kisaikolojia ya mhusika na kwa njia hiyo kumsaidia msomaji kuelewa hulka ya mhusika anayedhihirisha hisia hizo.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1965) tunaona matumizi ya uzungumzi nafsi kupitia mpelelezi Far Katy Wingo. Baada ya kuchunguza habari za vifo vingi bila kupata suluhu, mpelelezi Far Katy Wingo anasumbuka kutafuta namna ya kujikwamua. Kifo cha mamake Geva, Mary, kinatokea angali anachunguza mauaji ya mumewe, Mzee Jacob bila mafanikio. Anaamua kumpigia daktari simu kuja kuchunguza maiti ya Mary. Anapomaliza kupiga simu, anarudi kukaa akiwahoji Agnes na Geva. Msimulizi anasema,

> Baada ya kupiga simu, Inspekta Wingo alirudi Rufita na kukaa kumngojea daktari, Pherredge. Mle chumbani walikaa kimya, hali Wingo anavuta kiko chake. Akaanza kufikiri…Nani anaweza kuwa amemuua mama Mary? Je yule muuaji ni hasa alikuwa anamtafuta mama Mary? Looh! Je anaweza kuwa ni mwanawe Geva ndiye amemuua? Na kama ndiye kwa nini? Sioni sababu. Yeye Geva amekuja kutoka Dodoma, kakuta baba kauawa. Hapa haionyeshi kuwa Geva anaweza kuwa amemuua babake. Na kama hakumuua babake basi ina maanisha kuwa alikuwa anampenda. Geva bila shaka alichukizwa na mtu aliyemuua babake…Kila siku ya mauaji ya Rufita mimi hupata simu kutoka kwa 'Fambo' nisiyemfahamu. Ndio kusema kuwa Fambo ndiye muuaji au la? Ni lazima awe anaielewa mipango hiyo vyema kabisa.(uk.67)

Katika mkondo wa ung'amuzi huu, tunaona hali ya kisaikolojia ya mpelelezi inayohusu usumbufu anaopitia anapopigiwa simu ya kuripoti vifo vya watu mbalimbali huku akiwa hajamaliza kuchunguza mauaji ya hapo awali. Mkondo huu wa fikira unafichua si tu wasifu wake kama mtu anayeipenda kazi yake ya upelelezi, bali pia unafanikisha usawiri wa wahusika wengine kama vile Geva. Kulingana na fikira yake, anamuondolea Geva lawama kwa kumuona kama aliye na mapenzi kwa babake. Pili, mhusika Fambo ambaye ndiye anapiga simu kuripoti visa hivi analaumiwa na kushukiwa. Kushukiwa kwake kunatokana na ukweli kwamba yeye hushuhudia kila aina ya mauaji na kila mara anapopiga simu hasemi yuko wapi wala kujitambulisha. Mhusika Fambo hata hivyo ni muhimu katika riwaya hii kwa kuwa anazidisha taharuki na uajabu unaohusishwa na utanzu wa riwaya ya kiupelelezi.

Kulingana na nadharia ya utanzu, kila kijitanzu cha fasihi huwa na sifa maalum zinazokitenganisha kijitanzu hicho na tanzu nyinginezo. Utanzu huu hutambulikana zaidi kutokana na sifa ya kushtukiza inayohusiana na usawiri wa mandhari na wahusika kwa njia za kiajabu. Ushtukizaji unajitokeza katika riwaya hii kupitia kuripotiwa kwa vifo wakati ambapo mpelelezi yupo katikati ya kuchunguza mauaji ya awali. Kando na uajabu huu, Danyte (2011) anaeleza kwamba mpelelezi

aghalabu hujipata katika hali ya upweke mwingi. Hii ni kutokana na ukweli kuwa wapelelezi vielelezo anaowarejelea kama vile Auguste Dupin na Sherlock Holmes hawakuwa na familia wala marafiki wengi. Sherlock Holmes kwa mfano, anaishi na Dkt.Watson tu huku wakati wake mwingi ukitumika katika uchunguzi. Hii ndio hali inayomkumba mpelelezi Wingo kwani tegemeo lake sasa ni daktari anayemtarajia kufika kumfafanulia kitendawili cha mauaji. Kuwepo kwa mhusika asiyejulikana kama Fambo katika riwaya hii kunazidisha taharuki miongoni mwa wasomaji na kuifanya riwaya ivutie. Mwisho, dondoo hilo hapo juu linatuwasilishia mhusika mwenye uwezo wa kuchanganua masuala ili kuwaondoa wengine lawamani na kuelekeza shutuma kwa wengine.

Mbinu ya uzungumzi nafsi pia imetumika katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kuusawiri wasifu wa Kasim. Kwa kuwa Kasim ana mazoea ya kuombaomba pesa kutoka kwa babake huku akizifuja katika kuchezea kamari na kushiriki ulevi, hana hakika kama akimwendea baba mara hii atamfaa au la. Anapoamua kuenda kumrai babake ampe anashikwa na mfadhaiko kwa kuogopa kuulizwa maswali kuhusiana na jinsi anavyotumia pesa kwani huzimaliza haraka tu anapopewa. Najum anasema, ‘Potelea mbali, nitakwenda’. (uk.3)

Uzungumzi nafsi huu unatuashiria sifa za Kasim kwamba ni mtu mwenye mapuuza na ujasiri kwa kuwa ingawa anaelewa kuwa tabia yake ya kufuja pesa si nzuri na kwamba babake haipendi, anendelea kushiriki mchezo huo na pesa zake zinapoishia huko anapata ukakamavu wa kumdai babake nyinginezo. Kama tulivyoona hapo juu, jukumu la mbinu hii ni kufichua hisia au matamanio fiche na katika usemi wa Kasim ni wazi kuwa alikuwa na mgogoro wa kihisia, hajui ikiwa aende ama awache kuenda. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* (1968) pia tunaona mbinu hii ikitumika. Mwana wa Giningi alipoibiwa kisanduku cha dhahabu alichopewa na babake, anasumbuka kiakili kwa kuwa anakisiakisia ni nani anayeweza kuwa ndiye mwizi. Kwanza anamshuku bwanake Vuai kwa kuwa Mwana wa Giningi alikuwa ameambiwa na mganga, Fundi Mangungu, kwamba Vuai alikuwa ameenda kumchukulia urogi ili autumie kuiba mali yake. Msimulizi anasema kuwa Mwana wa Giningi alizikata fikira zake akawa anasema kidogo:

> Ah! Mimi sikumhini! Yeye mwenyewe tu kawa na tamaa ya kumfata shetani hata kenda kuniloga kwa Fundi Mangungu ili nife apate kurithi! Japokuwa ndio wosia wa baba, lakini ndio nikae na yeye tu, adui kama huyo! (uk.23)

Katika dondoo hili, tunapata ufunuo mwingi kuhusu sifa za wahusika kadhaa. Kwanza, Vuai anajitokeza kama mhusika mwenye tamaa na kiu kikubwa cha mali. Mtu ambaye anaweza kufanya

lolote ikiwemo kuua ili kurithi kisicho chake. Kwa kuwa alikuwa ameenda kutafuta urogi ili amuue Mwana wa Giningi, basi hii ni ithibati tosha kwamba pia ni mshirikina. Hata hivyo, hukumu hii ni ya kutiliwa mashaka kwani kama Msa anavyodhihirisha baadaye, Fundi Mangungu ni muongo na kuna uwezekano kwamba alimpa Mwana wa Giningi habari za uongo kama njia rahisi ya kumpa jawabu la ni nani aliyeiba mali yake. Pili, Mwana wa Giningi pia ana tabia ya kishirikina kwani anatupatia habari alizoambiwa na Fundi Mangungu kumaanisha kwamba yeye kama Wanaginingi wengine ana itikadi ya uchawi. Sifa ya babake Mwana wa Giningi kama mtu anayewajali watu wengine katika jamii inajitokeza. Hii ni kutokana na kitendo chake cha kumpa wosia kwamba aishi kwa amani na Vuai ili amkidhi kwa kuwa Vuai hakuwa na utajiri kama ule alionao Mwana wa Giningi. Kufuata wosia wa babake kunamsawiri Mwana wa Giningi kama mhusika mwadilifu ingawa kunamweka katika mtanziko wa kuishi na mtu anayemwona kama adui.

Katika mfano huu na ule wa awali kutoka katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, tunaoa kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya dhima za uzungumzi nafsia na mkondo wa ung’amuzi, kwamba mhusika anapokumbwa na mtirirko wa mawazo (mkondo wa ung’amuzi) mara nyingine mawazo hayo yanajitokeza wazi wazi (labda bila kukusudia) na kuwa usemi unaoweza kusikika na wahusika wengine, yaani mkondo wa ung’amuzi unakuwa uzungumzi nafsi. Mbinu za usemi na vitendo vya wahusika zinaonyesha uwezo mkubwa wa kuwasawiri wahusika kwa kutumia uhusiano wa kiusababishi. Kwa mfano, katika dondoo la hapo juu kutoka riwaya ya *Kisima cha Giningi*, hali ya mtanziko aliyonayo Mwana wa Giningi imesababishwa na mambo kadhaa; kwanza kuibiwa kwa kisanduku chenye hazina ya dhahabu na pili, haja ya kutaka kuheshimu wosia wa babake unaomlazimu kuishi na Vuai.

#### 4.2.2.3 Mwonekano wa nje kama kiashiria cha Uhusika

Mhakiki Ewen (1980:16) akinukuliwa na Rimmo-Kenan anasema kwamba mtindo wa kulinganisha umbo la nje la mhusika na wasifu wake ni mkongwe na ulitumiwa kuthibitisha kwamba kuna uhusiano baina ya umbo la nje la mhusika na wasifu wa mhusika huyo. Naye Rimmon-Kenan anatuambia kuwa mtindo huu uliasisiwa na mwanafalsafa wa Uswizi, Lavater (1741-1801). Lavater alichanganua maumbo ya nyuso za watu mashuhuri wa kihistoria na kuonyesha kwamba kulikuwa na uhusiano baina ya umbo la nje la mhusika na tabia za mhusika huyo. Shlomith anafafanua kuwa ingawa nadharia ya Lavater ilipingwa sana na kuonyeshwa kukosa mashiko, waandishi wengi wameendelea kuonyesha uhusiano wa umbo nje na wasifu wa

kihusika katika kazi zao. Anatueleza kuwa kuna baadhi ya sifa za nje ambazo mhusika hana uwezo wa kuzithibiti kama vile urefu wake au unene wake huku akiwa na uwezo wa kuthibiti baadhi ya sifa kama vile mavazi yake au mtindo wa uvaaji pamoja na mtindo wa nywele.

Umbo la nje la mhusika laweza kuashiriwa kwa kutumia njia mbalimbali za mahusiano kama vile uhusiano wa kisinekidoki (sehemu kuwakilisha jumla). Uhusiano wa kisinekidoki unaweza kuashiria ujumla wa umbo nje kama vile mwandishi anaposema, '*Jicho lake la kuogofya lilimnyamazisha mshukiwa'.* Umbo hili la nje linatumia sehemu ndogo, 'jicho', kuwakilisha ujumla wa umbo lake nalo umbo nje hili linaashiria wasifu wa mhusika mwenye nguvu na ujasiri mwingi hivi kwamba kumtazama mtu pekee kunamnyamazisha. Mohamed (1995:80-91) naye anafafanua namna ya kumfinyanga mhusika kwa hatua tatu ambazo ni; kuzingatia wasifu wa nje, pili, wasifu wa tabia na matendo na tatu, kuzingatia wasifu wa ndani wa kisaikolojia. Huku tukikubaliana na mhakiki huyu kuhusu njia hizi tatu za ufinyanzi wa uhusika, tunaona kwamba wasifu wa nje unaweza kutumiwa kuashiria wasifu wa tabia pamoja na wasifu wa kisaikolojia.Yaani, **Umbo Nje→Wasifu wa tabia→wasifu wa kisaikolojia**, ambapo umbo la nje ni jumla ya wasifu wa tabia pamoja na wasifu wa kisaikolojia. Tunaweza kutumia kielelezo hiki kwa mfano, kuhakiki hulka ya mhusika Kasim ya kuvaa vibaya katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kwa njia ifuatayo:

Kwa nini Kasim havai vizuri? (**umbo nje**)→Ulevi (**wasifu wa tabia**)→kwa nini analewa→Malezi mabaya kwani alidekezwa na babake ( **wasifu wa kisaikolojia**). Vile vile wasifu wa kitabia ni kielekezi cha wasifu wa kisaikolojia na vile vile wasifu wa kisaikolojia nao waweza kutumiwa kuelekeza kwenye kisababishi cha tabia fulani. Kwa mfano,

Kwa nini Kasim analewa **(wasifu wa tabia**)→ → → Babake alimdekeza katika malezi yake **(wasifu wa kisaikolojia)**

**(**wasifu wa kitabia) ← ← ← (wasifu wa kisaikolojia)

Kijumla mbinu hizi tatu za usawiri wa wahusika zinakamilishana na kuchangiana kwa kuwa maelezo yatolewayo kwa njia moja kumhusu mhusika, hufafanuliwa zaidi kupitia usawiri mwingine. Kwa mfano, mwandishi anaweza kutumia sehemu za kimaumbile kama vile nywele, macho, pua na mengineyo kutilia mkazo taathira aikusudiayo kuitokeza kumhusu mhusika huyo. Mara nyingi mwandishi hutumia umbo nje la kupendeza kama ishara ya wasifu bora wa mhusika

na kwa njia hii kudhihirisha mtazamo wake kumhusu mhusika huyo au dhamira inayoendelezwa na mhusika huyo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, mwandishi anafafanua umbo nje la Sichana kwa njia ya kupendeza kama ishara ya umbo ndani lake. Msimulizi anasema:

> Sicha alikuwa msichana mtoto kabisa. Ni msichana mzuri wa sura na mwenye maungo yaliyokatika kike; na uzuri huo anao tena katika hali yake hii iliyoambatana na maafa ya dunia, basi angaliweza kupelekwa katika mashindano ya wazuri wa dunia, naye angeshinda kwa kujinyakulia cheo cha 'Bibi Ulimwengu'.uk.28.

Baada ya kutoa maelezo kuhusu umbo nje hili, sasa msimulizi anaoanisha uzuri wake wa nje na uzuri wa ndani hasa tabia yake njema. Msimulizi anasema, 'Kwa tabia, Sicha alikuwa mwungwana wa kutosha'…uk.29.

Kinyume chake pia ni kweli kwani waandishi wanaweza kusawiri umbo nje la kuchukiza kama njia ya kuchimuza sifa hasi kama vile uovu wa mhusika. Sifa kama hii tunaiona katika riwaya za kiuhalifu ambapo aghalabu mhusika mhalifu huonyeshwa kama mwenye umbo nje lisilopendeza. Katika riwaya ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu*, umbo nje la mhalifu Karikenye linaelezwa hivi; 'Inspekta Kombo alimtazama kwa makini kijana huyu mrefu mwenye sura mbaya na uso uliojaa makovu yaliyofanywa na vitu kama visu, panga au silaha kali'.(uk.10).

Katika mfano huu, ni wazi kwamba maelezo ya umbo nje ni kiashiria cha tabia ya mhusika huyu ya wizi, utekaji nyara na uharibifu wa mali unaofanywa na Karikenye na genge lake. Maelezo ya umbo nje kwa njia ya kuchukiza yanamsaidia mwandishi kuifikia dhamira yake ya kuonya dhidi ya uhalifu. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa,* mhusika Jeejee amesawiriwa akiwa na umbo nje la kuchukiza kwa kiasi kinachoweza kuashiria uovu wake.  Msimulizi analieleza umbo nje lake kea njia ya kuchukiza hivi:

> Yeye mwenyewe Jeejee hakushughulika na kubadilisha nguo-Kama alikuwa na nazo nguo za kubadilisha-lakini, bila shaka, zile nguo zake za kazini ndizo zilizompendeza yeye kwa kutembelea nazo popote pale. Ujusi wa harufu yake utakutamanisha-utatamani tu, lakini huthubutu-kuziba pua kila akiwa karibu yako. (uk.29)

Maelezo kama haya yanamsawiri kwa mwonekano wa nje ambao unatuelekeza kukisia kuwa msimulizi ana mtazamo hasi na mhusika huyu. Kuthibitisha ishara ya hulka mbaya inayotokana

na umbo nje hili, baadaye msimulizi anasema, ‘Yule afriti aliyepewa msimbo wa jina lisilotambulikana, Jeejee. Juma jeuri ni jitu jahili lisilojali, halina malezi mazuri, halina adabu, na daima lenye kujisifu kwa ufidhuli na ujeuri’.uk.29.

Katika riwaya ya kiupelelezi aghalabu mhusika mpelelezi husawiriwa kama mwenye umbo nje la kupendeza jambo linalowaelekeza wasomaji kwenye wasifu wake kama vile ujasiri, uzalendo na mtendaji mambo ya ajabu katika juhudi za kukomesha uhalifu. Kwa kuwa riwaya hizi zina fomyula ya kuishia kwa adhabu kutolewa kwa mhalifu, aghalabu mhusika mpelelezi ndiye mhusika anayewakilisha mtazamo wa mwandishi. Katika riwaya za Abdulla na za Mtobwa, wapelelezi Msa na Joram Kiango aghalabu huchorwa kwa misingi hii. Kwa mfano, katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*? mpelelezi Joram anaelezwa hivi; ‘Yule kijana mwenye umbo refu, kakamavu lililokaa kiriadhariadha na sura nzuri yenye dalili zote za hekima, ushujaa na ucheshi.’ (uk.1)

Maelezo haya ya umbo la nje kumhusu Joram ni kielekezi cha wasifu wa tabia zake. Kama inavyooneka ana umbo la kupendeza la urefu, si mnono wala mwembamba. Sifa hizi za kupendeza kwa nje zinaakisi wasifu wa ndani wa kupendeza pia. Msomaji anaambiwa kwamba ni mtu mwenye hekima hata kabla ya kuanza kuona matendo yake ya hekima. Kwa hivyo kadri msomaji anavyoendelea kusoma anajua anataraji kuona ucheshi na hekima kama inavyotajwa mwanzoni mwa hadithi ikiwa kama kiona mbele. Kwa njia hii, mwandishi anafanikiwa kutumia maelezo ya umbo la kuvutia ishara ya wema wa mhusika.

Mpelelezi katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* Far Katy Wingo, vile vile anaelezwa kwa njia ya kuvutia kama hii.  Mwandishi analisawiri umbo la nje kwa njia ya kupendeza kama ishara ya wasifu bora alionao. Msimulizi anafafanua sifa za Inspekta Far Katy Wingo hivi:

> Ni mtu mnene, mrefu, mweusi, uso wake mpana na wa kupendeza. Ana mwanya mkubwa uonekanao anaposema. Kichwa chake ni kikubwa chenye nywele fupi na nyeusi. Inspekta Wingo ni wa ajabu kidogo kwa mambo yake.
> Akiwa kazini anaonekana mkali, amenuna wala hataki mzaha. Akiwa nyumbani anaonekana mchangamfu, mtu mcheshi na mkarimu, kila wakati anatabasamu tu. (uk.2-3)

Katika dondoo hili, msimulizi anaanza kwa kufafanua umbo la nje la Inspekta Wingo kwa kategoria za kileksika teule kama vile mrefu, uso mpana na wa kupendeza na mtu mwenye mwanya

kati ya meno. Kupendeza kwake katika umbo nje kunaweza kuonekana kama kielekezi cha umbo ndani, yaani wasifu wake wa kisaikolojia kama inavyoonekana baadaye katika usimulizi. Msimulizi anataja kwamba anapokuwa kazini huwa makinifu na huwajibika kazini na akiwa nyumbani huwa mkarimu na mchangamfu. Kupitia mifano hii, tunaweza kuhitimisha kwamba kuna uhusiano wa karibu kati ya maelezo ya umbo nje la mhusika na wasifu wake wa ndani, yaani tabia. Maelezo ya mpelelezi kwa njia hii yanaboresha uaminifu wake kwa wasomaji na kwa hivyo kufanikiwa kupitisha itikadi ya mwandishi. Sifa hii pia inashuhudiwa katika kazi za Abdulla kwani mpelelezi katika riwaya hizi, Msa, anasawiriwa akiwa na umbo la kuvutia. Kupendeza kwa umbo lake kunawafanya watu wengi waliowahi kumsikia wamtambue haraka wakimwona. Maelezo yanayotolewa na mwandishi humsawiri kama mtu asiye wa kawaida na mwenye sifa zisizokuwa na watu wengi. Hivi ndivyo asemavyo msimulizi kumhusu Msa katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* (1973):

> Bwana Msa, hapana asiyemjua, ni yule kijana wa Kiafrika, mwenye weusi wa rangi iliyotia shani, mtaratibu wa tabia na shupavu wa sifa. (uk.43).

Usawiri wa wahusika kwa kuwapa umbo nje la kupendeza kunawasaidia wasomaji kujinasibisha na yeye kwa kuwa kufikia mwishoni mwa hadithi kama ada yeye ndiye humnasa mhalifu ama kuwaelekeza polisi kwenye mhalifu huyo. Kwa njia hii anachangia katika kuukomesha uhalifu na kurudisha hali ya kawaida iliyokuwepo katika jamii kabla ya uhalifu huo kufanyika. Kwa kupambana na uhalifu kwa njia ya upelelezi na kuwapatiana wahalifu kwa polisi ili kupewa adhabu, kunamsawiri mpelelezi kama kiwakilishi cha itikadi ya mwandishi. Aghalabu itikadi hiyo kama tunavyoiona katika riwaya za Godfrey Levi, Abdulla na Mtobwa ni kuwa uhalifu haulipi na wema una nguvu kushinda uovu.

#### 4.2.2.4 Mandhari na Uhusika

Katika riwaya za kiupelelezi, mandhari huchukua nafasi muhimu na hutumika kwa njia maalum kuliko inavyokuwa katika tanzu nyinginezo za riwaya. Kwa kuwa hizi ni riwaya zinazotumia taharuki kwa kiasi kikubwa, mandhari hutumika kama kigezo cha uajabishaji unaokuza taharuki na kuwa msingi mkuu katika msuko. Aghalabu uhalifu unapotendeka, wahalifu hupatikana katika majumba mahame au uhalifu wenyewe kutendwa katika katika majumba kama hayo. Pia sehemu za miji zenye mandhari ya kuogpfya hutumika kwa njia hiyo. Kwa hivyo, maelezo ya kimandhari yanaishia pia kuathiri uhusika.

Mazingira anamoishi mhusika kama vile sehemu ya mji anayoishi, chumba au mtaa anaoishi pamoja na mazingira ya kijamii kama vile familia yake, tabaka lake vinaweza kuwa viashiria vya wasifu wa mhusika huyo. Kwa mfano mhusika ambaye makazi yake ni chumba kilichobomokabomoka na chenye uchafu ndani na harufu mbaya yaweza kuwa ishara ya uozo wa tabia zake, umaskini unaomkumba au ubwete wake. Kinyume chake pia ni kweli kwa kuwa mazingira ya kuvutia kama vile jumba kubwa na lenye samani ghali huweza kuchukuliwa kama kielekezi cha mhusika tajiri. Waandishi hutumia usawiri wa kimandhari kama mkakati wa kuchimuza sifa za wahusika ambazo hazikuelezwa moja kwa moja au kupitia vitendo. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* (1973) mazingira ya pale anapoishi mzee Hakimu Marjani yameelezwa kwa njia ambayo inamuelekeza msomaji kwenye utajiri na maisha mema ya mhusika huyo. Hivi ndivyo msimulizi anavyoeleza:

> Kasim alipanda ngazi pana zilizotandikwa zulia au blanketi nene, zilizoongoza kufikia ghorofa akaayo baba yake. Taa zenye nuru kali, moja kwa juu mwisho wa ngazi na moja kwa chini kwa mwanzo wa ngazi zilimmulika Kasim.(uk.1)

Mandhari ya jumba hili pia yanaashiria kwamba mwenyeji ni wa tabaka la juu kwa kuwa hali yake ya kiuchumi inaonekana kutokana na ukubwa wa nyumba na uzuri wake wa nje unaoashiriwa na mwangaza wa taa kadhaa zilizoko nje. Wasifu wa mkaazi wa jumba hilo, Hakimu Marjani, unaojengeka kutokana na mandhari haya ni kwamba ni mtu mwenye nasaba ya kibwanyenye na kiwakilishi cha tofauti kubwa za kiutabaka zilizokuwako katika Unguja kabla ya mapinduzi ya 1964. Hii ndio hali tunayoiona ikijitokeza katika kazi za waandishi wengine wa kutoka Unguja kama vile Mohamed Said Ahmed na Mohamed Suleiman Mohamed. Riwaya kama vile *Kiu* na *Nyota ya Rehema* zinasawiri tofauti za kitabaka za wakati huo pia. Akitilia mkazo umuhimu wa mandhari katika kusawiri wasifu wa wahusika, Wamitila (2002:30) anafafanua kwamba kama vile mhusika anavyoweza kumwathiri mwingine, mandhari nayo pia huweza kumuathiri mhusika

Mandhari ya kijamii kama vile hali ya dini, ndoa na elimu huweza pia kuwa viashiria vya sifa za mhusika. Kwa misingi hii kwa mfano, mhusika ambaye ni kasisi humfikirisha msomaji kuwa anawakilisha wema hivyo kuathiri msimamo wake hata kabla ya kusoma riwaya. Katika riwaya ya *Uchu* (2000) kwa mfano, tunaona hali ya kindoa ikiathiri mitazamo ya wahusika Chifu na Willy Gamba. Katika maongezi ya simu baina ya Chifu na Willy Gamba, Chifu anamuomba Willy akubali kutumwa kuchunguza mzozo wa Rwanda kwa niaba ya Umoja wa Wanaharakati wa

Afrika (PAM). Katika maongezi hayo, Willy anaonyesha dalili za kukataa wito huo kwa sababu ya ndoa. Anasema kuwa ameoa hivi majuzi na mkewe ana mimba. Hata hivyo Chifu anamshawishi kwa kumsifu huku akimfananisha na mchezaji dondi George Foreman. Mazungumzo yao yanaenda hivi:

> Umesikia George Foreman amerudi ulingoni na kutwaa ubingwa? Chifu aliuliza.
> Si kusikia tu nimeona kwenye televisheni.
> Basi nataka nawe pia urudi ulingoni, Chifu akasema kwa tabasamu huku akiupaka mkate wake siagi.
> Mimi! Mimi nimeoa na mke wangu ana mimba, mchezo huo sifanyi, sitafanya ng'o.
> Kwani mimi sijui umeoa? Kwani mimi sijui mke wako ana mimba? Najua. Lakini nakutaka ulingoni. Kwani George Foreman hana mke na watoto; mbona karudi ulingoni? Sikia, mimi ndiye niliyekuruhusu uache kazi na kukushauri uoe na nisingependa uharibu ndoa yako.(uk.8)

Kutokana na mazungumzo haya tunagundua kuwa Willy Gamba anaipenda familia yake na kuthamini ndoa yake. Pili, inadhihirika kuwa Willy ni mzalendo kwani kwa miaka mingi anaitumikia nchi yake kisha mambo ya familia nayo baadaye. Chifu pia anajitokeza kama mhusika anayeithamini ndoa kama tunavyoona akisema ndiye aliyemshauri kuoa. Pili, yeye pia ni mzalendo kwa kuwa anamtafuta mtu shujaa ambaye anaweza kutumwa nchini Rwanda kupeleleza kwa niaba ya viongozi wa PAM. Kutokana na mfano huu, tunaona kuwa mazingira ya kijamii ni njia inayoweza kutuelekeza kwenye wasifu wa mhusika.

#### 4.2.2.5 Analojia katika ukuzaji wa Uhusika

Analojia ikitumika kivyake si mbinu tosha ya kuonyesha wasifu wa mhusika bali inatumika tu kutilia mkazo wasifu uliodokezwa kwa kutumia mbinu nyinginezo (Rimmon-Kenan, 2002:69-72). Kwa hivyo mbinu hii inatumia usawiri wa awali wa matendo, usemi wa mhusika, mazingira au uelezaji wa moja kwa moja unaofanywa na msimulizi au mwandishi kumhusu mhusika. Analojia huonyesha uhusiano wa hali mbili au vitu viwili katika matini bila kuwa na uhusiano wa kiusababishi (no causality relationship). Mhakiki Rimmon-Kenan anatambua mbinu tatu ambazo kwazo analojia huweza kutumika katika usawiri wa wahusika. Katika njia zote tatu, analojia huweza kutumika kutilia mkazo mfanano baina ya elementi mbili. Kando na mfanano baina ya elementi hizo, analojia yaweza kutumika kwa njia inayoonyesha tofauti zilizopo baina ya elementi hizo. Sifa nyingine maarufu kuhusu analojia ni kwamba, inaweza kutumika kwa njia iliyo wazi na

hivyo kuwa rahisi kuitambua au kwa njia fiche hivi kwamba msomaji analazimika kumakinika zaidi ili ajue namna ulinganisho huo unavyofanywa. Zifuatazo ni aina tatu za analojia na jinsi zinavyodhihirika katika riwaya za kiupelelezi zinazochunguzwa:

4.2.2.5.1 Analojia ya Majina ya majazi

Kama tulivyodokeza hapo juu kuhusu namna analojia inavyotegemea mbinu nyingine, vivyo hivyo majazi kama mbinu ya usawiri wa wahusika huwa tegemezi kwa mbinu nyingine ili kufanikisha usawiri wa wahusika kufikia kiwango kilichokusudiwa na mwandishi. Mbinu ya kimajazi huelekeza msomaji kufananisha jina la mhusika na matendo au usemi wa mhusika. Ewen (1980) akinukuliwa na Rimmo-Kenan, anafafanua mikakati minne itumikayo katika kumuumba mhusika wa kimajazi; (i) Kwa kutumia maumbo ya kitahajia ya jina ili kuashiria umbo nje la mhusika. Kwa mfano, jina la mhusika linaloanza kwa herufi ‘O’ linaweza kutumika kumsawiri mhusika mwenye umbo la unene na mvingo, herufi ‘I’ nayo huweza kutumika mwanzoni mwa jina la mhusika kuashiria umbo la urefu na uembamba. (ii) Muundo wa kiakustika- Mwandishi anaweza kutumia jina lenye mtindo wa kionomatopia ili kuashiria tabia fulani kama vile kejeli.(iii) Jina lenye ishara ya kifonetiki kama vile matamshi yasiyo ya kawaida kuashiria wasifu wa mhusika. Kwa mfano, mhusika Grad-grind katika riwaya ya Dickens, *Hard Times* (1854) ambapo kulitamka jina hilo kunahitaji nguvu nyingi na jinsi ya utamkaji wa jina hilo kunaweza kuashiria sifa za mhusika huyu (iv) Jina lenye muundo maalum wa kimofolojia kama vile jina lenye viambishi mbali mbali vyenye maana tofauti na ile maana ya mzizi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, mhusika Jeejee kama mwenye jina lenye muundo maalu wa kimofolojia. Kando na aina hizi nne, Ewen anaeleza kwamba njia ya kisemantiki ndio inayotumika zaidi katika kusawiri majina ya majazi ambapo kipiengee cha maana itokanayo na jina la mhusika ndicho kielekezi kikuu cha hulka ya wahusika. Anatoa mifano ya wahusika kama vile ‘Pride’, ‘Goodman’ na ‘Lust’ ambapo maana ya majina haya ni vielekezi vya hulka zao.

Katika riwaya tunazohakiki mtindo wa kisemantiki umetumika kusisitiza wasifu wa wahusika. Kwa mfano, katika riwaya za Mtobwa kuna wahusika kadhaa wenye majina ya kimajazi. Katika riwaya zake zote mkuu wa polisi Inspekta Kombora ana ushujaa mkubwa. Msamiati ‘Kombora’ ni aina ya kifaa hatari cha kivita kinachotumiwa na jeshi kupigana na adui. Mhusika huyu kama mkuu wa kitengo cha upelelezi wa polisi, anaheshimika sana miongoni mwa askari anaowasimamia na zaidi ya yote ni mtu anayeogopwa mno na wahalifu. Kwa hivyo, kama

kombora linavyotumiwa na jeshi vitani, yeye anatumika katika vita dhidi ya uhalifu. Ndiye dira ya serikali yake kuhusu ujasusi wa ndani na nje ya nchi lakini akishirikiana na mpelelezi wa kibinafsi, Joram Kiango. Katika riwaya hii pia kuna mhusika wa kike, Waridi, ambaye ni mwandani wa Joram Kiango. Msamiati 'Waridi' humaanisha ua la Mwaridi linalovutia kwa harufu yake nzuri. Uzuri wa ua hili unatumika kianaolojia kuashiria umbo lake la nje lenye kuvutia kutokana na urembo wake. Msimulizi anaeleza wasifu wake hivi; 'Yu msichana mwenye sura nzuri, umbo nzuri, mwendo mzuri na kila kitu kizuri'.

Mwandishi Abdulla naye pia huitumia mbinu ya majazi mno katika riwaya zake kuashiria sifa anazokusudia wahusika wake wawe nazo. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* (1968) kuna mhusika Mzungu, Mr Light ayehusishwa na uajabu wa eneo la Kisima cha Giningi. Mahali kisima kipatikanapo kuna uajabu wa taa iliyowekwa hapo kitambo. Taa hii imekaa miaka mingi bila kuzimika wala kuhitaji kuwekwa mafuta wala utambi. Mzungu mmoja alipofika katika eneo hili alishangazwa na taa hiyo na kwanza alifanya bidii kuchunguza namna taa hii ilivyowaka maisha yake. Jina la Mr.Light linatumika kimajazi kwa njia ya kinyume kwa kuwa baada ya kuichokorachokora akiichunguza, taa hiyo ilizimika na haijawahi kuwaka tena hadi leo. Hata wenzake kutoka Ulaya hawakuweza kumsaidia kuirudisha katika hali iliyokuwa. Kwa hivyo aliuzima mwangaza wake na hata kusababisha idadi ya wageni waliokuwa wakizuru eneo hili kujionea miujiza yake kupungua. Maelezo haya yanazidisha uajabu wa Kisima cha Giningi na kufichua udhaifu wa Mr.Light. Wahusika wengine wa kimajazi ni mhusika Hakimu Marjani katika riwaya ya *Duniani kuna Watu.* Neno Marjani ni aina ya jiwe lenye dhamana kubwa. Katika muktadha wa riwaya hii, mhusika huyu ni tajiri mwenye mali yenye dhamana kubwa. Kwa mfano, ana jumba kubwa la ghorofa, magari kadhaa, mashamba, jahazi nne zinazosafiri hadi Maskati na Bombay na mashua za uvuvi nne. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, mhusika Sikudhani anadhihirisha maana ya jina lake katika mahusiano yake na dadake, Twajuana Binti Abdalla.'Sikudhani' anamwamini dadake mno mpaka anashindwa kuutambua uovu wake. Uovu huo unajitokeza wakati Twajuana anapopanga kumuua Sikudhani kwa kumwangushia jiko kichwani. Hii ni kumzuia Sikudhani asiende kuripoti kwa polisi kesi ya ulaghai ya Twajuana. Twajuana Binti Abdala alikuwa ametumia pesa za Amanulla alizopewa ili azitumie kumlea, akazifuja kwa kujinunulia nyumba na kisha kumtupilia mbali mtoto huyo, huku akimfukuza kwake. Kwa hivyo, jina hili, 'Sikudhani' limetumiwa kuashiria mhusika asiye na shuku kwa dadake na anazandiki kwa haraka.

Wamitila (2002) katika makala ya ‘What is in a name: Towards a Literary Onomastics in Kiswahili Literature’, anachunguza umuhimu wa kufasiri jina la mhusika kama mchakato wa kurahisisha usomekaji na uelewekaji wa kazi ya Kifasihi. Anasema kuwa majina ya wahusika ni kama ishara za kiisimu zinazofanikisha ubunifu wa kazi ya kifasihi. Kulingana na mhakiki huyu, majina ya wahusika hayatumiki tu kuashiria wasifu wao bali pia huweza kudokeza maudhui, itikadi na mtazamo wa mwandishi.

Katika baadhi ya kazi za kifasihi, majina ya wahusika pia huweza kunyambuliwa kwa kuongeza au kupunguza viambishi hivi kwamba yanaishia kuwa mafupi au marefu kuliko kawaida. Kuhusu urefushaji tunaona sifa hii katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa* ambapo mhuska Juma anapachikwa jina Jeuri na wenzake anapotagusana nao. Hii ni kufuatia vitendo vyake vya kijeuri kama vile kupigana na kutusiana. Jina hili baadaye linageuzwa na kuchukua sifa za kifonetiki ‘Jeejee’ ili kuashiria kejeli inayohusiana na utovu wake wa nidhamu. Kutokana na badiliko hili, jina lake halisi ‘Juma’ karibu lisahaulike. Mhusika Amanullah pia anajulikana kwa jina hilo kwa muda mrefu lakini uchunguzi wa Msa unabainisha kuwa jina hili limenyambuliwa kutokana na jina lake halisi Emmanuel. Kwa sababu ya kurahisisha matamshi linafupishwa na kuwa Manu. Mabadiliko haya yanasababisha mhusika mmoja kujulikana kwa majina tofauti tofouti na wahusika mbali mbali na kusababisha usuli wake uwe changamano zaidi. Katika riwaya za *Kosa la Bwana Msa* (1984) na ile ya *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976), jina la mhusika Mwanatenga linafupishwa pia na kuwa Tenga.

Mbinu kadhaa hutumiwa katika ufupishaji wa jina la mhusika ingawa inayotumika zaidi kama tulivyoona katika mifano ya riwaya za Abdulla, ni ile ya kudondosa silabi. Mbinu nyingine huhusu matumizi ya akronimi ambapo herufi zinazowakilisha jina la mhusika huweza kutumika badala ya jina lenyewe. Huu ni mkakati wa ukwepaji kutambulikana kwa mhusika kutokana na sababu kadhaa hasa ikiwa mwandishi anasimulia jambo la kisiasa ambapo sifa za mhusika huyo zinaweza kuhusishwa na mwanasiasa mashuhuri ama hali fulani tatanishi iliyomo nchini, hali ya kihalisia ya wakati maalum au mahali. Wamitila (1999:36) akizungumzia hali hii, anasema kwamba majina ya wahusika yanaweza kuhusishwa na mandhari ya kimahali au wakati. Kijumla, matumizi ya akronimi kama majina ya wahusika yanaweza kuashiria hali za kiuchumi, kisiasa na kijamii zilizopo nchini wakati wa kwandikwa kwa kazi hiyo. Katika riwaya ya kiupelelezi ya *Black Star Nairobi*, kuna mhusika anaitwa ‘O’, ufupi wa Odhiambo, ambaye alikuwa mkuu wa upelelezi

nchini Kenya, anaungana na Ishmael, askari wa kutoka Madison, Wisconsin, Marekani na wanaanzisha shirika la kiupelelezi liitwalo, Black Star. Kwa kulitumia jina la kiufupisho kama hili, mwandishi anaepuka kumhusisha mtu yeyote halisi na kazi hiyo.

Katika riwaya ya Marjorie Oludhe iitwayo *Coming to Birth* (1986) ambayo inahakiki usaliti wa viongozi wa Kenya dhidi ya wananchi wao baada ya uhuru, kuna mhusika mbunge wa Gem anayejulikana kama Mr. M. Mr. M kama kiwakilishi cha usaliti huu, anajiwa na wananchi wa eneobunge lake kwake nyumbani ili awasaidie lakini anajificha ndani ya jumba lake na kusema wananchi hao waambiwe yuko kanisani. Hata hivyo, anawaagiza wafanyikazi wawapikie wananchi hao ugali walie chini ya Mwembe kabla ya kuondoka. Kama tulivyosema hapo juu, mwandishi katika muktadha kama huu analazimishwa na sababu za kisiasa kuepuka kulitaja jina la mhusika na kuamua kutumia akronimi badala ya kutumia nomino ya kipekee kumtaja mhusika. Hii pia ni njia ya kuashiria kuwa mhusika huyu anaweza ni mwanasiasa yeyote yule. Kwa njia hiyo, mwandishi anafanikiwa kujumlisha kundi la wanasiasa katika jina la mhusika mmoja.

Katika riwaya ya *Uchu* (2000) muktadha wa kisiasa uliohusu mauaji ya halaike nchini Rwanda unaoangaziwa katika riwaya hiyo, unamlazimu mwandishi kutumia akronimi kumtaja mhusika mkuu ambaye ni mwanasiasa na kiongozi wa ngazi za juu katika serikali ya Tanzania. Anapewa jina JKS. Kando na kuhusika katika mzozo wa Rwanda, kiongozi huyu anapania kuunyakua urais wa nchi ya Tanzania kwa kusaidiwa na mataifa ya Kimaghribi hususan Ufaransa. Kwa kuwa JKS anahusika sana katika siasa za Tanzania na kujiunga na mrengo mmoja katika mzozo wa Rwanda, inakuwa bora kwa mwandishi kumpa jina JKS. Kwa kutumia njia hii, mwandishi anaepuka hali ambapo hatashutumiwa kwa kumhusisha mtu halisi na mizozo hii ya kisiasa. Jina la kiakronimi pia ni njia maarufu ya kumchimuza mhusika ili atambulikane kwa urahisi miongoni mwa wasomaji na wahakiki.

#### 4.2.2.5.2 Analojia ya kimahali

Rimmon-Kenan anarejelea uhusiano uliopo baina ya eneo la kijiografia anamoishi mhusika na wasifu wake. Tasnifu yake ni kwamba mahali aishipo mhusika kunaweza kutumika kama kiashiria cha sifa zake. Uhusiano huu unaweza kujengeka kwa njia ya moja kwa moja ama kwa njia ya kinyume. Kwa mfano, mhusika anayeishi katika eneo la jangwa akisawiriwa kama anayekosa sifa za uaminifu na ukweli, hili laweza kuonekana kama dhihirisho la moja kwa moja kuhusu uhusika wake. Ikiwa mhusika anaelezwa kuishi katika eneo lenye utulivu na amani lakini naye aonyeshwe

kama mhalifu au mwenye fujo nyingi, huu utakuwa udhihirishaji wa wasifu kwa njia ya kinyume. Hata hivyo tunaona maelezo ya mhakiki huyu yakiingiliana mno na usawiri kupitia mandhari tuliouzungumzia hapo awali. Mpaka wa udhihirishaji wa wahusika baina ya njia hizi mbili ni finyu mno na kwa sababu hiyo hatuoni mfano mwafaka katika riwaya teule tunazohakiki.

#### 4.2.2.5.3 Analojia ya Kiulinganuzi wa wahusika

Katika mbinu hii wahusika wanawekwa sambamba ili tofouti zao pamoja na kufanana kwao kujidhirishe. Ulinganuzi huo unatilia mkazo sifa za kila mmoja na namna anavyotofoutiana na mwingine kwa kuzingatia sifa maalum kama vile kwa kuzingatia misingi ya wema na uovu. Katika riwaya za kiuhalifu na za kiupelelezi, msingi wa wema na uovu ni mkakati wa kifomyula unawatofautisha wahusika. Hii ni kwa sababu wapelelezi (wawe wa polisi ama wa kibinafsi) pamoja na wasaidizi wao husawiriwa daima wakiwakilisha wema, utu na urudishaji wa hali ya kawaida huku kwa upande mwingine, wahalifu nao daima wakisawiriwa kama waovu na adui wa sheria na amani. Hivi ndivyo tunavyowaona wapelelezi kama vile Msa (katika kazi za Abdulla), Joram Kiango (katika kazi za Mtobwa), Far Katy Wingo (katika kazi ya Katalambulla), na Willy Gamba (katika kazi za Musiba) na Inspekta Paul katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa.* Hawa wote ni wapenda amani, utulivu na udumishaji wa sheria kinyume na wahalifu ambao huwakilisha vinyume vya sifa hizo. Wanawakilisha uvunjwaji wa sheria kupitia vitendo vya wizi, uuaji, kurithi mali isiyokuwa yao na wahujumu wa uchumi na kisiasa wanaovuruga mataifa huru ili kujitajirisha wao tu.

Katika riwaya ya kiupelelezi kuna ulinganuzi unaohusu mpelelezi na msaidizi wake. Aghalabu mpelelezi husawiriwa kama mhusika mwenye uajabu mwingi katika nguvu zake za kimwili na za kiakili, ujasiri na umakinifu mwingi unaofaa katika harakati za kuwasaka wahalifu. Msaidizi wa mpelelezi kwa upande mwingine naye husawiriwa kama kiumbe dhaifu, asiye na uwezo kama ule wa mpelelezi. Katika riwaya za Abdulla, mpelelezi Msa na msaidizi wake, Najum wanalinganishika kwa njia hii. Msa ni mpelelezi anayedhihirisha umahiri katika fikira yake na matumizi ya mantiki katika kuchanganua kadhia mbali mbali huku msaidizi wake, Najum akikosa kabisa sifa kama hizo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani kuna Watu* (1973), Najum mwenyewe anakiri udhaifu wake anaposhuhudia ujasiri na urazini wa Msa. Najum anasema hivi:

> Sasa Bwana Msa, unatarajia nini zaidi kutoka kwangu? Wewe mwenyewe unajua kuwa wewe ndiwe nahodha, mimi ni baharia tu. (Uk.53)

Najum anapotoa jibu kama hili, linamshangaza Msa kwa kuwa anamtaraji Najum awe amepata uzoefu mwingi kwa sababu amekuwa pamoja na Msa kwa muda mrefu. Msa haelewi ni kwa nini Najum anashindwa kutofautisha picha za watoto wa Mzee Hakimu Marjani anapoonyeshwa picha hizo katika gazeti, ilihali kuna sifa fulani inayoonekana kuwapambanua picha hizo zikiangaliwa kwa jicho la ndani. Msa anamuuliza Najum;

> Juu ya hayo Najum, lakini baharia mwenyewe amekaa na nahodha wakasafiri pamoja katika bahari nyingi kubwa kubwa, basi ni lazima atarajiwe kuwa kapata ustadi na maarifa ya kutosha.(uk.53)

Katika kuhitimisha sehemu hii ya analojia, tunasisitiza kwamba huu ni mkakati wa kutilia nguvu wasifu wa mhusika ambao umedokezwa kwa kutumia mbinu nyinginezo kama vile maelezo ya moja kwa moja au kwa njia mbali mbali za uashiriaji kama vile usemi au vitendo vya wahusika. Tumejadili aina tatu za analojia ambazo ni majina ya majazi, analojia ya kimahali na analojia ya kiulinganuzi, zote zikitumika aidha kuashiria mfanano au tofauti baina ya elementi za kuashiria na wasifu unaoashiriwa. Tumeona kuwa jina la kimajazi lenye maana kinyume na wasifu wa mhusika, humsawiri mhusika kama anayekejeliwa.

Kwa kuwa waandishi wa riwaya za kiupelelezi wana mtindo wa kuwatumia wahusika walewale katika kazi zao nyingi, pana haja ya kuichunguza hali hiyo katika riwaya teule. Baadhi ya waandishi wamewasawiri wahusika hao wakitumia vielelezo vya waandishi wa Kimagharibi, hususa kazi za Conan Doyle wa Uingereza na Raymond Chandler. Kwa kuandika katika mtindo huu, kazi za kiupelelezi za Kiswahili zina uhusiano wa kimwingilianomatini.

## 4.3 Uhusika wa Kimwingilianomatini

Mahusiano ya kimwingilianomatini yanaweza kujitokeza katika viwango kadhaa vya kidhamira na kimtindo. Kwa mfano, kuhusiana na mtindo, riwaya zinaweza kuwa na umwingilianomatini na riwaya nyinginezo katika viwango vya uhusika, usimulizi, kimandhari, kimotif, miongoni mwa vipengele vinginyo. Kihusika, mwingilianomatini unajitokeza kwa njia mbili. Hizi ni; urejeleaji wa wahusika walewale waliotumika katika kazi za awali na, pili, kuna urejeleaji wa wahusika

wapatikanao katika riwaya za waandishi wengine. Mtindo wa kwanza ni maarufu sana katika kazi za Mohammed Said Abdulla ambapo wahusika Bwana Msa, Najum na Spekta Seif waliojitokeza katika riwaya ya kwanza, *Mzimu wa Watu wa Kale*, wametumika katika riwaya zake takribani zote zilizoifuata hii. Pia kuna wahusika wengine wajenzi waliotumika katika zaidi ya riwaya moja. Kwa mfano, Mwanatenga na Amanullah ni wahusika walioko katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa* na *Kosa la Bwana Msa.* Tangu kuoana kwao katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, wanajitokeza tena katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* kama bibi na bwana.

Katika riwaya za Ben Mtobwa, wahusika wakuu wapatikanao katika riwaya yake ya kwanza ya *Lazima Ufe Joram* (1983), ni Joram Kiango kama mpelelezi, Judor Proper kama mhalifu na Inspekta Kombora. Wahusika hawa wameendelea kutumika katika riwaya nyingi za baadaye wakiwa na sifa zilezile. Baadhi ya riwaya wanakojitokeza ni *Tutarudi na Roho Zetu? Salamu Kutoka Kuzimu*, *Dimbwi la Damu*, *Najisikia Kuua Tena* miongoni mwa nyinginezo. Ukweli huu unasisitizwa na Gromov (2012) anaposema kuwa wahusika hawa wanapatikana katika riwaya kumi kati ya riwaya kumi na tano za mwandishi huyo. Katika riwaya tatu za mwisho, *Roho ya Paka* (1996), *Nyuma ya Mapazia* (1996) na *Mtambo wa Mauti* (2004), mhusika mhalifu mwingine, Adrian, alijitokeza. Riwaya za Musiba vile vile, zimetumia mtindo huo ambapo mhusika mkuu na mpelelezi, Willy Gamba ametumika katika riwaya zote nane za mwandishi huyu. Riwaya hizi ni, *Kufa na Kupona* (1974), *Kikosi cha Kisasi* (1979), *Kikomo* (1980), *Njama* (1981), *Hofu* (1986), *Hujuma* (1996), *Uchu* (2000) na *Kivuli* (2019).

Katika kiwango cha pili, mwingilianomatini hujitokeza wakati kazi ya mwandishi mmoja inapoirejelea kazi ya mwandishi mwingine. Kuhusu uhusika, baadhi ya waandishi wa riwaya za kiupelelezi za Kiswahili, wanaonyesha kuathiriwa na waandishi wa Kimagharibi katika usawiri wa wahusika wao. Katika riwaya za Abdulla kwa mfano, mpelelezi Bwana Msa, amesawiriwa kwa kielelezo cha mpelelezi Sherlock Holmes wa riwaya za Conan Doyle. Wahusika wapelelezi hawa wanafanana kwa njia kadhaa. Kwanza, wote ni wapelelezi wa kibinafsi, pili, Holmes kama Msa, anawapiku wapelelezi wa polisi katika uchunguzi, tatu, wote wanatumia mantiki na urazini katika uchanganuzi na utatuzi wa mgogoro, nne, wote ni wavutaji sugu wa tumbako. Msa na Holmes wanavuta kiko kila wakati wanapokuwa na masuala yanayohitaji umakinifu na uwazaji wa ndani. Mwisho, wapelelezi hawa wana wasaidizi wao wasiokuwa na maarifa mengi kama wao tofauti

ikiwa kwamba msaidizi wa Holmes, Dkt.Watson, ndiye pia msimulizi katika baadhi ya hadithi ilhali za Conan Doyle, huku msaidizi wa Msa, Najum, siye msimulizi katika riwaya za Abdulla.

Tofauti nyingine ni kuwa Sherlock Holmes analipwa kwa uchunguzi wake huku Msa akijitolea kwa uzalendo wake kuwasaidia polisi. Zaidi, Holmes anatumia teknolojia katika uchunguzi wake. Kwa mfano, katika *A Study in the Scarlet,* Sherlock Holmes anachunguza majivu ya aina aina ili kujua aia za tumbako na kuzihusisha na watu wazivutazo. Katika *Mzimu wa Watu wa Kale*, Najum akishangazwa na uwezo wa Msa anawita, 'Sherlock Holmes' huku naye Msa akimjibu, 'Simple my dear Watson'. Uk.41. Pia katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, kuna maongezi (uk.46) baina ya Mwanatenga na Bibie Shali ambapo wanasema kuwa Bwana Msa anapenda kulinganishwa na Father Brown kuliko na Sherlock Holmes. Maongezi haya yanayorejelea waandishi wa Kimagharibi, ni ithibati kuwa mwandishi wa kazi hizi, Abdulla, ameathiriwa na usomaji wa kazi za kiupelelezi za Kimagharibi kama vile za Conan Doyle na za G.K. Chesterton. Kazi za Abdulla pia zimewaadhiri waandishi waliofuatia baadaye kama vile Katalambulla katika usawiri wa mhusika mkuu, huku naye Katalambulla akiwaadhiri waandishi waliojitokeza baada yake miaka ya themanini kama vile Mtobwa. Mbatiah (2020:11) anaeleza kuwa uhusika wa Joram Kiango katika kazi za Ben Mtobwa umeathiriwa na riwaya ya *Simu ya Kifo* kwa kuwa umakinifu na uzalendo wa Joram Kiango ni sawa na ule wa Wingo katika *Simu ya Kifo.* Pia kuna mfanano mkubwa baina ya usawiri wa Willy Gamba na Joram Kiango. Mbinu zao za kupambana na adui zinafanana kwani wote wanatumia silaha mbalimbali na wamejifunza mbinu za kupigana za karate na judo. Hawa wamesawiriwa kwa misingi ya Filamu za Kimagharibi. Katika riwaya ya *Njama*, Willy Gamba mwenyewe anajigamba akijiita, 'Komandoo'. Msambao wa athari za uandishi wa riwaya za kiupelelezi kutoka kwa waandishi wa Kimagharibi hadi kwa waandishi wa Kiswahili unaweza kuonyeshwa hivi:

Edgar Allan Poe→Conan Doyle→Mohamed Said Abdulla→Faraj Katambulla→(Ben Mtobwa, Elvis Musiba). Katika mchoro huu, waandishi waliopo kwenye mabano wanaweza kusemwa kuwa walizipata athari kutoka wa watangulizi wao wakati mmoja, yaani kuanzia miaka ya themanini).

### 4.4 Uhusika wa Kifomyula katika Riwaya ya Kiupelelezi

Kazi za kifasihi huwekwa katika tanzu mbalimbali kulingana na kuwepo kwa sifa na kaida zilizokubalika za utanzu huo. Vilevile, katika utanzu mmoja wa kifasihi, kazi zinazofuata mtindo

fulani huwekwa katika kijitanzu chake. Hivyo, katika riwaya ya Kiswahili, kuna vijitanzu kadhaa ambavyo hubeba kazi zilizoandikwa kwa kufuata sifa na kaida za kijitanzu hicho. Kwa hivyo, kazi ya kifasihi inaweza kukubalika kuwa ni aina ya utanzu fulani tu ikiwa imezingatia fomyula za utanzu huo. Riwaya ya kiupelelezi kwa mfano, inaainishwa kama utanzu wa kifomyula kwa kuwa inafuata kaida zinazoweza kutabirika za kifani na kidhamira. Katika tanzu za kifomyula kama vile riwaya ya kiupelelezi, ufomyula hujitokeza kupitia uhusika, mandhari na muundo wa kimsuko. Wahusika wapatikanao katika riwaya za kiupelelezi husawiriwa kwa njia maalum ya kifomyula kama inavyoonyeshwa hapa chini.

Sifa moja maalum ya kifomyula ni uwekaji wahusika katika makundi ya wahusika watatu. Kimura (1992), anatambua matumizi ya sifa ya utatu katika usawiri wa wahusika wakuu katika utanzu huu. Wahusika hao ni;

(i) Mpelelezi/ mbabe

(ii) Mhalifu/Mkosaji

(iii) Mhasiriwa/Mkosewa.

### 4.4.1 Uhusika wa Mpelelezi

Kimura anataja kwamba kuhusiana na mhusika mpelelezi, kuna aina nyingine ya utatu unaoweza kudhihirika; yaani kuwepo kwa mpelelezi wa kujitegemea au wa kibinafsi, pili, kuna msaidizi wa mpelelezi wa kibinafsi na, tatu, kuna mpelelezi anayewakilisha polisi. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki wapelelezi wa kibinafsi ni Msa, katika riwaya za Abdulla, Joram Kiango, katika riwaya za Mtobwa na Willy Gamba katika riwaya za Musiba. Wapelelezi wa polisi katika riwaya hizo nao ni kama vile Inspekta Seif katika riwaya za Abdulla, Inspekta Kombora katika riwaya za Mtobwa, Inspekta Far Katy Wingo katika riwaya ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo*, Inspekta Paul katika riwaya ya Simbamwene ya *Kwa Sababu ya Pesa* na Mzee Kombo katika riwaya ya Levi ya *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu*. Nafasi ya mhusika msaidizi wa mpelelezi inadhihirika vyema katika riwaya za Abdula kupitia mhusika Najum ambaye humfuata Msa katika kila kisa akichunguzacho akimhimiza au kumkumbusha (Tutarejelea nafasi ya mhusika msaidizi baadaye).

Kulingana na mwasisi wa utanzu huu, Edgar Allan Poe, mpelelezi wa kibinafsi ni mkwezwa na mtendaji mkuu mwenye akili ya kiajabu. Baadhi ya sifa hizi zilijitokeza katika kazi yake ya

kwanza ya *Murders in the Rue Morgue* (1884) na hadithi fupi nyinginezo zilizofuata. Mpelelezi apatikanaye katika kazi za Poe anachunguza migogoro kwa kutumia mantiki na urazini bila hujiingiza katika hatari. Kijumla, mhusika mpelelezi kama mhusika mtendaji huwa na wasifu maalum unaomtenga na wahusika wengine. Umaarufu wa akili na nguvu zake zinamsawiri kama binadamu asiye wa kawaida. Umaarufu wa mpelelezi kama anavyosawirika katika riwaya teule unajitokeza kwa njia zifuatazo:

Kwanza, huyu ni mhusika msiri mno. Usiri wake unatokana na hali ya kazi aifanyayo ambapo uwekaji wa siri humsaidia kuepuka mitego ya wapinzani. Pili, usiri wao unawatenga na wananchi wa kawaida hivyo kuzidisha uajabu wa wasifu wao. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, Amanullah anapatana na Msa katika chombo cha kusafiria na anapomuuliza Msa ikiwa yeye ndiye yule mpelelezi hodari, hasemi ndio au la. Anajibu tu,‘Sijui nikujibu nini bwana Mdogo’.uk.3. Kupitia kauli hii, ni wazi kwamba Msa hataki kujulikana ikiwa ndiye mpelelezi. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, Joram Kiango pia anajitokeza kama mhusika msiri mno kama njia ya kuhifadhi usalama wake. Mpelelezi Joram Kiango akiongea na msichana Unono, aliyekuwa wa kwanza kushuhudia kwamba Joram hakufa wakati makazi yake ya siri yalipolipuliwa kwa bomu, anamuomba Unono kuweka siri:

> Jambo lingine nitakalokuomba ni la siri, tafadhali sana usimfahamishe mtu yeyote kuwa unaishi na mtu hapa. Wala usimfahamishe mtu yeyote kwamba mtu huyu alinusurika ajali ya bomu. Tafadhali iweke vyema siri hiyo. Ningependa kuishi hapa kwa wiki moja bila mtu yeyote kufahamu. (uk.80)

Pili, sifa ya kipekee zaidi ya mhusika wa kipelelezi ni uajabu wao. Wanazungukwa na uajabu katika matendo yao, tabia zao na hata mazingira wafanyiapo kazi. Mgeni (1983) alichunguza uajabu katika kazi za Abdulla na kugundua kuwa mpelelezi anaonyesha uajabu kwa njia kadhaa. Kwa mfano, uwezo wa Msa wa kutatua migogoro mikubwa kwa kuchunguza mambo madogo madogo na kwa kutumia umakinifu mwingi, unamdhihirisha kama mtu wa ajabu. Pili, Mgeni anasema kuwa Msa anatumia kitabu kiitwacho ‘Kinyume cha Mambo’ kinachozidisha uajabu wake. Uajabu huo unatokana na kweli kwamba, haijulikani kitabu hiki Msa alikitoa wapi kwa kuwa hamna nakala nyingineyo popote. Rafiki yake wa karibu, Najum, pia anashangaa jinsi kitabu hiki kinavyompa Msa maarifa mengi.

Katika riwaya ya *Duniani kuna Watu* kwa mfano, Bwana Msa anatumia mantiki na urazini kutatua kadhia iliyohusu kupotea kwa mali ya Mzee Hakimu Marjani pia kwa njia ya kuwashangaza wengi. Anachunguza picha za watoto wa Hakimu kwenye magazeti na kwa kutumia elimu yake ya 'Genetics'. Anathibitisha kwamba Kasim hakuwa mtoto halisi wa Hakimu. Msa pia anadhihirisha uwezo wa ajabu kwa kuchunguza aya za msahafu na kuzitunia kufahamu mahali mali ya Bwana Hakimu ilimofichwa. Kwa mfano, katika msahafu, kuna aya iliopigiwa msitari ikisema, 'Kwa hakika idadi ya miezi kwa Mwenyezi Mungu ni kumi na miwili'. Naye Msa anakifasiri kifungu hiki kumaanisha kwamba mali iliyopotea ya Hakimu Marjani imefichwa maili kumi na mbili kutoka nyumbani kwa Hakimu Marjani. Kuhusu ukiushi wa uhalisia wa kihusika wa Msa, Spekta Seif anasema:

> Zote hizi habari za aya kufasiriwa kwa namna hiyo unavyofasiri wewe, kuziunganisha na mambo ya Bwana Hakimu ni jumla ya tasinifu zako, humo katika kufuata akili yako inavyokupeleka…Mimi Singeshughulika hata kidogo kuona aya hii imepigiwa msitari chini yake au aya ile imepigiwa msitari juu yake.(uk.28)

Sifa hii ya uajabu ni mojawapo wa sifa maalum zinazopambanua riwaya ya kiupelelezi na riwaya ya kiuhalifu kwa kuwa uhalifu katika riwaya ya kiupelelezi hufanyika kwa njia za kiajabuajabu ilhali uajabu huo si lazima uwepo katika riwaya ya kiuhalifu. Kuhusiana na usawiri wa Msa kwa njia hii, baadhi ya wahakiki wanahisi kuwa mwandishi Abdulla ameathiriwa na riwaya za Kimagharibi mno. Kwa mfano, Hussein (1971:21-26) na Kezilahabi (1975:37) wanahisi kuwa usawiri huu umetokana na mwandishi kuzisoma riwaya za kina Doyle. Wanasema kuwa mwandishi Abdulla asingepata kichocheo cha kumuumba mhusika kama Msa katika Afrika Mashariki. Hussein anasisitiza kwamba, mhusika Msa si binadamu wa kawaida hasa katika janibu za Afrika Mashariki kwa kuwa wakati wa kihistoria ambapo Msa anapojitokeza katika riwaya za Abdulla suala la upelelezi wa kibinafsi halikuwa limefika katika maeneo ya Unguja. Hii ndio sababu Hussein anasema kwamba Msa ni kioo cha Sherlock Holmes kwa kuwa analandana naye kwa njia kadhaa. Hata hivyo, kwa kuwa utanzu huu ni mgeni na change katika fasihi ya Kiswahili, mfanano wa Msa na Sherlock Holmes unaweza kusemwa kuwa ni suala la sifa ya kiutanzu tu.

Uwezo wa Msa usio wa kawaida pia unajitokeza kuhusiana na jinsi alivyotatua kitendawili cha wa mauaji ya Mwana wa Giningi katika riwaya ya *Kisima cha Giningi.* Kwa mfano, katika riwaya hiyo, mpelelezi wa polisi, Inspekta Seif, anamtia mbaroni mhusika asiye kwa kuwa hana uwezo

wa kumpata mhalifu mwenyewe. Anamtia mbaroni Vuai kwa kuwa ni mumewe Mwana wa Giningi na kwa kuwa anashukiwa na huyo mkewe. Msa anachunguza mabaki ya sigara aina ya 'Cent' kwenye meza na unyevunyevu uliokuwa kwenye sakafu. Analinganisha watu wavutao aina hiyo ya sigara na mtu ambaye ana mdomo wa chini mkubwa zaidi ya ule wa juu, na ambaye ni mfupi (kwa kuwa mshukiwa alipanda juu ya meza ili kufikia sehemu ya dari kisanduku kilipokuwa), anayetokwa na jasho jingi kwenye vidole vya miguu na mikono na kutambua kuwa sifa hizo ni za Ali Makame, kwa hivyo ndiye mwizi. Msa alibaini kuwa jasho la vidole ndilo lililosababisha kubaki kwa alama za vidole kwenye meza, upana wa mdomo wa chini nao ukasababisha sigara kukatika kabla ya kuvutika yote. Matumizi ya uchanganuzi mambo kwa mantiki na kutumia urazini mwingi, ndiyo mambo yanayowashangaza wahusika wengine kumhusu Msa.

Utafiti huu umebaini kwamba uajabu wa mpelelezi haujitokezi tu kupitia matumizi ya akili na urazini kwa njia ya kipekee bali pia kupitia; (a) Matumizi ya nguvu za kimwili na (b) Kupitia ujigeuzaji. Kuhusu matumizi ya nguvu za mwili kwa njia za kiajabu, mhusika anatumia nguvu zake kupigana na wahalifu kando na kutumia viungo mbalimbali vya mwili kama vile ngumi, mateke kando na kuwa shujaa katika utumiaji wa silaha za aina nyingi. Hii ndio sifa tuionayo kumhusu Willy Gamba katika riwaya ya *Uchu*. Willy anaonyesha ujasiri mwingi katika kupigana na maadui wa kimataifa wanaopania kumwangamiza ili asifichue ukiukaji wa haki nchini Rwanda. Inapobidi anatumia silaha mbalimbali kama vile bunduki, bomu na silaha nyinginezo. Anadhihirisha matumizi ya akili kwa njia isiyo ya kawaida anapoivamia mitambo ya adui na kuisambaratisha. Kama mhandisi, anaunganisha nyaya na vifaa vya aina nyingi katika kiwanda cha kuhifadhi silaha za mahasimu wake na kukifanya kiwanda hicho kilipuke baadaye akiwa tayari ametoroka. Kuhusu nguvu zake za upiganaji kwa kutumia misuli, msimulizi anatuambia hivi kumhusu:

> Willy alijitayarisha na kujibanza kwenye ukuta utadhani ni buibui. Yule mtu alikuja akinyata taratibu. Alipofika hapo tu, kama simba anavyomrukia swala, Willy alimtia kabali kwa nguvu zake zote.Yule mtu hata hakuweza kuguna maana kabali ile ilikuwa kali; na huku akitumia utaalamu kumuua kimya kimya kwa kumnyonga.(uk.96)

Katika riwaya ya *Njama*, wahusika, Sherriff na Veronika wanashangazwa na uwezo wa akili yake, Willy Gamba, kulingana na utafiti waliofanya kumhusu. Sherriff anamweleza jinsi yeye

alivyomchunguza Willy Gamba katika mtandao pamoja na faili zao zilizokuwa kwa tarakilishi ili kujua historia yake. Anasema, 'Kompyuta ilizidi kuonyesha kuwa Willy Gamba ana I.Q. ya hali ya juu sana… Sasa naamini ukiambiwa mtu ana I.Q. ya hali ya juu, lazima utambue kuwa kila jambo unalotaka kulifanya, yeye yuko hatua nyingi mbele yako'. (uk. 56).

Kando na riwaya za Musiba, sifa kama hii ya matumizi ya akili kwa njia za kimiujiza inapatikana pia katika riwaya za mtobwa. Katika baadhi ya riwaya za Mtobwa kwa mfano, mpelelezi Joram Kiango anaitumia akili kama mhandisi au mtaalam wa teknolojia kwa kuwa anatumia vifaa mbalimbali vya kielektroniki ili kujikinga dhidi ya adui zake. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* Joram anathibitisha kuwa ana ushujaa si wa kutumia misuli tu bali pia akili katika kutimiza lengo lake. Kana kwamba yeye ni mtaalam wa uhandisi, anatega mabomu katika majumba mbalimbali ya adui waliokuwa wakipanga kuivamia nchi yake. Anaposafiri Afrika Kusini kuwasaka maadui hao, anaunganisha mitambo na kulipua na kuyateketeza majumba kadhaa mjini Johannesburg. Uajabu wake wa kiakili unajitokeza zaidi wakati anapomaliza kutega mabomu hayo na kuendesha ndege ya adui zake na kutorokea mbali. Mwandishi anasema kwamba Joram alikuwa na ujuzi wa nadharia tu kuhusu uendeshaji wa ndege, lakini ilimbidi kujilazimisha kujikumbusha kwa kivitendo. Anaelezwa kama mtu ambaye alikuwa na uwezo wa kuendesha chombo chochote cha usafiri vikiwemo vya majini na ardhini. Ingawa sifa hizi zimetiliwa chumvi, usawiri huu unamsaidia mwandishi kumchora Joram kama binadamu asiye wa kawaida. Hii ni sifa ya kimwingilianomatini kwa kuwa, kupitia uchunguzi wa chimbuko la utanzu huu pamoja na tathmini ya mihimili ya nadharia ya utanzu, tumebaini kwamba kazi za waasisi wa utanzu huu kama vile Allan Poe na Conan Doyle pia ziliwasawiri wahusika kwa mtindo huu wa kiajabu. Wahusika wao walionyesha matumizi ya fikira na mantiki kwa njia ya ajabu mno. Tangu hapo basi watunzi waliofuata wameendelea kuwasawiri wahusika wapelelezi kwa kielelezo kilichowekwa na wasisi hawa. Kwa hivyo, hii ni sifa maalum ya kiutanzu.

Kando na matumizi ya akili kwa njia za kimiujiza, uajabu wa mhusika mpelelezi unajitokeza kupitia sifa ya ujigeuzaji unaohusisha kujibadili sura, kubadili jina, makazi na hata kusingizia kifo, zote zikiwa njia za kujiepusha na mitego ya adui ama kama njia ya kuwatia mtegoni wahalifu. Wasifu huu wa kihusika tunaushuhudia katika riwaya za Mtobwa na Musiba. Katika riwaya za Mtobwa mpelelezi, Joram Kiango anabadili umbo lake hasa ngozi na uso kwa njia mbalimbali. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, anavalia ngozi ya mtu mweupe. Anapoivaa, anafanana

na wazungu wengine na kukodi nyumba katika hoteli maarufu, ambako wageni walitarajiwa kuwa na kikao, ili apeleleze mipango ya adui ambao walikuwa wakipanga kuwaua viongozi wa Afrika waliotarajiwa kuwa na mkutano katika hoteli hiyo, mjini Arusha. Anapokodi chumba cha hoteli hiyo, pia anabadili jina lake na kujisajili kama Dancan, mtoto wa tajiri aliyeko Ulaya. Akiwa katika hali hii ya Uzungu, anawachunguza wafanyikazi wote wa hoteli hii. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* Joram pamoja na msichana msaidizi wake, Nuru, wanajivisha ngozi nyeupe ili waweze kutoroka Afrika Kusini kwa urahisi bila kugunduliwa na walinda usalama. Hii ni baada ya kuyalipua majumba kadhaa na kuharibu mitambo iliyokusudiwa kuyaadhibu mataifa ya msitari wa mbele katika ukombozi wa mataifa ya Kusini (Namibia, Msumbiji, Angola na Afrika Kusini).

Katika riwaya ya *Uchu*, mpelelezi Willy Gamba akikabiliwa na hatari ya kujulikana wakati wa kusafiri kutoka Tanzania hadi Rwanda. Kwa kuwa ni mtu maarufu, anajifanya afisa wa Msalaba Mwekundu ili aweze kuingia nchini Rwanda wakati wa hatari kuchunguza mauaji ya halaiki ya mwaka 1994. Pia anatumia ndege ya shirika hilo na anapofika nchini humo, anapokelewa kama mfanyikazi wa Shirika la Msalaba Mwekundu. Hii ni kutokana na habari za siri zilizoonyesha kwamba angelipuliwa na maadui ikiwa angetumia ndege ya kibinfsi. Akiwa Rwanda, anapangiwa kuuawa kabla ya kufanya upelelezi wake. Anapokuwa katika kupambana na majangili waliokuwa wamelipwa na Bibiane wamuue, Willy anamuua mmoja wao, anamvua shati lake na kujivisha shati hilo ili wale wahalifu waliobaki wamuone kama mwenzao. Njia hii ya kuijibadili kwa mavazi na kwa mbinu nyinginezo ilimfaa Willy katika kuwamaliza mahasidi wake kwa urahisi. Kama sifa ya kiutanzu, tunaona kuwa ujigeuzaji si mtindo mpya bali ni sifa iliyochimbuka kutokana na wasisi wa utanzu huu. Kwa mfano, mwanariwaya za kiupelelezi, Conan Doyle, alimsawiri Sherlock Holmes kama mhusika aliyetumia mtindo wa kujigeuza alipokuwa akichunguza visa mbalimbali.

Ujigeuzaji hauhusu umbo na mavazi tu bali pia ugeuzaji wa majina hutumika kama mbinu ya kuepuka kutambulikana kwa wahusika katika mchakato wa upelelezi. Kabla ya Willy Gamba kusafiri Rwanda kuchunguza hali ya kivita huko kwa niaba ya PAM, ilibidi atumie jina la kughushi ili asitambulikane yeye ni nani. Chifu alimtafutia pasipoti kwa jina la Gerorge Mambo. Kwa hivyo anapofika Rwanda na kudadisiwa katika uwanja wa ndege, yeye si Willy Gamba bali ni George Mambo. Kama tulivyoona katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, Joram Kiango pia alibadili jina na kujiita Dancan ili apeleleze kwa usiri. Hata hivyo, utafiti huu umegundua kuwa ujigeuzaji umbo na majina si mbinu ya wapelelzi tu bali pia hutumiwa hata na wahalifu ili na wao waepuke

kutambulikana haraka. Hii ndio maana utanzu huu unakuwa ni kama mashindano ya mizungu baina ya wahalifu na wapelelezi.

Mara kadhaa, mhalifu maarufu katika riwaya za Mtobwa, Proper ana anajigeuza ajuza, mlemavu, mwanamke na mara nyingine kuwa mzungu ili kuepuka mitego ya Inspekta Kombora. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, anajigeuza chongo na nusu kiwete na kutembea kwa mkongojo. Katika hali hii, anamtembelea Nuru na kumlaghai kwamba amevutiwa na urembo wake. Kwa sababu hiyo, anampa zawadi ya kidani na kumuomba akivae kila wakati bila kumpa mtu mwingine. Inafahamika baadaye kuwa, kidani hicho kilikuwa na tepu ya kurekodi mazungumzo baina ya Nuru na Joram. Kwa hivyo, hii ni njia ya mhalifu ya kuchunguza mienendo ya mpelelezi ili asipatikane.

Anyango (2016) alichunguza usawiri wa uovu katika riwaya za Mtobwa na namna mpelelezi hukabiliana na uovu huo. Baadhi ya mbinu anazotambua zitumiwazo na mpelelezi katika kusuluhisha uovu ni kujigeuza sura, kutumia vifaa mbalimbali, kusaidiwa na wasaidizi wake pamoja na wananchi wengine, kushirikiana na polisi miomgoni mwa mbinu nyinginezo. Katika riwaya za Musiba na Mtobwa, wapelelezi hutumia vifaa vingi vya kielektroniki vikiwemo, bunduki, bomu na kemikali za aina nyingi. Matumizi ya kemikali na vifaa vya kisasa ni badiliko kuu linalozitofautisha kazi za Mtobwa na Musiba kwa upande mmoja na zile za Abdulla. Tofouti hii ikiletwa na tofouti za kiwakati waandishi hawa walipotoa riwaya zao. Abdulla aliandika riwaya zake miaka ya sitini na sabini wakati teknolojia haikuwa imepevuka huku Mtobwa na Musiba wakichapisha kazi zao katika kipindi cha miaka ya themanini hadi miaka ya elfu mbili.

Kuhusu kutofautiana kwa kazi za kiupelelezi za mapema na zile za miaka ya hivi karibuni, Gromov (2008:151-160) katika makala iiywayo ‘Generic Innovations in the Recent Swahili Crime Fiction’ anasema kuwa Mtobwa na Musiba wameleta kijitanzu kipya kinachounganisha sifa za upelelezi na sifa za ujasusi. Mhusika mpelelezi katika kazi zao si kama yule wa Abdulla, Msa, wa kusuluhisha migogoro midogo midogo kama vile urithi na mauaji ya kinyumbani kama yale yanayoshuhudiwa katika riwaya ya *Simu ya Kifo*. Mpelelezi wa kazi za Musiba na Mtobwa aghalabu husuluhisha migogoro ya viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika riwaya ya *Uchu* na ile ya *Tutarudi na Roho Zetu*?, Wapelelezi wanafanya kazi zao katika viwango vya kimataifa na upelelezi wao unaenda nje ya nchi, tofouti zao zikiwa tu kwamba Willy Gamba katika *Uchu* ni ajenti wa kisiri huku Joram akiwa mzalendo anayejitolea mwenyewe.

Sifa ya tatu maarufu kumhusu mhusika mpelelezi ni kwamba ni mwenye majivuno**.** Aidha mpelelezi anajisifu mwenyewe ama kusifiwa na wahusika wengine hususan msaidizi wake au msimulizi kuzisifu tabia na mienendo ya mpelelezi. Uchunguzi wa kihistoria kuhusu chimbuko la utanzu huu umetubainishia kwamba sifa ya kumsawiri mpelelezi mwenye majivuno ilianza katika riwaya za Kimagharibi za waasisi wa utanzu huu kama vile Conan Doyle. Hii ni kwa sababu wapelelezi wenye majivuno tunawapata katika kazi za Allan Poe na Conan Doyle. Ingawa Edgar Allan huchukuliwa kuwa ndiye baba wa utanzu huu katika Ulaya, sifa hii ya majivuno si maarufu sana katika kazi zake kama ilivyo wazi katika riwaya za Conan Doyle. Katika riwaya ya *A Study in Starlet*, Sherlock Holmes akizungumza na msaidizi wake, Dkt.Watson, anasema hakuna mpelelezi mwingine kama yeye ulimwenguni mzima kwa kuwa hata wapelelezi wa kiserikali wanaposhindwa na kazi zao humuomba usaidizi. Anautukuza uwezo wake wa uchunzaji na umakinifu kwa kumpa maarifa ya kipekee. Mwasisi wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, Abdulla, naye aliendeleza matumizi ya usawiri huu katika riwaya zake. Mpelelezi Msa anasifiwa sana kwa upelelezi wake wenye mantiki kubwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, Inspekta Seif anapochunguza wizi wa mali ya Mwana wa Giningi na kushindwa, anamwandikia Msa barua aje kumsaidia kupeleleza. Katika barua hiyo, anamsifu Msa mno, kudhihirisha kwamba visa vinavyomshinda yeye, mkuu wa polisi, Msa anaviweza. Hivi ndivyo mkuu wa polisi anavyokiri:

> Nakumbuka tangu kuisha ile kadhia ya 'Mzimu wa Watu wa Kale' ambayo kama si wewe kutambua siri ya mambo yale, mimi na uispekta wangu singeweza kuifahamu. (uk.8)

Katika kifungu hiki, Msa anajitokeza kama mtu anayeitumia akili yake kwa kiwango kinachowazidi watu wengi wakiwemo polisi. Kwa hivyo, kama Msa alivyoweza kudhihirisha uwezo wake katika kesi ya hapo awali, Inspekta Seif anataraji kwamba atamfaa mara hii pia. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, Msa anadhihirisha umahiri wake katika upelelezi wa kupotea kwa pesa za Hakimu Marjani. Kabla ya kumwalika Msa kutoa ufafanuzi wake, Inspekta Seif anawaeleza waliohudhuria wasifu wa Msa kwa kumumiminia sifa nyingi. Seif anawaambia hivi:

> Mimi niliwahi kukutana naye mara kadha wa kadha, na mara zote hizo mtu yule alinishangaza kwa shani ya akili yake katika kugundua mambo yaliyofichwa na alinifadhaisha kwa uhodari wake katika kutatua mtanziko au kufumbua fumbo.

(uk.77)

Mpelelezi Joram Kiango katika riwaya za Mtobwa pia anajisifu na kusifiwa na wahusika wengine mara kadhaa kutokana na uwezo wake wa kiakili na nguvu za mwili. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, mpenzi wake, Neema, anapousifu ujasiri wake, yeye pia anakubali kuwa hana hofu yoyote. Anasema, 'Sijui hofu ni kitu cha aina gani kweli, labda itabidi nimpate daktari mzuri anipime na kuona kama ninazo chembechembe za kitu hicho kinachoitwa hofu moyoni mwangu'. (uk.16). Katika riwaya za Musiba, mhusika mpelelezi anasawiriwa vilevile akiwa na majisifu mno. Katika riwaya ya *Njama* kwa mfano, Willy Gamba anawaambia wahusika wasaidizi wake jinsi alivyo maarufu. Akimweleza Eddy jinsi alivyoepuka kuuawa na adui zao, Willy Gamba anasema, 'Mimi nikiwa na silaha ya namna ile hata likija jeshi la watu mia hawaniwezi'. Katika muktadha mwingine katika riwaya hii, Willy Gamba anapofanikiwa kuwapata rafiki zake kwa haraka anamwambia msomaji hivi, 'Lazima utambue Willy ni mtu mwenye bahati siku zote. Hiyo ndiyo inayoitwa bahati ya kuzaliwa; na MamaWilly alinitoa nayo tumboni'. (uk.28). Kufikia mwishoni mwa riwaya, Willy anapotumia mbinu kadhaa za upiganaji kama vile Karate, Judo na kuruka hewani kwa mtindo wa Kung Fu, wenzake, Eddy na Sherriff walishangaa. Kujibu mshangao wao, Willy anawaamia, 'Kuwa Komandoo siyo Mchezo'. Uk.94. Mifano hii ni dhihirisho kuwa mhusika mpelelezi hupenda kujisifu ama kusifiwa.

Usawiri wa wahusika wapelelezi kwa kuwasifu au kwa mpelelezi kujisifu mwenyewe ni njia mojawapo ya kuzua taharuki kumhusu mhusika na kuongeza mvuto katika riwaya nzima. Hii pia ni mbinu ya kiutanzu inayotumiwa vilevile kuongeza uajabu katika ploti za riwaya za kiupelelezi. Kama alivyogundua Mgeni (1983:48), usawiri wa mpelelezi akiwa na uwezo usio wa kawaida huongeza uajabu katika kazi za Abdulla. Knight (1980:67) anaeleza kwamba usawiri wa mpelelezi kwa njia ya ajabu ni mtindo uliotumiwa mno na Conan Doyle na usawiri huu uliishia kuathiri namna waandishi wa baadaye walivyowaumba wahusika wapelelezi. Anasema kwamba athari zake zilijitokeza sana katika riwaya za Kimarekani za kipindi cha 1920-1930. Athari za Doyle zilijitokeza katika fasihi ya Kiswahili kupitia kazi za Abdulla na kusambaa baadaye.

Nne, mhusika mpelelezi aghalabu ni mvutaji tumbaku sugu. Wapelelezi wengi wameonyeshwa kama wenye uraibu wa kuvuta tumbaku aidha kwa kiko ama kama sigara kwa sababu mbalimbali. Uchunguzi wetu umebaini kwamba hii pia ni sifa ya kihistoria na ya kiutanzu kwa kuwa kielelezo kilichowekwa na Conan Doyle ambacho ni Sherlock Holmes ndicho kinaigwa. Holmes alikuwa

mvutaji sugu wa kiko. Baadhi ya sababu alizotoa Holmes kuhusiana na tabia hii inakaribiana na majivuno kwani anadai kuwa uvutaji wa tumbako unamsaidia kuituliza akili yake inayokwenda mbio sana (Wakati hana kesi ya kuishughulisha akili hiyo). Holmes alikuwa pia na uwezo wa kuchunguza aina mbalimbali za tumbaku na aina za kiko kitumiwacho na mhusika na kuweza kubaini saikolojia ya mhusika atumiayo aina hiyo ya tumbaku au kiko. Mpelelezi wa kwanza katika riwaya ya Kiswahili, Msa, ana tabia ya kuvuta kiko wakati anapochunguza kesi yoyote na hasa wakati anapotoa ufafanuzi kuhusu namna alivyompata mhalifu au akitoa suluhu la mgogoro mwishoni mwa hadithi. Kulingana na Msa, uvutaji wa kiko humsaidia kufikiria kwa umakinifu. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, msimulizi anadhihirisha usugu wa uvutaji wa Msa hivi; "Halo! Spekta Seif", aliamkia Bwana Msa na huku kasimama na kumkaribisha, na kiko chake kisichomtoka mdomoni. (Uk.44)

Uvutaji wa Msa ni kama uraibu kwa kuwa kama tunavyoona akielezwa kiko chake hakimtoki mdomoni. Kama inavyoelezwa kwingine, kiko kinapopoa tu, Msa hukichokorachora kwa msumari wa mwavuli ili kiendelee kuwaka ama kwa kutumia kidole chake cha shahada. Kwa Msa uvutaji wa kiko na nguvu za uwazaji ni mambo yaliyooanishwa kama inavyodhihirika alipokuwa anachunguza kupotea kwa mali ya Hakimu Marjani katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu.* Msimulizi anasema kwamba kwa siku kadhaa, Msa alijifungia chumbani bila kula wala kuoga akivuta kiko tu na kuwaza. Msa mwenyewe anakiri usugu wake wa uvutaji na uwazaji hivi:

> Baada ya kuvuta kiko changu kwa wakati mrefu nikiwaza na kuifikiri aya hii, akili yangu ilirejea nyuma kwenye tarehe tatu zile zilizoandikwa mwanzo.(uk. 105)

Usambavu wa usawiri wa mpelelezi kwa njia hii ulimpata Katalambulla kwani mpelelezi wake katika *Simu ya Kifo*, Far Katy Wingo pia anadhihirisha usugu wa uvutaji wa sigara. Kama Msa pia yeye anavuta sigara anapokuwa na kesi ngumu inayohitaji kuifikirisha akili yake. Kwa mfano, Wingo anapopigiwa simu mara ya kwanza na kuambiwa mauaji ya Mzee Jacob, simu inakatika ghafla kabla hajapata kumfahamu aliyeipiga wala mahali alipo. Kufuatia utata huu, anakoleza kiko chake na kuanza kuvuta bila kusema lolote. Msimulizi anasema:

> Akakunja uso kama mtu aliyetaka kukumbuka jambo. Akainua kopo moja la tumbaku. Akarudi kitini akaketi. Akakishindilia kiko chake kikajaa, kisha akakiwasha. Akavuta mara mbili huku anaangalia moshi unavyopaa. (Uk.33)

Kando na uvutaji wa tumbaku kwa kiko kuna wapelelezi wengine wanaotumia uraibu wa sigara. Mpelelezi wa kazi za Mtobwa, Joram Kiango kwa mfano, ni mvutaji sugu wa sigara hasa anapokuwa na jambo la kumfikirisha. Hali hii inaoana na kipindi cha wakati waandishi hawa walipoandika kwani miaka ya 1980 na 1990 anapoandika Mtobwa uvutaji wa kiko ulikuwa ukififia na nafasi hiyo kuchukuliwa na uvutaji wa sigara. Hata hivyo, mwandishi Abdulla ndiye anayeonyesha kuathirika zaidi na mfumo wa Kimagharibi. Mpelelezi Msa ana tabia nyingi za Sherlock Holmes kama vile kurandaranda chumbani akielezea namna alivyogundua jambo. Kama vile Holmes alivyokuwa na hulka ya kuchunguza aina ya sigara avutayo mshukiwa ili kuthibitisha kesi yake, Msa katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, anachunguza mabaki ya sigara aina ya 'Cent' na kuihusisha na washukiwa kadhaa. Mwishowe, anagundua kuwa Ali Makame huvuta aina hiyo ya sigara. Pamoja na ushahidi mwingine inagunduliwa kuwa Ali Makame ndiye mwizi.

Sifa ya tano ya mhusika mpelelezi ni kwamba yeye ni kiwakilishi cha itikadi ya mwandishi au ya jamii yake. Kwa mujibu wa Msokile (1992:48), itikadi ni mfumo wa mawazo ambayo ni msingi wa nadharia za mfumo wa utawala kama vile itikadi ya kihalisia, itikadi ya kijamaa, itikadi ya kibepari, itikadi ya kidini na kadhalika. Nafasi ya itikadi katika kazi za kifasihi inasisitizwa na Chuachua (2011:27) anayesema kwamba itikadi ni dira inayowaelekeza wasomaji kwenye sababu za mwandishi kwandika kazi yake. Kwa hivyo, usomaji wa kazi za kifasihi unaweza kuwaelekeza wasomaji kwenye imani inayomwongoza mwandishi huyo. Katika riwaya za kiupelelezi aghalabu itikadi inayotwala ni ile ya, 'Uhalifu haulipi au wema huushinda uovu'. Hii ndio sababu katika sehemu ya mwisho ya ploti za riwaya hizi, mhalifu huonyeshwa akishikwa na kupewa adhabu huku mpelelezi akiepuka maumivu yoyote na kuibuka kama shujaa. Katika riwaya nyingi za Mohammed Said Abdulla, kwa kifupi Msa, mpelelezi wake ni Msa. Kwa hivyo Msa ni kama kioo cha mwandishi na kupitia mpelelezi huyu, tunaweza kupata itikadi ya mwandishi, yaani mpelelezi ni kiwakilishi cha itikadi ya mtunzi ama itikadi ya jamii yake. Katika kazi za Abdulla kuna itikadi mbili zinazobebwa na mhusika mpelelezi; Kwanza ni kuwa uhalifu haulipi. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, Ali Makame anapoiba mali ya *Mwana wa Giningi* na baadaye kumuua, naye anatorokea ziwani na baadaye maiti yake inapatikana. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mhusika mhalifu Kasim baada ya kumhangaisha Mzee Hakimu anayemlea, mwishoni inagunduliwa kuwa yeye si mtoto halisi wa mzee huyo na hivyo hapati urithi wowote.

Itikadi ya pili, inahusu nguvu na ubora wa watu weusi kama ishara ya usawa wa kibinadamu. Kupitia mpelelezi Msa, mwadishi anawasifu watu weusi (Waafrika asili) na kuonyesha udhaifu wa Wazungu na Waarab. Kwa kurudiarudia weusi wa Msa na kuusifu ujasiri wake na uwezo wa akili yake unaowashinda Spekta Seif na Najum, wasio weusi, anatilia mkazo itikadi hii. Kwa kuwa ni kweli Spekta Seif anashindwa na kumtegemea Msa, ni ishara kuwa anajivunia Uafrika wake. Katika *Kisima cha Giningi*, anamweleza hivi, 'Yule Kijana wa Kiafrika anayeonekana upesi kwa rangi yake iliyozidi kukoza weusi'. Baadaye Msa anapojiunga na Spekta Seif na Najum kwenda kuchunguza kesi ya Mwana wa Giningi, Mwana wa Giningi anapowaona watu watatu wanakuja anasema, 'Yule Spekta Seif na Sajini Paolo na mtu mwingine mweusi wanakuja' uk.22. Kwa hivyo itikadi ya mtunzi huu ni kwamba binadamu wote wana uwezo sawa wa kiakili na watu weupe hawafai kufikiriwa kama wenye uwezo zaidi kuliko watu weusi. Tatu, kuna itikadi inayojengeka katika kazi za waandishi wengi wa kazi za kiupelelezi akiwemo Mtobwa na Musiba kwamba wapelelezi wa kibinafsi ni bora kuliko wapelelezi wa kidola. Kila mara hawa ndio wapelelezi wanaotatua mizozo inayowashinda wapelelezi wa polisi.

Kuna itikadi inayojengeka kuhusiana na uwezo wa polisi kama wachunguzi wakilinganishwa na wapelelezi wa kibinafsi. Katika riwaya zote tulizozichunguza, sifa ya udhaifu wao katika uchunguzi ina uzito zaidi. Itikadi bayana tunayoiona katika kazi za Abdulla, Mtobwa, Katalambulla na Musiba ni kuhusiana na namna idara ya polisi inavyoshindwa kukabiliana na wahalifu wa ndani na nje ya nchi na kwa sababu hii, wachunguzi wa polisi wanatafuta msaada wa wapelelezi wa kibinafsi. Waandishi hawa wanaashiria kuwa uchunguzi wa wapelelezi wa kibinafsi ni bora kuliko ule wa maofisa wa polisi. Katika kazi za Abdulla, Msa anawashangaza polisi kupitia uajabu wa upelelezi wake. Katika riwaya ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo*, Inspekta Wingo anapofika mwisho wa nguvu zake anatafuta msaada kwa mpelelezi mwingine, Bwana Tojo. Katika riwaya za Mtobwa, Joram Kiango ndiye huwasaidia polisi katika kuukomesha uhalifu. Vivyo hivyo, katika riwaya ya Musiba ya *Uchu*, Willy Gamba ni mpelelezi wa kibinafsi anayejulikana ndani ya nchi yake na nje kwa sababu ya uwezo wake. Hii ndio sababu mataifa ya PAM yanampa Willy Gamba jukumu la kupeleleza mauaji ya halaiki nchini Rwanda.Wapelelezi wa Musiba na Mtobwa wana umaarufu wa kutumia silaha mbali mbali, nguvu za kimwili na za kiakili katika kupambana na wahalifu kuliko wapelelezi wa Abdulla na Katalambulla. Mtindo wa Mtobwa na wa Musiba kwa kiasi kikubwa unashabihiana na mtindo wa riwaya za Kimarekani maarufu kama,

‘Hard-Boiled’ uliozuka wakati wa 1930. Ni riwaya zenye mtindo wa kuwasawiri wahusika wakuuu wakitumia mbinu kadhaa za upelelezi zikiwemo mbinu za kupigana kama vile kwa kutumia ala za kisasa. Zina vitendo vya kasi, taharuki kuu na hukitwa kwenye mandhari ya miji mikubwa.

Usomaji wa riwaya za Mtobwa na Musiba unadhihirisha itikadi nyingine ambayo ni kwamba uzalendo ndio nguvu murua ya kuushinda ubeberu na ukoloni mamboleo. Mpelelezi wa kazi za Mtobwa (Joram Kiango) na Willy Gamba katika kazi za Musiba, wanachunguza magenge ya Kimataifa yanayotumwa kuzua migogoro ya kisiasa katika maeneo ya Afrika Mashariki. Huku Willy akichunguza wachochezi wa mzozo wa Rwanda, Joram anapambana na wahalifu wanaopania kupindua serikali zinazokataa matakwa yao. Kwa kuwa masuala haya yanafumbata uhalisia wa kihistoria, utafiti huu unasisitiza kwamba kama riwaya dhati, nazo riwaya za kiupelelezi zina wajibu huo huo kando na kuburudisha.

Kwa kuwa tunajadili suala la utatu katika usawiri wa mhusika mkuu, yaani, mpelelezi, mhalifu na mhasiriwa, sehemu ijayo itadokeza machache kumhusu mhusika mhasiriwa. Tumejadili kuhusu mhusika mhalifu katika sehemu ya ubapa wa mhusika, kwa hivyo hatumrejelei chini ya utatu.

### 4.4.2 Usawiri wa wahusika Wahalifu

Kezilahabi (1975:37-41) anatathmini ufaafu na udhaifu wa riwaya ya kiupelelezi katika jamii na kugundua kwamba sifa moja hasi inanyohusishwa na riwaya hizi ni usawiri wa mhusika wa kiuhalifu. Anasema kwamba ikiwa mhusika wa kihalifu atasawiriwa kama mhusika mkuu, anaweza kuigwa na wasomaji na kuchochea upotoshaji wa maadili. Bila shaka mhakiki huyu alikuwa akirejelea uwezekano wa wasomaji kumuiga mhusika wa kiuhalifu kwani yeye ni kinyume cha mhusika mpelelezi kiwasifu. Hata hivyo, mtazamo wake ulibadilika baadaye kuhusu ubora wa riwaya za kiupelelezi. Akizungumza na mmoja wa wasimamizi wa utafiti huu (K.W.Wamitila), alimwambia kuwa aliposoma kitabu cha Earnest Mandel kiitwacho, ‘Delightful Murder; A Social History of the Crime Story’, ndipo alipooutambua kuwa riwaya ya aina hii pia huweza kuakisi jamii kama riwaya dhati.

Mhusika mhalifu huwakilisha uovu unaohusu ukiukaji wa sheria kupitia matendo ya mauaji, wizi, uharibifu wa mali na uvurugaji wa amani. Kwa mfano, katika riwaya za Abdulla, mhusika mhalifu hupokonya wengine urithi wao, huiba na hata kuua. Riwaya za Mtobwa humsawiri mhusika

mhalifu akipanga mauaji ya halaiki na kuharibu miundo msingi kama vile majumba huku Simbamwene akiwaonyesha wahusika wahalifu hao wakishiriki wizi wa benki.

Mhusika wa kihalifu huweza kusawirika si katika vitendo vyake tu bali katika mipango ya kihalifu aipangayo pia. Mipango hii inaweza kuwa ya kueneza propaganda au kufadhili makundi ya kihalifu kama tuonavyoona katika kazi za Musiba. Wahusika wahalifu katika kazi za Musiba huvuka mipaka kwani wanaonyeshwa wakivuruga amani hata nje ya nchi yao. Katika riwaya ya *Uchu* kwa mfano, JKS ni mhusika msaliti anayeshirikiana na wageni wa Kimagharibi kuchukua urais wa nchi yake kwa njia zisizo za kidemokrasia kando na kuhusika katika mzozo wa Rwanda. Mhusika Jean akiwa Ufaransa anamtumia JKS kuzidisha mgogoro wa Rwanda huku akimuahidi JKS kwamba angemsaidia kuuchukua urais wa nchi ya Tanzania.

Sifa ya kifomyula inayohusishwa na uhusika wa kihalifu ni kwamba kufikia mwishoni mwa hadithi, aghalabu mhalifu hushindwa na nguvu za kidola, vitendo vyake huwekwa wazi na adhabu kali hutolewa. Hii ndio sababu tumeonyesha katika sura ya pili, kuwa kuwepo kwa fomyula kadhaa katita utanzu huu, kunaakisi chimbuko lake katika fasihi simulizi. Kimura (1992:192) anasema kwamba ni katika miishio hii ya kifomyula ambapo riwaya za kiupelelezi hufanikiwa kufunza kuwa itikadi kwamba uovu haulipi.

Kuna mara chache ambapo mhusika mhalifu hushinda nguvu za kidola. Sifa ya mhalifu kushinda nguvu za kidola mwishoni mwa hadithi huwekwa wazi zaidi katika riwaya ya kiuhalifu ambapo aghalabu mhalifu hukwepa mitego yote aliyowekewa na polisi na kwa njia hii kuibuka kama mshindi na kielelezo kibaya kinachoweza kupotosha maadili. Hii ndio hali tuipatayo katika riwaya za kihalifu za John Kiriamiti kama vile *My life With A Criminal* na *My Life in Crime.* Hofu iliyotolewa na Kezilahabi (1975:37) basi inaweza kuthibitika zaidi katika utanzu wa riwaya ya kihalifu wala si katika riwaya ya kiupelelezi kama alivyosema kwa kuwa katika riwaya ya kiupelelezi mhalifu ni mhusika mshinde (Villain) ilhali katika riwaya ya kiuhalifu, mhalifu ni mshindi (Hero).

Kwa maoni yetu, mhusika wa kiuhalifu anaweza kupendwa na msomaji katika miktadha kadhaa; akidhihirisha sifa za kizalendo kama vile kupigana na maadui wa nchi yake ama kufanya uharibifu fulani kwa niaba ya taifa lake ama akitenda uhalifu wa aina yoyote kwa mhalifu mwingine kama kisasi au kama mkakati wa kuzuia uhalifu zaidi. Vile vile, anaweza kuwavutia wasomaji ikiwa

mhalifu huyo anamuua mhusika mwovu zaidi. Danyte (2011:18) anasema kwamba wasomaji wanaposhuhudia mhalifu akiteseka hususan kupitia kisasi, huburudika. Kwa misingi hii basi, Joram Kiango anaweza kuchukuliwa na baadhi ya wahakiki kama mharibifu kupitia baadhi ya matendo yake. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* anasafiri Afrika Kusini na kuharibu viwanda vya adui na kuwauawa askari kadhaa. Usawiri huu hutegemea mtazamo wa mwandishi au msomaji. Kwa hivyo, katika riwaya hii, kwa mtazamo wa makaburu Joram ni mhalifu lakini kwa mtazamo wa Watanzania na Waafrika kwa ujumla, Joram ni mzalendo kwa kuwa anatetea uhuru na msimamo wa taifa lake.

Mhusika mkuu wa kihalifu huwa na msaidizi wake ama kundi la wasaidizi kama anavyofanya mhusika mpelelezi. Mara nyingi mhalifu mkuu humtumia mhusika wa kike, asiye na ujanja mwingi kama wake. Kwa njia hii, msaidizi wa mhalifu hutegemea maelekezo anayopewa na mhalifu mkuu. Mara nyingine kwa kuwa msaidizi huyu wa mhalifu hana nguvu na ujanja kama wake, analazimishwa kutenda vitendo vya kukiuka sheria. Katika miktadha mingine, mpango wa uhalifu unapotimia, mhusika mshirika huyo wa kike hutupiliwa mbali, hutengwa na hata kuuawa mara nyingine. Katika riwaya ya *Kiu* kwa mfano, Idd anamtumia Bahati kuiba pesa za Mzee Mwinyi na wanapofanikiwa, Idd ananunua kipande cha ardhi na kujenga nyumba ya kifahari katika eneo la pwani na kuanza kumtenga Bahati huku akitafuta mpenzi mwingine. Katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa* (1972), Rashid anapanga namna ya kuziiba pesa kutoka kwa benki, lakini kwa kuwa yeye hafanyi kazi benkini, yeye ni tarishi kwingine, anafanya urafiki na msichana, Salima, anayefanya kazi ya ukarani katika banki ili amtumie kuiba pesa za benki. Salima anakubali kuzichukua kutoka kwa sefu ya benki na kumpa Rashid. Mradi huu unapokamilika, Rashid anamwacha Salima na kumtafuta mpenzi mwingine, Rehema. Rashid anadhihirisha tamaa kubwa ya maisha ya hali ya juu ilhali hana uwezo wa kifedha.

Wahusika wa kiuhalifu huchochewa na mambo kadhaa katika kutenda vitendo vyao vinavyoenda kinyume na kaida za kijamii. Baadhi ya vichocheo hivi ni tamaa ya utajiri, msukumo wa kulipiza kisasi, siasa kama vile mauaji yenye lengo la kuwaondoa wapinzani wa kisiasa au hata msukumo wa kujiokoa kutokana na hali inayohatarisha maisha. Svendsen (2010:26) anasema kwamba kuna baadhi ya wahalifu wanaoongozwa na itikadi maalum katika kutenda uhalifu hasa mauaji. Anatoa mifano ya wahalifu wa kihistoria walioongozwa na itikadi kama vile Adolf Hitler, Mao Tse Dong na wale wa hivi karibuni kama Osama Bin Laden. Anafafanua kwamba wahusika kama hawa huwa

na unyama mwingi unaowafanya kufurahia wanapotenda uovu. Kwao uovu ni wema. Utafiti wetu umebaini kuwa uhalifu unozingatia itikadi aghalabu huwa na nguvu nyingi na ndio husababisha maafa makubwa. Hii ni kwa sababu itikadi huwapa wahusika motisha inayoridhisha matamanio yao kama vile dini. Katika riwaya za Mtobwa kwa mfano, itikadi ya ubora wa rangi nyeupe unatumiwa na makaburu kuzishambulia nchi za msitari wa mbele[6] katika ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika. Afrika Kusini kwa mfano, inasawiriwa ikiikandamiza Tanzania kwa sababu ya kuunga mkono juhudi za uhuru wa Afrika Kusini, Namibia na Angola.

Ohly (1981:22) anatoa sababu nne zinazowapa wahusika wa kiuhalifu msukumo wa kutenda namna watendavyo ambazo ni; Kwanza ni hamu ya kujitajirisha kwa haraka ili kuifikia ndoto ya kimaisha ya kupendeza. Hali kama hii ndio tuionayo katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa* ambapo Rashid angetaka kuishi maisha ya viwango vya juu asivyoweza na kuamua kuiba pesa za benki. Pia katika riwaya ya *Mpelelezi Hodari na Genge la wahalifu*, wahalifu Rono, Dali na Mita wanajiingiza katika wizi wa kimabavu ili kuishi kama matajiri. Pili, kuongeza kiasi cha utajiri alicho nacho mhusika, kama inavyobainika katika riwaya ya *Ndoto ya Mwendawazimu* ya Eddie Ganzel. Sababu ya tatu ni msukumo wa kulipisha kisasi kama inavyobainika katika riwaya ya Katalambula ya *Simu ya Kifo* ambapo Agnes anaiua familia ya mzee Jacob ili kulipisha kisasi cha mauaji ya babake yaliyofanywa na Jacob. Msukumo wa nne anaoutambua Ohly, ni sababu za Kinyama (Sadism). Katika riwaya ya *Salamu kutoka Kuzimu*, mhalifu Proper anadhihirisha unyama kupitia mipango yake ya uovu ya kupanga mauaji ya marais wa Kiafrika wanaohudhuria kongamano mjini Arusha. Proper anafanya hivi kwa niaba ya Mataifa ya Kimagharibi ili ‘Afrika iwapigie magoti’. Ingawa mpango huu haukufaulu kwa kuwa ulisambaratishwa na mpelelezi Joram Kiango, Proper amewaua watu kadhaa wakiwemo rafiki na wasaidizi wa Joram Kiango kama vile, Waridi. Kuhusu unyama wa Proper, Joram anamwambia Proper:

> Dunia haijapata kumuona mwendawazimu kama wewe. Una roho chafu kuliko mnyama yeyote yule. Ni ajabu kwamba huna mkia. Unyama wako umewazidi Hitler na Mussolin. Umewazidi Idd Amin na Bokassa. Hata kaburu Voster na Smith hawakufikii.(Uk.120)

[6] Hizi ni nchi zilizoongoza juhudi za kuyakomboa mataifa ya Kusini mwa Afrika. Tanzania ilikuwa mojawapo wa nchi za msitari wa mbele

Kutokana na dondoo hili inadhihirika kwamba unyama ni kichocheo kikubwa cha kutenda uovu miongoni mwa wahalifu. Kwa hivyo, mawazo ya Ohly na Svendsen yanaakisi ukweli unaothibitika katika riwaya ya kiupelelezi ya *Salamu Kutoka Kuzimu*. Wahusika wa kiuhalifu katika riwaya za Abdulla pia wanajitokeza kama wanaoongozwa na unyama katika vitendo vyao. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* kwa mfano, Ali Makame analipa wema anaofanyiwa na Mwana wa Giningi kwa kumuibia mali yake aliyoachiwa na babake na kumuua baadaye ili arithi shamba lake. Kwa hivyo, tamaa ya mali inasababisha baadhi ya wahusika kuwa na unyama. Hata hivyo, wahalifu wanaopatikana katika riwaya za Abdulla wanaongozwa na itikadi mbili; Kwanza itikadi inayojikita katika mfumo wa ubepari unaowatajirisha watu wachache kwa kunyonya nguvu za watu wa kawaida wanaofanya kazi katika kampuni au mashamba makubwa makubwa. Ili kufidia dhuluma hizi za kiuchumi, baadhi ya wahusika wanajiingiza katika uhalifu. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi* kwa mfano, babake Mwana wa Giningi alifanya biashara ya magendo na kufanikiwa kupata utajiri mkubwa kwa kuwalaghai watu katika biashara hii. Aliweza kupata dhahabu nyingi aliyomwachia bintiye katika kisanduku kilichoibiwa. Kutokana na biashara hii, alinunua shamba kubwa ambalo pia alimrithisha bintiye. Ali Makame anaposhuhudia utajiri wa aina hii ilhali yeye ni maskini, anaamua kufanya uhalifu wa kumuua Mwana wa Giningi ili kusawazisha hali yake na ile ya ndugu yake.

Kwa kuchukulia itikadi kuwa uatajiri huja kwa dhuluma, wahusika wahalifu wanapata msukumo wa kuendeleza dhuluma dhidi ya wenzao. Huu ni uovu unaotokana na itikadi ya kibepari. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, mwandishi anakejeli mwonoulimwengu huu kwa kuwasawiri wahusika wanaoongozwa na itikadi hii kama wanaoshindwa, wenye ubwete na wanaokimbilia uhalifu kabla ya kujaribu mbinu nyinginezo za kuinua hali zao za kiuchumi. Dhuluma zao zinagunduliwa na kuadhibiwa mwishoni mwa hadithi. Katika riwaya hii, Twajuana Abdalla anamwambia Sikudhani Binti Abdalla:

> Hujui dunia inavyokwenda, dunia ndugu yangu inakwenda kwa hadaa na dhuluma. Tazama weye madhalimu na wajanja ndiwo wanaoendewa sawa na yao; watu waaminifu na wanyonge utawaona daima wako chini. Tukiyatazama hayo tunapata mafunzo ya kutufaa katika maisha yetu. Nayo ni kwamba, 'Utovu wa uaminifu ndio uongozi bora duniani, ndiwo unampeleka mtu mbele, ndiyo maendeleo yake. (uk.50)

Tunaweza kuona kutokana na fikira ya mhusika huyu kwamba, dhuluma ndiyo dira inayoongoza watu wanaooenekana wakiwa na maisha mazuri. Itikadi hii inawaaminisha wengi kuwa utovu wa nidhamu ndio uongozi bora. Jambo hili linatudhihirishia kwamba katika jamii ya Unguja, kumekuwa na udhalimu wa tabaka la juu kuwanyanyasa wanyonge kwa kiwango kinachowafanya wanyonge nao watamani kuwadhulumu wanyonge wenzao ili waweze kuishi kama mabwanyenye wawaonao miongoni mwao. Kwa kwamini hivi, mhusika Twajuana, anaamua kumnyima Amanullah mali aliyoachiwa na wazazi wake, anaitumia kununua nyumba katika eneo la kifahari la Vuga na kuondoka katika mtaa wa kimabanda wa Kwahani. Twajuana na dadake wanapohamia eneo hili bora, wanamtenga mtoto huyu Amanullah na kumtupilia mbali. Kwa kuitumia njia hii, wanabadili maisha yao kwa kupata nyumba nzuri katika eneo la watu wa tabaka la juu. Kwa hivyo, itikadi ya kibepari inakuwa msukumo wa kuendeleza uovu kando na kuwa chanzo cha uovu huo.

Itikadi ya pili inayohusishwa na uhalifu katika riwaya za Abdulla ni imani za kichawi. Kuna baadhi ya wahusika wahalifu wanaoamini kuwa uchawi una kani inayoweza kuwafaa kutenda uhalifu kwa urahisi ama wanatenda uhalifu na kusingizia kwamba kitendo hicho kilitendwa na wachawi ama kilifanyika ili kufanikisha shughuli za kiuchawi. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, Fundi Mangungu ni mhusika mchawi anayetembelewa na watu kadhaa ili awafae katika kutekeleza uhalifu. Mhusika mmoja anayeamini katika nguvu hizi ni Ali Makame kwani alitafuta usaidizi wa Fundi Mangungu ili kumtenganisha Mwana wa Giningi na bwanake, Vuai kisha baadaye amuue na kurithi mali yake. Kwa hivyo, Ali Makame anasaidiwa na nguvu za kiuchawi kufanikisha uhalifu wa kuua na kurithi mali isiyo yake. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, wahalifu wanamuua Bwana Ali Boman na kutupa kiwiliwili chake kwenye eneo la mzimu ili mwili ukipatikana baadaye, polisi waseme wachawi ndio waliofanya hivyo ili wavitumie viungo vya mwili huo katika uchawi. Kwa njia hii basi, uchawi unatumika kuwaficha wahalifu. Kama ushahidi wa Msa unavyoonyesha baadaye, Bwana Ali alikuwa ameualiwa na baadaye mwili wake ukabebwa na watatu hadi sehemu ya makaburini.

Wahusika wahalifu vile vile husawiriwa kama wasio na maarifa mengi mengi wakilinganishwa na mpelelezi au afisa wa polisi. Kwa sababu hii, wanafanya makosa madogo madogo yanayomfanya aanguke kwenye mitego ya polisi au kwa mpelelezi na kukamatwa au kuuawa. Udhaifu wao unjitokeza pia wakati wanapohojiwa na wapelelezi kwani wanaishia kujielekeza kwenye mitego ya kimantiki ya mpelelezi. Hii ni hali inayoonyesha uhalisia wa maisha ya kihalifu kwani kawaida,

wahalifu huingia katika mitego ya polisi. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* mwandishi anasema waziwazi kwamba mhusika Kasim, ambaye anaharibu mali ya babake na kumletea genge la majambazi nyumbani ili liibe pesa hizo, hana uelewa wa mambo yanayotolewa na Msa. Msimulizi anasema, 'Kasim ambaye alikuwa ni mzito wa kufahamu, hasa mzungusho wa Bwana Msa, alianza kukunja uso na kuhema.' (Uk.87). Kasim kama mhalifu anasawiriwa kama mhusika ambaye ana akili isiyoweza kufuata maelezo marefu yanayotolewa na Msa kuhusiana na uhalali wa watoto wa Hakimu Marjani. Udhaifu huu unamfanya asiulize maswali ili kufafanuliwa ni vipi anakosa urithi.

Sifa ya mwisho kuwahusu wahusika wa kihalifu ni kwamba kama kanuni, wahalifu husawiriwa kama watu wa tabaka la chini na mara nyingi kama watu wasio na umuhimu sana katika jamii yao. Kwa sababu hii, mhusika mhalifu anapotiwa mbaroni au kuuawa analeta kitulizo kwa wasomaji ambao wangetarajia kuona wema ukiushinda uovu na hali ya utulivu kurejea. Wahusika kama hao ni Ali Makame na Fundi Mangungu katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* Kasim na genge la wezi katika *Duniani Kuna Watu*, Vumilia na Rashid katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa*, Agnes katika *Simu ya Kifo,* JKS na Jean katika riwaya ya *Uchu* na Proper na washirika wake katika riwaya za Mtobwa. Wote, isipokuwa JKS, wamechorwa kama wa tabaka la chini na ubapa wao unahusu uvunjaji wa sheria na kuendeleza uovu wa aina ainati.

Kuhusu jinsia ya wahalifu, wahusika wa jinsia ya kiume ndio hutumika zaidi kama kanuni ya kimuundo wa riwaya hizi kuliko jinsia ya kike. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, ukweli huu unajitokeza isipokuwa katika riwaya ya *Simu ya Kifo* ambapo mhusika wa kike, Agnes ndiye mhalifu ambaye pia ndiye mhusika mkuu ingawa katika vitendo vyake anasaidiwa na mpenzi wake hasa katika kumuonyesha namna ya kutumia bastola na kemikali za aina aina hasa sumu inayotiwa kwenye sigara. Labda ujitokezaji wa wanaume kama wahusika wa kihalifu kwa wingi kumetokana na mtazamo wa jamii kwamba jinsia ya kike ina udhaifu wa kutoweza kutenda vitendo hatari kama wanaume. Rowlands (2001:15) anasema kwamba hali hii ya matumizi ya jinsia ya kiume katika usawiri wa wahusika wahalifu, inatokana na mtazamo wa kihistoria unaombagua mwanamke ambao huchukulia mwanaume kuwa na sifa pendwa za kuwa na urazini, mwenye ubabe wa kivitendo, mwenye utobinafsi na mwenye haki. Wakati huohuo, mtazamo huo wa kihistoria unamuonyesha mwanamke akiwakilisha kinyume cha sifa hizo kando na kumsawiri kama mtu anayestahili kuonyeshwa njia na kupitia ubabedume. Zaidi ya hili, Rowlands anasema usawiri huu

unatokana na kweli kwamba kutoka kitambo sheria imekuwa ikidumishwa na wanaume katika taasisi za polisi, mahakama na uwakili. Muundo wa jamii kwa misingi hii nao ukasababisha fani nyingi za kisanaa kuchukua mfumo wa ubabedume.

### 4.4.3 Usawiri wa Wahusika Wahasiriwa

Hawa ndio wahusika wanaohasiriwa na tendo linalofanywa na mhalifu au wahalifu. Mhusika mhasiriwa anaweza kuwa ameathiriwa moja kwa moja au akawa anaripoti kesi kwa niaba ya mtu wa akraba yake kama vile mhusika anayeripoti kupotea au kuuawa kwa mtu aliye karibu naye. Kwa kawaida wahusika wa aina hii huwa na unyonge fulani au kasoro fulani ya kijamii au kiuchumi inayowaweka katika hali hatari ya kudhulumiwa. Hali za kiunyonge zinazowaweka katika hali ya hatari ni kama vile umasikini, ukiwa au upweke. Pia kuna unyonge wa kimaumbile kama vile tofauti ya kijinsia ambapo jinsia yenye nguvu zaidi, aghalabu ya kiume, hudhulumu ile isiyo na nguvu. Matukio ya kiasilia kama vile kulemaa, magonjwa au kufiwa ni matendo yanayoweza kuchochea uhasiriwa.

Tusomapo kazi za Abdulla kama vile *Kisima cha Giningi* na *Duniani Kuna Watu*, tunaona hali mbalimbali za unyonge zinazomweka mhusika katika hali ya kuhasiriwa. Kwa mfano, Mwana wa Giningi hakuzaliwa katika eneo analoishi kwa kuwa babake alitoka naye kwa mwanamke aliyekuwa bibi wake zamani. Kwa hivyo, yeye ni mgeni katika eneo analoishi. Pili, babake alimlazimisha kuolewa na Vuai ambaye anamshuku kuwa ndiye aliyemuibia, kwa hivyo anaishi na mtu asiyempenda, tatu, anaishi na mjombake Ali Makame, mtu mwenye tamaa kubwa ya mali. Hali hizi za unyonge zinamweka katika hatari ya kudhulumiwa na Ali Makame kwa kumuibia mali yake na kumuua baadaye ili arithi shamba lake kubwa aliloachiwa na babake. Katika riwaya hii, basi tunaona kwamba hata utajiri ni hali inayoweza kumweka mhusika katika hali ya hatari ya kudhulumiwa na wahalifu. Motif kama hii pia inashuhudiwa katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, ambapo mhusika Hakimu Marjani anadhulumiwa kwa sababu ya utajiri wake. Mtoto wake Kasim anazoea kumuomba babake pesa za kuchezea kamari na kulewa na babake anapokataa kumpa pesa hizo siku moja, Kasim anamkaba koo na kumlazimisha kumpa. Siku nyingine anatafuta wezi ambao wanavamia jumba lake na kujaribu kuiba mali ingawa hawakufanikiwa. Kwa hivyo, utajiri wake miongoni mwa watu maskini wa kijiji chake unamweka katika hali ya kuwa mhasiriwa wa uhalifu.

Katika riwaya za Mtobwa tunaona hali ya uhasiriwa ukichukua mkondo wa kijinsia kwa kuwa wanaoumia zaidi ni wanawake. Baadhi ya wahusika wa kike wanapitia dhuluma za kunyanyaswa kingono, kupigwa na hata kuuawa mara nyingine. Katika riwaya ya *Salamu kutoka Kuzimu*, mhusika Neema Idd anadhulumiwa na mhalifu Proper, anayesakwa na polisi kwa maasi mengine. Proper anamlazimisha kushiriki mapenzi naye na anapomaliza anampa sumu. Neema Idd kwa hivyo anahasiriwa kwa sababu ya unyonge unaotokana na jinsia yake. Mhusika Salima katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa* ya Simbamwene analazimishwa na mpenzi wake, Rashid kuziiba pesa za benki ili ampe akatumie kujifurahisha na mradi huu unapotimia, Rashid anamtupilia mbali Salima ambaye anashikwa baadaye na polisi. Mhusika huyu pia anateswa kutokana na unyonge wa kijinsia.

Kuna wahasiriwa wanaodhulumika kwa sababu ya kisasi kitokanacho na ukosefu wa haki. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* Mzee Jacob aliidhulumu familia ya Agnes kwa kumuua baba na mamake Agnes ili achukue mali yao na pesa zilizoachwa benkini kwa ajili ya kutumiwa na Agnes. Agnes aliamua kulipisha kisasi kwa kuiua familia ya Mzee Jacob. Kwanza, anamuua Jacob kwa sumu iliyotiwa kwenye sigara, siku chache baadaye akamuua bintiye, Mary kwa kumpiga risasi na mwisho Agnes anamuua mamake Mary. Hawa wote ni wahasiriwa wa kisasi cha Agnes. Kisasi hiki nacho kinasukumwa na tukio la ukosefu wa haki kwa kuwa familia ya Agnes ilikuwa imedhulumiwa na Jacob. Katika muktadha huu, Jacob, mke wake na binti yake ni wahusika wahasiriwa wa kisasi cha Agnes, ikiwa ishara ya itikadi kwamba uhalifu haulipi. Katika kisa hiki pia udhaifu wa polisi unajitokeza kwa kutochukua hatua yoyote wakati Jacob alipowaua wazazi wa Agnes, wakati huo hivyo kuwafanya wanajamii kujichukulia sheria mikononi. Ukweli kuhusu udhaifu wa polisi unadhihirika kupitia kauli ya mpelelezi wa polisi, Inspekta Far Katy Wingo, 'Basi bwana Mkubwa, serikali ilijitahidi kufanya upelelezi wake, lakini haikufaulu' uk.100.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, inadhihirika pia kwamba mhasiriwa anaweza kujipata katika hali ya utatanishi ikiwa anajaribu kuzuia ushahidi kupatikana. Hali hii inajitokeza mno ikiwa kesi husika ni ya uhalifu wa mauaji ambapo mshukiwa wa mauaji anamuua aliyeshuhudia kitendo hicho. Hii ndio hatia iliyomkumba mhusika Mary katika riwaya hii. Alimuona Agnes akiziweka sigara zenye sumu katika kijaluba cha babake (baba Mary). Kwa hivyo, ili kumzuia asitoe siri hii, Agnes akaamua kumuua Mary ili asimripoti kwa polisi ama asije kuwa shahidi. Hii ndio hali anayojikuta Neema Idd pia katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*. Mhalifu Proper anapompata

na kumlazimisha kutoa siri azijuazo kumhusu mpelelezi Joram Kiango, anamuua ili Neema asimjulishe Joram kuchukua tahadhari zaidi.

Kuhusiana na riwaya zinazosawiri uhalifu katika kiwango cha kimataifa mhasiriwa pia huweza kuwa taifa au kundi la watu liishilo katika eneo fulani la kijiografia. Taifa hilo huathirika kwa sababu ya kuchukua mtazamo fulani kuhusiana na siasa au itikadi fulani ya kimataifa. Katika riwaya za Mtobwa na zile za Musiba kwa mfano, taifa la Tanzania linahasirika kwa sababu ya kuunga mkono siasa za ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika. Kutokana na hutua hii, taifa kama mhusika linapata uharibifu mkubwa.

Mwisho, mhusika mhasiriwa anaweza kujipata katika hali ya kuhasiriwa kutokana na kukosa umakinifu katika kazi zake au kutokana na tabia ya mapuuza ya mambo madogo madogo. Katika riwaya ya *Kwa Sababu ya Pesa,* Mzee Jumbe anakosa umakinifu kama meneja wa benki kwa kukosa kufunga sefu ya benki inayohifadhi pesa mara kadhaa. Kosa hili linamvutia karani wa benki, Salima, ambaye anaziiba pesa kutoka kwa sefu hilo. Salima anamwambia mpenzi wake Rashid, 'Mara nyingi huwa anasahau kulifunga kabati hilo la chuma ambalo linaficha fedha ambazo wewe na mimi tunazihitaji sana. Basi tegemeo letu liko hapo' uk.34. Kosa la meneja wa benki si kukosa umakinifu tu bali pia anamuomba karani kumsaidia kulifunga kabati hilo. Udhaifu huu wa meneja, Jumbe, wa kusahau kufunga sefu, unamfanya kuwa mhasiriwa kwani wizi unapotendeka anajutia makosa hayo. Kwa hivyo uhasiriwa wa mhusika unaweza kutokana na udhaifu wa hulka yake kama hii ya usahaulifu. Meneja Jumbe ana hulka ya kusahausahau na kwamini wafanyikazi wake zaidi, mambo yanayomchongea.

Katika sehemu hii, tumejadili motif ya utatu wa kihusika kwa kurejelea, mpelelezi, mhasiriwa na mhalifu kama wahusika wakuu wa kifomyula katika utanzu wa riwaya ya kiupelelezi. Tumeona pia kuwa kuna aina tatu za mhusika mpelelezi. Kwa kumalizia kuhusu matumizi ya uhusika wa kimakundi, tunaongeza aina nyingine ya utatu inayojitokeza tu katika riwaya za Abdulla. Aina hii ya utatu wa uhusika inaohusiana na dhamira zipatikanazo katika riwaya za Abdulla. Dhamira hizi ni urithi, dhuluma na uanaharamu. Wahusika wa kazi hizo basi wanaweza kuwekwa katika makundi matatu haya ya kidhamira. Katika *Kisima cha Giningi* kwa mfano, Mwana wa Giningi ni mwanaharamu aliyeletwa na babake kutoka mbali ili arithi mali ya babake. Ali Makame naye anaona kuwa kakake, Mzee Makame wa Makame hana mtoto halali kwa hivyo, anataka arithi mali hiyo yeye. Kwa sababu hii, anakuwa mhalifu kwa kumuua na kumwibia Mwana wa Giningi. Yeye

ni kiwakilishi cha mhusika dhalimu. Katika *Duniani Kuna Watu,* Kasim ni mwanaharamu aliyechukuliwa na kulelewa na Hakimu Marjani tangu utotoni mpaka akajiona kama mtoto asili wa mzee huyo. Anaendeleza dhuluma kwa kumlazimisha Hakimu kumpa pesa za vileo na siku moja akawaleta wezi nyumbani. Saleh analelewa kama Mwanaharamu pia kwa kuwa aliokotwa akiwa mchanga lakini kisadfa akachukuliwa na familia ya Hakimu. Kupitia upelelezi wa Msa, inabainika baadaye kwamba, warithi halali wa mali hiyo ni Saleh na Selume. Kwa hivyo, dhuluma inajitokeza kama njama ya kuwazuia warithi halali wasirithi mali kwa kuwa, awali wamekuwa wakidhaniwa kuwa 'wanaharamu'.

### 4.5 Uhusika Usaidizi

Veselska (2014:31) akihakiki kuhusu maendeleo ya uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Uingereza anaona kwamba kila shujaa huitaji msaidizi wake na kwa sababu hiyo, hata shujaa wa riwaya ya kiupelelezi pia hajasazwa. Kwa kuwa shujaa katika riwaya za kiupelelzi ni mpelelezi, basi hana budi kuwa na msaidizi wake. Veselska anaendelea kusema kwamba msaidizi wa mpelelezi ni mhusika anayetumika kuchimiza sifa zile bora za mpelelezi na kuzififiza sifa zake hasi. Katika riwaya tunazozichunguza, mtindo wa kutumia msaidizi wa mpelelezi unatumiwa zaidi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla.

Dhana ya uhusika usaidizi inaweza kuelezeka kuwili; yaani hutumika kurejelea umuhimu wa mhusika msaidizi katika kumsaidia msomaji kumuelewa mhusika mkuu ama mhusika anayemsaidia mhusika mkuu kutenda wajibu wake na kufanikisha dhamira ya mtunzi. Tunaitumia maana hii ya mwisho katika kufafanua nafasi ya uhusika usaidizi. Kinyume na tanzu nyingine za riwaya, utanzu wa riwaya za kiupelelezi humtumia mhusika msadizi kwa njia maalum. Kwa sababu hii, katika sehemu hii tunachambua umuhimu wa mhusika msaidizi katika riwaya za kiupelelezi. Katika riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi kwa mfano, mhusika msaidizi wa mpelelezi aghalabu ndiye msimulizi na hurekodi matendo ya mpelelezi huku akiwafafanulia wasomaji matendo ya mpelelezi. Kwa mfano, katika riwaya za Conan Doyle, Dkt.Watson ndiye msaidizi wa Sherlock Holmes na ndiye msimulizi wa hadithi zake nyingi. Katika kutekeleza jukumu la usaidizi, ndiye humpeleka msomaji kutalii matukio yote ya Holmes, akifafanua masuala kadhaa, hivyo kuyakidhi masilahi ya wasomaji.

Kama tulivyoonyesha katika sura ya pili, watunzi wengi wa Kimagharibi waliuendeleza mtindo huu wa kwandamanisha mpelelezi na msaidizi wake akiwa na jukumu maalum. Katika riwaya ya

kiupelelezi ya Kiswahili, Mohamed Said Abdulla, ndiye aliyezingatia mtindo huu kwa kuwa katika kazi zake nyingi anamtumia Najum kama msaidizi wa Msa. Najum kwa kiasi fulani ana sifa kama za Dkt.Watson. Kwanza kama Watson, Najum ana kiwango cha chini cha maarifa akilinganishwa na mpelelezi. Kwa sababu hii, anamuuliza mpelelezi maswali ili aelewe na kwa njia hii anasaidia kumuelekeza msomaji. Anapojibiwa maswali yake na mpelelezi, nao wasomaji wanakata kiu cha taharuki kwani wao pia wangependa kuuliza maswali kama hayo. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, baada ya Msa kuwaeleza waliohudhuria namna maisha ya Hakimu Marjani yalivyojawa na uajabu, Najum anauliza swali ambalo pia linawajibia wasomaji usumbufu wa swali hilo, ‘Na sijui kwa nini Bwana Hakimu akamuoa Bi. Mariam Mkembe kwa jina la Abdulla Salum?’ (uk 116). Ujibiwaji wa swali hili unawasaidia wahusika wengine akiwemo mkuu wa polisi, Inspekta Seif, kuielewa hadithi kwa upesi. Msa anaeleza hivi:

> Ivo hujui Najum? Hujui na nimekuambieni sasa ivi hapa kwamba marehemu huyu alikuwa kigeugeu, alikuwa mtu wa vilinge, alikuwa hataki hata yeye mwenyewe kujijua kuwa yeye ndiye yeye.( Uk.116)

Maelezo ya Msa baadaye yalifichua kwamba kulikuwa na sababu nyingine ya Hakimu Marjani kuoa kwa kutumia jina lingine, kwamba hakutaka mke wa kwanza ambaye hakuwa na mtoto, aijue siri hiyo. Kwa hivyo alioa kisiri kwa kuwa alikuwa na hamu ya kupata mtoto wake mwenyewe, ambaye angemrithi. Uhusika usaidizi huu wa Najum katika dondoo hilo hapo juu pia unatuashiria wasifu wa Hakimu kama mtu msiri na kigeugeu. Kwa kumsawiriwa Najum kama mtu mwenye maarifa kidogo kuliko mpelelezi, mwandishi anaboresha usawiri wa mhusika mpelelezi kiulinganishi, yaani anapodhihirisha udhaifu wake, anautokeza zaidi uajabu wa Msa. Kwa mfano, katika *Duniani Kuna Watu*, Msa anapomuonyesha Najum picha za watoto wa Hakimu kwenye gazeti ili atambue tofouti iliyopo, Najum anashindwa kutambua tofouti yoyote. Najum anasema, ‘Mimi sioni jambo lolote la kumshangaza mtu katika picha hizi tatu’. (uk.51). Udhaifu huu unamshangaza Msa kwa kuwa Msa anatarajia Najum awe na umakinifu zaidi kufuatia tajiriba ya miaka mingi ya kukaa pamoja na Msa.

Kando na kuzichimuza sifa za mpelelezi, Najum anamfaa Msa kwa njia nyinginezo ingawa anakosa uangalifu hapa na pale. Anamshauri Msa kufuata mtazamo mwingine katika uchunguzi wake. Kwa mfano, kuhusu kutumia picha za magazeti katika kuamua ni yupi mtoto halali wa Hakimu, Najum anamkumbusha Msa kuhusu elimu ya ‘Genetics’. Anamshauri kwamba kulingana

na somo la ‘Genetics’, mtoto anaweza kufanana na babu yake badala ya baba yake. Kwa sababu hiyo, Kasim ingawa hafanani na Hakimu Marjani anaweza kuwa anafanana na babu yake. Mchango wa Najum katika muktadha huu unapanua fikira ya Msa kuhusu uhalali wa watoto wa Hakimu Marjani.

Mwisho mhusika msaidizi wa mpelelezi anaboresha viwango vya taharuki katika msuko wa hadithi ya riwaya ya kiupelelezi. Taharuki ni kipengele cha kimuundo katika utanzu huu na kupitia maswali anayouliza, kabla ya kujibiwa na Msa, hamu ya kujibiwa inajengeka miongoni mwa wasomaji. Kwa kuuliza maswali haya, Najum anazidisha uajabu wa mpelelezi kwani anamsawiri kama tegemeo kuu lake na wahusika wengine. Kwa mfano, anapompata Msa akilikodolea macho gazeti lenye picha za watoto wa Hakimu Marjani, anauliza, ‘ Kwani umeona nini katika gazeti hilo Bwana Msa?’ Taharuki inayowapata wasomaji inahusu ni nini kipya kinachoonekana katika picha hizo ambacho wengine hawakioni. Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* Msa anapopata barua ya mwaliko kutoka kwa Inspekta Seif, Najum anamkumbusha Msa kwamba wana safari siku ya jumatano. Kutajwa kwa safari ya kuenda kumsaidia Seif katika uchunguzi kunazua taharuki si kuhusiana na safari na kinachochunguzwa pekee bali pia taharuki kuhusu ukumbusho wa kesi ya *Mzimu wa Watu Kale* ambayo Najum na Msa walikuwa wamechunguza awali.

Katika baadhi ya riwaya ambapo mpelelezi hana msaidizi, basi mpelelezi huyo anaandamwa na wanawake warembo na jasiri ambao humfaa wakati anapoingia katika hatari. Baadhi ya wanawake hawa wana sifa za kishujaa kama vile ujasiri na uwekaji siri, na ikibidi hudhihirisha matumizi ya nguvu za mwili katika kupigana. Katika utanzu wa riwaya ya kihalifu na ya kiupelelzi, wahusika kama hao hujulikana kama *Femme Fatale.*

### 4.5.1 Mhusika Msaidizi wa Kike

Hawa ndio wahusika wanaomuokoa mhusika mpelelezi anapojipata mikononi mwa mhalifu kwa kuwa aghalabu ni wapenzi wake na wanazijua mbinu zake. Danyte (2011:20) anasema kwamba wahusika wa kike hawakutumiwa katika riwaya za kiupelelezi hadi kufikia miaka ya 1980 na kwamba katika riwaya chache walimojitokeza walipewa nafasi finyu kama vile kuwa wahasiriwa ama wapenzi wa mpelelezi tu. Hii ndio sababu hatuwaoni wahusika wa kike wakijitokeza kuchukua nafasi muhimu katika kazi za awali za kiupelelezi katika Kiswahili kama vile zile za Abdulla. Wahusika kama hawa huwa na ujasiri unaowawezesha kuwasaidia wapelelezi katika kazi

zao ama kuwaokoa wanapotekwa nyara na wahalifu. Tunawapata katika kazi za Mtobwa, Simbamwene na Musiba. Danyte anatuambia kwamba mhusika wa aina hii (Femme Fatale) aliibuka huko Ufaransa wakati wa mwamko wa Ufeministi. Baadhi ya sifa za wahusika hawa ni;

(i)Wana urembo wa kupindukia na hamu kubwa ya kuhusiana kimapenzi, inayokiuka tamaduni zilizozoeleka.

(ii) Hawafuati kaida nyingi zinazobainisha wasifu bia wa wanawake. Kwa mfano, wao hudhihirisha bayana kuwa hawako tayari kuongozwa na wanaume.

(iii) Kuwa na uhusiano nao huweza kuleta maafa aidha kwa mpelelezi ama kwao wenyewe.

(iv) Wana ubabedume uanawazuia kuonyesha hisia za kilio, furaha, uchungu na nyinginezo kwa kuwa hisia zao zimethibitiwa.

(v) Huwa tayari kutumia nguvu kupigana ikibidi ili kufikia malengo yao.

(vi) Huwa hawana hamu yoyote ya kuwa bibi au mama wa mtu-Hawako tayari kuchukua majukumu ya umama wala kufungwa na familia, miongoni mwa sifa nyinginezo.

Katika riwaya za Mtobwa, wanawake wanaoandamana na mpelelezi Joram Kiango, wanadhihirisha baadhi ya sifa zilizobainishwa na Danyte. Baadhi ya wahusika hao ni Neema, Nuru na Waridi. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* Nuru ndiye anayemuokoa Joram mara kadhaa akitumia silaha kama vile bastola. Joram Kiango anapofumaniwa akiharibu mitambo ya adui huko Afrika Kusini, Nuru anafika wakati Joram akihitaji msaada zaidi. Msimulizi anaeleza hali hii hivi, “Bastola ilikuwa imara mikononi mwa Nuru, macho yake yasiyo na mzaha yakitangaza shari, ‘Pokea chako muuaji mkubwa’, Nuru alinong’ona akifyatua bastola”. (Uk.159). Joram naye anatambua umuhimu wa Nuru kwa kumuokoa mara nyingi. Joram anataja baadhi ya sifa zilizodokezwa na Danyte za *Femme Fatale* kama vile ujasiri na urembo wa kupindukia. Msimulizi anasema:

> Uzuri wa Nuru haukustahili kuharibiwa na kaburu yeyote katili. Ushujaa wake ulikuwa nguzo ambayo Joram alitegemea sana. Yote aliyokuwa ameyatenda, hekima na juhudi za Nuru zilikuwa zimemsaidia. Mungu amsaidie arudi salama. Joram alimuombea.

Mhusika wa kike mwenye sifa za *Femme Fatale* tunamwona pia katika riwaya ya Musiba ya *Uchu* (2000). Katika riwaya hii, mwanamke Bibiane anashirikiana na Mfaransa, Jean kusambaratisha juhudi za kutafuta suluhu la mgogoro wa kisiasa wa Rwanda. Huyu ndiye mhusika wa kike anayechukua nafasi kubwa katika riwaya hii. Kwa mfano, anatumiwa pesa na Jean kutoka Ufaransa ili azitumie kulipa genge la kupambana na mpelelezi Willy Gamba. Kama tulivyoonyesha katika kanuni za wahusika wa kike wa utanzu huu, wanakuwa na ushujaa, ubabedume na hushiriki katika mapenzi na yule wanayemsaidia. Bibiane kama msaidizi wa Jean anakuwa mpenzi wake kila mara Jean anaposafiri nchini Rwanda kutoka Ufaransa kando na kuwa mhusika wa kuogopwa kutokana na ujasiri wake. Katika riwaya ya *njama*, mhusika wa kike, Veronika Amadu anawasaidia Willy Gamba na wapelelezi wenzake kupambana na majasusi wa makaburu ili kukomboa silaha zilizokuwa zimeibiwa bandarini. Ubabe wa Veronika na umaarufu wake umetokana na mafunzo makali aliyopokea katika nchi mbalimbali. Kumhusu Veronika, Willy Gamba anasema:

> Anajulikana kuwa msichana mwandishi jasiri sana, amewahi kusafiri na majeshi ya kupigania uhuru wa Sahara Magharibi dhidi ya majeshi ya Morocco…Mwandishi huyu alilazimika kwenda Japan kujifunza namna ya kujikinga kwa mikono. Hivyo, mwandishi huyu, amehitimu katika judo na karate na kupata mkanda mweusi. Ingawa anauawa katika mapambano hayo, anadhihirisha ushujaa mkubwa. Katika mazishi yake, vyama vya upigania uhuru vinawapeleka wajumbe kuhudhuria mazishi hayo. (uk.57).

Kutokana na nukuu hili, tunaona kuwa kutokana na ushujaa wa Veronika, anashirikishwa katika majeshi kama mwandishi wa habari ili kuwasilisha kwa shirika lake habari alizozishuhudia mwenyewe. Pia tunaona kuwa amejifunza mbinu za upiganaji za karate na judo nah ii ndio sababu anawasaidia Willy Gamba na Sherriff kupigana na makaburu vikali.

Inabainika pia kwamba, wahusika wa kike wanaweza kutumika kama wasaidizi wa mhalifu. Sifa maarufu inayojitokeza kuhusiana na msaidizi wa mhalifu ni kuwa siri zitumiwazo na mhalifu zinapotoka nje, msaidizi huyo huuawa. Jean anapogundua kwamba Bibiane ametagusana na mpelelezi Willy Gamba katika kazi yake, anaamua kutafuta wauaji wa kulipwa kummaliza, lakini kisadfa anaokolewa na Willy Gamba. Kwa hivyo, katika utanzu wa riwaya za kiupelelezi, wahalifu wanaposhindwa kumteka au kumuua mpelelezi wanamteka msaidizi wake ili afichue siri. Vilevile, wapelelezi nao wanamteka msaidizi au mwandani wa mhalifu kama mkakati wa kulifikia lengo

lao la kumteka au kumwangamiza mhalifu. Hivi ndivyo Willy anavyofanya kwa kumuokoa Bibiane ili amshawishi kutoa siri za Jean na washirika wake wanaochochea mzozo wa Rwanda. Kando na kulazimishwa kutoa siri, mhusika wa kike ambaye ni msaidizi wa mpelelezi hupitia dhuluma nyinginezo kama vile ubakaji au/na mauaji. Kwa mfano, Neema Idd aliyekuwa katibu wa Joram anabakwa na baadaye kuuawa na mhalifu Proper, Waridi naye anauawa kwa kuwa mpenzi wa mpelelezi Joram, Nuru pia analazimishwa na Proper kuvua nguo kabla ya kuuawa lakini wakati huo huo anaokolewa na Joram.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, mhusika Agnes ni mhusika wa kike mwenye ujasiri na ushujaa wa kutumia silaha mbali mbali kama vile bastola na sumu katika ulipishaji wa kisasi. Ana sifa tulizozitaja hapo juu kuhusiana na *Femme fatale* za ujasiri na ushujaa. Kwa sababu ya ushujaa wake, anamteka mpelelezi Far Katy Wingo na kumuamuru kuweka mikono juu na kumwekea kikombe kwenye kila kiganja cha mkono wake. Anatishwa kwamba akiangusha hata kikombe kimoja angepigwa risasi. Zaidi ya ujasiri wake, ana ubabedume unaodhihirika katika lugha aitumiayo kumdhihaki mpelelezi, Far Katy Wingo. Danyte (2011) anaeleza kwamba sifa moja ionyeshayo ukali na ukatili wa wahusika hawa wa kike ni matumizi yao ya lugha kama ya wanaume iliyojaa kejeli, ukali wa toni na ujanja wakati wanapozungumza na adui zao. Katika riwaya hii, Agnes anatumia lugha yenye vitisho, matusi na kejeli kwa Wingo hivi:

> Haya bwana, leo ndio utauelewa upumbavu wako vizuri. Leo utajuta ni kwa nini umezaliwa, wewe mbwa. Utaona leo, utalia, utagumia, utanitambua kuku wewe. Inspekta nitapenda kujua, marehemu Jacob alikuwa baba yako? 'Hapana',
> Alikuwa mjomba wako? 'Hapana'. Labda tuseme alikuwa mkeo? 'Hapana'. Sasa nini kinakusumbua kukazana kumfanyia upelelezi? Mwehu we!
> (Uk.93).

Baada ya mateso mengi mpelelezi wa kibinafsi, Bwana Tojo anakuja na kumuokoa Inspekta Wingo na kumlazimisha Agnes kukiri kuwa ndiye amekuwa akiwauawa watu wa familia ya Mzee Jacob kwa kisasi. Anapokiri namna familia yake ilivyoangamizwa na Mzee Jacob, suala la huruma linaingizwa na kuzuia mkondo wa kisheria kufuatwa. Inspekta Wingo anaamua kumsamehe Agnes kutokana na kuelewa kwamba polisi ndio walioshindwa kuzuia dhuluma za Mzee Jacob mwanzo. Katika riwaya hii, ni wazi kwamba, dhuluma za kihistoria ni kichocheo kikubwa cha ulipishaji kisasi kando na kuwa dhihirisho la msemo, 'Haki haizami.'

## 4.6 Ulinganisho wa Kihusika katika riwaya Teule

Wahusika wakuu tunaokumbana nao katika riwaya teule wanafanana na kutofautiana kwa njia kadhaa. Wahusika wapelelezi katika kazi za Ben Mtobwa na Elvis Musiba, wanafanana kuhusiana na namna wanavyopambana na wahalifu. Wao wanatumia silaha kama vile bunduki na mabomu pamoja na kuendesha vyombo mbalimbali vya usafiri kama ndege, magari miongoni mwa vifaa vinginevyo. Hii ni kinyume na mpelelezi apatikaye katika riwaya za Mohammed Said Abdulla, Msa, ambaye hutumia urazini na mantiki katika kusuluhisha migogoro. Kufuatia usambamba huu, ni wazi kwamba Abdulla ameathiriwa na mwandishi wa Uingereza, Conan Doyle, huku Musiba na Mtobwa nao wakizingatia zaidi mtindo wa Kimarekani wa ‘Hard-boiled’ ambapo mbinu za upiganaji kwa silaha hatari na mtindo wa kifilamu hutumika katika uandishi wa riwaya za kiupelelezi.

Wapelelezi, Bwana Msa katika kazi za Abdulla, Willy Gamba katika kazi za Musiba na Far Katy Wingo katika *Simu ya Kifo* wanashindwa kuzuia ufanyikaji wa kitendo cha uhalifu, wakijitahidi tu kumshika mhalifu baada ya uhalifu huo kufanyika. Wingo kwa mfano anachunguza mauaji ya Mzee Jacob na kabla hajamaliza mauaji mengine yanafanyika. Mwishowe, anashindwa kabisa kumpata muuaji. Mpelelezi Joram Kiango katika baadhi ya kazi za Mtobwa anazuia utekelezaji wa mauji kinyume na wapelelezi hawa wengine. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* anazuia mauji ya marais wengi kwa sumu ambayo Proper alikuwa anataka kuwaua kwayo.

Riwaya za Mtobwa na Musiba zinachunguza uhalifu katika viwango vya kimataifa na kwa sababu hii, hizi ni riwaya za kijasusi. Wahusika wapelelezi huwafuata wahalifu, nje ya nchi na kuzuru miji kadhaa wakiwasaka kwa niaba ya serikali zao au kwa niaba ya mashirika ya kimataifa. Kwa mfano, katika riwaya za Musiba kama vile *Uchu*, Willy Gamba anatumwa na PAM kuchunguza mzozo wa Rwanda na katika *Njama*, Willy Gamba anapeleleza wizi wa silaha bandarini, zilizokuwa za wapiganiaji uhuru Afrika Kusini. Anaisaidia serikali ya nchi yake na OAU kupigana na njama za makaburu za kuchelewesha uhuru katika mataifa ya Kusini mwa Afrika. Kinyume chake, mhusika Msa, katika riwaya za Abdulla, anachunguza masuala ya ndani ya nchi kama vile mizozo ya kifamilia, urithi na mauaji katika kiwango kidogo. Sawa na Abdulla, mhusika mpelelezi katika riwaya ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo,* anajikita katika uchunguzi wa uhalifu wa ndani ya nchi hususan mauaji ya kifamilia. Hata hivyo, mpelelezi wa riwaya ya *Simu ya Kifo*, Far Katy

Wingo, si mpelelezi wa kibinafi bali ni afisa wa polisi. Yeye pia anashindwa katika kuwatia mbaroni wahalifu, kinyume na wapelelezi wa kibinafsi wa kazi za Mtobwa, Musiba na Abdulla.

Wahusika wapelelezi katika riwaya za Mtobwa na Musiba ni wataalam walioemilishwa kupitia kupitia taasisi za mafunzo rasmi kuhusu upelelezi lakini mpelelezi, Msa, katika kazi za Abdulla hajapitia mafunzo hayo. Katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* kwa mfano, inadhihirika kwamba, Joram Kiango amewahi kufundishwa kuhusu upelelezi nchini Marekani na kurejea baadaye nchini Tanzania ambako alianzisha upelelezi wa kibinafsi. Katika riwaya ya *Njama*, imedhihirishwa kwamba Willy Gamba naye alipata mafunzo yake kutoka nchi kadhaa: China, Japan, Urusi, Marekani, Uingereza na Cuba. Alipokuwa huko Japan, alifunzwa mitindo ya Kininja na kung-Fu. Katika *Njama*, Sherriff akisaka habari za Gamba kwenye kompyuta, anaripoti kwamba kompyuta ilimwonyesha kuwa:

> Willy Gamba amepata mafunzo katika nchi mbalimbali kama Uingereza, Cuba,Urusi, Marekani, China na Japan. Kutokana na mafunzo haya alionekana mtu hatari katika kutumia aina yoyote ya silaha. Vilevile, anajua Karate na Kung-fu ya hali ya juu kwani akiwa Japan, aliwahi kushindana na Inoki na kutoka sare naye…Zaidi ya haya, amehitimu mafunzo ya kikomandoo. Kompyuta ilionyesha kuwa ameifanyia 'OAU' kazi nzuri sana hasa kuhusiana na ukombozi wa Afrika Kusini. (Uk.56)

## 4.7 Hitimisho

> Sura hii imeshughulika na suala la uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili kwa kuchunguza aina za wahusika na mbinu mbalimbali zitumiwazo kuwasawiri wahusika. Mbinu hizo ni kama vile matendo na usemi wa wahusika. Mihimili ya nadharia ya umitindo, utanzu na naratolojia imetumika. Tumezingatia zaidi mbinu za usawiri wa wahusika za Rimmon-Kenan (2002) pamoja na maoni ya Forster (1986). Imebainika kwamba kigezo cha lugha za wahusika ni muhimu katika kufichua wasifu wao na wasifu wa wasemewa. Sifa maalum za wahusika zibainishao utanzu huu ni kama vile mgao wa wahusika katika makundi matatu wa ambapo utanzu huu, husawiri wahusika wakuu wa aina tatu. Hawa ni mhusika mpelelezi, mhusika mshukiwa na mhusika mhasiriwa. Kumhusu mpelelezi, pia tumeona sifa ya utatu unaohusishwa na kuwepo kwa mpelelezi wa kibinafsi, msaidizi wa mpelelezi wa kibinafsi na mpelelezi wa polisi.

Imebainika kwamba baadhi ya riwaya tunazohakiki zina wapelelezi wa aina moja huku nyingine zikiwa na wapelelezi wa aina mbili. Riwaya za Abdulla, Mtobwa na Katalambulla zina mpelelezi

wa kibinafsi na mpelelezi wa polisi. Aghalabu polisi wanashindwa kuwatia mbaroni wahalifu sugu na wanapata usaidizi kutoka kwa wapelelezi wa kibinafsi. Riwaya zilizo na mpelelezi wa aina moja, ambaye aghalabu ni wa polisi ni zile za Simbamwene na Levi. Katika kazi hizi, polisi ndio hupambana na wahalifu na kuwafikisha mahakani. Tumeona kuwa wahusika wapelelezi wa riwaya za Mtobwa na Musiba, aghalabu huvuka mipaka katika upelelezi wao kwani husafiri katika mataifa jirani kuwaandama wahalifu huko. Yaani panapotokea wahalifu wa kimataifa, pia wapelelezi hushiriki katika ngazi ya kimataifa huku wakitagusana na wahusika wenye asili tofouti na wa kutoka mabara mbalimbali.

Kuna tofouti wazi baina ya wahusika wapelelezi wa Abdulla kwa upande mmoja na wale wa Mtobwa na Musiba kwa upande mwingine katika mbinu zao za kiutendaji. Mpelelezi wa kazi za Abdulla, Msa, anadhihirisha matumizi ya urazini na mantiki katika upelelezi wake huku mpelelezi wa kazi za Mtobwa, Joram Kiango, akidhihirisha matumizi ya silaha za kisasa, uwezo wa kupigana kwa viungo vya mwili na matumizi ya kemikali za aina aina kama vile sumu. Utafiti huu umegundua kuwa tofouti hii imeletwa na mabadiliko ya kiteknolojia katika vipindi vya kihistoria ambavyo waandishi hawa walimoandikia.

Imebainika kuwa kuna mtindo wa kutumia wahusika wale wale katika riwaya za mtunzi mmoja. Sifa hii ya riwaya ya kiupelelezi inaonekana katika kazi za Abdulla na Mtobwa. Katika riwaya za Abdulla, wahusika Msa, Najum na Spekta Seif ndio wahusika wakuu katika takribani riwaya zote tofauti ikijitokeza katika wahusika wajenzi tu. Katika riwaya za Mtobwa, wahusika Joram Kiango, Proper na Inspekta Kombora ndio wametumika katika riwaya zake nyingi.

## SURA YA TANO

## MSUKO KATIKA RIWAYA ZA KIUPELELEZI ZA KISWAHILI

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tunachunguza namna mbinu mbalimbali za kimtindo zinavyochangia katika ujenzi wa msuko wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Kando na kuzichunguza mbinu za kimtindo zinazojenga mtindo, sura hii pia inachunguza mbinu zitumiwazo kuchelewesha kilele cha msuko. Msuko ni mfuatano wa matukio ya hadithi kiusababishi (Wamitila, 2003:142). Forster (1986:86) amefanya juhudi za kutofautisha msuko na hadithi akieleza kwamba, hadithi ni mfuatano wa matukio kiwakati huku msuko ukiwa mfuatano wa matukio kiusababishi. Kwa hivyo, msuko ni jinsi tukio moja linavyosababisha utokeaji wa tukio lingine. Forster anatumia kielelezo kifuatacho kuiweka tofauti baina ya dhana hizi wazi:

**Hadithi**: Mfalme alifariki na kisha malkia akafariki.

**Msuko**: Mfalme alifariki na kisha malkia akafariki kutokana na mshtuko wa kufiwa.

Kulingana na maelezo ya Forster, msuko na hadithi huhusu mpangilio wa matukio kiwakati lakini kuhusiana na msuko, dhana ya usababishi inachukua uzito zaidi kuliko mpangilio wa visa. Katika msuko, msisitizo huwa kwenye swali la ‘kwani nini.’ Wanaurasimu wa Kirusi walizitumia dhana ‘*syuzhet*’ na ‘*fabula*’ kurejelea msuko na hadithi mtawalia ingawa walichukulia kwamba fabula ni hadithi yenye miishio ya kimaadili. Huku kukiwa na makubaliano kwamba muundo wa hadithi huwa na fabula na syuzhet, hakuna makubaliano kuhusu ni kipengele kipi muhimu zaidi kuliko kingine. Baadhi ya wanaurasimu waliamini kwamba fabula ilikuwa na hadhi ya chini ikilinganishwa na syuzhet, fabula ikiwa malighafi ambayo hufanywa kuwa sanaa kupitia syuzhet. Todorov (1977:48) anasema kuwa msuko hupo lakini si muhimu kushinda hadithi yenyewe. Foster naye anatumia msamiati ‘*sujet*’ kurejelea dhana ya Wanaurasimu ya syuzhet. Akizungumzia viwango vya sujet na fabula, pia anakubaliana na maoni ya wanaurasimu kwa kusema kuwa fabula ina hadhi ya chini ikilinganishwa na syuzhet. Anasisitiza kwamba syuzhet (msuko) ndio huonyesha mahusiano ya kiusababishi baina ya vitushi.

Baadhi ya wahakiki waliojitokeza katika karne ya ishirini waliyasaili mawazo ya wanaurasimu na kuonyesha baadhi ya kasoro zake. Brooks (1992) kwa mfano, katika *Reading for the Plot* anachukulia kwamba msuko ni elementi changamano inayojengwa na fabula na Sujet, yaani kwake, msuko ni mpangilio wa matukio pamoja na hadithi yenyewe. Kwa hivyo, msuko ni matokeo ya mtagusano baina ya sujet na fabula. Mwanaumuundo-baadaye Jacques Derrida anakosoa fasihi za Kimagharibi kwa kuchukulia kuwa kila wakati sujet ni muhimu zaidi ya fabula. Msisitizo wake ni kwamba hadithi (fabula) hubeba maana kwa kina kama ulivyo msuko

Hata hivyo suala la msuko lina historia ndefu katika fasihi kwa kuwa liliibuliwa mara ya kwanza na Aristotle katika maelezo yake kuhusu muundo wa tanzia. Kulingana na Aristotle tamthilia ilipaswa kuwa na sehemu sita ambazo ni msuko, wahusika, uteuzi maalum wa maneno, fikira, vituko na nyimbo. Anaeleza kwamba kati ya vipengele hivi, kilicho muhimu zaidi ni msuko kwa kuwa tanzia inahusu mpangilio wa matukio wala si mpangilio wa wahusika. Kwake, tanzia haiwezi kukamilika bila vitendo

Kuhusu ujenzi wa msuko, Aristotle anaelekeza kwamba sharti kuwe na sehemu tatu kuu; mwanzo, kati na mwisho. Anaeleza kwamba msuko uliojengwa vizuri unapaswa kuwa na urefu utakaoruhusu mabadiliko mbalimbali kama vile yanayohusu kubadilika kutoka kwa hali ya huzuni hadi ya furaha. Ingawa Aristotle alizungumzia msuko katika muundo wa tamthilia, baadhi ya sifa za kimsuko kama vile urefu na usababishi wa matukio zinaweza kuchunguzwa pia katika tanzu nyinginezo za fasihi kama vile riwaya.

Kando na Foster na Aristotle, suala la msuko pia limeangaziwa na wahakiki wengine wengi. Kwa mfano, Freitag, akinukuliwa na Wamitila (2003:78) anafafanua muundo wa msuko na kusisitiza kwamba msuko wa tamthilia unafaa kwanza kwa ufafanuzi ambapo mtazamaji au msomaji anafaa kuelezwa hali iliyopo na kutangulizwa kwa wahusika. Hatua ya pili ni mkweo wa tendo ambalo huelekea kwenye tato, kisha kwenye upeo. Baada ya upeo kunakuwa na mgeuko na kisha mshuko wa tendo ambapo tukio la kuhuzunisha hutokea. Katika riwaya ya kiupelelezi, sehemu ya ufafanuzi kwa mfano, huhusu kutajwa kwa uhalifu, hususan mauaji na kutangulizwa kwa mpelelezi, msaidizi wake au afisa wa polisi anayechunguza uhalifu huo. Aghalabu sehemu hii ya ufafanuzi huhusu kupatikana kwa mwili au jumba ambako uhalifu umetendekea. Sehemu ya mkweo wa tendo nayo inaweza kuhusisha hatua za kumsaka mhalifu huku upeo ukifikiwa panapokuwa na makabiliano baina ya mpelelezi na mhalifu.

Nadharia ya utanzu itatumika katika sura hii kuchanganua sifa za kikaida zinazoubainisha utanzu wa riwaya ya kiupelelezi na kuitenga na aina nyingineyo za riwaya. Kulingana na Robert (1989) akinukuliwa na Chandler (1997:2), jukumu la nadharia ya utanzu ni kuugawa ulimwengu wa fasihi katika aina za tanzu na kuzipa aina hizo majina kulingana na sifa zake bainifu. Utanzu wa riwaya za kiupelelezi una sifa bainifu kama vile kuwepo kwa mhusika mpelelezi, mhusika mhalifu, mhusika mfoili pamoja na sifa za kifomyula kama vile utoaji wa adhabu kwa mhalifu kufikia mwishoni mwa hadithi. Ili kudhibiti utunzi na upekee wa utanzu wa riwaya ya kiupelelezi, baadhi ya wahakiki wametunga sheria za kuwaelekeza watunzi na wahakiki wa riwaya za kiupelelezi. Kwa mfano, Huntington Wright akitunga kwa jina la kimsimbo la S.S.Van Dine alichapisha sheria ishirini za uandishi wa hadithi za kiupelelezi katika jarida la *The American Magazine*. Baadhi ya kazi zake za kiupelelezi ni kama vile *The Benson Murder Case, The Greene Murder Case, The Bishop Murder Case, The Winter Murder Case* miongoni mwa nyingine.

Katika kusanyiko la sheria hizo, kuna baadhi ya kanuni zilizohusu msuko kama vile; riwaya ya kiupelelezi isiwe na vifungu virefu ili kuepuka kuingiza mambo yaliyo nje ya hadithi, mpelelezi au msaidizi wake hapaswi kugunduliwa ndiye mhalifu kufikia mwishoni mwa hadithi, mtuhumiwa wa uhalifu agunduliwe tu kupitia njia za kirazini wala asigunduliwe kiajali, kisadfa au kwa kulazimishwa kukiri jambo bila sababu maalum. Baadaye, mwaka wa 1928, Ronald Knox alitunga sheria kumi za uandishi wa riwaya ya kiupelelezi zilizojulikana kama *The Detective Decalogue* kwa lengo la kudhibiti utunzi wa hadithi za kiupelelezi. Sheria yake ya kwanza inahusu sehemu ya kwanza ya msuko, kwamba, uhalifu ni sharti uwe umetajwa mwanzoni mwa hadithi hiyo. Itagunduliwa katika sura hii kuwa, baadhi ya kanuni hizi zimejitokeza katika viwango tofautitofauti katika msuko wa riwaya za kiupelelezi zinazochunguzwa. (Kwa mengi kuzihusu sheria hizi, rejelea sura ya pili ya tasnifu hii).

Akichunguza riwaya za kiupelelezi kutoka nchi za Kiafrika zilizotawaliwa na Ufaransa, Meintel (2008:128-136) anamnukuu W.H Auden (1962) aliyefafanua vijenzi sita vya msuko wa riwaya ya kiupelelezi. Vijenzi hivyo ni: (a) Kuwepo kwa amani na utulivu mwanzoni mwa simulizi, (b) Uharibifu wa amani na utulivu huo kupitia tendo la uhalifu, (c) Mwanzo wa uchunguzi ambao aghalabu hutatizwa na ushahidi wa uongo na uibukaji wa uhalifu mwingine, (d) Utatuzi wa uhalifu huo, (e) Kukamatwa kwa mhalifu na (f) Hali ya amani na utulivu kurejelewa tena. Uhakiki wetu utajaribu kudhibitisha ikiwa riwaya zinazochunguzwa zinatumia kaida hizi pamoja na zile za Knox

(keshatajwa) katika msuko wake au la. Kando na kanuni hizi za kiutanzu, sura hii pia itatumia baadhi ya vipengele vya nadharia ya umitindo ili kufafanua mchango wa mbinu kama vile dayalojia, hotuba na anakroni katika kuujenga msuko.

## 5.2 Mbinu za Kimtindo na Msuko

Katika sehemu hii, tunahakiki baadhi ya mbinu za kimtindo ambazo zina mchango wa kukuza msuko katika riwaya zinazochunguzwa. Hii inatokana na ukweli kwamba usimulizi wa namna matukio yanavyofuatana si wa moja kwa moja, bali mwandishi anayawasilisha matukio hayo kwa njia kadhaa za kimtindo kama vile hotuba, barua miongoni mwa nyinginezo. Baadhi ya mbinu hizo za kimtindo na kimuundo zinaonyeshwa hapa chini.

### 5.2.1 Usambamba wa Hadithi Mbili

Todorov (1977) akinukuliwa na Malmgren (2001:121) anafafanua kwamba kuna mwendelezo wa hadithi mbili katika msuko wa hadithi ya kiupelelezi. Hadithi ya kwanza inahusu uhalifu nayo ya pili inahusu uchunguzi wa uhalifu huo. Hadithi ya kwanza inahusu ni nini kilifanyika huku hadithi ya pili nayo ikifafanua ni vipi kitendo hicho cha uhalifu kilivyofanyika. Katika riwaya nyingi za kiupelelezi hususan zilizo na msuko sahili, hadithi ya uhalifu ndiyo hutangulia ili kuweka msingi wa hadithi ya pili. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kwa mfano, hadithi ya uhalifu inatangulizwa kwa kuiweka wazi historia ya Hakimu Marjani, familia yake, utajiri wake pamoja na historia ya uhalifu uliowahi kutendeka nyumbani kwake lakini ukatibuliwa na dereva wake. Katika sehemu hii ya mwanzo, msimulizi pia anaweka vidokezo kadhaa ambavyo vinaweza kumuelekeza msomaji kuhusu ni nani anayeweza kuwaelekeza wahalifu katika nyumba hiyo. Sehemu hii ya kwanza inaishia kwa kuripotiwa kwa kifo cha Hakimu Marjani na kupotea kwa mali yake. Hadithi ya pili inajikita katika upelelezi wa ni nani aliyeiba mali hiyo. Afisa wa polisi anamshuku mtoto wa Hakimu Marjani, Kasim kutokana na vitendo vyake vya utovu wa nidhamu vya awali. Upelelezi unaofanywa na mpelelezi wa kibinafsi, Msa, unafichua kuwa Kasim siye mwizi bali Hakimu Marjani alikuwa ameuza mali hiyo na kuficha pesa hizo katika shamba la Kazole.

Katika riwaya ya *Uchu*, hadithi ya kwanza inahusu tukio la uhalifu lenye uhalisia wa kihistoria kuhusu mauaji ya halaiki nchini Rwanda. Hadithi hii ya kwanza inafafanua jinsi mauaji hayo yalivyokuwa yamepangwa, jinsi masuala ya dhuluma za kikoloni yalivyochochea siasa za kikabila,

wafadhili wa ghasia za kikabila na mahusiko ya mataifa ya Kimagharibi kama vile Ufaransa katika kuchochea vita hivyo. Hadithi ya pili nayo inahusu upelelezi unaofanywa na Willy Gamba kwa niaba ya nchi za Umoja wa Wanaharakati wa Afrika (Pan African Movement-PAM). Katika riwaya hizi, msimulizi anahakikisha kuwa matukio makuu ya hadithi zote yamefafanuliwa. Anachukua tahadhari asije kuendeleza hadithi moja na kuisahau ile ya pili. Sifa hii ya usambamba wa hadithi mbili ndiyo inayoipambanua riwaya ya kiupelelezi na riwaya ya kiuhalifu. Riwaya ya kiuhalifu ina hadithi moja tu ambayo huhusu uhalifu na harakati za mhalifu (mhusika mkuu) au kundi la wahalifu za kuwakwepa polisi.

Ingawa riwaya za kiupelelezi zina usambamba wa hadithi mbili, baadhi ya wahakiki wanahisi kwamba kuna hadithi iliyo na dhima kubwa kuliko nyingine. Malmgren (1997:116) kwa mfano, anasema kuwa kuna hadithi moja ambayo dhima yake ni kuitumikia ile nyingine. Anafafanua kuwa kiwakati, hadithi ya uhalifu ndiyo husababisha ya pili, kwa kuwa kila wakati inapatikana katika wakati uliopita. Hadithi hii ya kwanza nayo inaisha baada ya kusuluhishwa kwa migogoro yote. Kama tulivyotaja katika utangulizi, sehemu hii ya mwisho huwa ni kama mwanzo kwa kuwa amani na utulivu hurejeshwa kama ilivyokuwa kabla ya uhalifu. Huu ndio wakati ambapo pia hadithi ya upelelezi inapoisha. Todorov (1977:47) anaeleza kwamba ingawa hadithi ya kiupelelezi ina hadithi mbili, hadithi iliyo muhimi zaidi ni ile ya uchunguzi wa uhalifu ambayo inahusu jazira ya mpelelezi ya kumtambua mhalifu. Kwa hivyo, mwisho wa upelelezi ndio hatima ya hadithi zote mbili; ile ya uhalifu na hadithi ya upelelezi. Hadithi hizi mbili zinatimiza masilahi ya wasomaji kwa kuwajibia maswali ya ni nani mhalifu na ni vipi uhalifu huo ulivyofanywa. Hadithi ya uchunguzi inakuzwa kupitia uunganishaji wa vidokezo vidogovidogo, mara nyingine vinavyopotosha, lakini mpelelezi hutia jitihada kwa kutumia urazini ili kupata uhusiano wa kiusababishi. Malgren (1997:22) katika *The Anatomy of Murder*, anafafanua kwamba kadri mpelelezi anavyoendelea kuviunganisha vidokezi hivi kiurazini, ndivyo hamu ya msomaji inavyozidi kubadilika kutoka kwa 'ni nani' hadi kwa 'ni kwa nini,'

### 5.2.2 Anakroni na Msuko

Bal (2017:70) anafafanua dhana ya anakroni kama tofouti baina ya mpangilio wa matukio na mpangilio wa utokeaji kiwakati. Anafafanua kwamba kuwepo kwa anakroni ni ukiushi wa kiakronolojia katika msuko wa hadithi. Kulingana naye, riwaya zote huwa na ukiushi huu katika viwango tofautitofauti. Wamitila (2008:153) anaeleza kwamba anakroni ni utokeaji wa matukio

ambapo mkondo asilia hukiukwa. Wahakiki wengine hutumia isitilahi tofautitofauti kuirejelea dhana hii ya mpangilio wa matukio kiwakati. Kwa mfano, Genette anatumia misamiati analepsia na prolepsia kurejelea mbinu rejeshi na mbinu elekezi mtawalia. Mchango wa mbinu hizi ni muhimu katika kukidhia mapengo ya kisimulizi yaliyoachwa aidha kabla ya matukio ya sasa ama ya baadaye. Kulingana na Bal (2017) kuwepo kwa msuko changamano hubidi urejeleaji wa matukio ya wakati uliopita. Sababu ya kuwepo kwa anakroni katika hadithi ni kuwepo kwa haja ya kuunganisha vijihadithi kadhaa ili kupata muwala wa hadithi moja kuu. Anaeleza kwamba katika riwaya za dhati kuna msisitizo wa kuanza usimulizi katikati mwa fabula, hivyo kumfanya msomaji kufaidika na ufafanuzi wa masuala ya kitambo (ya kabla) na ya baada ya usimulizi. Kwa kuwa mpangilio wa matukio kiwakati huathiri msuko kwa kuangazia masuala ya kitambo na ya baadaye, hapa chini tunachunguza mbinu rejeshi na mbinu elekezi.

#### 5.2.2.1 Mbinu Rejeshi


Ni mbinu ya kimsuko ambapo msimulizi hurudia masuala ya nyuma ili kufafanua muktadha wa sasa. Mbinu hii hutumika kwa njia maalum katika riwaya za kiupelelezi kwa kuwa, masimulizi huanza kwa tendo la uhalifu likifanyika katika wakati uliopita. Kwa sababu hii, mbinu rejeshi pia inakuwa mbinu ya kifomyula katika uandishi na usimulizi wa matukio. Muda mrefu hutumiwa na mpelelezi akijaribu kuoanisha vidokezo mbalimbali vitakavyomwezesha kutambua namna uhalifu ulivyotekelezwa ili ausuluhishe mgogoro huo. Uchunguzi huo huenda ukahusisha mpelelezi kulitembelea eneo la uhalifu, kuwatafuta mashahidi na kuwahoji, miongoni mwa hatua nyinginezo ili kuelezea hali ya sasa ya ukosefu wa amani na utulivu. Kama asemavyo Malmgren (1997:116), miishio ya hadithi za kiupelelezi inafanana na mianzo yazo kwani hali ya amani na utulivu ya kabla ya uhalifu hurejelewa mwishoni.

Mbinu rejeshi hutekeleza majukumu kadhaa katika muundo wa msuko. Wamitila (2002:13, 2008:90-91) anafafanua majukumu kadhaa ya mbinu hii. Kwanza, kuweka msingi au usuli wa wahusika kwa kuyamulika maisha yao ya kabla, pili, kubainisha misukumo ya matendo ya wahusika, tatu, kuweka msingi wa kidhamira wa kazi husika na mwisho, mwandishi anaweza kuitumia mbinu rejeshi kukuza taharuki (anapouwacha mkondo fulani wa hadithi kwa muda).


Bal (2017:78-85) anafafanua aina mbili za mbinu rejeshi, mbinu rejeshi ya ndani na mbinu rejeshi ya nje. Anaeleza kwamba mbinu rejeshi ya nje inaeleza maisha ya awali ya wahusika na usuli wao,

ikiwa usuli na historia hiyo itasaidia kuyafasiri matukio ya sasa. Mbinu rejeshi ya ndani nayo hujitokeza katika maelezo ya sasa ya hadithi. Wamitila (2008:155-156) anafafanua kuwepo kwa aina hizi mbili za urejeshi lakini anaongezea aina nyingine za mbinu ya rejeshi ndani na na mbinu rejeshi ya nje. Anaeleza mbinu rejeshi ndani kama hali ambapo urejeshi unaohusika haupo nje ya wakati unaodokezwa na mwanzo wa matini. Yaani inajitokeza baada ya mwanzo wa mwendo-wakati/kronolojia ya hadithi kuu. Wamitila ameutumia mchoro ufuatao kuonyesha aina hii ya urejeshi:

**Kielelezo5.1. Mchoro unaoonesha mbinu rejeshi ndani(Wamitila 2008)**




Mbinu rejeshi nje nayo, anaendelea kusema kuwa, ni pale urejeshi unaotokea unapatikana nje ya pale hadithi inapoanzia. Ni mbinu rejeshi inayoanza na kumalizika kabla ya sehemu unakoanzia msuko wa hadithi. Hali hii inaonyeshwa na kielelezo kifuatacho.




**Kielelezo5.2. Mchoro unaoonesha mbinu rejeshi nje(Wamitila 2008)**

Bal anajadili kuwa mbinu rejeshi ndani inaweza kuwa na majukumu kadhaa. Kwanza, kufidia mapengo ya kisimulizi hususan mapengo yanayohusu udondoshi wa kimsuko. Pili, inaweza kufafanua taarifa ambazo zimetolewa awali. Hata hivyo, ufafanuzi huu unaweza kuchukuliwa kama urudiaji. Urudiaji huu pia ni muhimu kwa kuwa unalipa wazo mwanga mpya kupitia msisitizo tofouti (uk.17). Hata hivyo, Bal anatahadharisha kwamba mbinu rejeshi ndani ikikuzwa sana inaweza kuwa na umuhimu unaoipiku hadithi kuu. Mbinu rejeshi ndani ina dhima kuu wakati msimulizi anapotaka kumtanguliza mhusika mpya. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, mbinu rejeshi inatumika katika baadhi ya riwaya. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka*

*Kuzimu* (1987), kuna mbinu rejeshi ndani wakati Jodor Proper anajitokeza mara ya kwanza (uk.1) kama mwenyekiti wa mkutano wa kupanga mauaji ya Joram Kiango, bila jina lake kutajwa. Anapojitokeza mara ya kwanza, wajumbe wake wanasikia sauti yake tu bila kuona uso wake wala kulijua jina lake. Utangulizi kumhusu unajitokeza baadaye (uk.5) wakati msimulizi anapoeleza kwamba Proper ana wasifu wa kujigeuza kisura, miondoko yake na hata kutumia majina tofautitofauti kutegemea dhamira zake. Katika riwaya hii, mbinu rejeshi ndani inatumika tena katika kufafanua wasifu wa Waridi. Kiusuli anaelezwa kama aliyezaliwa baina ya wazazi wa rangi tofauti ambao ni Wahindi na Waafrika weusi na kwamba alikuwa amezaliwa kutokana na vitendo vya ukahaba vya mamake Waridi. Mbinu rejeshi hii inamfahamisha msomaji kuwa Waridi, kama mamake, alikuwa akifanya biashara ya ukahaba. Waridi alikuwa amezuru miji kadhaa kwa ajili ya biashara hii kabla ya kuhamia katika vitongoji duni vya Dar es Salaam ambapo alikutana na Bomba Kimara na kumuua ili achukue pesa zake. Mbinu rejeshi inatumika ili kumtanguliza kwa kuwa mara ya kwanza tunampata akiwa mikononi mwa Jodor Proper anayemlazimisha kumuua Joram Kiango. Mbinu rejeshi hii inasaidia kufidia pengo la kwa nini Jodor Proper anamwambia Waridi amuue mtu wa pili. Inaturejesha katika tukio la awali kuhusu jinsi Waridi alivyokuwa amumuua mtu wa kwanza. Kwa muktadha huu, urejeleaji huu unafifiza taharuki iliyokuwepo kuhusu ni nani aliuawa na Waridi, vipi na kwa nani. Pia inamaliza taharuki kuhusu ni vipi Jodor Proper alivyofahamu mambo haya. Kwa hivyo, mbinu rejeshi inaboresha msuko kwa kupunguza mapengo yahusuyo habari kama hizi.

Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, habari nyingi kuhusu usuli wa Mwana wa Giningi, mumewe, Vuai, na Ali Makame yanatolewa kupitia mbinu rejeshi ndani. Kupitia mbinu hii, tunaelezwa kwamba babake Mwana wa Giningi alifanya biashara nyingi zikiwemo biashara haramu na kwamba kupitia biashara hizi alipata mali nyingi kama vile mashamba na dhahabu ambavyo anamrithisha Mwana wa Giningi. Inatueleza pia ni kwa nini Mwana wa Giningi aliishi katika upweke mwingi bila kutagusana na jirani zake na kwa nini jirani hao walikuwa wakimwita mwana wa kuokotwa. Vilevile mbinu rejeshi hii inatufafanulia ni kwa nini hakumpenda bwanake, Vuai. Mbinu rejeshi hii inauweka msingi bora unaomfaa msomaji kuelewa msukumo wa matendo ya Mwana wa Giningi. Kwa mfano, anapomshuku Vuai kwa wizi, mbinu rejeshi hii inatufafanulia kuwa hakumpenda Vuai tangu mwanzo kwa kuwa alikuwa amelazimishwa na babake kumkubali Vuai kama mumewe. Kurudi nyuma huku kimsuko pia kunakidhi haja ya kupata muwala katika msuko kwa kuhakikisha kuwa hakuna pengo la kisimulizi linaloachwa.

Mbinu rejeshi ya nje pia inatumika mwanzoni mwa baadhi ya riwaya za Mohamed Said Abdulla. Kwa mfano, mwanzoni mwa riwaya ya *Kisima cha Giningi* kuna barua ya Spekta Seif kwa Bwana Msa akimuomba Bwana Msa kuja katika sehemu ya Giningi ili amsaidie katika upelelezi. Katika barua hiyo, inabainika kwamba Bwana Msa alikuwa amemsaidia Spekta Seif katika upelelezi wa kisa kingine (*Mzimu wa Watu wa Kale*) kisichohusiana na kisa cha sasa.

5.2.2.2 Mbinu Elekezi

Wamitila (2002:14) anasema kuwa mbinu elekezi ni kama kinyume cha mbinu rejeshi kwa kuwa inahusu uangazaji wa matukio kabla ya kutokea kwake. Hali hii hutokea mno katika kazi zenye mielekeo ya kinjozi au za kiutabiri. Wamitila (2008:157) anaeleza kwamba mbinu elekezi inautoa mkazo wa taharuki kutoka kwa swali la kwa 'nini kinahusika' hadi kwa 'vipi kinatokea', yaani hamu ya msomaji kuhusu nini kitatokea inapunguzwa. Kinachobakia ni vipi jambo hilo litakavyotokea**.** Kwa mfano, katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, Amanullah alikuwa ameota usingizini akiambiwa, 'Nenda Darsalama, mafanikio yako, yako Darsalama'. Uk.9. Kwa kuwa ndoto hiyo ilijirudia mara kadhaa, Amanullah aliamua kuifuata na kusafiri hadi Dar es Salaam na alipofika huko, akapewa barua iliyoachwa na babake katika kituo cha polisi pamoja na nauli yake ya kusafiri hadi Unguja. Alitakiwa kwenda Unguja kukutana na babake Bwana Soarez kupatiwa urithi wake. Kwa hivyo, ndoto yake inakuwa mbinu elekezi kwani kwa kweli alipokwenda Dar es Salaam alianza kupata fanaka ya kumjua babake, aliyemwita Unguja. Amanullah anaripoti kwa Bwana Msa kwamba alipofika Dar es Salaam, rafiki yake alimpa habari kuwa kulikuwa na mtu kutoka Unguja aliyetaka wakutane. Amanullah anasema:

> Yuko mtu huko Unguja ananitafuta, na ansema kwamba yeye ni mzee wangu; kaleta barua katika mikono ya serikali na hundi la posta kwa jina langu, nikapokee posta Sh.200/- nifanya safari kurudi Unguja na yeye huyo 'mzee wangu'nitamkuta gatini, ananingoja. uk.10

Taharuki inayoletwa na mbinu hii inahusu ni vipi Amanullah atakavyoafikia ndoto yake. Hii ndio sababu Mieke Bal (2017:83) anasema kuwa mbinu elekezi inaweza kuashiria jaala ya mhusika ikiwa imejitokeza mwanzoni mwa simulizi. Uelekezaji huu unasaidia kumvuta msomaji ili pia ayapate matukio mengine katika msuko. Safari ya Amanullah inamfaa pia Msa kwa kuwa wanakutana na Amanullah katika meli, jambo linalomsaidia Msa kuuelezea usuli wa Amanullah

wakati Msa anapotoa hotuba yake kufafanua mgogoro wa hadithi. Msa anawaeleza waliohudhuria historia ya Amanullah, uhusiano wake na walezi wake na uhusiano wake pia na Bwana Soarez.

Bal (2017:83) anafafanua kwamba mtindo mwingine unaofanikisha ujitokezaji wa mbinu elekezi ni matumizi ya muhtasari wa hadithi, ikiwa muhtasari huo umetolewa mwanzoni. Anasema kwamba katika baadhi ya riwaya, kuna mtindo unaohusu fomyula ya ufunguzi kutolewa kabla ya usimulizi kuanza. Katika mbinu hii, kidokezi kuhusu hadithi kinatolewa huku sehemu yote ya hadithi iliyobaki ikifafanua utangulizi huo wa kimuhtasari. Katika riwaya ya *Mzimu wa watu wa Kale*, tunaona matumizi ya utangulizi huu wa kumuhtasari ukiashiria mwisho wa hadithi. Muhtasari huu unajitokeza katika ukurasa wa kwanza hivi:

> Najum karudi jana kutoka shamba, yeye na Msa, baada ya kukunjwa kwa tanga la Bwana Ali, na wamemwacha Ahmed, mfiwa, huko shambani akitengeneza zaidi mambo yaliyomhusu maiti, baba yake. Uk.1.

Katika nukuu hili, tunaona masuala makuu kuhusu msuko wa hadithi yakijitokeza. Kwa mfano, mbinu elekezi inataja mauaji ya Bwana Ali Bomani ambayo bado hayajatendeka na kuyaleta mwanzoni huku msimulizi akiwajuliza wasomaji hata kuhusu mipango ya mazishi. Muhtasari huu vilevile unaelezea kuhusu safari ya Msa na Najum ambayo tayari imekamilika na wakarudi kutoka huko shambani. Kwa hivyo, sura ya kwanza, kwa kutumia kielekezi hiki, inaashiria mwisho wa hadithi kwa kuwa sura zote zinazofuata zinafafanua wazo linalorejelewa katika muhtasari huu. Kisa hiki kinaipunguza taharuki ya hadithi na pia kuizidisha wakati huohuo. Kwanza, kutolewa kwa taarifa za wahusika wakuu kama vile Msa, Ali Bomani, Ahmed na Najum, kuuawa kwa Ali Bomani na kubaki kwa mtoto wake akipanga mazishi kunapunguza hamu ya kutaka kujua ni nani aliyeuawa. Pili, maelezo kwamba uchunguzi tayari umekamilika na Msa na Najum wamekurudi kwao, yanapunguza taharuki. Hata hivyo, kuna taharuki inayohusiana na sababu za mauaji, nani aliyeuawa, vipi muuaji alivyomuua Ali Bomani na ni vipi atakavyopatikana. Bal anafafanua kwamba matumizi ya mihtasari kama hii ni ishara kuwa matukio yanadhibitiwa na jaala na kwamba msomaji analazimika kushuhudia tu matukio kwa kuwa hakuna liwezalo kufanywa kuzuia utokezaji wake.

Baadhi ya wahakiki (Toolan, 1991:53, Bal, 2017:84) wanaamini kwamba riwaya zinazosimuliwa kwa nafsi ya kwanza ndizo zenye uwezo mwingi wa kutumia mbinu elekezi. Bal kwa mfano,

anasisitiza kwamba ikiwa msimulizi anaweza kuhadithia habari zake mwenyewe, kuna uwezekano wa kuashiria matamanio yake ya baadaye. Kwa kuwa riwaya za kiupelelezi, zikiwemo zile tunazohakiki husimuliwa kwa nafsi ya tatu, hatuoni mhusika akitabiri hali yake ya baadaye. Wamitila (2008:92) anatambua aina nane za mbinu elekezi, lakini hapa tunachunguza aina mbili ambazo zinajitokeza katika msuko wa riwaya za kiupelelezi tunazozichunguza.

5.2.2.2.1 Mbinu Elekezi Yakini

Hii ni aina ya mbinu elekezi ambayo inatanguliza jambo ambalo kwa hakika litatokea katika ulimwengu wa hadithi. Katika riwaya ya Duniani *Kuna Watu*, Spekta Seif na Msa wanapozuru nyumbani kwa Mzee Hakimu Marjani ili kumpelekea Saleh Msahafu ulioachwa na Mariam Mkembe katika kituo cha polisi, walipofika walimtazama Saleh na Msa akagundua kuwa alikuwa ameiona sura ya Saleh hapo awali. Msa anauliza, 'Wapi nimemwona kijana yule kabla ya leo, lakini nimeshindwa, sijui wapi…juu ya hayo naona sura yake kama nimepata kuiona pahala, lakini sijui' uk.60. Maswali ya Msa kuihusu taswira ya Saleh yanathibitishwa baadaye Msa anapotoa hotuba yake kuhusu asili ya familia ya Hakimu Marjani. Katika hotuba hiyo, Msa anakumbuka kwamba hakuwa amemwona Saleh awali bali ni picha ya Hakimu Marjani aliyoiona gazetini. Mbinu hii elekezi inathibitika baadaye katika ukurasa 91. Mbinu hii inamsaidia Msa kutoa ushahidi wake kuwa Saleh ni mtoto asili wa Hakimu na kwamba Kasim si mtoto wa Hakimu Marjani. Msa anawaambia waliohudhuria hivi:

> Hebu watazame Saleh na Selume, mliwalinganishe watu hao na marehemu Bwana Hakimu, wale pale, watazameni, mwatambue. Ipo tofauti baina ya watu hao? Hakuna abadani. Bado; kwa kuwa mimi nimeiona picha ya Bwana Hakimu- mtu ambaye sijapata kumwona maisha yangu kabla sijamwona Saleh ambaye na yeye sijapata kumwona maisha yangu-niligumiwa nilipomwona Saleh uso kwa uso. Nimemwambia Spekta Seif kuwa mtu yule, yaani, Saleh, nimepata kumwona mahali na nisiweze kupajua wapi. Nimefahamu baadaye kuwa nilikuwa nimetekewa na picha ya Bwana Hakimu, ndipo nilipomwona Saleh kwa mara ya kwanza, nikadhani kuwa nimepata kumwona pahali. Uk.91

Kwa hivyo, mbinu elekezi tunayoipata katika ukurasa 61 ni mbinu elekezi yakini kwa kuwa, kwa hakika taswira aliyo nayo Msa kumhusu Saleh inathibitika baadaye katika ukurasa 91. Katika riwaya hii pia, mwanzoni mwa usimulizi (uk.4), Hakimu Marjani anamshuku Kasim kuwa

mchezaji kamari kwa kuwa mara nyingi huja kumuomba pesa bila kueleza namna anavyozitumia. Babake Kasim, Hakimu Marjani anamwambia:

> Sikatai kukupa mwanangu, lakini nataka kujua ni vipi wewe unatumia pesa zako?...hata iwe juzi umechukua shilingi mia,jana jumanne, leo jumatano unataka mia nyingine. Unacheza kamari nini wewe? (uk.4).

Uelekezaji huu unathibitika baadaye tunapomwona Kasim akiungana na rafiki zake, Bob na Puto kwa Baniani (uk.11) ili wacheze kamari na kunywa pombe. Kwa hivyo, utabiri wa babake unakuwa wa ukweli baadaye.

5.2.2.2.2 Mbinu Elekezi Isoyakini

Hii ni aina ya mbinu elekezi ambayo inagusia jambo ambalo kutokea kwake si kwa hakika (Wamitila, 2008:158). Inaweza kuhusishwa na matumaini ama ndoto za mhusika anayejaribu kutafakari ni matokeo gani yanayoweza kutokea baadaye. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, Judor Proper anapania kumuua mpelelezi wa kibinafsi, Joram Kiango, ili mipango yake ya kuipindua serikali ifanikiwe**.** Proper ana ndoto kuwa atatwaa mamlaka na kuwapa vikaragosi wake nyadhifa kuu serikalini. Katika juhudi zake za kumuua mpelelezi Kiango, Proper anamlazimisha Waridi kumuua Joram Kiango kwa sumu. Proper anasema, 'Baada ya muda mfupi atakuwa marehemu. Itaonekana kafa kutokana na magonjwa ya kawaida tu. Hakuna atakayefikiria kama wewe na mimi tunahusika kwa kifo chake.'uk.13. Hata hivyo, mipango hii haikufanikiwa kwa kuwa Joram aliyeonekana kama kizingiti kikuu hakuuawa. Kwa hivyo, mpango huu unabakia kuwa matumaini tu ya mhalifu Judor Proper.

Baadaye Judor Proper anapanga kuwaua marais kadhaa na mawaziri wa nchi za Kiafrika waliotarajiwa kuhudhuria kongamano mjini Arusha, kwa kutumia sumu maalum. Pia matumaini haya hayakuzaa matunda kwani kufikia mwishoni mwa hadithi, njama hizi zinatibuliwa na mpelelezi Joram Kiango. Joram Kiango aliweza kuichukua podari yenye sumu na kuibadilisha na nyingine isiyokuwa na sumu. Matamanio ya mhalifu Proper yanabakia kuwa ndoto tu.

Akifafanua dhima ya mbinu elekezi katika ujenzi wa msuko, Bal (2017:84) anasema kwamba inasaidia kuepuka udondoshi wa kisimulizi wakati ujao kwenye hadithi. Pia anafafanua kwamba mbinu elekezi inamsaidia mwandishi kuweka hoja fulani wazi mapema ili baadaye anapoitaja iwe ni kuongeza msisitizo wake kama aina ya urudiaji. Anaeleza njia mbili kuu za ujenzi wa mbinu

elekezi ambazo ni utoaji wa tangazo na utoaji wa kidokezo. Kulingana naye, tangazo la hali au kitu fulani linapotolewa kabla ya ujitokezaji wake katika usimulizi, ni ishara yenye nguvu zaidi katika uelekezaji kuliko kuliko utoaji wa kidokezo. Tangazo la hali fulani linapotolewa mapema pia linaongeza taharuki kwa wasomaji kwani sasa wanataraji kwa hamu matokeo ya tangazo hilo. Tunaona hali kama hii katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* ambapo mtu asiyejulikana anampigia simu inspekta wa polisi na kumtangazia kwamba angetaka kumuua mtu fulani. Tangazo hili linaijenga mbinu elekezi kwa kuwa kwa hakika baadaye (sura ya pili), mwandishi mashuhuri, Kondokondo Kitenge ambaye pia ndiye mkurugenzi wa Black Power Publishers aliuawa. Tangazo lililotolewa hapo awali linaimarisha uelekezaji zaidi ya ikiwa kidokezo kingetumika badala yake. Bal anazidi kueleza (uk.85) kuwa katika riwaya za kiupelelezi, hata vidokezi vinaweza kuchangia uwepo wa taharuki hususan vidokezi vya uongo vinavyomwelekeza msomaji kwenye mambo yasiyo na uzito au yasiyo muhimu katika msuko. Katika riwaya za kiupelelezi hata hivyo, msimulizi sharti achukue tahadhari anapotoa vidokezi asije akatoa jibu la fumbo mapema. Kufanya hivyo kuna hatari ya kuharakisha msuko kufika kileleni kabla ya mwendo-wakati na kupunguza taharuki. Utoaji wa vidokezi visivyo wazi ili msomaji aviwazie zaidi ndio msingi unaotumiwa na baadhi ya wahakiki kudai kuwa usomaji wa riwaya za kiupelelezi ni sawa na mchezo wa ushindani baina ya msomaji na mwandishi.

### 5.2.3 Mwingilianomatini na Msuko

Wamitila (2008:111-112) anafafanua kwamba msingi mkuu wa nadharia ya umwingilianomatini ni msisitizo wake kuhusu namna kazi za kifasihi zinavyohusiana, kuumbuana na kuchangamana. Kulingana na nadharia hii, kazi ya kifasihi inazalika kutokana na taswira ya kazi nyingine kama hiyo. Kwa sababu hiyo, riwaya husika inahusiana na kuingiliana na riwaya nyingine inayojulikana. Wamitila anahisi kwamba nadharia ya umwingilianomatini inaakisi mawazo ya Plato kuhusu mwigo kama msingi wa matendo ya kibinadamu. Kulingana na Kristeva (1980:36), waandishi huwa hawatoi matini moja kwa moja akilini bali huzizalisha kutokana na nyinginezo zinazohusiana nayo. Yaani, matini ya sasa ni matokeo ya uboreshaji na mwendelezo wa matini nyinginezo, wala si mfumo funge. Kwa hivyo, riwaya zinaweza kuhusiana kwa njia kadhaa kama vile kupitia mahusiano ya kidhamira, kimotifu, kimaudhui au kimtindo. Riwaya za kiupelelezi zinaonyesha mahusiano ya kimwingilianomatini kwa njia zifuatazo:

#### 5.2.3.1 Urejelezi wa riwaya za awali za mwandishi mmoja

Baadhi ya waandishi wa riwaya za kiupelelezi wanatumia mtindo ambapo kazi zao za awali zinafungamanishwa na riwaya zao za baadaye. Njia hii inawawezesha kuunda sanjari ya riwaya ambapo usomaji wa riwaya ya kwanza unambidi msomaji kuitafuta riwaya ya pili ili kukidhi hamu ya kitaharuki inayoziunganisha. Kwa kufuata mtindo huu, kila riwaya inakuwa kama sura moja katika msururu mzima. Kwa kurejeleana kwa njia hii, mwandishi anawatumia wahusika wale wale katika riwaya za baadaye ili kujenga muwala baina ya kazi hizo na kuboresha mahusiano ya kazi hizo. Kwa mfano, katika riwaya za Mohamed Said Abdulla karibu zote, mwandishi huwatumia wahusika wakuu Spekta Seif na Msa. Naye mpelelezi Msa karibu kila wakati huwa na msaidizi wake, Najum. Katika kazi za Mtobwa, wahusika wakuu katika riwaya nyingi zake huwa mpelelezi Joram Kiango na Inspekta Kombora. Kwa kutumia mbinu hii ya wahusika walewale kunawavutia pia wasomaji wanaposoma riwaya moja kuitafuta nyingine ili kuufuatilia uhodari wa mpelelezi na mapambano yake dhidi ya wahalifu. Elvis Musiba pia aliandika riwaya zake kwa usanjari uliomhusu mpelelezi Willy Gamba. Willy Gamba anajitokeza katika riwaya zake saba, akijitokeza mara ya kwanza katika *Kufa na Kupona* (1974).

Kwa sababu ya matumizi ya mtindo ule ule wa kiusanjari na wahusika walewale, baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili ina mwingiliano mkubwa na riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi. Khamis (2008:161) kwa mfano, anahoji ikiwa mpelelezi Msa katika kazi za Mohamed Said Abdulla ni mwigo wa mpelelezi Sherlock Holmes wa kazi za Conan Doyle. Khamis anathibitisha kuwa Abdulla amefanikiwa kumuumba mpelelezi aliye na sifa za Kimagharibi lakini akaweza kudumisha sifa zenye uhalisi wa Unguja wakati huohuo.

Sifa ya utunzi wa riwaya kiusanjari katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili inatokana na athari za watunzi wa Kimagharibi ambao waliandika riwaya zao za kiupelelezi kwa mtindo huo. Kama anavyosema Khamis, huko Uingereza mwandishi Conan Doyle ameutumia mtindo sawa katika karibu riwaya zake zote hususan kuhusu uhusika. Wahusika wake wakuu ni Sherlock Holmes ambaye ndiye mpelelezi katika takribani kazi zake zote. Msaidizi wake ni Dkt.John Watson, ambaye anaandama naye katika kuchunguza masuala mbalimbali. Inaweza kusemwa kwamba mtindo wa kuwatumia wahusika walewale uliasisiwa na Edgar Allan Poe kabla ya kuendelezwa na waandishi wengine wa Kimagharibi kwa kuwa hadithi zake nyingi zina wahusika wale wale. Mhusika mpelelezi katika kazi za Edgar Allan Poe ni Auguste Dupin, naye Agatha Christie

alimtumia mpelelezi Hercule Poirot katika riwaya zake kadhaa na Miss Marple katika baadhi ya hadithi nyingine. Naye mpelelezi Father Brown ametumika katika kazi za G.K Chersterton ambazo pia zimetumika kwa usanjari. Katika Afrika Kusini, MCcall Smith ameendeleza mtindo huo wa Kimagharibi na kumtumia mhusika mpelelezi yuleyule, Mma Ramotswe katika kazi zake alizoandika katika msururu wa The NO.1 Ladies Detective Agency.

Kwa misingi hii basi inatosha kusema kuwa riwaya za Kiupelelezi za Kiswahili zina mwingilianomatini na zile za Kimagharibi, kimtindo, hasa kupitia uhusika na urejelezi wa riwaya za awali ili kuunda msuko mpana katika riwaya za mtunzi mmoja. Katika riwaya ya pili ya Abdulla kwa mfano, kuna urejelezi wa riwaya ya kwanza, *Mzimu wa Watu wa Kale*. Urejelezi huu unafanyika kupitia barua ya mwaliko ambayo Spekta Seif anayomwandikia Msa. Seif anasema katika barua hiyo, " Nakumbuka tangu kuisha ile kadhia ya 'Mzimu wa Watu wa Kale' ambayo kama si wewe kutambua siri ya mambo yale, mimi na Uispekta wangu wote nisingeweza kuifahamu".uk.7. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu,* kuna urejelezi wa riwaya ya *Siri ya Sifuri*. Msa anaporudi Pemba anajiwa na mgeni, Spekta Seif na katika mazungumzo yao, Msa anamkumbusha Spekta Seif riwaya ya *Siri ya Sifuri*, na jinsi Msa alivyosaidia katika uchunguzi wa kisa hicho. Msa anamwambia Spekta Seif, 'Uko mjini sasa? Mimi nilidhani bado uko kule kule pande za Kusini tulikokutana safari ile katika kadhia ya 'Wasiwasi Malifedha'. Vilevile katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa* kuna urejelezi wa riwaya ya *Siri ya Sifuri*, kuhusiana na utafutaji wa Saidi. Riwaya ya *Siri ya Sifuri* inarejelewa tena wakati Msa anapozungumza na Mwanatenga wakati wa arusi yake. Wanamtaja Bwana Hafifu Malifedha ambaye ni mhusika katika katika *Siri ya Sifuri.*

Sifa ya urejelezi wa riwaya za awali pia ipo katika kazi za Ben Mtobwa. Katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*, mwandishi anarejelea riwaya za awali za *Dimbwi la Damu* na *Lazima Ufe*. Msimulizi akimsifu Joram Kiango kwa ushujaa wake anasema, 'Machache kati ya aliyoyafanya yaliwavuta waandishi hata wakayaandikia vitabu na kuviita *Dimbwi la Damu* na kile kitabu kiitwacho *Lazima Ufe'*.uk.42. Katika riwaya *ya Salamu Kutoka Kuzimu* kuna urejeleaji wa riwaya ya *Dimbwi la Damu* na ile ya *Najisikia Kuua Tena* mara tu hadithi inapoanza. Urejeleaji huu unatokea wakati Proper akiwahutubia ajenti wake kuwaonya dhidi ya kufanya mapinduzi kabla ya kumuua Joram Kiango. Anawakumbusha ushujaa wa Joram kutokana na matendo yake ya awali katika riwaya

zilizotangulia. Kuhusiana na ushujaa wa Joram Kiango, msimulizi anawafahamisha wasomaji kuuhusu ushujaa wa Joram Kiango. Anasema:

> Haijasahaulika alivyowakorofisha wale mashujaa waliotaka kuuangusha utawala wa nchi ya Ngoko katika tukio lile lililoitwa *Dimbwi la Damu*. Kadhalika hatujasahau alivyosababisha vifo na kuharibika kwa harakati za majasusi waliotaka kuiharibu nchi hii katika mkasa ambao mtu ameuandikia kitabu na kukiita *Najisikia Kuua Tena.* Uk.1

Mwanzo wa msuko kwa njia hii ya kumrudisha msomaji kwenye riwaya za awali kunasaidia kuimarisha uhusiano wa kazi hizo, kuongeza uzito wa taharuki na mshikamano wa riwaya zote. Urejelezi huu pia unamlazimu pia msomaji kusoma riwaya zote za awali ili kuuelewa uhusiano wa riwaya ya awali na ya sasa. Katika *Tutarudi na Roho Zetu?* tunakumbushwa pia kuhusu uhusika wa Nuru katika riwaya ya awali ya *Salamu Kutoka Kuzimu* (uk.3). Kupitia urejelezi wa kazi za awali, kila riwaya inajitokeza kama sura katika msururu mzima.

5.2.3.2 Urejelezi wa Riwaya za Waandishi Wengine

Kando na urejelezi wa riwaya za mwanzo za mwandishi mmoja, kuna mtindo wa kuzirejelea kazi za waandishi wengine. Urejelezi wa riwaya za waandishi wengine ni sifa inayopatikana pia katika riwaya dhati na tanzu nyinginezo za fasihi. Hata hivyo, katika riwaya za kiupelelezi, sifa hii inakuwa wazi zaidi ya inavyokuwa katika tanzu nyinginezo za kifasihi. Urejelezi huo ni ishara kuwa mwandishi ameathiriwa na kazi zilizotangulia za waandishi wengine. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, kwa mfano, kuna urejelezi wa riwaya za Conan Doyle na mhusika mpelelezi katika kazi hizo, Sherlock Holmes. Katika riwaya hii, Mwanatenga anamsifia Bibie Shali uhodari wa Msa katika upelelezi na kumfananisha Msa na Sherlock Holmes. Hata hivyo, Msa anapolinganishwa na Holmes anakasirika akisema kwamba yeye si mpelelezi wa siri kama alivyo Holmes. Anashikilia kuwa upelelezi wake ni tofauti na ule wa Sherlock Holmes na kwa hivyo angependa kuitwa 'Mchunguzi wa Mambo'. Kumhusu Msa, Mwanatenga anamwambia Bibie Shali hivi:

> Kulinganishwa na Sherlock Holmes yeye anaona katukanwa, kavunjiwa heshima yake. Bado-bado anaridhi kulinganishwa na Father Brown, na nafikiri anapenda hasa kulinganishwa naye maana nilipata kumsikia hasa akisema, vipi analinganishwa na Sherlock Holmes, na Sherlock Holmes ni mpelelezi wa siri,

anaachwa kulinganishwa na Father Brown ambaye ni mchunguzi wa mambo kama yeye? (uk.47).

Mwandishi Mohammed Said Abdulla anapowarejelea wahusika wapelelezi katika riwaya za waandishi wa Kimagharibi (Father Brown ni mpelelezi katika riwaya za G.K.Chesterton na Sherlock Holmes akiwa mhusika mpelelezi katika riwaya za Conan Doyle) ni ithibati kuwa ameathiriwa na usomaji wa kazi za waandishi hao. Kwa sababu hii, riwaya za Abdulla zina uhusiano wa kimwingilianomatini na riwaya za kiulaya. Baadhi ya wahakiki wamedai kuwa kazi za Abdulla ni mwigo wa kazi za Kimagharibi kwa kuwa wakati alipoanza kuandika kazi za kiupelelezi, miaka ya sitini, wapelelezi wa kibinafsi hawakuwa wamejitokeza katika maeneo ya Unguja (Kezilahabi, 1975:11, Williams 1972:36, Lindfors, 1994:91).

Urejelezi huu wa kimwingilianomatini unaojitokeza katika mazungumzo baina ya Bibie Shali na Mwanatenga una jukumu la kuuweka msingi wa uchunguzi kuhusu kupotea kwa watoto wake Bibie Shali, kwa kuwa tangu hapo, wanakubaliana kumtafuta Bwana Msa ambaye sasa matukio mengi ya kimsuko yanamhusu pamoja na uchunguzi wake hadi mwishoni mwa hadithi. Kando na hili, urejelezi huu pia unachelewesha kilele cha msuko.

Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* mwandishi, Ben Mtobwa anadhihirisha kuwa ameathiriwa na usomaji wa riwaya za kiupelelezi za waandishi wengine. Kwa mfano, mhusika mpelelezi katika riwaya nyingi za Mtobwa, Joram Kiango, anaonyesha kuvutiwa na mpelelezi apatikanaye katika riwaya za Elvis Musiba, Willy Gamba. Joram Kiango akizungumza na Nuru anasema, ‘Kama mpelelezi mwenzangu anayeitwa Willy Gamba alivyowahi kusema, kazi ni dawa. Mpelelezi ni binadamu vilevile. Lazima astarehe na kuburudika’. (uk.53). Kwa hivyo, katika muktadha huu, riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, inazirejelea riwaya za Elvis Musiba. Riwaya hizo basi zina uhusiano wa kimwingilianomatini katika kiwango cha uhusika. Mwingilianomatini baina ya riwaya za Musiba na Mtobwa pia unajitokeza katika kiwango cha kidhamira na kimtindo. Katika riwaya za Musiba kama vile *Uchu,* mwandishi analimulika suala la uhusiano wa kimataifa na hali ya nchi za Kiafrika baada ya Uhuru. Katika *Uchu,* suala la vita vya kikabila nchini Rwanda pamoja na jinsi mataifa jirani yalivyochangia katika vita hivyo linaangaziwa. Vilevile, katika riwaya za Mtobwa kama vile *Tutarudi na Roho Zetu*, Mtobwa anachunguza mahusiano baina ya

Afrika Kusini na mataifa ya Kusini mwa Afrika hususan kuhusiana na mchango wa Tanzania katika ukombozi wa mataifa hayo.

Kimtindo, waandishi Mtobwa na Musiba wanaonekana kuathiriwa na filamu za Kimagharibi kwa kuwa riwaya zao zinawawasawiri wahusika wakuu, mpelelezi na mhalifu wakipambana kama inavyokuwa katika filamu hizo. Wapelelezi Willy Gamba na Joram Kiango wameumbwa kwa kuzingatia kielelezo cha James Bond, mhusika na mtendaji maarufu katika filamu pendwa nyingi za Kimagharibi. Kama James Bond, wapelelezi Willy Gamba na Joram Kiango wanatumia vifaa na ala mbalimbali katika kupambana na wahalifu. Kando na kutumia silaha anuwai, wana uwezo wa kuendesha vyombo vya usafiri tofautitofauti kama vile magari, ndege na nyinginezo. Wanatumia pia viungo vya mwili mbalimbali katika mapigano hayo. Plotell na Charney (1978) wakiifasiri dhana ya usemezano ya Bakhtin, wanasema kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambamo kuna majibizano baina ya matini hizo katika usemezano uliotanuliwa. Kwa hivyo, riwaya za *Uchu* ya Musiba na *Tutarudi na Roho Zetu* ya Mtobwa, zina uhusiano wa kiusemezano.

Kwa kuwa Mtobwa aliandika nyingi ya riwaya zake katika miaka ya themanini, ameathiriwa na riwaya za waandishi wa awali hususan Faraj Katalambulla kupitia riwaya yake ya *Simu ya Kifo* (1965). Riwaya ya Mtobwa ya *Najisikia Kuua Tena* na ya Katalambulla ya *Simu ya Kifo*, zina mwingiliano mkubwa kahusiana na muundo wa kisimulizi na mpangilio wa msuko. Kwanza, riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* inaanza kwa mhalifu kupiga simu kwa inspekta wa polisi kuripoti kwamba anataka kumuua mtu na kisha kuikata simu hiyo bila kusema yuko wapi, mtu yupi anayetaka kumuua na kwa nini. Hali hii inazidisha taharuki inayomnata msomaji na kumpa msukumo wa kutaka kusoma riwaya yote haraka ili ajijibie maswali haya. Nayo riwaya ya *Simu ya Kifo* ina mwanzo sawa na huu kwa kuwa Inspekta Far Katy Wingo anapigiwa simu na mtu asiyejulikana na kumjulisha kuwa Mzee Jacob ameuawa nyumbani kwake. Baadaye, vifo vingine vinapotokea katika katika familia hiyo, mtu yuleyule ndiye anayepiga simu kwa Inspekta Far Katy Wingo kuhusu mauaji hayo. Kama mhusika anayepiga simu katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*, yeye pia hasemi yuko wapi wala jina lake. Pia haelezi ni vipi anavyoweza kuwa katika eneo la mauaji kila wakati mauaji yanapotokea. Maswali kama haya pia yanazidisha kiwango cha taharuki katika riwaya ya *Simu Ya Kifo.* Kwa kutumia mtindo unaokaribiana, mwandishi anaelekea kujifunga katika kaida za kifomyula za riwaya za kiupelelezi kama vile matumizi ya wahusika

wale wale, mandhari ya kuajabisha, mbinu za kuzua taharuki miongoni mwa mengineyo. Kwa mfano, mbinu ya kumpigia simu inspekta wa polisi na kutoa habari chache inaboresha uajabu unaozingira mauaji.

Sifa hii pia inajitokeza katika hadithi za Kimagharibi kama vile *Murders in the Rue Morgue*, ambapo mauaji yanafanywa kwa njia tatanishi na katika mazingira ya kiajabuajabu. Katika kurasa za baadaye kwenye riwaya hii ya *Najisikia Kuua Tena*, mtobwa anairejelea riwaya hii ya *Simu ya Kifo* kwa uwazi zaidi. Kumhusu muuaji aliyemuua mwandishi Bazile na ambaye alikuwa amepiga simu awali kuripoti mauaji hayo, msimulizi anasema, 'Sauti katika simu ile haikuwa ya kike, wala Kombora hakuona kama mwanamke huyu mlevi wa gongo angekuwa na haja ya kumhadaa mtu na kupigia simu polisi kama hadithi ile ya *Simu ya Kifo*. uk.23

### 5.2.4. Taharuki na Msuko

Sifa moja kuu inayoubainisha utanzu wa riwaya za kiupelelezi ni namna waandishi wake wanavyotumia taharuki kusuka ploti za hadithi hizo. Ni sifa inayozifanya riwaya za kiupelelezi, kihalifu na za kijazira zivutie. Wamitila (2003:212) akieleza dhana ya taharuki anasema kwamba ni ile hamu ya kutaka kujua yatakayotokea hadithini wakati wa usomaji. Anafafanua kwamba wahakiki wengi wanaichukulia taharuki kama kaida ya kimsuko katika riwaya nyingi. Anasisitiza kwamba taharuki huchukua nafasi kubwa katika baadhi ya tanzu, hususan riwaya za kiupelelezi, ambapo wasomaji wanaweza kuwa na hamu ya kujua ni nini kitatokea na kwa jinsi gani. Kuna mikakati mbalimbali inayotumiwa kuichimuza taharuki katika riwaya za kiupelelezi ambayo huzifanya riwaya hizo zitofautiane na riwaya dhati. Hapa chini tunachunguza baadhi ya mikakati ya kujenga taharuki.

#### 5.2.4.1 Vijenzi vya Taharuki katika Riwaya za Kiupelelezi

Kwa kuwa utanzu huu unatawaliwa na taharuki kwa kiwango kikubwa katika msuko wake, aghalabu waandishi hutumia njia kadhaa kuijenga taharuki hiyo. Kwanza ni kupitia wasifu wa mhusika mpelelezi. Mhusika mpelelezi, awe mtaalam au mwanagenzi hupewa sifa zinazokiuka uhalisia wa binadamu wa kawaida. Kwa mfano, wapelelezi wengi wa kibinafsi husawiriwa wakiwa na kiwango cha juu cha utumiaji wa urazini na mantiki, jambo ambalo huwashangaza wahusika wengine. Symons (1972:9) anasema kuwa katika riwaya za kiupelelezi, mpelelezi husawiriwa kama mtu asiyeweza kufanya makosa, mwenye ujuzi wa juu wa takribani kila kitu,

mwenye ujasiri mwingi unaomfanya kujiingiza katika hatari waziwazi na mwenye maarifa yanayozidi yale ya polisi katika uchunguzi. Kuwepo kwa mhusika mpelelezi mwenye sifa kama hizi kunaongeza mvuto katika usomaji kwa kuwa msomaji anahisi kumfuata mpelelezi ili azijue mbinu zake za utatuzi wa mgogoro hasa maelezo yake kuhusu namna uhalifu ulivyofanywa na kwa nini. Hata hivyo, cha kuridhisha zaidi kwa msomaji ni jinsi mhalifu atakavyoadhibiwa. Utoaji wa adhabu kwa mhalifu hakumridhishi tu msomaji bali pia wanajamii kijumla kwani wanahakikishiwa usalama kupitia kitendo hicho. Kwa hivyo maelezo kuhusu uwezo alionao mpelelezi ni mkakati wa kuikuza taharuki.

Sifa za mpelelezi anazozizungumzia Symons pia tunazipata kuhusiana na wasifu wa mpelelezi Msa katika riwaya za Mohamed Said Abdulla. Msa anatumia urazini na mantiki kwa kiwango cha juu kufichua wahalifu. Hii ndio maana katika riwaya nyingi za Abdulla, Spekta Seif anaposhindwa katika uchunguzi wake anamwita Msa kumsaidia. Uwezo wa fikira yake unawashangaza wengi wakiwemo maafisa wa polisi kama vile Spekta Seif. Wapelelezi wanaopatikana katika riwaya za Musiba na Mtobwa wanatofautiana na mpelelezi katika kazi za Abdulla kwa kuwa wao badala ya kutumia urazini na mantiki, wanatumia silaha na kupambana na wahalifu kimabavu. Hata hivyo, wao pia wana uwezo unaozidi ule wa binadamu wa kawaida kupitia jinsi wanavyoyumia silaha na vyombo anuwai vya kivita. Kwa mfano, wanendesha chombo chochote, kutega na kutegua bomu na vilipuzi vingine miongoni mwa vifaa vingine vya kiteknolojia.

Mkakati wa pili wa kujenga taharuki unahusu usawiri wa mandhari. Mandhari katika riwaya za kiupelelezi huwasilishwa kwa njia yenye mnato mkubwa unaomshughulisha msomaji kuifuatilia hadithi nzima ili kugundua mandhari hayo yana mchango gani katika msuko wa hadithi hiyo. Wamitila (2003:30) anaeleza kwamba mwandishi anaweza kuyasawiri mandhari kwa njia ambayo inachangia kuukuza msuko wa kazi fulani. Katika riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi yanatumika kuboresha uajabu wa kazi hizo na kuikuza taharuki. Kwa mfano, magofu ya majumba yaliyoachwa sehemu za mashambani, majumba yasiyotumiwa na watu kutumika kama pahali pa uhalifu, maeneo ya kuogofya kutumika kama maficho ya wahalifu na mengineyo. Katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili tunazohakiki, mandhari yanachukua nafasi kubwa katika kuikuza taharuki. Katika *Kisima cha Giningi*, maelezo ya kisima chenyewe yanavuta taharuki. Mahali kisima kilipo, zamani kulikuwa jengo lililokuwa maskani ya watu, karibu na kisima, kuna mti mkubwa unaotanda kama mwavuli na chini yake hakunyeshi. Uajabu wa mti huu unashangaza

hata wizara ya kilimo kwani hata jina lake halijulikani. Tena panapo karibu na kisima kuna mnara mkubwa wa saruji. Juu ya mnara pametundikwa karabai inayowaka bila kuzimika, tangu zama za zama, bila mafuta wala utambi. Ndani ya kisima chenyewe na mambo ya kiajabuajabu zaidi. Kwa mfano, humo kuna sauti zinazosikika na ambazo wenyeji hawawezi kuzifananisha na chochote (uk.66). Haya ni maelezo ya kimandhari yenye mchango mkubwa katika kujenga taharuki katika hadithi hii. Kwa hivyo, maelezo ya kimandhari yanachangia kuukuza msuko.

Mgeni (1983:55) anakiri kwamba uajabu ambao Abdulla anaukuza kupitia usawiri wa mandhari, unatokana na uhalisia wa baadhi ya matuko ya kihistoria kisiwani Pemba. Kwa mfano, anasema kuwa karabai isiyozimika inayozungumziwa katika *Kisima cha Giningi*, ni upujufu wa kiubunifu kuhusu aina ya taa iliyokuwa inakaa sehemu ya Mangapwani (uk.55). Kuhusu shimo ambalo kwalo maji ya Giningi huchiririzikia, Mgeni anasema kwamba kulikuwa na pango la Mangapwani lililokuwa na sifa kama hizi.

Mandhari ya baadhi ya riwaya za Abdulla yanafungamana na itikadi kuhusu mizimu na uchawi kwa njia inayoibua uajabu zaidi. Katika *Mzimu wa Watu wa Kale,* sehemu ya mzimu inaelezwa kwa njia ya kuogofya. Hili ni eneo linalowatishia watu wengi kwani iliaminika kwamba kupitia karibu na eneo hilo ni kuwasumbua mizimu katika maombi yao na kuwa kutembelea eneo hilo kungeleta madhara makubwa. Mgeni (uk.51) anasema kwamba wakati wa adhuhuri na baada ya jua kuchwa, eneo hili halikuwa linapitika, na kuwa ikiwa mtu angepitia hapo, ilimbidi kuipigia saluti mizimu. Katika riwaya hii, ugonjwa unaomsumbua Kipwerere unaaminika kutokana na kukiuka kaida hii ya kuonyesha heshima kwa mizimu. Inaaminika kwamba Kipwerere alipitia sehemu hii akila ndizi. Kutokana na imani hii, hata tumbili wanaoishi sehemu ya mzimu wanaheshimika na wanaruhusiwa kuyavamia mashamba yaliyo karibu na kujichukulia mazao kama vyakula vyao. Msa na Najum wanapotembelea eneo hili wakichunguza mauaji ya Ali Bomani wanakutana na kundi la wanyama hawa na inafichuliwa baadaye kuwa ndio waliomwangusha Najum na kumpiga Msa kumbo hadi toza yake ikaruka (uk.26). Kando na uajabu huo uliowapata Msa na Najum huko mzimuni, pia kuna mapango ambamo inaaminika mizimu huishi, ingawa kwa hakika ni makima na tumbili wanaokaa ndani. Msa alipochungulia tundu moja alipigwa na bumbuazi. Msimulizi anasema:

> Bwana Msa alichungulia tena. Ndani mlikuwa na giza kama uwanda wa Ahera. Kimya kilikuwa kimetapakaa, kinavuja. Sauti za komba na mabundi wasiojua kama

> kumekwisha kucha zilihanikiza sauti kote. Sauti moja ilivuma kuliko zote kama ya maporomoko ya maji (Uk.25-26).

Katika dondoo hilo hapo juu, tunaona jinsi mandhari yanavyosawiriwa kwa njia za kiajabuajabu ili kuikuza taharuki kama mbinu ya kimsuko. Uajabu wa mazingira halisi yanayoonyesha makaazi ya wanyama na mapango waishimo unaboresha kuijenga itikadi ya wakaazi kuwa eneo hili ni la mizimu na kwamba kuisumbua mizimu hiyo kungewaletea balaa.

Riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi kama tulivyotaja hapo awali, zilitumia mandhari yaliyohusu majumba yasiyokamilika, mahame au maeneo ya ajabuajabu pia ili kuyapa mandhari uzito zaidi. Katika riwaya ya Mtobwa ya *Salamu Kutoka Kuzimu*, mwandishi ametumia mandhari ya jumba lililoko nje ya jiji lisilokamilika katika ujenzi wake kama eneo la uhalifu. Jumba hili lilikuwa limezungukwa na kichaka ambapo kijia cha uchochoro kilitokea hadi kwenye mitaa ya nje (uk.35). Wahalifu kadhaa kama vile Ruta Bagambe na wenzake waliishi humo. Watu wasiokuwa na makaazi pia walilala humo. Joram Kiango aliamua kujificha humo kama mkakati wa kuwafanya adui zake waamini kuwa alikuwa amekufa.

Tatu, mkakati mwingine utumiwao kuijenga taharuki ni kuwepo kwa vidokezi vinavyotajwa bila ufafanuzi. Barthes, akinukuliwa na Whitehead (1992:41-61) anafafanua misimbo mitano ya kidiskozi ambayo ni msimbo wa kiheminitiki, msimbo wa kivitendo, msimbo wa kiutamaduni, msimbo wa kiishara na msimbo wa kisemantiki. Anaeleza msimbo wa kiheminitiki kama elementi yoyote katika hadithi ambayo haijaelezwa na kwa hivyo inaweza kumzulia msomaji maswali yanayohitaji ufafanuzi. Kulingana na Barthes, kuwepo kwa vidokezi vya kimsimbo kunaficha maelezo muhimu ili kuongeza taharuki katika hadithi. Taharuki hii inatokana na hamu ya kutaka kupata ufichuzi wa maelezo hayo yaliyofichika. Hii ndio hali inayoshuhudiwa katika msuko wa hadithi nyingi za kiupelelezi ambapo mauaji hutajwa mwanzoni mwa msuko huku vidokezi kuhusu ni nani muuaji na kwa nini vikitolewa kwa njia isiyokuwa wazi kwa msomaji. Vidokezi hivi ndivyo humsaidia mpelelezi kuunganisha matukio mbalimbali kimantiki ili kutoa ufafanuzi wake wa migogoro mwishoni mwa simulizi. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo* kwa mfano, kuna vidokezi kadhaa vinavyoweza kutuelekeza kuhusu ni nani muuaji wa watu wa familia ya Mzee Jacob. Kwa mfano, msimulizi anasisitiza, kwa kurudirudia, hulka ya mhusika mmoja aliyekuwa rafiki wa kiume wa mmoja wa wanawake waliokuwa wanaishi nyumbani kwa Mzee Jacob kwa

njia ambayo inaweza kumwelekeza msomaji kukisia kuwa huenda mhusika huyo ndiye mhalifu. Kwa kutumia kidokezo cha mhusika kisicho wazi kumhusu mshukiwa, taharuki inakuzwa. Msimulizi anasema:

> Askari walipoingia, wale wanawake wakapunguza kulia, wakaanza kuwaangalia askari. Jambo lililomshangaza Inspekta Wingo ni kwamba alipoingia, wale wanawake waliokuwa wakilia, walinyamaza na kumwangalia, lakini **yule mwanaume mzee** mle chumbani hakushtuka kumwangilia wala kugutuka. uk.3

Nukuu hili linamwelekeza msomaji kwenye kidokezi kinachohusiana na mshukiwa. Ni wazi kuwa msomaji makinifu anaweza kugundua kwamba mwanaume mmoja ambaye hakushtuka wakati askari walipoingia anaweza kuwa ndiye aliwapigia polisi simu. Hamu ya wasomaji ya kutambua maana ya kidokezi hiki inaongeza taharuki inayowachochea wasomaji kusoma hadithi hadi mwishoni ili wapate jibu mwishoni mwa riwaya. Kama sheria katika uandishi wa riwaya za kiupelelezi, msimbo wa kihemenitiki (kidokezi) hutolewa mapema katika msuko wa riwaya ili msimbo huo umpe msomaji msukumo wa kuifasiri migogoro mapema. Katika riwaya hii ya *Simu ya Kifo*, msimbo wa kiheminitiki unatolewa mapema na kufikia mwishoni mwa riwaya, inagunduliwa kwamba mwanaume huyo ndiye aliyekuwa akimpigia simu Inspekta Wingo kila wakati mauaji yanapotendeka katika familia ya Mzee Jacob. Inajulikana kuwa alikuwa mpenziwe Agnes, ambaye alikuwa akimsaidia Agnes kulipiza kisasi dhidi ya mauaji ya wazazi yake.

Baadaye msimulizi anatoa kidokezi kingine ambacho ni kielekezi muhimu kumhusu ni nani mshukiwa. Inspekta Wingo anapowauliza wanawake na waombolezaji wengine pale nyumbani kwa Mzee Jacob ikiwa wamewahi kulisikia jina FAMBO, Agnes anashtuka kidogo lakini akaogopa kujibu. Mshtuko huu ni kidokezi ambacho kama mpelelezi angekifasiri vyema, angelimhoji Agnes mapema na kujua kuwa ndiye muuaji. Hata hivyo, jambo hilo linawachwa ili taharuki itande na kuupeleka msuko mbele. Katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*, kuna kidokezi mwanzoni mwa msuko kuhusu ni nani anayeweza kuwa muuaji wa mwandishi maarufu, Kitenge. Mwanamke, Machozi Rashid, inaripotiwa kuwa alikuwa mpenzi wake wa zamani lakini Kitenge naye akajitenga naye. Mwanamke huyu alikuwa amemtishia kumuua Kitenge hivi, ‘Tutakapoonana tena, ujue huo ndio utakaokuwa mwisho wa uhai wako.’ Ikiwa itathibitika kwamba mwanamke huyu ndiye muuaji wa mwandishi huyu au la ndio taharuki kuu. Taharuki hii inapata mnato zaidi inaporipotiwa kwamba siku mwandishi huyo aliyouawa kulikuwa na mtu

mwingine aliyefika ofisini mwake na kuahidi kumuua Kitenge (uk.19). Kuwepo kwa vidokezi kuhusu washukiwa wawili, wote waliokuwa wamemtishia mwandishi huyu, kunakuza taharuki zaidi. Msomaji anapogundua kuwa mmoja wa washukiwa hao ndiye mhalifu kufikia mwishoni mwa hadithi, anaridhika kwa sababu makisio na chukulizi zake zinathibitika. Jambo hili linawiana na maoni ya Cawelti (1977). Cawelti akinukuliwa na Malgren (1997:120) anasema kwamba furaha ya wasomaji katika hadithi ya kiupelelezi ni mwishoni mwa msuko wanapoona kuwa vidokezi walivyoona awali hadithini vilikuwa na maana kuu. Kulingana na Weiss (2014:4-7), utumiaji wa vidokezi vyenye maana iliyofichika na ambavyo maana yake hufichuliwa baadaye, ndiyo mbinu inayoufanya usomaji wa riwaya za kiupelelezi zionekane kama mchezo wa kimaarifa baina ya mwandishi na msomaji au baina ya msomaji na mpelelezi. Weiss anendelea kusisitiza kwamba chama cha waandishi wa riwaya za kiupelelezi wa London walisisitiza kuwa kila mwandishi anapaswa kuwapa wasomaji wake vidokezi vya kutosha na vinavyofaa ili kuwe na usawa katika mchezo huu. Baadhi ya sheria hizi zilijitokeza katika andiko la Ronald Knox, 1928 kuhusu kanuni kumi za utunzi wa riwaya za kiupelelezi.

Nne, njia nyingine ya ukuzaji wa taharuki katika riwaya za kiupelelezi ni kupitia matumizi ya majina ya wahusika kwa njia inayowavutia wasomaji. Mohamed Said Abdulla anatumia miundo tofautitofauti ya majina ya wahusika ili kufikia malengo fulani ya kiumbuji. Kwa mfano, jina la mhusika mmoja linaendelezwa kwa tahajia tofauti, jambo linalowafanya wasomaji wajiulize ikiwa mhusika wanayemsoma kwa sasa ni mhusika mwingine au ni yuleyule waliyemsoma awali. Msomaji angetaka kujua ni kwa nini mhusika fulani anarejelewa kwa njia zinazotofautiana. Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, mhusika, Amanullah anarejelewa kwa jina hilo na baadhi ya wahusika huku wahusika wengine wakimwita Emmanuel. Kwa mfano, Bwana Soarez anapojitokeza na kumpa urithi alioachiwa na babake, nduguye Bwana Soarez, anamwita Emmanuel (uk.17-18). Wahusika wengine kama vile Msa, Sichana na Mwanatenga wanamwita Amanullah (uk. 25, 76, 121). Mhusika Sichana pia anarejelewa kama Sicha na katika muktadha mwingine anaitwa Shannon. Msa akieleza namna Sicha alivyouawa na Jeejee anasema, ‘Picha ile ikawa ndio sababu ya kifo chake Sicha au Shena au Shannon-Jeejee alipomrukia akamkaba roho’. uk.105. Matumizi ya majina kwa njia kama hii yanauchangamanisha usomaji kwa kuwa msomaji analazimika kufumbua kiini cha matumizi hayo. Urejelezi huu ni sehemu ya taharuki inayosaidia kuukunjua msuko hadi mwisho. Kulingana na maelezo ya Msa, majina halisi ambayo wazazi

waliwapa watoto hawa waliopotea ni Emmanuel na Shannon (uk.78) na mabadiliko kuhusu majina haya ni matokeo ya malezi waliyopata mikononi mwa walezi wao.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* mtu anayepiga simu kwa Inspekta Wingo kuripoti mauaji ya famila ya Mzee Jacob anajiita FAMBO. Jina hili linamtatiza mpelelezi Inspekta Wingo na anapowahoji wahusika kadhaa, hawaelekei kumjua mtu anayeitwa hivyo. Jina hilo linazua taharuki kwa kuwa wasomaji wangependa kujua ni nani huyu anayepiga simu hii na kwa nini anachukua jukumu la kuripoti mauaji hayo kwa njia ya simu na kukataa kujitambulisha. Maswali haya yanajibika mwishoni mwa riwaya inapobainika kuwa FAMBO ni ufupisho wa Francis Andrew Mbozia, yule daktari mpenziwe Agnes, ambaye Wingo alikuwa amemwona mara ya kwanza nyumbani kwa Mzee Jacob alipoenda kufanya uchunguzi.

Katika riwaya ya *Njama,* kuhusiana na uchunguzi wa wizi wa silaha za wapiganiaji uhuru wa PLF, kuna shaka kumhusu tarishi, George Kiki, aliyepata kazi katika ofisi za kamati ya ukombozi ya OAU kama tarishi. Mpelelezi Willy Gamba anashuku kwamba huenda ndiye anakusanya habari kuhusu makundi ya upiganiaji uhuru na kuzipeleka kwa makaburu. Shaka hii ni kidokezi ambacho kinathibitishwa baadaye kuwa alikuwa akiwafanyia makaburu upelelezi akijifanya tarishi. Kidokezi kingine kinahusiana na mwendawazimu aliyekuwa anakaa karibu na lango la ofisi za bandari ambako silaha zilikuwa zimeibiwa. Kichaa huyu alikuwa akiombaomba pesa na Kiswahili chake kilionyesha hakuwa mtu asili wa Tanzania. Pia alizoea kusema 'SozaAfrika' kila anapopewa kitu. Uwezo wake wa kuzungumza Kiingereza na Kiswahili kisicho fasaha na kusemasema 'sozaAfrika' ni vidokezo ambavyo vinazua taharuki kuhusiana na ikiwa yeye pia ni mpelelezi wa kisiri au la. Kufikia mwishoni mwa riwaya inabainika pia kuwa alikuwa jasusi wa makaburu wa Afrika Kusini na jukumu lake lilikuwa kuripoti watu waliokuwa wakiingia katika ofisi hiyo ya bandari.

Mtobwa pia ameitumia mbinu hii ya kubadili majina ili kuikuza taharuki. Katika *Salamu Kutoka Kuzimu,* Joram Kiango anajibadili sura kwa kujivisha ngozi ya kizungu ili asitambulikane na adui zake. Pia anabadili jina na kujiita Dancan (uk.121). Kujibadilisha huku kunamsaidia kuisambaratisha mipango ya mhalifu, Proper ya kuwaua marais waliokuwa wakihudhuria mkutano wao jijini Arusha.

Tano, majina ya anwani za riwaya pia ni nyenzo nyingine inayokuza taharuki. Baadhi ya riwaya za kiupelelezi zina majina yanayoibua taharuki kutokana na maswali yanayoibuliwa na anwani

hizo. Mtobwa kwa mfano, anatumia mtindo huu mno. Anwani *Salamu Kutoka Kuzimu*, kwa mfano, inaibua swali la je, watu huenda kuzimuni na kurudi? Na ni nani aliyeenda huko? Anwani, *Tutarudi na Roho Zetu?* inaashiria hatari na hofu na kwa njia hii kuongeza taharuki. Nayo anwani *Simu ya Kifo*, pia ni anwani yenye taharuki kuhusu ni nani anayepiga simu na ni vipi inahusu kifo.

Mbinu nyingine ya ujenzi wa taharuki inahusu kuwepo kwa vifaa vya kisiri ambavyo matumizi yake hayajulikani, pamoja na maandishi ya kigeni. Taharuki hii inatokana na kweli kwamba mwenye chombo hicho au maandishi hayo ndiye tu mwenye ujuzi kuhusu matumizi yake. Kwa hivyo, msomaji pia anapania kupata ujuzi kama huo ili aweze kufumbua migogoro iliyopo riwayani. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, na riwaya nyingine za Mtobwa, kuna vifaa vya kieletroniki ambavyo ni wapelelezi tu ama wahalifu wanaojua kuvitumia. Matumizi ya vifaa vya kisiri pia yanapatikana katika *Uchu.* Joram Kiango katika *Tutarudi na Roho Zetu* anapoingia chumbani mwa Chonde, jasusi wa kutoka Afrika Kusini, alipata mifuko ya kisiri katika begi lake na ndani yake kulikuwa na vifaa aina aina na maandishi ya kimafumbo (uk.27) pamoja na kijaluba kimoja kilichofungwa kwa kufuli. Hali hii inazidisha taharuki si kwa msomaji tu bali pia kwa mpelelezi Joram Kiango kwani ana hamu ya kujua maana ya maandishi hayo pamoja na matumizi ya vifaa hivyo. Pia mpelelezi anashangaa vipi ataweza kufunua kijaluba hicho.

Njia nyingine inayosababisha taharuki ni kuwepo kwa msururu wa matukio hasa pale mpangilio wa matukio katika msuko unaharakishwa kufuatia ujio wa tukio lingine kabla ya suluhisho la tukio la kwanza kujulikana. Hali hii inamzidishia msomaji taharuki ya kutaka kujua ni tukio lipi litakalochunguzwa kwanza na mpelelezi na vipi, kati ya matukio kadhaa yanayotendeka kwa haraka. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* kwa mfano, tukio la muaji ya Mzee Jacob linafuatwa na tukio lingine la mauaji ya mkewe kabla ya mpelelezi Far Katy Wingo hajatatua tukio la kwanza. Msururu wa mauaji unaendelea hadi familia ya Mzee Jacob inamalizwa isipokuwa mmoja.

Kando na njia hii, matukio mengine ya kitaharuki yanahusu vitisho kwa mpelelezi vinavyotolewa na mhalifu. Msomaji anayesoma kuhusu vitisho hivyo anajiuliza ikiwa mpelelezi atauawa, atanaswa au la, na ikiwa atauawa, ni nini kitafanyika kwa wahalifu. Mara nyingine msimulizi anaweza kumtambulisha mpelelezi au mhalifu na kumfanya kupotea hadithini kwa muda ili kuzidisha taharuki. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu,* mpelelezi anapotea kwa muda, na kujificha katika gofu la jumba fulani jijini. Adui zake wanafikiri kuwa alikufia katika mlipuko wa bomu lililokuwa limetegwa katika jumba hilo. Wasomaji pia wanachukulia hivyo hadi

wanapofahamishwa baadaye kuwa mpelelezi Joram Kiango yuko lakini anatembea kwa kujigeuza sura. Katika riwaya ya *Hofu* makaburu wa Afrika kusini wanaamua kuanzisha utawala wa hofu katika mataifa ya msitari wa mbele na kuivamia Namibia ili kuifanya koloni lao. Ili kufanikisha hofu kutanda, makaburu wanafadhili makundi yanayopinga serikali kama vile MNR ili izue hofu Msumbiji, kundi la UNITA nalo lizue hofu Angola huku kundi la LLA likipewa jukumu la kusambaratisha serikali Lesotho na Botswana. Makundi haya yanatoa vitisho katika nchi kadhaa zinazounga mkono ukombozi wa Afrika Kusini huku nalo shirika la upelelezi la Afrika Kusini likiamua kuwakomesha Waafrika weusi waliomo ndani ya Afrika Kusini. Vitisho hivi vinazua taharuki kuhusiana nan i nchi ipi itakayopigwa kwanza, lini, sehemu ipi ya nchi na vipi.

5.2.5 Sadfa na Msuko

Ni utokezaji wa matukio mawili au zaidi bila kuwa na uhusiano wa kiusababishi. Wamitila (2003:186) anaeleza dhana hii kama matukio kwa wakati mmoja na aghalabu kwa namna inayoshangaza au inayoashiria bahati. Anasisitiza kwamba sadfa ni mbinu ya kiutanzu katika riwaya za kiupelelezi na za kiuhalifu. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, mbinu hii imetumika sana hususan katika riwaya za Abdulla na zile za Mtobwa. Katika *Salamu Kutoka Kuzimu* kwa mfano, Joram anajificha katika jumba lililoachwa bila kukamilishwa ili asipatikane na adui zake. Kisadfa, adui hao wanagundua kuwa Joram anaishi humo na kuamua kulitega bomu humo ili limuue. Msimulizi wa hadithi hii hasemi ni vipi magaidi walivyojua kuwa anaishi humo. Kwa hivyo, sadfa hii inauharakisha msuko wa hadithi kwa kuwa inayaacha maelezo kama hayo. Katika kisa hiki, sadfa nyingine inatukia na ambayo inamuokoa Joram kutokana na hatari ya bomu hilo. Kijana mzururaji, Ruta Bagamba, alikuwa anaishi katika jumba hili na alichukulia kuwa ni yeye tu aliyeishi humo na ndiye aliyemwona mtegaji bomu. Kutokana na hamu ya kutaka kujua nini kilichofichwa, Ruta Bagamba anaenda kuvuta nyaya za bomu hilo na mlipuko uliofuatia ulimfanya apae juu na viungo vya mwili kutawanyika. Sadfa hii ina mchango mkubwa katika kumwokoa Joram Kiango kwani adui zake walifikiria kuwa ndiye aliyekuwa ameuawa. Kupitia njia hii, Joram alipata nafasi ya kuwahadaa adui zake kwa muda mrefu na katika kipindi hicho, aliendeleza upelelezi wake kisiri ili kuisambaratisha mipango ya adui. Katika mkasa huu, sadfa nyingine inajitokeza kupitia mhusika Unono. Unono alikuwa amelitembelea jumba hilo, akimtafuta mwanaume wa kumkimu na ndiye aliyemtoa Joram katika vifusi vya jengo hilo na kumficha nyumbani kwake. Kupitia sadfa hii Joram hakukutwa katika jumba hilo na adui zake.

Kwa hivyo, kuwepo kwa Unono katika eneo la mkasa ni sadfa pia. Sadfa hii inatumika kuukuza msuko kwa kuwa inamsaidi mwandishi kukwepa maelezo yanayohusu ni vipi hakukutwa katika eneo la mkasa.

Akichangia kuhusu muundo wa msuko na nafasi ya sadfa katika kuukuza msuko, Dannenberg (2017:89) anaeleza kuwa hadithi yoyote yenye kisababishi na tokeo katika msuko wake haihitaji matumizi ya sadfa. Hata hivyo, anakiri kuwa taktibani simulizi zote huwa na angalau tukio moja la kisadfa. Kwa mfano, katika hadithi za kihalifu na za kiupelelezi, anauliza ni vipi mpelelezi na mhalifu hukutana. Anakiri kuwa aghalabu mhalifu na mpelelezi au afisa wa polisi hukutana kisadfa uso kwa uso. Katika riwaya za Mtobwa na zile za Musiba, wahalifu aghalabu wanafumaniwa kisadfa tu. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* mpelelezi Joram Kiango na jasusi wa kisiri, Chonde, kutoka Afrika Kusini wanakutana katika baa kisadfa na kuanza maongezi ya kuchunguzana na kutishana. Sadfa hii inampa Joram nafasi ya kumjua adui yake zaidi. Kisadfa wanakutana tena katika hoteli ya New Africa, chumba namba 104. Katika sadfa hii Joram anaingia chumba hiki cha adui yake akitumia funguo maalum na kufanikiwa kupata habari muhimu kumhusu Chonde, kama vile maandishi ya kiupelelezi na silaha kadhaa. Kisadfa, Chonde anarudi na kumpata Joram katika chumba hicho. Joram alipofumaniwa, kwa mshangao, aliuliza, ‘’Tuseme nimefumaniwa?’ Naye Chonde akamjibu, ‘Umefumaniwa. Na una bahati mbaya kuwa umefumaniwa na kifo. Binadamu hachezi na mimi na akaendelea kuishi’’.uk.28. Hii ni sadfa ambayo inaweza kusemwa kuwa imeletwa na bahati tu. Laurence (2017) anaeleza kwamba kando na kuwa na sadfa inayojitokeza kibahati tu, kuna aina za sadfa zinazosababishwa na matukio ya kiasilia na yale ya kijaala. Anasema kuwa katika kazi za kifasihi, sadfa hutokana na mambo kadhaa kama vile ukosefu wa motisha kwa upande wa mhusika ambapo vitendo vyake havichochewi na sababu yoyote. Pia inawezekana ikawa mwandishi ameshindwa kudhibiti mapengo yote katika msuko. Anaendelea kufafanua kuwa nafasi ya sadfa katika kazi za kinathari inachukuliwa na mbinu ya *Deus ex Machina*[7] katika tamthilia. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu?* (uk *34-35)* tunapata mfano wa sadfa ya kibahati, yaani ambayo imeletwa na kitendo kisicho na motisha. Wakati Kombora na askari wenzake wanapotaka kumlazimisha Joram kuwasaidia katika uchunguzi wao, wanaamua kumwandikia barua ya kumtisha. Wanapoipeleka barua hiyo katika chumba chake, kisadfa wanakuta kuwa chumba kiwazi. Sadfa hii ya kibahati inawawezesha

[7] Deus ex Machina ni njia ya utatuzi wa mgogoro katika tungo za kidrama, ambapo Mungu huteremshwa ili kumwokoa shujaa. Ni mbinu iliyotumika katika tungo za kidrama za Wayunani.

kuiacha barua hiyo juu ya meza. Hatuoni sababu ya Joram kukiacha chumba chake bila kufungwa. Kwa sababu hii, kitendo cha Joram hakina motisha.

Dannenberg (2018:89) akijadili muundo wa tukio la kisadfa, anaeleza kwamba elementi za sadfa mbili kuu ni mahali na wakati, kwamba sadfa inahusu utukiaji wa matukio mawili au zaidi wakati mmoja bila usababishi au utokeaji wa matukio hayo mahali palepale bila kuwa na uhusiano wa kiusababishi. Katika mfano wa hapo juu, Kombora na askari wenzake wanapopeleka barua ya kumtisha Joram ili awasaidie katika upelelezi, wanapoingia katika chumba chake kisadfa wanakuta barua nyingine ya vitisho juu ya meza. Barua hii ni ya adui wa nchi yake wakimuonya dhidi ya kujiingiza katika upelelezi. Barua hii pia inamjulisha kuwa mpenzi wake ametekwa nyara. Kwa hivyo, tukio la Kombora na askari wake la kuipeleka barua katika chumba cha Joram na tukio la maadui kuileta barua yao ya vitisho katika chumba chake, ni matukio mawili yanayotendeka mahali palepale.

Sadfa ya kiwakati inajitokeza pia katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa* wakati Bibie Shali anapoanzia kumtafuta mpelelezi wa kisiri ili amsaidie kuwasaka watoto wake wawili waliopotea. Bibie Shali anasema, 'Tutampata nani wa kututafutia. Hapa si kama Ulaya. Kama tutakwenda kwa mpelelezi wa siri tumtume kufanya kazi hii.' Wakati anapomaliza kutaja haya tu ndio Mwanatenga anapokumbuka kuwa kuna mpelelezi wa siri anayeitwa Msa na wanaamua kumwita aje kuwasaidia. Dannenberg (2008:91) anafafanua kwamba ujenzi wa sadfa huhusisha hatua tatu:

(a)Kuwepo kwa uhusiano wa awali/kihistoria
(b) Mkutano wa kisadfa-mtagusano wa hali mbili au watu wawili au matukio mawili
(c) Mchakato wa kiurazini au kiakili unaohusu ugunduzi au utambuaji wa pande husika hususan wahusika wa sadfa hiyo. Matukio yaliyomo baina ya (a) na (b) ndiyo yenye nguvu dhabiti kuhusu muundo wa suala la kisadfa. Hata hivyo, kiunzi (a) ndicho muhimu zaidi kwa kuwa pasi na historia au uhusiano wa awali, sehemu ya ugunduzi na utambuaji, '(c) inayokamilisha sadfa hii haiwezi kuwepo. Pia sehemu ya (a) haizalishi sehemu (b) moja kwa moja bali ni lazima pawe na utengano/uajinabishaji kabla ya kukutana kisadfa. Mhakiki huyu anashikilia kuwa mchakato wa ugunduzi na utambuzi unakuwa na taathira kubwa ya kirazini na kihisia ikiwa utahusishwa na mapatano ya kifamilia (uk.94). Hii inatokana na ukweli kwamba mahusiano ya awali hutiliwa nguvu na mtagusano wa kimapenzi, kindoa au kirafiki au hata uhusiano wa kiadui uliopo baina ya wahusika kabla ya kukutana kwao kisadfa. Kwa kuwa riwaya za kiupelelezi zinahusu kufanyika

kwa tendo la uhalifu na uchunguzi wa uhalifu huo, kukutana kwa mhalifu na mpelelezi kunazua mhemko kihisia na kusababisha taharuki kuu. Dannenberg (keshatajwa) anafafanua kwamba kwa kuwa familia ndio msingi wa mahusiano ya kibinadamu, kukutana na kupatana kisadfa kwa watu wa familia waliokuwa wametengana hapo awali, ndiko kunakoibua sadfa yenye hisia nzito zaidi. Motif ya kupatana na kuungana kwa familia kisadfa imetumika mno katika kazi za kifasihi hususan tamthilia za Kimagharibi kama vile *Oedepus Rex* ya Sophocles na komedia za Shakespeare kama vile *Twelfth Night.*

Katika riwaya ya *Mwana wa Yungi Hulewa*, Bwana Soarez na Bibie Shali anawatafuta watoto wao waliopotea, Emmanuel na Shannon. Wanamtafuta Msa ili kuwasaidia kwa kuwa walezi wao, Sikudhani Binti Abdalla na Twajuana Binti Abdalla walikuwa wamewatenganisha ili kuchukua urithi wao. Kisadfa, wazazi hawa wanawakuta watoto hao katika hali tatanishi. Soarez anafika wakati, Shannon/ Shena akiwa ameuawa na mpenzi wake, Jeejee, naye Emmanuel akiwa jela kwa tuhuma za mauaji ya Jeejee. Kisadfa, wazazi hawa wanagundua kuwa katika mpito wa wakati waliotengana na watoto wao, hata majina yao yalikuwa yamebadilishwa na walezi hao, Emmanuel akawa Amanullah na Shannon kuwa Sichana. Sadfa hii inaashiria usababishi wa kijaala. Wazazi wangetaka kuwapata watoto wao lakini wanamkuta mmoja akiwa maiti. Msa anamwaambia Soarez, ‘Yule pale mwanao mwingine Shena unayemtafuta lakini bahati mbaya, Shena amekwisha kufa’ (Uk.76). Mwandishi ameitumia sadfa hii ili kujenga upeo wa msuko wake. Kwa kumleta Bwana Soarez na kumkuta mtoto wake mmoja akiwa amekufa, kunamwezesha msimulizi kutoa taarifa, kupitia Msa, kuhusu jinsi Sichana alivyouawa, kueleza muuaji ni nani na kwa nini anauawa. Sadfa hii inasaidia kuuboresha ushahidi kuhusu ni nani muuaji kando na kuboresha dhamira ya malezi. Mwandishi anawakosoa wazazi ambao hutengana na watoto wao na kisha kuwasaka miaka mingi baadaye.

Katika *Duniani Kuna Watu*, watu wengi wanaohusishwa na familia ya Hakimu Marjani wanafahamu uhusiano wao baadaye kisadfa. Kwa mfano, Saleh ni mwajiriwa wa Hakimu Marjani na katika harakati za kutekeleza kazi yake anapendana na bintiye Hakimu Marjani, Selume na kuoana. Kisadfa inatukia kuwa Saleh ni mtoto wa Hakimu aliyepotea akiwa mchanga aliyemzaa na mwanamke mwingine, Mariam Mkembe. Habari hizi zinafichuliwa na Msa baadaye. Sadfa hii ni changamano kwa kuwa inafumbata masuala mengine ya kisadfa ndani yake. Kwanza, inaripotiwa kwamba mamake Saleh alikuwa ameenda naye Bagamoyo akiwa mtoto mdogo na

jahazi walilokuwa wanalitumia likapata ajali huku watu wengi wakipotelea majini. Kisadfa, Saleh aliokolewa, akapelekwa hospitalini na baadaye kwenye hifadhi ya mayatima. Alisomea udereva na tena katika sadfa yenye uzito zaidi akapata kazi kwa Hakimu Marjani, anayetangazwa na Msa kuwa ni babake. Pia Saleh anakutana na mamake kisadfa wakati Msa anapowaita watu kadhaa (uk.109) ili awaeleze matokeo ya upelelezi wake baada ya miaka mingi. Uzito wa kihisia anaozungumzia Dannenberg kuhusiana na muundo wa sadfa, unajitokeza tunapoona Saleh na mamake wakikumbatiana kwa karibu robo saa. Kutokana na hisia za furaha na mshangao wa kukutana huku, mamake Saleh anasema:

> ‘Ulikuwa wapi, baba’ngu we’, miaka yote hii na sasa Mungu kakurudisha tena mikononi mwangu, mama yako. Alhamdullilahi. Vilima tu ndo’ havikutani, lakini binadamu madhali wahai, ni lazima kukutana ( Uk 110).

Sadfa hii ya ukutanisho wa familia ya Hakimu Marjani inaibua mtafaruku mwingine kwa kufichua kuwa Kasim si mtoto halali wa Hakimu Marjani bali ni mtoto wa kuokotwa. Ugunduzi huu unamfanya Kasim kuomba radhi kwa makosa yake ya hapo awali ya kumvamia Hakimu Marjani na kwa kung’ang’ania urithi usiokuwa wake.

5.2.6 Vyombo vya Habari na Ukuzaji Msuko

Vyombo vya habari vinatoa habari muhimu ambazo zinachangia ujenzi wa msuko katika riwaya za kiupelelezi. Baadhi ya habari zinazomfikia msomaji hazitokani na msimulizi moja kwa moja bali msomaji anazipata kupitia matangazo ya vyombo vya habari kama vile magazeti, televisheni, radio na hata simu. Kwa kutumia njia hii, mwandishi anafanikiwa kuyajaza mapengo ya kisimulizi ambayo yangeachwa katika msuko. Baadhi ya taarifa za vyombo vya habari zinamsaidia msimulizi kuthibitisha jambo fulani au kutumiwa na mpelelezi kumpa mwelekeo na ushahidi wa mambo ayasemayo. Kwa mfano, katika baadhi ya riwaya za Mohamed Said Abdulla, Msa anatumia taarifa za magazeti kama ushahidi wa chanzo cha habari anazotoa. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, wakati Msa anaporudi kutoka Pemba kuja Unguja, Spekta Seif anampa gazeti la *Zanzibari Kila Wiki*, ili Msa apate habari ya kushangaza kuhusu namna Hakimu Marjani alivyouza mali yake yote hivi karibuni na jinsi habari hiyo inavyoingiliana na kifo chake Hakimu Marjani. Habari za gazeti zinaanza hivi:

> Tajiri mkubwa kabisa hapa Zanzibar Bw. Hakimu Marjani amefariki dunia tarehe 10 Agosti, 1961 katika umri wa miaka sitini na tano, naamehakifu watoto wawili,

> mwanamume, Kasim Hakimu Marjani, mwenye umri wa miaka thelathini na miwili, na mwanamke, Selume Hakimu Marjani, mwenye umri wa miaka ishirini na mitano. Mali yake, Manchali tatu zilizosafiri pwani yote ya Afrika Mashariki, aliziuza zote hivi karibuni. Jahazi nne, zilizosafiri kutoka hapa, Aden, Makati mpaka Bombay, kaziuza zote…(uk.45-46)

Gazeti hili linabeba habari nyingi ambazo ikiwa zingeachwa, msuko wa riwaya hii ungekuwa na mapengo mengi ya kisimulizi ambayo yangemtatiza msomaji mno. Usimulizi wa chanzo cha habari anazozitoa mpelelezi pia haungekuwa na ushawishi mkubwa ikiwa zingetolewa kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza au ya tatu. Pia habari hizi zinaaminika zaidi kwa kuwa zimetolewa na shirika la habari. Aidha, uwasilishaji wa matukio kwa njia hii unamsaidia msimulizi kuharakisha usimulizi wake na kuondoa ukinaifu wa kisimulizi. Kwa hivyo, msuko unapelekwa mbele kupitia usomaji na uchambuzi wa habari hizi baina ya wahusika Msa na Spekta Seif. Taarifa hii ya gazeti inaathiri matukio mengine katika msuko kwa kuwa picha zilizomo katika gazeti hili zinatumiwa baadaye na mpelelezi Msa kama chanzo cha maelezo yake kuhusu usuli wa familia ya Hakimu Marjani mwishoni mwa riwaya. Katika maelezo yake, Msa anawaonyesha waliohudhuria picha za Hakimu Marjani, Kasim, Saleh na Selume na kuwathibitishia kwamba Kasim anatofautiana na wengine kwa hivyo, yeye si mtoto asili wa Hakimu Marjani. Pia anawaelezea ni kwa nini gazeti hilo linamrejelea Hakimu Marjani kama Abdulla Salum; kwamba alipomuoa Mariam Mkembe alitumia jina Abdulla Salum ili kuhifadhi siri kwa kuwa alikuwa na mke wa awali, Shena (Uk.82). Kwa hivyo, kupitia gazeti hili, msomaji anapata uelewa wa matukio mengine ya kihistoria kama vile habari za ndoa ya Hakimu Marjani na uhusiano wake na Mariam Mkembe.

Katika riwaya za kiupelelezi za Mtobwa, mchango wa habari za magazeti katika msuko pia ni mkubwa. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu,* kwa kuwa dhamira kuu ni mahusiano ya kimataifa hususan baina ya Tanzania na mataifa ya Kusini mwa Afrika, mwanzoni mwa msuko, mwandishi anaweka msingi wa hali tatanishi iliyokuwepo baina ya mataifa haya. Anaonyesha jinsi Afrika Kusini ilivyoyashambulia mataifa yaliyokuwa yakiwasaidia watu weusi nchini humo kupigania uhuru na kuumaliza ubaguzi wa rangi. Mwandishi anazitumia habari za magazeti kadhaa kuisawiri hali hiyo. Msimulizi anasema kwamba magazeti kote duniani yalibeba habari za kusikitisha. Kwa mfano, gazeti moja liliandika:

> Watu mia nne wamefariki, mia sita wamejeruhiwa na maelfu kuponea chupuchupu katika ajali ambayo si ya kawaida huko Lagos, Naijeria. Moto umelipuka na kubomoa uwanja mzima wa michezo wakati wa shindano baina ya timu ya nchi hiyo na Zaire. Wachunguzi wa mambo wanahisi kuwa utawala wa Afrika Kusini unahusika.(uk.8)

Gazeti lingine kutoka Harare nalo linaripoti, 'Maghala manane ya serikali yameungua moto kwa pamoja, ingawa yalikuwa katika wilaya tofautitofauti za nchi. Kuna mashaka kwamba tukio hili linahusiana na tukio la Naijeria' Gazeti lingine nalo liliripoti, 'Leo asubuhi Tanzania imepatwa na pigo zito. Jengo la benki kuu ambalo lilikuwa limekamilika baada ya marekebisho ya ule moto wa awali limeungua tena. Chanzo cha moto huo hakijafahamika.' Habari hizi zinachochea mkunjuko wa ploti kwa kuwa ndizo zinauweka msingi wa upelelezi unaotawala riwaya nzima. Ongezeko la mikasa hii katika nchi kadhaa linawazindua polisi kuanza kuchunguza wanaoendeleza uharibifu huo na wanaposhindwa wanamwalika mpelelezi wa kibinafsi, Joram Kiango kuwasaidia. Inabainika kufikia mwishoni mwa msuko kuwa Afrika Kusini ndio iliyokuwa ikiendeleza uharibifu huo dhidi ya nchi zilizokuwa za msitari wa mbele katika ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika. Katika riwaya ya *Tutarudi na Roho Zetu*, mwandishi hajihusishi na suala la uhusiano wa kimataifa tu bali pia, uhusiano wa nchi za Kiafrika na mataifa ya kikoloni yaliyozitawala. Nchi za kikoloni zinaonyeshwa kama zinazoendeleza ukoloni mamboleo. Baada ya Joram Kiango kuziiba pesa za kigeni na kuzitumia kuzuru miji kadhaa akiwasaka maadui wa nchi yake, magazeti ya Ulaya yaliandika habari hiyo, kwa njia zilizoashiria misimamo yao kuzihusu nchi za Kiafrika. Gazeti moja la Uingereza liliandika:

> Ndivyo walivyo Waafrika. Kati yao hakuna aliye mwaminifu… Kila wanapofanya madhambi huko kwao hukimbilia huku. London imejaa watu weusi wengi ambao wanaishi wanavyotaka baada ya kufanya maovu-au mema ambayo yanaonekana maovu huko makwao. Uingereza haiwezi kustahimili huyu Joram Kiango.(uk.73-74)

Taarifa za gazeti hili zinaashiria mitazamo hasi ya mataifa ya Kimagharibi kuyahusu mataifa ya Kiafrika. Gazeti linawasilisha habari zinazoshabihiana na maoni ya Said (1977:xv) katika *Orientalism* kuhusu jinsi Wazungu wanavyowaona Waafrika na Waarab kama watu wanyonge, walionyuma kimaendeleo na waliokosa maadili. Kuhusiana na wizi huo wa pesa za kigeni, nacho kituo kimoja cha televisheni kilitangaza, 'Tanzania isipate msaada wowote wa kimataifa bila ya

pesa hizo kupatikana. Tunaamini kilichofanyika ni njama tu, baina ya Joram na viongozi wa serikali wake.' uk.74.

Kwa kuwa riwaya za Mtobwa na zile za Musiba zinachunguza uhalifu na upelelezi katika kiwango cha kimataifa, inakuwa bora kwa mwandishi kutoa taarifa kuwahusu majasusi na wahalifu wanaofanya vitendo vyao nje ya nchi. Njia inayoaminika katika utoaji wa habari hizo ni vyombo vya habari. Utoaji wa habari hizo unapanua msuko wa hadithi. Ikiwa usimulizi wa kawaida ungetumika badala ya vyombo vya habari katika kutoa taarifa zilizo nje ya nchi, msomaji angebaki na maswali ya ni wapi msimulizi anapopata taarifa za matukio ya Harare, Lagos, London na miji mingine mikuu. Joram Kiango kwa mfano, anapata taarifa za jinsi wizi wake unavyotangazwa kupitia vyombo vya habari akiwa London. Katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena,* Joram anazipata habari za mauaji ya mwandishi mashuhuri kupitia usomaji wa gazeti. Anapopata habari hizi anaamua kuchunguza kesi hiyo ili kumpata muuaji. Msimulizi anasema:

> Hahari mbaya husafiri haraka zaidi ya habari njema. Hii ya mauaji ilienea mara mbili zaidi. Habari zilitolewa na magazeti chini ya vichwa mbalimbali. Gazeti moja liliandika, 'MUUAJI WA HATARI AZUKA JININI' na gazeti lingine likaandika, 'THE MURDERER STILL AT LARGE'.(uk.41).

Msimulizi anatumia njia hii ya mawasiliano ili kurahisisha utoaji wa masimulizi marefu kuhusu muktadha wa tukio. Kwa njia hiyo, kando na kuzua taharuki kwa wasomaji, habari za vyombo vya habari zinapunguza ukinaifu wa kisimulizi na kuongeza uaminikaji wa habari zitolewazo.

Riwaya za Mtobwa na Musiba zinadhihirisha utumikaji wa vyombo vingine vya habari na mawasiliano kwa kuwa riwaya hizo zimejitokeza wakati wa maendeleo makuu ya kiteknolojia. Baadhi ya vyombo hivyo huenda vikawa vya kufikirika tu au kuzalika kutokana na ubunifu wa mwandishi tu. Hata hivyo, kwa kuwa teknolojia inakua kwa kasi, inaweza kuwa vifaa hivyo vya mawasiliano vipo. Katika *Tutarudi na Roho Zetu* (1984:91), msimulizi anasema kuwa majasusi walisikiliza taarifa kutoka kwa mtambo bila kusema ni mtambo wa aina gani. Msimulizi anasema, 'Jasusi mmoja alikuwa anawaarifu kwa chombo maalum juu ya msafara wake na matukio ya shughuli zake'. Uk.97.

Simu kama kifaa cha kisasa cha mawasiliano, imetumika kama chanzo cha taarifa muhimu zinazoathiri mfuatano wa matukio katika matukio. Katika *Simu ya Kifo,* kifaa kinachotoa taarifa

muhimu kuhusu mauaji kila mara yanapofanyika, ni simu. Katika mwanzo wa msuko wa riwaya hii, simu inapigwa kwa Inspekta Wingo kuripoti mauaji ya Mzee Jacob. Kwa hivyo, taarifa hii ndio chanzo cha matukio yanayofuata ya uchunguzi, na kwa njia hiyo kukuza msuko. Katika *Najisikia Kuua Tena*, taarifa za simu pia zinakuwa muhimu katika kuukuza msuko kwa kuwa msuko unaanza kwa simu inayopigwa kwa mkuu wa polisi, Inspekta Kombora. Inaweka msingi wa uchunguzi unaofuata.

Radio pia inatoa taarifa zinazokuwa nguzo kuu ya msuko. Katika *Kisima Cha Giningi*, habari muhimu kuhusu ni nini kilifanyika kwa wahalifu, Ali Makame na mwenzake, Hamadi Mshenga zinajulikana kupitia tangazo la radio, Sauti ya Unguja. Kufikia mwishoni mwa riwaya inaripotiwa tu kwamba walitorokea ziwani lakini hairithishi hamu ya msomaji kwani adhabu waliyopata haitajwi. Kukidhia haja hii, mwandishi anatoa maelezo kupitia tangazo la radio badala ya usimulizi wa kawaida. Tangazo linasema kuwa maiti ya Ali Makame iliokotwa hapo ufukoni ikiwa imechokolewa macho na samaki. Naye Mshenga Hamadi wa Kidoti alinusurika kifo na kurudi kwao. Tangazo hili linayajibu maswali muhimu kuhusiana na taharuki iliyoletwa na pengo kuhusu ni vipi walitoroka na kwa nini muuaji kama Ali Makame hapewi adhabu. Kwa njia hii, tangazo hili linashughulikia mahitaji ya wasomaji na hata ya jamii pana. Utolewaji wa adhabu ni motif muhimu katika riwaya za kiupelelezi kando na kuwa sheria moja kati sheria kumi za uandishi wa riwaya ya kiupelelezi zilizoasisiwa na Ronald Knox (1929). Baada ya Msa kusikiliza hili, alifurahishwa na kifo cha Ali na kumwambia Spekta Seif, ‘Mhini na mhiniwa njia yao ni moja.’ uk.90. Katika riwaya ya Njama, matangazo ya radio yanachukua nafasi kubwa kufikia mwishoni mwa riwaya kwa kuwa matangazo hayo ndiyo yanayoukamilisha msuko wa riwaya hii. Baada ya mapambano baina ya Willy Gamba, Veronika Amadu na Sherriff kwa upande mmoja na majasusi wa makaburu kwa upande mwingine kuhusu ukombozi wa silaha zilizoibiwa bandarini, radio inatangaza kuwa Veronika aliuawa na kwamba mwili wake utasafirishwa hadi Freetown. Matangazo hayo pia yanafichua hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na serikali katika juhudi za ukombozi. Tangazo hili linaenda hivi:

> Ifuatayo ni taarifa kutoka Radio Tanzania, Dar es Salaam, Msomaji ni Gedfrey Chalamila. Kwanza habari kwa ufupi. Majasusi wawili walioshiriki katika njama za kuiba silaha za chama cha PLF bandarini wamekamatwa. Mwili wa msichana mwanamapinduzi Veronika Amadu aliyeuawa katika harakati za kufichua njama za wizi wa silaha utasafirishwa kwenda Freetown, Siera Leone. Serikali imetaifisha

> makampuni yote yaliyokuwa chini ya kampuni la Kibepari la Euro-Afro. Wakati huo huo kamati ya ukombozi ya OAU imelaani njama hizi za makaburu na kusema kuwa ni lazima makaburu wajue kuwa Afrika iko macho na haiku tayaru kuchezewa. (uk.110).

Kama inavyoonekana katika nukuu hili, tangazo la redio hii linabeba taarifa nyingi na muhimu katika ukuzaji wa msuko wa riwaya hii. Hii ni kwa sababu msimulizi anajitenga na usimuliaji na kuwacha taarifa hizo zitolewe kupitia chombo hiki. Kama tangazo lisingekuwapo hadithi ingemwacha msomaji katika taharuki kuu kuhusu mazishi ya Veronika, kuhusu makampuni ya makaburu ambayo yanavuruga amani nchini Tanzania miongoni mwa maswali mengine.

Katika riwaya za Godfrey Levi kama vile *Fedheha ya Fedha*, msimulizi anazipata habari nyingi kuhusu wahalifu na uhalifu kupitia matangazo ya radio za polisi. Kwa mfano katika *Fedheha ya Fedha,* matangazo ya radio za polisi yanafanikisha uchunguzi kwa kuwaelekeza wachunguzi waliko wahalifu. Kwa mfano, Sajini Boke akiwasaka wezi, Mbogo, Bambola na karani wa benki, Twalib anazingatia taarifa zinazotumwa kutoka makao makuu ya polisi. Msimulizi anasema:

> Dakika mbili baadaye, Sajini Boke alijibiwa kwa radio kutoka makao makuu. Radio hiyo ilimjulisha kisiri jinsi polisi walivyochukua hatua ya haraka kwa kumpeleleza na kumweka nguvuni yule karani wa benki, Twalib aliyehojiwa vikali na kuonyesha dalili za kukiri kuwa alifahamu mipango ya hila kuhusu unyang'anyi wa benki (uk.64-65).

Kulingana na dondoo hili, taaria inayotolewa na radio inamfaa msomaji pakubwa katika kuunga kuuelewa msuko zaidi bila kusimuliwa na msimulizi. Taarifa hizi kwa mfano zinamjulisha msomaji ni vipi wahalifu walivyopatikana.

### 5.2.7 Barua na Maandishi Mengine katika Msuko

Barua ni njia ya mawasiliano baina ya watu wawili inayohusu udhihirishaji wa hisia, matukio au majadiliano. Denkova (2015:2) anaeleza kwamba sifa muhimu katika matumizi ya barua katika fasihi ni uwezo wake wa kiusemezano kwa kuwa, msomaji wa barua hiyo anatakiwa kutoa jibu. Mwandikiwa wa barua anaposhiriki katika kujibu maswala ya barua aliyoipokea, naye anashiriki katika ukuzaji wa msuko. Anafafanua kuwa mwandishi wa barua ya kibunilizi pia huwa na mpokeaji wa kidhahania (msomaji) kama ilivyo katika misimbo yote ya kimawasiliano.

Mtindo wa uandishi wa riwaya za kibarua ulivuma sana katika karne ya kumi na nane ambapo baadhi ya watunzi waliandika riwaya zao kwa mtindo wa barua. Katika mtindo huu kuliibuka aina tatu za riwaya ya kibarua.: (a) riwaya ya kimonolojia (riwaya zilizohusu barua za mwandishi mmoja), (b) riwaya ya kidayalojia (Riwaya zilizohusu ubadilishanaji wa barua baina ya waandishi wawili) na (c) riwaya za kipolilojia (inayohusu barua zilizoandikwa na zaidi ya watunzi wawili).

Matumizi ya barua katika riwaya yana dhima kadhaa. Kwanza, kiwango cha uaminikaji baina ya mwandishi na msomaji kinaimarika. Hali hii hutegemea ikiwa barua husika ni rasmi au ya kirafiki. Denkova (keshatajwa) anasisitiza kuwa barua baina ya mwandishi na mpokeaji huonyesha umbali au ukaribu wa uhusiano wao. Pili, barua ina dhima ya kusababisha athari kuhusu mtazamo wa msomaji kuhusiana na masuala kadhaa kama vile uhusika na dhamira. Tatu, humjulisha msomaji kuhusu matukio makuu ya kimsuko zikimwelekeza msomaji katika tatizo halisi lililopo. Nne, kufumbata muktadha na uhalisia wa hali iliyopo. Mtindo wa kuandika riwaya kwa njia ya kibarua umepitwa na wakati kutokana na mabadiliko ya ukuaji wa kiteknolojia ya mawasiliano ambayo yalileta aina nyingine za kupitisha jumbe kama vile simu na barua pepe. Wamitila (2008:123) anaeleza kuwa fasihi ya Kiswahili haina riwaya iliyoandikwa kiasilia kwa njia ya kibarua. Hata hivyo, matumizi ya barua kama mbinu ya kimsuko yapo katika baadhi ya riwaya za Kiswahili. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki barua zinatumika kufikia dhamira mbalimbali.

Katika riwaya ya *Kisima cha Giningi,* Spekta Seif anamwandikia Msa barua kumuomba usaidizi wake katika upelelezi. Katika barua hiyo, matukio kadhaa ya kimsuko yanaibuka. Kwanza, inaoanisha riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kisima cha Giningi* kwa kutufahamisha kuwa Msa alikuwa ameshiriki katika uchunguzi wa kesi nyingine awali katika riwaya ya awali. Pili, barua hii inafichua udhaifu wa polisi katika upelelezi kwa kuwa Spekta Seif anakiri katika barua hiyo kwamba kama si Msa asingaliweza kutatua kadhia ya *Mzimu wa Watu wa Kale.* Tatu, wasifu wa Msa kama mpelelezi hodari unajitokeza, kwa kuwa Seif anaisifia akili ya Msa. Mwisho, kupitia barua hii, Spekta Seif anaandika, 'Mimi sasa nimepata uhamisho kuja huku Giningi pahali panaposifika kwa uchawi-na kweli, maana hata mazungumzo ya watu wa huko ni uchawi na kulogana'.uk.8. Ni wazi kuwa barua hii ina mchango mkubwa katika msuko wa riwaya hii kwa kuwa kando na utangulizi wa wahusika, inatanguliza pia migogoro kuu ya hadithi hii. Kwa mfano, itikadi ya uchawi inatangulizwa katika mwanzo wa ploti kabla ya kurejelewa baadaye. Kwa hivyo, barua hii ni kama muhtasari wa riwaya nzima. Inachochea tukio la Msa na Najum kufunga safari

ya kuenda eneo la Giningi kusaidia katika uchunguzi. Kwa njia hii inakuza msuko. Kwa kuwa barua hii haijibiwi, inawakilisha mawasiliano ya upande mmoja, yaani ya mwandishi mmoja.

Katika riwaya za Abdulla, uchambuzi wa barua ni mkakati mkuu wa uthibitishaji wa kesi mbalimbali. Msa anatumia njia kadhaa za kiupelelezi zikiwemo ushahidi unaotolewa na watu binafsi, habari za magazeti, uchambuzi wa picha za watu na hali mbalimbali pamoja na ushahidi wa nyaraka zilizoandikwa na wahusika mbalimbli. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, Msa akiwahutubia waliohudhuria kuhusu historia ya familia ya Hakimu Marjani, anafananisha picha za watoto wa Hakimu zilizomo gazetini. Anawaelekeza waliomo kutambua kuwa Saleh anafanana na Hakimu Marjani sana na kuwa Kasim hafanani na yeyote katika familia hiyo, hivyo si mtoto wa Hakimu Marjani. Anawaambia kuwa Saleh ndiye mtoto halisi wa Hakimu. Kando na ithibati ya uchunguzi wa picha, Msa anawaeleza kwamba ametumia barua kutafuta habari zaidi. Msa anawaambia:

> Kwa sababu nilimwandikia barua rafiki yangu mmoja mwenye cheo katika serikali ya Tanganyika anitafutie mada na habari zilizomhusu kijana mmoja wa huko aitwaye Saleh Abdulla aliyetoka huko kuja huku Unguja kiasi cha miaka mitano iliyopita. Jawabu niliyoipata inalingana sawasawa. Bwana huyo kaandika katika barua yake kuwa Saleh huyo niliyemuulizia aliokolewa na wavuvi baharini baada ya watu wengine kwisha kuokolewa na motaboti ya serikali, jahazi yao ilipovunjika, wavuvi hao walimpeleka hospitalini na alipotoka, serikali ilishindwa kuwapata wazee wa mtoto yule, ilimpeleka katika nyumba ya mayatima kulelelwa (Uk 119-120).

Barua hii inafupisha na kuharakisha msuko wa riwaya hii kwa kuyamaliza maswali yanayomsumbua msomaji. Maswali hayo hayamsumbui msomaji tu bali pia Spekta Seif na Najum kwani kama wahusika wengineo, nao pia wanauliza maswali ya kufafanuliwa. Barua hii inakamilisha sehemu ya tendo la mshuko wa ploti. Umuhimu wake unajitokeza katika uelezaji wa usuli wa Saleh na kumsaidia Msa kuthibitisha madai yake.

Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, uchunguzi wa barua kama chanzo cha ushahidi unachukua nafasi kubwa. Inspekta Wingo anaenda nyumbani kwa Mzee Jacob kuchunguza mauaji yake na mara Agnes anakuja na barua tatu na kumpa Geva, mwanawe Mzee Jacob. Geva anazipeleka mdomoni ili azichane kwa haraka. Kitendo hiki kinazua taharuki inayomlazimu inspekta Wingo kuzichukua. Anagundua kuwa mbili zilikuwa za marehemu Mzee Jacob lakini zilikuwa zimeandikwa kabla ya kifo chake na moja ikiwa ya marehemu Mary. Barua moja ya Mzee Jacob ilimtaka kufunga safari

ya kwenda Igalula lakini sababu ya safari haitajwi nayo ya pili alikuwa ametumiwa na mtu asiyejulikana ikimjulisha kuhusu bei ya mashine ya unga. Barua ya Mary nayo ilikuwa barua ya mapenzi aliyokuwa ametumiwa na mwalimu Kipindular. Uchunguzi wa barua hizi unachelewesha ufikaji kilele wa msuko (zinachunguzwa kutoka sura ya 5 hadi sura ya 8) kwa kuwa zinamwelekeza mpelelezi na hata msomaji kwenye watu wasiohusika na mauaji hayo. Hata hivyo, wakati huohuo zinaukuza msuko kwani zinatoa baadhi ya taarifa muhimu katika msuko kama vile kuwa Mary alikuwa na mpenzi wa kisiri, mwalimu Kipindular na kuwa kabla ya kuuawa, Jacob alikuwa na mipango ya kununua mashine ya unga. Zaidi ya hayo, ugunduzi wa barua hizi unamchochea mpelelezi Wingo kuenda Igalula kufanya uchunguzi zaidi kuhusu historia ya Mzee Jacob. Pia anaenda katika mtaa wa Majangwa Namba 61 kumsaka tu aliyeandika barua ya pili kwa Mzee Jacob, Kokona. Inspekta Wingo anachukulia kuwa kwa kuwa barua hizi zimepatikana baada ya vifo hivi, zina uhusiano mauaji hayo.

Mtobwa pia katika riwaya zake ameitumia mbinu ya waraka kuyafikia malengo mbalimbali ya kimsuko. Baadhi ya barua hizo zimetuka kuongeza taharuki katika msuko, kukuza ploti, na kuchimuza dhamira kuu. Katika *Salamu kutoka Kuzimu*, jasusi Proper anatumiwa na mashirika ya kimataifa kuendesha shughuli za kupindua serikali kisiri katika nchi mbalimbali za Kiafrika. Ili kuanzisha utawala mpya. Katika uchunguzi wake, mpelelezi Joram Kiango, anaipata barua iliyokuwa na herufi moja tu juu, ‘P’, akairarua kwa haraka na kushangazwa na harufu ya poda au manukato yaliyotoka katika bahasha hiyo. Akaanza kuisoma:

> Ajenti 034/x/P
> Tumepokea taarifa yako na kuipitia kwa makini. Tumeshangazwa na wazo lako la kinyama. Hujui ni kwa nini uko hapo. Tumekuweka hapo si kwa kutenda ukatili bali kulinda masilahi yetu, kiuchumi na kisiasa. Kadhalika, kati ya hao unaokusudia kuwateketeza hujui kama tunao watu wetu tunaowategemea ingawa hadharani tunawaruhusu wajifanye kutulaani. Kuondoka kwao madarakani kuna hatari ya kuja watu wapya ambao huenda tukashindwa kuwamiliki.

Ingawa barua hii ya kisiri ilikusudiwa kusomwa na ajenti wa majasusi wa kimataifa, mwandishi anaiwasilisha kwa wasomaji ili kufichua msukumo wa vitendo vya Proper na kuwaelekeza wasomaji kwenye dhamira za riwaya hii. Suala la ukoloni mamboleo linajitokeza kupitia jinsi mashirika ya kigeni yanavyoshirikiana na nchi jirani na viongozi wasaliti wanaoungana na kupindua serikali ili kuyafikia matakwa yao ya kiuchumi na kisiasa. Inadhihirika kupitia barua hii,

kuwa viongozi wa kiserikali wanamilikiwa na mataifa yenye nguvu za kiuchumi na kisiasa na ndio huamua mwelekeo wa kisera wa nchi changa. Maudhui ya ufisadi, utegemezi na uongozi mbaya yanajitokeza pia kupitia waraka huu. Mwandishi anaufumbata uhalisia wa mataifa mengi ya Kiafrika baada ya uhuru ambayo yameendelea kutawaliwa nan chi zenye nguvu za kiuchumi na kisiasa hususan za Ulaya.

Kando na barua pia kuna maandishi mengine na stakabadhi za aina nyingi ambazo zina mchango mkubwa katika mwendelezo wa msuko. Katika riwaya za Mohamed Said Abdulla kuna stakabadhi kadhaa kama vile wosia na vyeti vingine. Katika *Mzimu wa Watu wa Kale kwa mfano,* kuna cheti kuhusu makubaliano ya mauzo ya shamba baina ya Ali Bomani na Seti Sumatra. Mkataba huo unaonyesha masharti ya uuzwaji wa shamba hilo. Msa na Najum walikiokota cheti kikiwa ndani ya mfuko mweusi katika sehemu ya Mzimu walipokuwa wakiisaka maiti ya Bwana Ali. Wanakiokota cheti hiki kisadfa kwa kuwa Najum alikuwa amegongwa na kuangushwa na tumbili waliokuwa wakitoroka. Kutokea kwa tumbili hawa kighafla na kumpiga Najum, kulizua mtafaruku uliowafanya wasimame ili kutathmini pigo hilo. Katika hali hii, wanaouona mfuko mweusi na karatasi hiyo ya makubaliano ikichomoza. Msa alipoitoa aliisoma hivi:

> Mimi Ali Bomani, nimeuza mali yangu yote, ya shamba na ya mjini, nyumba mbili za mjini No.25 na No.112; shamba langu lote liliko Baraste pamoja na nyumba iliyomo ndani yake, ng'ombe wangu wote, makoo, fahali na ndama. Nimeuza kila kitu kinachonihusu mimi kwa Shs.60,000/= kwa Seti Sumatra (Baniani) wa hapa Unguja. Mimi, Ali bin Boman, nakiri kwamba nimestakabadhi kwa Seti B. Sumatra, Shs.50,000/= leo na zimebaki Shs.10,000/=nitastakabadhi kesho kwake mjini. (Uk.29)

Maandishi haya yanamfaa Msa baadaye katika maelezo yake ya mwisho anapowafafanulia Spekta Seif, Najum, Seti Sumatra na Boi wake kuhusu ni nani aliyemuua Ali Boman na kwa nini. Kwa sababu hii, kuokotwa kwa karatasi hii katika sehemu ya Mzimu kunasaidia kujaza mapengo ya kimsuko na kumaliza taharuki kuhusu maswali ya ni nani muuaji na kwa nini Ali Bomani aliuawa. Katika maelezo yake Msa, (uk.66-81), mfuko mweusi aliouokota pamoja na maandishi haya ya makubaliano yanasaidia kuthibitisha kuwa Seti Sumatra alizichukua shilling 50,000 alizokuwa amempa Ali Bomani kwa mauzo ya shamba. Maandishi haya pia yanafichua wasifu wa Msa kama mpelelezi hodari huku Seti Sumatra akijitokeza kama mwongo, mlaghai na mfanyabiashara katili. Katika maelezo ya Msa, inabainika kwamba Baniani (Seti Sumatra), mkewe na Boi wake ndio

walioubeba mwili wa Ali Bomani na kwenda kuutupa huko mzimuni ili Baniani azichukue pesa alizokuwa amempa Ali Bomani (uk.71).

Matini nyingine yenye dhima kubwa katika ujenzi wa msuko katika riwaya za Abdulla ni msahafu. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, uchanganuzi wa msahafu unafichua mambo mengi yanayosaidia kuweka wazi matukio kadhaa katika msuko. Mariam Mkembe anauleta msahafu aliokuwa amepewa na Abdulla Salum, katika kituo cha polisi ili polisi wamtafute na kumpa Saleh. Kuhusiana na umuhimu wa msahafu huu, Msa anaeleza, 'Fikira ya mwanawe na Mariam Mkembe ilimshawishi auchukue msahafu ule mpaka Kazole ampe yule bibi, mama wa mwanawe mwanamume aliyepotea baharini tangu mchanga.' Uk.116. Abdulla Salum, alikusudia Mariam Mkembe auweke msahafu huo kwa kuwa hakujua ikiwa mwanawe huyu aliyepotea yuko hai. Hata hivyo, kisadfa, Mariam Mkembe anaamua kuupeleka katika kituo cha polisi ili Saleh apewe. Msahafu huo, kulingana na uchambuzi wa Msa, ulikuwa siri kubwa ambamo mlifichama habari muhimu kuhusu ni wapi mali yake yalikofichwa. Msa anauchambua akifuatia kwa kina maana ya ndani ya mistari iliyokuwa imepigiwa misitari na kugundua mambo kadhaa. Msa anasema, 'Sasa nilikuwa na kazi kubwa ya kupekua msahafu, sisikii wala sioni, nimeishika kazi hiyo hiyo tu. Hata ndugu yangu Najum, yule pale, alikasirika na mimi akawa ananikimbia kwa sababu hapati mazungumzo. Alikuwa ananiona nina wazimu'. Katika aya kadhaa Msa anaeleza kuwa alipata baadhi ya maneno, virai ama vifungu fulani vya maneno vilivyokuwa ishara muhimu katika uchunguzi wake. Kwa mfano kifungu, 'Mali na watoto ni pambo la uhai duniani' maneno mawili tu, 'Watoto' na 'Mali' ndiyo yaliyopigiwa mstari. Katika aya nyingine alipata kifungu, 'Kutoka kwenye mti wenye Baraka Mzeituni'. Katika sentensi hii, neno moja tu, 'Mzeituni' lilikuwa limepigiwa msitari. Msitari mwingine nao ulikuwa hivi, 'Hakika idadi ya miezi kwa mwenyezi Mungu ni kumi na mbili' ambapo maneno 'Kumi na mbili' yalikuwa yamepigiwa msitari.

Kulingana na Msa neno 'Mzeituni' lilimwelekeza kujua kwamba Bwana Hakimu Marjani alikuwa na shamba lenye Mizeituni huko Kazole nayo maneno 'Kumi na mbili' yakamsaidia kujua kwamba shamba hilo liko maili kumi na mbili kutoka nyumbani kwa Bwana Hakimu Marjani. Kwa kuunganisha vidokezi vya msahafu, Msa anaweza kupata taarifa za kutosha kuwathibitishia waliohudhuria kuwa Bwana Hakimu ameficha madebe mawili ya pesa katika shamba lake la Kazole umbali wa maili kumi na mbili na kuwa madebe hayo yako karibu na Mzeituni. Habari

hizi za msahafu zinaukuza msuko pakubwa na kufanikisha utoaji wa suluhu mwishoni mwa riwaya kwa kuyajibu maswali ya ni vipi Msa alivyopata ushahidi wa habari azitoazo.

Matini nyingine yenye mchango mkubwa katika ukuzaji wa msuko wa riwaya za Abdulla ni kitabu cha ajabu ambacho Msa anakitumia kuchota baadhi ya maarifa yake, kiitwacho 'Kinyume cha Mambo'. Kitabu hiki kina uajabu mwingi unaomsawiri Msa pia kama mtu wa ajabu. Kwa mfano, kitabu hiki haijulukani Msa alikipata wapi kwa kuwa hamna mtu mwingine amewahi kuwa nacho. Mwandishi wake pia hajulikani wala hamna nakala nyingine inayopatikana popote. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, Najum anapomtembelea Msa nyumbani kwake, anashangazwa na jinsi Msa anavyoandika maneno yenye maana kinyume. Najum anaamini kwamba Msa ameutoa uwezo huo kutoka kwa kitabu hicho. Anapofika na kukuta chumba cha Msa ki wazi, Najum anaamua kukitafuta ili akisome kabla ya Msa kurejea lakini anapoingiza mkono wake tu kwenye koti lake, anauchomoa mkono wake haraka kama mtu aliyedungwa na sindano.

Kwa kukipa kitabu hiki uzito katika kuujenga wasifu wa Msa, mwandishi anaelekea kukubali kwamba maarifa ya Msa na uwezo wa juu wa akili yake ni athari za usomaji wa kitabu hiki. Vilevile, hii inaweza kuwa njia ya mwandishi ya kuipunguza taharuki kwa msomaji ambaye angeshangazwa na uwezo wa Msa. Bila kukirejelea kitabu hiki, wasifu wa Msa kama mtu mwenye uwezo unaozidi wa binadamu wa kawaida ungejengeka kwa udhabiti zaidi. Msimulizi anamwelekeza msomaji kwenye athari za kitabu hiki kwa Msa anaposema kwamba maneno ya Msa ni makubwa anapotaka kumjulisha mtu uwezo wa akili yake. Maneno ya Msa aulizwapo ni wapi hupata maarifa yake huwa 'Ukitaka kujua raha ya mtu aliyesoma, tazama taabu ya mtu asiyesoma, au ukitaka kujua asili ya mwangaza, ingia gizani'. Matumizi ya maneno yenye vinyume kama hivi yanaashiria uwezo wa Msa wa kutumia mantiki kueleza hali fulani za kimaisha. Ingawa kauli za Msa zimejaa kinyume, zimeficha ukweli mwingi ndani yake. Mgeni (1983:48) anajadili kuwa kuwepo kwa kitabu hiki na jinsi Msa anavyokitumia ni njia moja inayozidisha uajabu wa Msa.

### 5.2.8 Hotuba ya Mpelelezi na Ukuzaji wa Msuko

Hotuba ni maelezo marefu yanayotolewa kufafanua msimamo wa mtu kuhusu jambo Fulani au kutoa mwelekezo. Hotuba pia ni maneno anayotamka mhusika wa kifasihi kumhusu mhusika mwingine, suala au mada fulani (Wamitila, 203:63). Katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili,

hotuba ya mpelelezi ina nafasi kubwa katika kuyafafanua matukio ambayo hayakuelezwa na msimulizi. Maswali mengi na migogoro yenye utata yanajibika kupitia maelezo yanayojitokeza katika hotuba ya mpelelezi. Katika riwaya za Abdulla, hotuba za mpelelezi, Msa, zinatolewa mwishoni mwa riwaya ambapo Msa huwakusanya wahusika wanaoathiriwa na matukio tofautitofauti ili kuwaelezea matokeo ya upelelezi wake. Bila maelezo hayo, pangekuwa na mianya mingi ya kisimulizi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, Spekta Seif anamtanguliza Msa awahutubie waliohudhuria na kwanza anawatajia sifa zake alizozijua kutokana na uhusiano wao wa awali. Spekta Seif anatambua ushupavu wa akili ya Msa katika kugundua mambo yaliyofichika. Msa anapokabidhiwa nafasi kuwahutubia anaanza, 'Labda wasikilizaji wangu watukufu maneno nitakayozungumza nanyi hii leo yatawachoma wengine, yatawashangaza wengine, yatawahudhi wengine, yatawashtua wengine, na wengine watavunjika moyo'.(uk.74).

Katika mwanzo wa hotuba yake, Msa anahakikisha kuwa amewatayarisha wasikilizaji wake kwa mishangao na mishtukizo itakayofuata. Anaendelea kutoa majibu ya maswali mengi yanayowatatanisha wasomaji. Kwa mfano, katika hotuba hii, anawabainishia kuwa Kasim si mtoto halisi wa Hakimu Marjani, na kwamba Saleh ndiye mtoto halisi wake. Anawajulisha kwamba, Hakimu Marjani alikuwa amemwoa mke mwingine, Mariam Mkembe kwa kutumia jina Abdulla Salum. Kwa njia hii, anawasaidia waliohudhuria kuielewa historia ya familia ya Hakimu Marjani, ndoa yake, watoto wake na mali yake. Kutokana na maelezo yake Msa, inabainika ni nani mrithi halisi wa mali ya Hakimu Marjani. Msuko haungekamilika pasi na kuwa na maelezo haya yanayopitishwa kwa hadhira kupitia hotuba. Hotuba ya Msa pia inaweka wazi kitendawili kuhusu yalipo mali ya Hakimu Marjani. Anawaeleza kuwa kupitia upekuzi wake wa msahafu amegundua kwamba mzee huyo kabla ya kifo chake alikuwa ameuza mali yake na kuzificha pesa hizo katika shamba lake liliko Kazole, mahali penye Mzeituni, maili kumi nambili kutoka nyumbani. Maelezo kuhusu yalipo mali haya yanamaliza taharuki na kukidhia kujaza mapengo ya kisimulizi hivyo kusaidia kukamilisha msuko.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, hotuba ya Msa inadhihirisha mambo kadhaa ambayo hadhira haikuyafahamu kabla ya maelezo hayo. Baadhi ya maswali hayo ni; ni wapi na vipi Bwana Ali alivyopata mali yake, ni nani aliyemuua Bwana Ali na kwa nini na ni nani aliyebeba mwili wa Bwana Ali hadi sehemu ya Mzimuni. Pia Msa anawafafanulia kuhusu historia ya familia ya Bwana Ali Bomani, kwamba babake Bwana Ali alikuwa mfanyabiashara huko Kongo.

Hotuba ya Msa inaweka wazi kuwa Bwana Ali na mgeni, Mmanga, waliyefanya naye biashara huko Kongo ndiye aliyemuua Bwana Ali. Hii ni kwa sababu Bwana Ali alikuwa ameharibu ndoa ya Mmanga. Maelezo haya yote na mchango wake katika ukamilishaji wa msuko hayangetimia bila hotuba hii kutolewa. Vivyo hivyo katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, hotuba ya Msa inachukua nafasi kubwa katika mwendelezo wa msuko wa hadithi hii. Ni kupitia hotuba hii ndipo masuala kuhusu ni nani aliyemuua mwana wa Giningi, kwa nini na vipi yanapojibika. Hotuba ya Msa pia inafafanua ni nani aliyeiba mali ya Mwana wa Giningi na kwa njia hii, inawaondoa lawamani washukiwa wanaodhaniwa na Spekta Seif kama vile, Vuai. Msa anawaeleza waliohudhuria, hatua kwa hatua na kwa mantiki kuwa Ali Makame ndiye aliyeingia kisiri katika nyumba ya Mwana wa Giningi na kuiba kijaluba kilichokuwa na dhahabu yake. Hotuba ya Msa pia inadhihirisha kuwa ni Ali Makame aliyemuua Mwana wa Giningi pia ili kuficha uhalifu wa awali.

Mpelelezi, Msa, anatumia mbinu mbalimbali katika uwasilishaji wa hotuba yake. Kwa mfano, anarandaranda kutoka sehemu moja ya chumba hadi nyingine ili kuwapa waliohudhuria nafasi ya kuvuta makini na kuyatathmini waliyoambiwa. Pia, anavuta kiko kila wakati anapotaka kufikiri kwa kina au anapoulizwa kutoa maelezo marefu na yenye uzito wa ushtukizaji katika msuko. Mbinu nyingine aitumiayo ni kuiuliza hadhira maswali balagha huku akiyajibu mwenyewe.

Kando na hotuba ya mpelelezi, pia kuna hotuba nyinginezo ndogondogo zonazotolewa na wahusika wengine hususan hotuba ya mhusika mhalifu. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* mshukiwa mkuu katika mauaji ya Mzee Jacob anatoa hotuba inayoyajibu maswali kadhaa yanayowasumbua wasomaji kama vile ni nani aliyemuua Mzee Jacob pamoja na watu wengine wa familia yake, kwa sababu gani na kwa kutumia mbinu zipi. Katika hotuba ya mhalifu huyo, Agnes, anakiri mwenyewe kuwa ndiye aliyemuua Jacob, mkewe na bintiye kwa mbinu mbalimbali ili kulipisha kisasi kwa kuwa Mzee Jacob alikuwa amewaua wazazi wake Agnes na kuichoma nyumba yao. Kwa hivyo hotuba ya Agnes mwishoni mwa riwaya ni muhimu katika msuko kwa kuwa isingekuwapo, sehemu ya msuko ya mpomoko haingekamilika. Hotuba ya Agnes inamaliza taharuki zote zilizokita kwenye akili za wasomaji kuhusu maswali hayo.

### 5.3 Mbinu za Ucheleweshaji wa Msuko

Ufundi wa mwandishi unajidhihirisha kupitia namna anavyovisuka visa vyake kutoka mwanzo hadi mwishoni mwa hadithi. Miundo ya misuko hutofautiana kutegemea ufundi wa mwandishi na athari za kiujumi anazokusudia kusababisha katika kazi yake. Kuna hadithi zenye misuko inayoanza kwa kilele na kuendelea kwenye ufafanuzi na kisha mwisho. Kama kaida ya kiutanzu, riwaya ya kiupelelezi huanza kwa ufafanuzi na kuelekea kwenye kilele.. Hadithi inayofikishwa kileleni kwa kasi ya juu huenda ikakosa ujumi wa kiusanii, hali ambayo huweza kumkinaisha msomaji. Kwa sababu hii, waandishi aghalabu hutumia mbinu mbalimbali ili kudhibiti kasi ya usimulizi na ukunjufu wa matukio. Baadhi ya mbinu hizo ni kama vile urejeleaji mwingi wa masuala yaliyopita, misukumo pofu, mazungumzo na utokaji nje wa usimulizi. Katika sehemu hii, tunafafanua baadhi ya mbinu hizi za ucheleweshaji kilele na mchango wake katika kujenga msuko.

#### 5.3.1 Misukumo Pofu

Hii ni mikakati ya kiusimulizi inayoyapeleka mawazo ya wasomaji nje ya mgogoro mkuu ya msuko. Kutokana na misukumo hii, aghalabu msomaji huweza kufuata kidokezo cha uongo ambacho kimewekwa na mwandishi kimakusudi ili kumpotosha msomaji kwa ajili ya kumshtukiza baadaye. Mishtukizo hiyo inahusu migeuko katika msuko ambapo jambo lisilotarajiwa linaibuka. Kwa mfano, mhusika anayedhaniwa kuwa mhalifu anapogundulika kuwa siye. Katika riwaya za kiupelelezi misukumo pofu hutumiwa kuongezea kiwango cha taharuki, uajabu na kuchelewesha kilele cha msuko. Kuna mikakati kadhaa inayotumiwa kukuza misukumo pofu katika riwaya za kiupelelezi. Kwanza, kuna utolewaji wa habari nyingi zisizohusiana na upelelezi. Kwa kuwa msomaji wa riwaya za kiupelelezi huwa amepewa utangulizi kuhusu uhalifu mwanzoni mwa msuko, kinachobaki ni utambuaji wa ni nani aliyehusika katika uhalifu, kwa nini na zaidi ya yote, kujua namna uhalifu huo ulivyofanywa na aina ya adhabu mhalifu atakayopewa. Katika riwaya za kiupelelezi, ni kawaida kuona waandishi wakichelewesha upatikanaji wa habari hizo kupitia usimulizi wa matukio yaliyo nje ya upelelezi. Baadhi ya taarifa hizo zinahusu utoaji wa maelezo kuhusu famila ya mpelelezi au mhalifu. Maelezo hayo huweza kufichua usuli wa mhusika, ndoa yake au ikiwa zinamhusu mhalifu, zinadhihirisha chanzo cha uhalifu alio nao mhalifu. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, kwa mfano, msimulizi anaeleza jinsi mpelelezi Far Katy Wingo anavyowakumbuka watoto na mkewe akiwa kazini. Msimulizi anaeleza kwa kina jinsi kumbukizi

ya familia inavyoathiri utendakazi wake Wingo kwani inamsahaulisha visa vinavyongoja upekuzi wake. Haya ni mambo yasiyokuwa na uzito katika ukunjufu wa msuko. Msimulizi anasema:

> Wingo akaketi kitako na kwanza kumfikiria mkewe ambaye alikuwa ameondoka siku nyingi kwenda kwao. Moyoni, Inspekta akafurahi kuelewa kuwa jioni ile alikuwa anakwenda kumpokea mzazi mwenziwe na wanawe watatu. Akawasha kiko chake na kuanza kuuchezea moshi uliokuwa unatanda darini. Wingo hakuwa anaelewa analolifanya, ila alijiona mwenye furaha-ya kumwona mkewe mpenzi, kumwona mwanawe mkubwa, Rashid, mwenye umri wa miaka kumi na binti yake Abiba, mwenye umri wa miaka saba na yule mchanga, Heri. Uk.43

Katika muktadha huu, mwandishi anamsawiri mpelelezi mwenye uhalisia wa kimaisha kinyume na ilivyo mhusika mpelelezi katika kazi za Mohammed Said Abdulla, ambapo Msa kwa mfano, hana familia, haoi, hana watoto wala kuwa na matamanio ya kuanzisha familia. Kwa kutumia kielelezo cha Msa, Abdulla ameendeleza mfano wa usawiri wa mhusika mpelelezi katika kazi za Kimagharibi kama vile mpelelezi Sherlock Holmes. Katika kazi za Conan Doyle, mpelelezi Sherlock Holmes hana familia wala hashiriki katika mahusiano ya kimapenzi. Elvis Musiba pia amemtumia mhusika mpelelezi, Willy Gamba, mwenye uhalisia mwingi kwa kuwa ana familia na anaonyesha waziwazi kuwa mwenye mapenzi. Mara kadhaa katika riwaya ya *Uchu,* msimulizi anatuonyesha kupitia msukumo pofu jinsi mpelelezi Willy Gamba anavyoijali familia yake. Anapojitokeza riwayani mara ya kwanza, Willy Gamba anapigiwa simu na Chifu akimuomba kukubali kutumwa kufanya upelelezi nchini Rwanda. Anakataa wito huu kwa sababu ya familia. Anasema, ‘Mimi! Mimi nimeoa na mke wangu ana mimba. Mchezo huo sifanyi. Sifanyi ng’o’.uk.8. Baada ya habari kuhusiana na ndoa ya Willy Gamba na mkewe, Pepe, msimulizi anafafanua tena kuhusu ubora wa tabia ya Pepe na urembo wake, mambo ambayo hayasaidii katika mwendelezo wa msuko unaohusiana na uchunguzi. Msimulizi anasema:

> Mamake Willy alikuwa na wasiwasi sana na Pepe kutokana na jinsi mtoto yule alivyokuwa mzuri wa sura. Alifikiri kuwa msichana mzuri kiasi kile, hawezi kuwa mke wa nyumbani kwani lazima atakuwa na maringo. Lakini mamake.Willy alikuwa kakosea kabisa. Wazazi wake walimlea kwa kumtayarisha ili aje awe mke wa mtu. Licha ya uzuri usiozoeleka wa maumbile ya Pepe, tabia yake ilikuwa nzuri isiyoweza kuelezeka vilevile. Uk.13.

Katika dondoo hili, tunaona utolewaji wa habari nyingi kuhusu familia, malezi, elimu na utamaduni zikielekezwa si kuhusiana tu na mpelelezi bali pia mamake mpelelezi na wazazi wa mkewe (wazazi wa Pepe). Kupitia maelezo hayo, itikadi ya mwandishi kuhusu malezi inajitokeza. Udhaifu wa mpelelezi pia unajitokeza katika riwaya ya *Simu ya Kifo,* ambapo mpelelezi anatumia muda mwingi mno kuchunguza barua tatu alizopata na anapochoka nazo anaanza kuzungumza kuhusu familia yake kwa kina. Taharuki kuhusu barua hizi, inazidi kupitia kitendo cha Geva cha kuzichana barua hizo mara tu anapomwona Wingo akija kwao. Hali hii ni msukumo pofu kwa kuwa kitendo cha kuzichana barua hizo kinamwaminisha msomaji kuwa huenda Geva ndiye muuaji ilhali ishara nyingine zinamwelekeza msomaji kwingine. Zaidi ya haya, barua hizi zinafika baada ya wenyeji kufariki; Jacob na Mary. Hii ndio sababu Wingo anauliza, 'Ni nani anayeweza kuwa alizicheleweshа barua hizo mpaka wenyewe wakafariki? Je, mtu huyu alielewa kuwa wangalikufa karibuni? Uk.37

Pili, msukumo pofu pia unajitokeza kupitia udhaifu wa wapelelezi wa polisi. Wapelelezi hodari huwa na sifa tatu kuu zinazowawezesha kufanikiwa katika uchunguzi wao ambazo ni kipawa cha uchunzaji, kuwa na maarifa na uwezo wa kugundua. Kama mbinu ya kifomyula katika riwaya za kiupelelezi, kunakuwa na wapelelezi wa aina mbili kuu; mpelelezi wa polisi aliyeajiriwa na serikali na mpelelezi wa kibinafsi. Katika riwaya nyingi za kiupelelezi zikiwemo zile za Kimagharibi, wapelelezi wa polisi husawiriwa wakiwa na udhaifu katika kazi zao. Kwa mfano, wao hushindwa kuwatia mbaroni wahalifu na kwa hivyo wanatafuta usaidizi wa mpelelezi wa kibinafsi. Tunaona hali hii katika kazi za Abdulla, Katalambulla, Mtobwa, Musiba miongoni mwa wengine. Katika baadhi ya riwaya za Abdulla, Spekta Seif anawaelekeza wasomaji kwenye shahidi wa uongo na kuwatia mbaroni watu wasio na hatia. Kwa kufanya hivi anatuelekeza kwenye msukumo pofu na wakati huo huo kudhihirisha udhaifu wake kwa kushindwa kuwatambua wahalifu halali. Uelekezaji kwenye ukweli unafanywa na mpelelezi Msa ambaye anaonyesha ujuzi zaidi. Kwa mfano, katika *Kisima Cha Giningi,* Spekta Seif anamshuku mumewe Mwana wa Giningi, Vuai, kuwa huenda ndiye aliyeiba mali ya Mwana wa Giningi na kumuua baadaye ili kuuficha ukweli. Spekta Seif anatumia vigezo viwili tu kufikia maamuzi yake ambayo ni kuwa Vuai na Mwana wa Giningi hawakuwa na uhusiano mwema wa kindoa na kwamba Vuai alionekana katika eneo la mauaji. Huu ni msukumo uanoweza kufuatwa na msomaji akiamini hivyo hadi mwishoni mwa msuko ambako ukweli huwekwa wazi.

Vilevile, katika *Dunian Kuna Watu*, kuhusiana na kupotea kwa mali ya Bwana Hakimu Marjani, Spekta Seif kama mpelelezi wa polisi anadhihirisha udhaifu wake anapoelekea kuamini kuwa lazima pesa za mzee huyo ziwe zimeibiwa. Anaamini kwamba ikiwa pesa hizo haziko kwenye Sefu, basi lazima zimepotea kupitia wizi wa ndani. Yeye haoni uwezekano wa pesa hizo kuwa mahali pengine. Kwa hivyo, anawasababishia wasomaji kwamini kuwa kasri la Hakimu Marjani lilivamiwa na watu wasiojulikana waliozichukua pesa hizo, jambo linalothibitishwa na Msa kuwa si kweli. Baadaye, Spekta Seif anautilia nguvu zaidi msukumo pofu huu anapojenga haipothesia kwamba zamani kasri hilo lilikuwa limevamiwa na wezi walioletwa na Kasim na kwa sababu hii, Spekta Seif anaonyesha kuwa Kasim huenda ndiye mwizi. Anatumia vigezo viwili dhaifu pia kumtia mbaroni Kasim. Kwanza, katika tukio la wizi wa awali (uk.55), Kasim alikutwa akiwa amelala bila kujali kumsaidia babake kujiokoa, na pili, Kasim alipatikana akiwa na pesa, shilingi elfu moja na mia sita mfukoni mwake huku akicheza kamari kwa Rehani siku chache baada ya kupotea kwa pesa za babake. Spekta Seif anasema:

> Kasim Hakimu Marjani nimeshamtia ndani. Pale nilipoondoka hapa, akili yangu ilifanya kazi sawasawa. Niliwaza na kufikiri nani atakuwa na nafasi, wakati na faragha ya kuiba mali ya Bwana Hakimu. Lazima awe mtu wa ndani. Nilipofika hapo tu, nilimwona Kasim kasimama mbele yangu, nikaona hapana ila yeye…Nikaona mwonja haonji mara moja ( Uk. 55-56)

Katika dondoo hili, tuanona jinsi maamuzi ya haraka yasiyo na ushahidi mzito yakitumika kuelekeza lawama kwenye mshukiwa wa uongo na kumzuia msomaji asiupate ukweli mapema. Kutoa vidokezo hivi vya uongo kunacheleweshwa kilele cha msuko. Spekta Seif anajitokeza kama kielelezo cha jinsi polisi huwatia mbaroni washukiwa bila kufanya uchunguzi wa kina. Katika riwaya ya Mtobwa ya *Najisikia Kuua Tena* (uk.19) Sajini Abdalla anamwambia mkuu wa polisi, Inspekta Kombora kwamba sababu zilizomfanya amshuku mwanamke fulani katika mauaji ya mwandishi Kitenge, ni kuwa mama huyo alionekana mlevi. Hiki pia ni kigezo dhaifu kinachoelekeza kwenye udhaifu wa mpelelezi. Msukumu pofu huu pia unaweza kuwafanya wasomaji kwanini kuwa mwanamke huyu ndiye muuaji. Hata hivyo, kwa kuwa kidokezo hiki kinatolewa mapema katika msuko, msomaji mpevu anatilia shaka ni vipi suluhisho limepatikana mapema. Kwa hivyo, anataendelea kusoma kuona ikiwa kuna vidokezo vingine vinavyoelekeza msuko kwingine.

Kando na kuwepo kwa shahidi wa uongo, pia mwandishi anaweza kutumia vidokezo vingine vinavyomuondoa msomaji kwenye msuko mkuu. Kwa mfano, matumizi ya vijihadithi visivyohusiana moja kwa moja na utatuzi wa mgogoro vinaweza kuukwaza msuko wa riwaya zote, zikiwemo hata riwaya dhati. Hata hivyo, baadhi ya wahakiki wanaamini kuwa kuwepo kwa vidokezo vya uongo ni kumpotosha msomaji. Kulingana na Burns (1975:30-38) vidokezo vya uongo, kando na kuchelewesha kilele cha msuko pia ni ukiushi wa usawa baina ya msomaji na mwandishi. Anasema kwamba, kwa kuwa usomaji wa riwaya za kiupelelezi unachukuliwa kama mchezo baina ya msomaji na msimulizi, pana haja ya kuweka wazi sheria zote kama ilivyo katika michezo mingine. Burns (keshatajwa) anafafanua kuwa utumizi wa vidokezo unafaa kutumiwa kwa tahadhari kwa kuwa kutumia vidokezi vingi kunaweza kumwelekeza msomaji moja kwa moja kwenye mhalifu na sababu ya uhalifu, hivyo kumaliza hamu ya usomaji na kuuharakisha msuko kufika kileleni. Vilevile Burns anaonya kuwa utumizi wa vidokezi vichache mno ni kukiuka haki ya msomaji kwani kwa kufanya hivyo ni kuivunja kanuni ya udumishaji usawa baina ya msomaji na msimulizi.

Tatu, msukumo pofu pia unajitokeza kupitia utokezaji wa uhalifu mwingine kabla ya uhalifu wa kwanza kutatuliwa. Hali hii inapotukia, mpelelezi hujipata katika utata asijue ikiwa aendelee na uchunguzi wa kesi ya kwanza au aanze upelelezi kuhusu uhalifu mpya au achunguze yote kwa pamoja. Katika riwaya ya *Simu ya Kifo*, Wingo akichunguza kesi ya mauaji ya Jacob, simu inapigwa kuripoti mauaji ya mkewe. Kinachozua taharuki kinatokana na ukweli kuwa kila wakati mauaji yanapofanyika, Inspekta Wingo anapigiwa simu na mtu yuleyule, FAMBO. Baada ya siku chache baadaye, kifo cha bintiye, Mary kinaripotiwa na kabla ya kukamilisha uchunguzi wa mauaji hayo, mauaji ya mwanawe wa kiume, Geva yanaripotiwa na mtu yuleyule. Kando na kukuza taharuki, msururu wa matukio ya kihalifu unalemaza uendelezaji mbele wa msuko. Kwa hivyo, ufikaji kilele wa msuko unacheleweshwa. Katika *Kisima cha Giningi*, huku Spekta Seif na askari wenzake, Msa na Najum wakichunguza wizi wa mali ya Mwana wa Giningi, kisa cha mauaji ya Mwana wa Giningi kinatokea. Tokeo hili linafanya uchunguzi wa uhalifu wa kwanza kulemaa kwa muda huku macho yakielekezwa kwenye kesi mpya ya mauaji. Kukwama huku kimwendelezo wa uchunguzi kunadhibiti kasi ya msuko kwelekea kileleni, hivyo kumsaidia mwandishi kuandika hadithi ndefu kwa ubunifu na yenye mvuto.

Baadhi ya mambo mengine yaletayo misukumo pofu ni kuwepo kwa msaidizi wa mpelelezi aliye na uwezo mdogo wa kiakili na anayeuliza maswali mengi ambayo humlazimu mpelelezi kutumia muda mwingi akiyaeleza. Ingawa maswali haya pia huwafaa wasomaji, yanamrudisha mpelelezi nyuma hivyo kupunguza kasi ya ukunjufu wa msuko. Mhusika huyu pia ni kiwakilishi cha wasomaji kwani kupitia yeye, wasomaji wanaelewa msuko wa hadithi. Kwa mfano, katika kazi za Mohammed Said Abdulla, Najum anatekeleza wajibu huu. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale,* Najum anatoa maelezo kumhusu Boi wa Baniani aliyetoroka baada ya kuwaona polisi na katika maelezo hayo, Najum anaonyesha kuamini kuwa Boi wa Baniani ndiye muuaji. Najum anadhihirisha udhaifu wake kwa kutumia kigezo kimoja tu cha kutoroka kwa Boi huyo, kumshuku. Spekta Seif pia anaelekea kukubali kwamba kutoroka kwa Boi wa Baniani ni ishara kwamba alikuwa mhalifu. Huku ni kuelekeza kwenye kusiko kwani uchunguzi wa Msa unadhihirisha vingine (uk.59). Baadaye, Najum anauliza swali kudai ufafanuzi kuhusiana na usuli wa Bwana Ali, jambo ambalo pia ingawa linarudisha nyuma msuko, linawafaa wasomaji. Najum anauliza, 'Sasa ikiwa Bwana Ali siye babake Ahmed, je, unakusudia kusema, Bwana Musa, kuwa Ahmed ni mwanaharamu?' uk.76. Urejelezi wa mambo ya awali kama mkakati wa kujenga msukumo pofu unalemaza ukunjufu wa kimsuko lakini pia ni njia ya kujenga muktadha wa matukio ya sasa. Katika riwaya za kiupelelezi ni vigumu kuepuka urejelezi wa masuala ya awali kwa sababu kwa kuwa uhalifu, ambao ni kipengele cha msingi katika msuko, huwa umetendeka katika wakati uliopita, huku sehemu kubwa ya msuko ikihusika na usuluhishaji wa migogoro inayoletwa na uhalifu huo.

5.3.2 Mazungumzo

Mazungumzo huweza kukuza msuko kwa kuwa baadhi ya matukio hujitokeza kupitia maongezi baina ya wahusika si katika riwaya za liupelelezi tu bali pia katika riwaya dhati. Katika riwaya za kiupelelezi kwa mfano, mazungumzo baina ya mhalifu na mpelelezi yanaweza kufichua sababu za uhalifu huo na jinsi ulivyotekelezwa. Mazungumzo aina ya mahojiano, baina ya polisi na mhalifu yanachukua dhima kubwa katika upelelezi katika riwaya za Godfery Levi kama vile *Fedheha ya Fedha.* Hata hivyo, mazungumzo pia huweza kutumika kwa njia inayochelewesha ufumbuzi wa migogoro inayoletwa na uhalifu hivyo kuuchelewesha msuko kufika kwenye kilele.

Matumizi ya mazungumzo kama mbinu ya ujenzi wa msuko yana historia ndefu hususan katika tamthilia. Rimmon-Kenan (2002:22) akimnukuu Plato katika kitabu chake cha tatu cha *The*

*Republic*, anaeleza kuwa kuna njia mbili za utolewaji wa mazungumzo ambazo ni daijesia na mimesia. Kuhusiana na migao hii miwili, Rimmon-Kenan anaeleza kwamba, katika daijesia msanii mwenyewe ndiye msemaji lakini katika mimesia, mshairi hujaribu kuthibitisha kuwa siye anayezungumza. Kwa sababu hii, monolojia, dayalojia na uzungumzi nafsi zote ni njia za kimemesia. Baadaye, naye Aristotle katika *The Poetics* halitumii neno mimesia kurejelea uigaji wa kiusemi tu bali uigaji wa kivitendo kwa kuwa alijihusisha na uchunguzi wa drama.

Kando na aina hizi za mazumgumzo, wahakiki mbalimbali wameyaainisha mazungumzo katika kategoria kadhaa kwa kutumia vigezo tofauti. Kwa mfano, Rimmo-Kenan ameyaweka (uk.112) mazungumzo katika kategoria saba za kidiskozi kwa kutumia viwango vya uigaji. Anazipanga aina hizi za diskozi kwa kwanzia na daijesia wazi hadi mimesia wazi. Simpson (2004:33-34) naye anatumia kigezo cha uhuru wa usemi katika uainisho wake wa mazungumzo na fikira. Anazungumzia aina nne za uwasilishaji wa mazungumzo (usemi halisi, usemi wa taarifa, usemi halisi huru, usemi wa taarifa huru) na aina nne za uwasilishaji fikira. Wamitila (2008:97) anatumia uainishaji unaokaribiana na wa Simpson kwa kuwa yeye pia anapata aina nane za uwasilishaji mazungumzo katika kazi za kifasihi. Aina hizo ni usemi halisi, mawazo/mtindo halisi, usemi taarifa, mawazo/mtindo taarifa, usemi halisi huru, usemi wa taarifa huru, mawazo halisi huru na mawazo taarifa huru. Wahakiki wengine waliozungumzia mbinu za uwasilishaji wa usemi ni, Page (1973), Pascal (1977), Leech na Short (1981) na McHale (1983).

Kwa kuwa lengo la sehemu hii si kuchanganua muundo wa mazungumzo bali ni kuonyesha mchango wake katika kudhibiti mwendo wa msuko, hatutafafanua maana wala mifano ya aina zilizotajwa hapo juu za uwasilishaji wa usemi. Katika riwaya za kiupelelezi tunazohakiki, mazungumzo yametumiwa kuukuza msuko na vilevile kulemaza ukunjufu wake. Katika riwaya ya *Kisima Cha Giningi*, mazungumzo baina ya Spekta Seif na Msa kuhusu uchunguzi wa wizi wa mali ya Mwanna wa Giningi, yanatoka nje ya uchunguzi wanaoufanya wanapoelekeza maongezi yao kwenye mada ya uchawi na imani za kishirikina. Katika mazungumzo hayo, Msa anaeleza kwamba imani kuhusu uchawi imekita mno hata miongoni mwa watu waliosoma. Anakiri kuwa mtu yeyote anaweza kufanya uramali. Wawili hawa wanaanza kuhadithina visa mbalimbali vya uchawi walivyowahi kushuhudia maishani mwao. Mazungumzo haya yanachelewesha ufikaji kileleni wa msuko lakini pia yanachangia katika kuiendeleza taharuki.

Katika riwaya za Mtobwa na Musiba ambapo aghalabu mpelelezi hutumia fujo katika kupambana na wahalifu, mazungumzo yanatumika kuchelewesha mapambano baina ya mpelelezi na mhalifu. Urefushaji wa mazungumzo unamsaidia mpelelezi kutafuta namna ya kumnasa mshukiwa huku mshukiwa naye akiyatumia mazungumzo kupata habari za siri za mpelelezi ama kuchelewesha kukamatwa kwake au kukwepa mitego iliyowekwa. Katika *Tutarudi na Roho Zetu?* mpelelezi Joram Kiango anaingia katika chumba cha siri cha jasusi wa kigeni, Chonde, kukipekua ili kupata habari muhimu kumhusu Chonde lakini anafumaniwa. Anapokosa namna ya kujinazua, Joram anaanzisha mazungumzo ili kupata muda wa kufikiria cha kufanya. Chonde naye anachangia kuyarefusha maongezi hayo akimkejeli Joram na kumtishia. Mazungumzo yao yanaenda hivi:

“Mwanamapinduzi aliyekata tamaa”, Chonde alikuwa akisema. “Aibu ilioje kukata tamaa hali nchi yako iko mashakani? Si ungejaribu kutoa mchango wako?”. Joram hakumjibu. Kisha kama aliyekumbuka jambo, Chonde alisema ghafla.

“Nasikia msichana wako ametekwa nyara”.

“Umesikia Wapi?”

“Kwani ulidhani ni siri?”

Msimulizi pia anathibitisha kuwa Joram aliyatumia mazungumzo haya ili kutafuta muda wa kujiokoa. Anasema hivi, “Hata hivyo, alitegemea kitu kimoja tu kimsaidie **kutafuta muda wa kuokoa maisha yake**. Muda. Muda waweza kufanya maajabu. Hata asipookoka, si inapendeza endapo atafaidi uhai dakika chache zaidi?”.uk.45. Kutokana na ithibati ya msimulizi, ni wazi kwamba mazungumzo haya yana dhima ya kuuchelewesha msuko kwani hayapeleki mbele uchunguzi. Joram anayarefusha zaidi hivi:

“Najua ninakufa,” alisema. “Nadhani unajua kuwa nakufa kwa ajili ya tamaa ya kutaka kujua siri uliyoificha kwenye kisanduku hicho. Nifanyie basi wema wa mwisho. Nifungulie kisanduku hicho nife nikijua mna nini”.

Chonde alicheka, “Tatizo lako Joram ni kule kufikiria kuwa unacheza na mtoto mdogo. Unachojaribu kufanya ni **kuvuta muda**, waakati huo huo unaendelea na upelelezi wako ili enadapo lolote litatokea, utoroke na kuitoa siri hiyo nje”.Uk.46.

Joram akacheza tena karata yake ya mwisho, "Vipi ukiniua kwa mikono? Nadhani ni aibu na dalili ya woga kutumia risasi pasipo na umuhimu".

Chonde alicheka tena, Ningependa kukuua kwa mikono mitupu. Hata hivyo, sina muda wa kutosha. Umebakiwa na nusu dakika ya kuishi. Utapenda kufa ukiwa umefumba macho au nikuue ukitazama? uk.45-46.

Juhudi za Joram za kujiokoa kupitia mazungumzo haya zilifanikwa kwa kuwa kisadfa, Nuru alijitokeza na kumpiga risasi Chonde. Hii ni mbinu anayoitumia mwandishi kuzuia kifo cha mhusika mkuu akijua kwamba kifo cha mhusika mkuu kama mpelelezi Joram kungemaliza hadithi kabla ya kufikia upeo. Mjo wa Nuru wakati kama huu pia unamaliza taharuki iliyokuwa imetanda kufuatia vitisho vya mhusika mhalifu, Chonde. Katika riwaya ya *Uchu*, mazungumzo pia yanapewa jukumu kama hili la kurefusha muda ili kutoa nafasi ya kujiokoa. Xavier na Col.Gatabazi wanamkabili, Bibiane wakitaka kumuua wakisema kuwa wametumwa na mpenziwe, Jean. Badala ya kutekeleza mauaji hayo mara moja, wanaendeleza mazungumzo marefu (uk.97-98) hadi mpelelezi Willy Gamba anapojitokeza na kumwaokoa Bibiane kwa kuwapiga risasi Xavier na Col.Gatabazi. Mazungumzo hayo yanaendelezwa hivi:

> Nakwambia hivi, sisi tumetumwa tuje kukuua na huyo huyo bwana yako Jean. Faida yako kwake imeisha. Wewe ni mzigo na yeye hataki kubeba mzigo". "Wewe unatania. Jean hawezi kusema hivyo. Jean ni wangu wa kufa na kupona", Jean aliwajibu huku akionyesha sura ya hofu, maana aliwajua hawa ni wauaji.

Mazungumzo haya pia yanakuza taharuki kwa kuwa msomaji angependa kujua ikiwa Bibiane atauawa au ikiwa mazungumzo yao yangewafanya wauaji kubadili nia. Mazungumzo haya yanatimiza wajibu wa kumwokoa Bibiane, kwani baada ya muda mfupi, Willy Gamba alikuja. Kando na hili, pia yanachimuza wasifu wa mpelelezi kama mtu wa ajabu na mwenye ujasiri mwingi huku wakati huohuo yakidhihirisha udhaifu wa mhalifu. Dhamira ya wema kuushinda uovu inachimuzwa. Kuhusiana na jukumu hili la msuko, Wamitila (2002:84) anasema, 'Lazima mazungumzo yawe na dhima wazi ya kusimulia hadithi, kuendeleza msuko, kuikuza dhamira na kuyapanua maudhui ya kazi hiyo'.

Katika riwaya za kiupelelezi na zile za kiuhalifu, mazungumzo kando na kuchelewesha kilele, pia huwa na jukumu lingine la kutoa nafasi kwa mtu mpumbavu, hususan, mshukiwa kufichua habari

muhimu bila kukusudia kwa kutoa habari zaidi kwa mpelelezi, (Kimura, 1992:126). Hii ndio hali inayoshudiwa katika riwaya za Godfrey Levi kama vile *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu* na *Fedheha ya Fedha.* Katika riwaya hizi mbili, mazungumzo yanachukua mtindo wa mahojiano ambapo polisi wanawahoji washukiwa mbalimbali na mmoja anapohojiwa anakiri makosa na kuwataja wahusika wengine. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mpelelezi Hodari na Genge la wahalifu*, Inspekta Kombo anamhoji mshukiwa Karikenye na ndiye anayemwelekeza msituni walipo wahalifu wengine. Katika *Fedheha ya Fedha*, washukiwa Bambola, Mbogo na Twalib wanahojiwa na Sajini Boke na kukubali kushiriki wizi wa benki. Katika riwaya zote hizi mbili, kuna urudiaji mwingi katika mahojiano, jambo linalofanya msuko usifike kileleni haraka. Mahojiano yanayofanywa na polisi yanarudiwa tena na hakimu bila kuzua jambo lolote jipya kuhusu wahusika au silaha watumiazo.

Mbinu nyingine za ucheleweshaji kilele ni utokaji nje wa kisimulizi ambapo msimulizi hutoa habari za ziada za kumuktadhisha yale ayasemayo. Utokaji nje unajitokeza msimulizi, anapoeleza motisha ya vitendo fulani vya wahusika na pia kama mkakati wa kujenga taharuki. Kwa mfano, msimulizi anaweza kuliacha suala analolisimulia kwa muda na kusimulia lingine lisilohusiana na tukio la sasa na kwa njia hii, taharuki inajengeka kuhusiana na suala la kwanza. Dhima kuu ya utokaji nje ni kuboresha uelewekaji wa hadithi kijumla. Baadhi ya waandishi hutumia mbinu rejeshi au utoaji wa vijihadithi haswa visivyohusiana na msuko mkuu ili kuikuza mbinu ya utokaji nje. Kulingana na Rimmon-Kenan (102&131), utokaji nje kimsuko unaweza kufanywa kupitia utathmini wa msimulizi. Hii ni hali ambapo msimulizi huwacha kusimulia matukio makuu ya hadithi na kuanza kutathmini jinsi usimulizi wake unavyoendeshwa. Utathmini pia unaweza kufanywa kuhusiana na maudhui ya hadithi. Tathmini ya msimulizi aghalabu hujidhihirisha kupitia ufafanuzi wa ayasimualiayo, utoaji wa maoni na ujumlishaji.

## 5.4 Hitimisho

Sura hii imeshugulikia suala la msuko ambapo nafasi kubwa imejikita katika mbinu za kimtindo zinazofanikisha ujenzi wa msuko katika riwaya ya kiupelelezi za Kiswahili. Imethibitika kwamba hadithi ya kiupelelezi huwa na usambamba wa hadithi mbili, ile ya uhalifu na ile ya uchunguzi wa uhalifu huo. Tumebainisha kwamba baadhi ya mbinu za kimtindo huwa pia za kifomyula kwa kuwa kikanuni, zimekuwa sehemu ya muundo wa riwaya ya kiupelelezi. Mbinu hizo za kikaida ni kama vile taharuki, sadfa na urejelezi wa matukio ya awali. Nadharia ya Umwingilianomatini

imetufaa katika kufafanua jinsi urejeleaji wa riwaya za awali za mtunzi mmoja na urejelezi wa riwaya za watunzi wengine unavyochangia kuleta muwala wa msuko. Nadaharia ya utanzu na ile ya umitindo zimetufaa katika kufafanua sifa za kimtindo zinazoupambanua utanzu wa riwaya ya kiupelelezi na kategoria nyinginezo za riwaya.

Katika sura hii, nadharia ya umitindo ndio iliyotumika. Dhana ya mtindo kama mtu imetufaa sana kwa kuwa tumechunguza mbinu za kimtindo zizotumiwa katika riwaya za waandishi mbalimbali katika ujenzi wa misuko. Tumechunguza pia mbinu za kimtindo ambazo hutumiwa kuchelewesha kilele cha msuko kama vile misukumo pofu, utokaji nje kisimulizi na mazungumzo. Hizi ni mbinu zinazomsaidia mwandishi kuifuma hadithi ndefu bila kumchosha msomaji kwa kuhakikisha kuwa amemnasa msomaji kitaharuki na wakati huo huo akimzuia msomaji dhidi ya kuyapata majibu ya mgogoro haraka. Kwa kutumia mbinu hizi, mwandishi anamwelekeza msomaji kwenye utatuzi wakati ufaao wa mpomoko. Imeonyeshwa kwamba msuko wa riwaya za kiupelelezi huongozwa na kanuni zilizozoeleka zinazohusu kuripotiwa kwa uhalifu, uchunguzi wa uhalifu huo, kunaswa kwa mhalifu, utolewaji wa maelezo ya mpelelezi kuhusu jinsi alivyompata mhalifu ambapo anawaeleza waliohudhuria namna nadharia yake inavyofanya kazi, utolewaji wa adhabu kwa mhalifu na urejeshi wa hali ya amani na utulivu uliokuwapo kabla ya uhalifu.

# SURA YA SITA

# MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Utafiti huu umehusu uchunguzi wa usimulizi na muundo katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Kuhusu muundo, vipengele vya uhusika na msuko ndivyo vilivyoshughulikiwa. Hii ni kutokana na umuhimu wake na ujitokezaji wake katika riwaya za kiupelelezi. Sura hii, inaonyesha muhtasari wa utafiti huu, matokeo yake na mapendekezo kuhusu mapengo mengine yanayofaa kutafitiwa katika utanzu wa riwaya ya kiupelelezi.

## 6.2 Muhtasari

Kazi hii imegawika katika sura sita ambapo sura ya kwanza imeshughulikia usuli wa tatizo la utafiti. Sura hii imeweka msingi wa kazi nzima kwa kudhihirisha malengo ya utafiti ambayo yalikuwa; kutathmini namna usimulizi unavyotekelezwa katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, kuchunguza muundo wa uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili na kuchunguza mbinu za ujenzi wa msuko katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Kwa hivyo, utafiti ulizingatia malengo haya ambayo yalichunguzwa kwa misingi ya nadharia za utanzu, naratolojia na umitindo. Katika sura hii, pia tumefanya mapitio ya kazi za awali zinazohusiana na fasihi pendwa kijumla na riwaya ya kiupelelezi. Mbinu za utafiti, uchanganuzi wa data na maadili katika utafiti ni masuala mengine yaliyoshughulikiwa katika sura hii.

Katika sura ya pili, tumetathmini maendeleo ya ukuaji na maendeleo ya utanzu wa riwaya pendwa kijumla na kujikita baadaye katikka riwaya ya kiupelelezi. Tumechunguza chimbuko la utanzu huu kuanzia katika fasihi simulizi na hadithi za mapema za kiupelelezi zipatikanazo katika jamii mbalimbali za ulimwengu. Kwa mfano, tumechunguza vyanzo vyake katika jamii za Kimagharibi, maeneo ya Mashariki na Afrika. Nadharia ya utanzu imetumika kuonyesha, uandishi wa riwaya za kiupelelezi ulivyowekewa kanuni za kuwaongoza waandishi katika miaka ya 1920 na 1930. Aidha sura hii imeangazia masuala yaliyosababisha chimbuko la riwaya ya kiupelelezi katika janibu za Afrika Mashariki, sababu za maendeleo yake na sifa zinazoupambanua utanzu huo na tanzu nyinginezo za fasihi ya Kiswahili.

Sura ya tatu imejihusisha na lengo la kwanza la tasnifu hii ambalo ni kutathmini jinsi usimulizi unavyotekelezwa katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Tumetumia baadhi ya vipengele vya nadharia ya naratolojia katika uhakiki wa usimulizi katika riwaya teule. Vipengele vya usimulizi vilivyochunguzwa ni sauti za kisimulizi na mtazamo. Suala la mtazamo limeangaziwa katika sawia nne. Sawia hizi ni; sawia ya kisaikolojia, sawia ya kiitikadi, sawia ya kimwanda-wakati na sawia ya kiisimu. Nayo sura ya nne imehusu lengo letu la pili la utafiti la kutathmini uhusika katika riwaya teule za kiupelelezi. Tumechunguza uainishaji wa wahusika na mbinu za usawiri wao katika kazi husika. Uchunguzi wa uhusika umeongozwa na misingi ya usawiri wa wahusika ya mwana-naratolojia Rimmon-Kenan (2002) pamoja na misingi ya uainishaji ya Forster (1986).

Sura ya tano imehusu suala la msuko. Kwa kuchunguza ujenzi wa msuko katika riwaya za kiupelelezi za Kiswahili, sura hii imejibu swali letu la tatu la utafiti ambalo lilikuwa, 'Je ni mbinu zipi za kimtindo zinazotumika katika ujenzi wa msuko wa riwaya za kiupelelezi. Sura hii imechunguza kwa kina mbinu zinazokuza msuko na zile zinazochelewesha ukunjufu wa msuko huo. Mwisho, sura ya sita inaonyesha matokeo ya utafiti huu na mapendekezo ya tafiti za baadaye.

## 6.3 Matokeo ya Utafiti

Kwa kujikita katika malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia za utanzu, umitindo na naratolojia, yafuatayo yaligunduliwa:

Katika utafiti huu, tumebaini kuwa riwaya ya kiupelelezi kijumla ina chimbuko lake katika mataifa ya Ulaya ya Uingereza na Ufaransa ambapo iliivuka pindi tu taasisi ya polisi ilipoanzishwa. Kupitia ukoloni uliohusu usambazwaji wa utamaduni, riwaya ya kiupelelezi ilienea kote duniani. Kwa hivyo, riwaya ya kiupelelezi haina mipaka ya kijiografia wala kijamii. Imo Afrika, mataifa ya Kimashariki na yale ya Kimagharibi. Hata hivyo, riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili si nakala ya moja kwa moja ya riwaya ya kiupelelezi ya Kimagharibi. Pana tofauti za kidhamira na kimtindo ndogondogo. Kwa mfano,riwaya za Mohammed Said Abdulla kando na kutumia mandhari ya Afrika Mashariki huhusu dhamira zinazoonyesha uhalisia wa eneo la Afrika Mashariki kama vile itikadi za kiutamaduni. Pia nyingi ya kazi za kiupelelezi za Kiswahili husimuliwa kupitia nafsi ya tatu huku zile za waasisi wa utanzu huu huko ulaya zikisimuliwa kwa nafsi ya kwanza.

Kuhusu usimulizi imegunduliwa kwamba, riwaya nyingi tunazohakiki zimesimuliwa katika nafsi ya tatu, yaani kwa mtazamo wa nje ambapo msimulizi si mshiriki katika masuala ayasimuliayo.

Kwa hivyo, kazi za Mohammed Said Abdulla, Ben Mtobwa, Faraj Katalambulla, Geofrey Levi na John Simbamwene zimo katika mtindo huu. Baadhi ya riwaya za Elvis Musiba, *Njama* na *Kufa Kupona,* zinatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza ambapo mhusika mpelelezi, Willy Gamba, ndiye msimulizi na masuala mengi ayasimuliayo yanadhihirisha mtazamo wake. Uchunguzi huu umegundua kuwa mtazamo hujitokeza katika ngazi nne. Hizi ni ngazi za kiitikadi, kisaikolojia, kimwanda-wakati na kiisimu. Sawia hizi zinaingiliana na kuchangizana kwani sawia moja huweza kufumbata sawia nyinginezo ndani yake. Kwa mfano, utafiti huu umebaini kuwa katika sawia ya kisaikolojia, vipengele vya kiisimu kama vile maneno yaonyeshayo hisia na fikira hutumika ili kudhihirisha hisia mbalimbali katika usimulizi. Kwa hivyo, sawia ya kiisimu hutumika kuchimuza sawia ya kisaikolojia. Vile vile mtazamo katika sawia ya mwanda-wakati huonyeshwa kwa kutumia vipengele vya kisarufi kama vile viashiria vya mahali na wakati. Viashiria hivyo vinaonyesha umbali uliopo baina ya msimulizi na msomaji.

Mtazamo ndani una ushawishi zaidi kuliko mtazamo nje kwa msomaji kwa vile katika mtazamo ndani, msimulizi ni mshirika katika masuala ayasimuliayo kinyume na hali ilivyo katika kazi zinazosimuliwa katika mtazamo nje ambapo msimulizi anaripoti tu mambo aliyoyasikia ama kuyaona kwingine. Riwaya nyingi zilizoteuliwa na kuhakikiwa katika utafiti huu zimetumia mtazamo ndani. Imebainika pia kwamba suala la simulizi tegemezi halijitokezi kwa uwazi katika riwaya tunazohakiki. Hii inatokana na kweli kwamba katika riwaya za kiupelelezi, msuko huwa sahili. Kama sifa ya kiutanzu, riwaya za kiupelelezi, hukusudiwa kuburudisha na kwa sababu hii, misuko yake haifai kuwa na uchangamano unaoweza kutatiza usomaji. Hata hivyo, baadhi ya riwaya za Mohammed Said Abdulla zina sifa ya hadithi tegemezi.

Katika uchunguzi uliohusu lengo la pili la kutathmini uhusika katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, imeonyeshwa kuwa wasifu wa wahusika unaweza kuwasilishwa kwa njia ya moja kwa moja ama kwa njia ya kiishara. Usawiri wa wahusika kiishara unaweza kufanywa kwa njia kadhaa kama vile kwa kutumia analojia, majazi na mandhari. Utafiti huu umegundua kwamba kuna uhusiano wa karibu baina ya wasifu ndani wa mhusika na wasifu nje ambapo hali ya kisaikolojia aliyo nayo mhusika inaweza kujidhihirisha katika umbo la nje la mhusika huyo. Vilevile, hali ya mwonekano wa nje inaweza kuashiria umbo ndani (hali ya kisaikolojia) la mhusika. Katika riwaya za kiupelelezi, sifa ya ubapa imetumika kwa njia maalum kuwasawiri wahusika wakuu ambao ni wapelelezi na wahalifu. Wao wamesawiriwa waking'ang'ana kudumisha utulivu na amani huku

wakipinga uovu wa mhalifu. Nao wahusika wahalifu wamesawiriwa wakiendeleza uovu tu kupitia vitendo vyao vya kuendeleza uhalifu.

Imebainika pia kwamba uhusika wa mhusika mpelelezi ni changamano kwa kuwa aghalabu hujitokeza kama kundi la watu watatu. Hawa ni mpelelezi wa polisi aliyeajiriwa na serikali, mpelelezi wa kibinafsi na msaidizi wake. Hii ndio hali tunayoiona katika riwaya za Mohammed Said Abdulla na riwaya ya *Simu ya Kifo* ya Faraj Katalambulla. Vilevile, katika riwaya za Ben Mtobwa hali ni kama hiyo, isipokuwa mpelelezi wa kibinafsi hana msaidizi maalum ila marafiki wa kike. Kando na utatu huu unaomhusu mhusika mpelelezi, pia kuna utatu mwingine unawahusu wahusika wakuu kijumla. Yaani, wahusika wakuu wanaweza kuwekwa katika kategoria tatu ambazo ni mhusika mhalifu, mhusika mpelelezi na mhusika mhasiriwa. Msuko wa riwaya ya kiupelelezi unawahusu wahusika hawa kwa kiasi kikubwa sana. Mhusika mhasiriwa ndiye hutambulishwa kwanza kwa sababu uhalifu unamwathiri yeye kabla ya wahusika wengine. Mhusika wa kiupelelezi naye hutambulishwa kwa wasomaji baada ya mhusika mhasiriwa na mwisho, baada ya uchunguzi kukamilika mhusika mhalifu naye hujulikana kwa wasomaji.

Imebainishwa pia katika uchunguzi huu kwamba mhusika msaidizi wa mpelelezi naye husawiriwa kwa njia maalum. Yeye huwa rafiki wa dhati wa mpelelezi wa kibinafsi lakini asiye na maarifa mengi kama yeye. Aidha, pale pasipo na msaidizi huyu, mhusika wa kike ambaye pia ni rafiki wa mpelelezi wa kibinafsi huchukua wadhifa huo. Tumebaini pia kuwa, katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili, wahusika wapelelezi, wawe wa kibinafsi au wa polisi ni wa jinsia ya kiume. Utafiti huu umegundua kuwa kuna tofauti ndogondogo za kiutendakazi baina ya wahusika wapelelezi katika riwaya teule. Mpelelezi katika riwaya za Mohammed Said Abdulla anachunguza masuala ya kijamii kama vile ndoa, malezi, wizi na urithi. Mhusika mpelelezi katika kazi za Ben Mtobwa na kazi za Elvis Musiba anachunguza masuala ya kimataifa na kisiasa kama vile mapinduzi ya serikali, ukoloni mamboleo na mahusiano ya kimataifa hususan ukombozi wa mataifa ya Kusini mwa Afrika. Kwa hivyo, riwaya za Mtobwa na Musiba zinafanana sana kidhamira na kimtindo. Sifa hii ya kidhamira inazipa riwaya hizi jukumu la kisosholojia na kuzifanya zioane vyema na muktadha zilimoandikiwa. Upelelezi uliopo katika kazi za Godfrey Levi unahusu uhalifu unaotekelezwa mijini na hivyo ni uhalifu katika viwango vidogo sawa na riwaya za John Simbamwene. Kimtindo, riwaya za Levi na zile za Simbamwene zipo katika kiwango kimoja

kwani zinatumia lugha nyepesi mno, hazina wapelelezi wa kibinafsi, zina msuko mwepesi na wahusika wake hawajakuzwa vyema ikilinganishwa na kazi za Abdulla, Mtobwa na Musiba.

Tofauti nyingine ya kiutendakazi ni kwamba wapelelezi, Bwana Msa katika kazi za Abdulla, Willy Gamba katika kazi za Musiba na Far Katy Wingo katika *Simu ya Kifo* wanashindwa kuzuia ufanyikaji wa kitendo cha uhalifu, wakijitahidi tu kumshika mhalifu baada ya uhalifu huo kufanyika. Wingo kwa mfano, anachunguza mauaji ya Mzee Jacob na kabla hajamaliza mauaji mengine yanafanyika. Mwishowe, anashindwa kabisa kumpata muuaji. Mpelelezi Joram Kiango katika baadhi ya kazi za Mtobwa anazuia utekelezaji wa mauji kinyume na wapelelezi hawa wengine. Kwa mfano, katika riwaya ya *Salamu Kutoka Kuzimu* anazuia mauji ya marais wengi kwa sumu ambayo Proper alikuwa anataka kuwaua kwayo.

Kuhusiana na lengo letu la tatu ambalo ni kuchunguza mbinu zinazotumiwa katika ujenzi wa msuko, imebainika kwamba mbinu za kimtindo maarufu katika ujenzi wa msuko katika riwaya za kiupelelezi ni urejeshi, sadfa na taharuki. Imebainika kwamba urejeshi unaohusisha urejeleaji wa riwaya za awali za mwandishi mmoja ndio mbinu inayotumika kuzioanisha riwaya za mwandishi mmoja ili kuunda msururu mmoja. Hali hii imejitokeza kwa kina katika kazi za Mohammed Said Abdulla ambapo kila riwaya inarejelea ile iliyoitangulia. Mtindo huu pia umetumika katika baadhi ya riwaya za Ben Mtobwa. Pili, kuna urejeleaji wa visa mbalimbali vya awali katika riwaya moja, hali ambayo ni kawaida pia katika tanzu nyinginezo za riwaya. Imebainika pia kwamba mbinu ya taharuki inatumika kwa njia maalum katika utanzu wa riwaya za kiupelelezi. Hii ni mbinu ya kiutanzu inayozifanya riwaya hizi kuwavutia wasomaji na kuongeza uburudishaji wa riwaya husika. Waandishi hutumia mikakati kadhaa kujenga na kudumisha taharuki katika kazi zao ikiwemo usawiri wa mandhari kwa njia ya kiajabu, anwani za vitabu na kuwepo kwa vidokezo mwanzoni mwa hadithi ambavyo maana zake hazijafafanuliwa. Tumebaini kwamba mbinu ya kusawiri mandhari kwa namna ya kiajabu na kuogofya katika riwaya za kiupelelezi ni mkakati uliopitishwa kutoka riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi.

Mbinu nyingine iliyobainika kujitokeza kwa uwazi zaidi katika ujenzi wa msuko ni kuwepo kwa usambamba wa hadithi mbili. Hii ni sifa ya kiutanzu ambapo katika utanzu wa riwaya ya kiupelelezi, kuna hadithi inayohusu uhalifu inayojitokeza mwanzoni mwa hadithi na kisha inafuatwa na hadithi ya upelelezi ambayo ndiyo huchukua nafasi kubwa katika msuko. Hadithi inayohusu uhalifu huwa kama kitangulizi kwani inaweka wazi aina ya uhalifu uliofanywa kama

vile mauaji, wizi ama uhaini. Kufikia mwishoni mwa msuko, msimulizi huoanisha hadithi zote mbili anapotoa maelezo kuhusu mhalifu ni nani, alitekeleza uhalifu huo vipi na kwa nini. Maelezo ya mpelelezi pia yanaonyesha ni vipi yeye kama mchunguzi alivyomnasa mhalifu na mwisho huonyesha adhabu mhalifu anayopewa. Ni baada ya adhabu hii ndipo hadithi zote mbili hufika hatima na kuashiria urejeaji wa ile hali ya utulivu iliyokuwepo kabla ya uhalifu.

Ili kudhibiti mwendo wa usimulizi, tumebaini kwamba mikakati kadhaa hutumika. Mikakati hii husaidia msuko usifike kileleni mapema ili kuendeleza taharuki. Kuufikisha usimulizi kileleni haraka kunaweza kupunguza kiwango cha taharuki na kuifanya hadithi ya kiupelelezi kuwa chapwa. Baadhi ya mikakati hiyo ni matumizi ya misukumo pofu kama vile utokaji nje ya usimulizi, mazungumzo yanayorefushwa bila lengo maalum baina ya mpelelezi na mhalifu miongoni mwa mbinu nyinginezo.

## 6.4 Hitimisho

Utanzu wa riwaya za kiupelelezi umeonyesha kuathiriwa na riwaya za kiupelelezi za Kimagharibi kimuundo. Kwanza, athari hizo zinajidhihirisha kupitia uhusika kwa kuwa usawiri wa wahusika wakuu unafuatia mtindo uliowekwa na waasisi wa utanzu huu. Ubabe wa mhusika mpelelezi kwa mfano, umeendelea kudumishwa huku mhusika mhalifu akiendelea kuonyeshwa kama mshindwa. Pili, motifu ya wema kuushinda uovu na utoaji wa adili kuwa uovu haulipi imeendelea kuitawala miishio ya misuko ya kazi hizo. Miishio ya aina hii inashabihiana na tungo za kifasihi simulizi ambapo utoaji wa adili huwa sifa maalum katika baadhi ya vipera vya hadithi.

Tumeona kuwa utanzu wa riwaya ya kiuhalifu umekua na kujitanua katika vipera vingi kadri ya mpito wa wakati. Kwa hivyo, kando na vijitanzu vya riwaya za kiupelelezi na riwaya za kijazira, sasa kuna riwaya za kipolisi, riwaya za kijasusi na riwaya sisimuzi ya kibayolojia. Riwaya sisimuzi ya kibayolojia ni kipera kipya kinachohusu matumizi ya silaha za kemikali kama vile sumu badala ya zana asili za kivita kama bomu au bunduki. Mtobwa kwa mfano, amefanya jaribio la kuendeleza kipera hiki katika *Roho Ya Paka* (1996), ambapo mhusika Marlone na wanasayansi wawili wa kutoka Afrika Kusini wanajaribu kulipisha kisasi dhidi ya nchi za msitari wa mbele kwa kutumia sumu kali. Hata hivyo, wanashindwa katika jaribio hilo.

Umuhimu wa utafiti huu ni kwamba utakuwa msingi bora wa kurejelewa katika tafiti za baadaye zitakazohusu riwaya pendwa kijumla na riwaya za kiupelelezi. Hii ni kwa sababu kama

inavyoonyeshwa katika sehemu ya mapendekezo, utanzu wa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili una mapengo mengi yanayohitaji kutafitiwa. Kwa hivyo, tunahisi kuwa tasnifu hii itatoa mchango mkubwa katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Fauka ya hayo, tasnifu hii imejaribu kutetea nafasi muhimu ya fasihi pendwa ya Kiswahili na kuonyesha kuwa ina uwezo wa kumulika maswala mazito ya kijamii kama zilivyo riwaya dhati.

## 6.5 Mapendekezo

Tasnifu hii imechunguza vipengele vya kifani vya usimulizi, uhusika na msuko katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Kwa hivyo, kuna vipengele vingine vya kifani ambavyo havikuchunguzwa. Hivi ni matumizi ya lugha na mandhari. Mambo haya yanaweza kuchunguzwa katika riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili. Suala la mandhari kwa mfano, ni muhimu kwa kuwa katika riwaya za kiupelelezi, mandhari hutumika kwa njia maalum. Pia suala la muundo na usimulizi linaweza kuchunguzwa katika riwaya za waandishi wengine wa riwaya za kiupelelezi. Kazi yetu ilijifunga katika riwaya teule za Ben Mtobwa, Mohammed Said Abdulla, Elvis Musiba, John Simbamwene na Godfrey Levi. Watunzi wengine ambao riwaya zao zinaweza kuchunguzwa ni Eddie Ganzel, Hammie Rajab, Kassim Chande, Juma Mkabarah, Ntandu Abdul miongoni mwa wengine. Wahakiki wa baadaye pia wanaweza kuhakiki suala la usimulizi na muundo katika kazi za mwandishi mmoja. Zaidi ya haya, mhakiki anaweza kuyazamia masuala mengine katika usimulizi ambayo hatukuchunguza kama vile wakati, idadi-marudio na wakaa. Taharuki kama kipengele cha muundo wa msuko kina umuhimu na upana mkubwa unaopaswa kuchunguzwa katika kazi nyinginezo za kiupelelezi.

Tatu, kama tulivyoonyesha katika sehemu ya matokeo, riwaya ya kiupelelezi kando na kuwaburudisha wasomaji, pia inaangazia masuala muhimu ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ya jamii ya mwandishi. Kwa hivyo, utafiti zaidi unaweza kufanywa kudhihirisha jinsi riwaya ya kiupelelezi inavyotekeleza wajibu huu. Kama vile riwaya dhati inavyobadilika kiwakati na kuanza kufumbata masuala ibuka katika jamii kama vile masuala yanayohusu jinsia, dini, haki za kibinadamu, riwaya za kiupelelezi pia zimekua katika baadhi ya jamii na kuanza kuyamulika masuala haya. Katika jamii za Kimagharibi kwa mfano, riwaya hizi zimeanza kushughulikia masuala ya kiufeministi, mazingira na vijana. Kwa hivyo, pana haja ya utafiti zaidi ili kubaini ikiwa riwaya ya kiupelelezi ya Kiswahili imefikia upeo huu wa kuwa na: ufeministi katika riwaya

ya kiupelelezi, jinsia katika riwaya ya kiupelelezi, riwaya ya kiupelelezi ya vijana na watoto, riwaya ya kiupelelezi na mazingira mionngoni mwa maswala ibuka mengine.

Suala lingine muhimu linalofaa kuchunguzwa ni kwa nini hamna waandishi wengi wa kike katika utanzu huu. Vilevile, uchunguzi wetu umebaini kuwa waandishi wa riwaya za kiupelelezi kwa Kiswahili ni wachache mno katika mataifa ya Kenya na Uganda. Kufikia wakati wa ukusanyaji wa data ya utafiti huu, nchini Kenya kulikuwa na mwandishi mmoja tu wa riwaya za kiupelelezi kwa Kiswahili; Godfrey Levi. Hatukupata hata riwaya moja ya kiupelelezi ya mwandishi wa kutoka Uganda. Kwa hivyo, utafiti zaidi unaweza kufanywa kuelezea sababu za hali hizi. Kutokana na hali hii, pana haja ya waandishi zaidi kuibuka katika mataifa ya Kenya na Uganda na kuandika katika utanzu huu ili kuukuza zaidi. Fauka ya hayo, baada ya vifo vya waandishi mashuhuri wa riwaya za kiupelelezi wa Tanzania kama vile Mohammed Said Abdulla, Ben Mtobwa na Elvis Musiba ni vyema kwa waandishi wengine kujizatiti kuhakikisha kuwa utanzu haufifii.

Mwisho, itafaa kuchunguza jinsi tanzu nyinginezo za kifasihi kama vile drama, hadithi fupi na mashairi zinavyolishughulikia suala la upelelezi. Swali la kuzingatia ni ikiwa kuna tofauti au mfanano wa kimuundo, kisimulizi au kimsuko baina ya riwaya za kiupelelezi na hadithi fupi au tamthilia za kiupelelezi? Kwa hivyo, hili pia ni eneo la kufanyiwa uchunguzi zaidi ili kuweka wazi suala hili. Aidha, kazi hizi za kiupelelezi zinaweza kuchunguzwa kwa misingi ya nadharia nyinginezo kama vile uhalisia, ubaadaukoloni, sosholojia ya fasihi, umaksi miongoni mwa nyinginezo.

## 6.6 Changamoto za Utafiti Huu

Wakati wa utafiti huu, tulipata changamoto kadhaa. Tatizo kubwa lilihusu utafsiri wa dhana nyingi kutoka kwa lugha ya Kiingereza hadi kwa Kiswahili kwa kuwa matini nyingi zilizohusu masuala ya kinadharia zipo katika Kiingereza. Pili, nchini Kenya kuna uhaba wa riwaya za kiupelelezi za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wa awali kama vile Mohammed Said Abdulla na Faraj Katalambulla. Mtafiti alilazimika kunakilisha baadhi ya riwaya kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960) kutoka maktabani. Tatizo lingine lilikuwa la usafiri kuenda maktabani na chuoni kutokana na vikwazo vya Covid-19. Hali hii ilitulazimu mara nyingine kuchelewa kurudisha ripoti za maendeleo ya utafiti chuoni.

MAREJELEO

Abdulla, M. S. (1958). *Mzimu wa Watu wa Kale*. Nairobi: East African Literature Bureau.

________________(1960). *Kisima cha Giningi.* Nairobi: Evans Brothers Ltd.

________________(1973). *Duniani Kuna Watu*. Nairobi: East African Publishing House.

________________(1974). *Siri ya Sifuri*. Nairobi: East African Publishing House.

________________(1975). *Mke Mmoja Waume Watatu*. Nairobi: East African Publishing House.

________________(1976). *Mwana wa Yungi Hulewa.* Nairobi: East African Publishing House.

________________(1984). *Kosa la Bwana Msa*. Nairobi: East African Publishing House

Abbot, H. P. (2002). *The Cambridge Introduction to Narrative.* Cambridge: Cambridge University Press.

Adam, S. A. (1978). *Kuli.* Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Althusser, L. (1971). *Lenin and Philosophy and Other Essays*. New York & London: Francois Maspero Publishers

Arege, T. (2012). "Narration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Ras'l Ghuli" Unpublished Ph.D. Dissertation. University of Nairobi. (Haijachapishwa).

Anyango, P. A. (2016) 'Usawiri wa Uovu katika Riwaya Teule za Ben R. Mtobwa', Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Arnold, H. A. (1984). "Popular Literature in Tanzania" katika *Jarida la Kiswahili, Juzuu 51/1 na 51/2*. Dar es Salaam: TUKI.

Bajaj, A. (2015). 'Analysing the Detective Fiction of Agatha Christie: Two Approaches'. Unpublished PhD Thesis. Kamaun University Nainital.

.Bal, M. (2017). *Narratology; Introduction to the Theory of Narrative*. 4th Edition. Toronto: University of Toronto Press.

Bandura, A. (1976). *Social Learning Theory*. New York: Prentice-Hall.

Bentley, E. C. (2008). *Trent's Last Case.* London: House of Stratus.

Bjornson, R. (2002). *Writing & Popular Culture in Cameroon*, in Newell, (ed) *Readings in Africa Popular Fiction.* Indianapolis: Indiana University Press.

Brenn, E. W. (1973). *Alfu -Lela-Ulela*. Nairobi: Longman Publishers.

Bynion, T. J. (2001). *Murder Will Out; The Detective in Fiction.* New York: Palgrave Publishers.

Cawelti, J. (1987). *The Spy Story*. Chicago: University of Chicago Press.

Chandler, R. (1988). *The Simple Art of Murder*. New York: Vintage Books.

Chatman, S. (1978). *Story and Discourse.* New York: Cornell University Press.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi Katika Riwaya za Shaaban Robert.* Dar es Salaam: Taasisi ya Taluma za Kiswahili.

Culpeper, J. (2002). *Language and Characterisation: People in Plays and Other Texts* Harlow: Longman.

Danyte, M. (2011). *Introduction to the Analysis of Crime Fiction*. Kaunas: Vytautas Magnus Universty Press.

Derrida, J. (1981). *The Law of Genre.* In W. S.T. Mitchell (ed) *On Narrative*. Chicago. University of Chicago Press.

Dickens, C. (1853). *The Bleak House.* London: Bradbury and Evans.

Dow, U. (2002). *The Screaming of the Innocent.* Gaborone: Spinifex Press.

Doyle, C. (1887). *A Study in the Scarlet.* Spencer and Blacket: London.

Ebersohn, W. (1981). *Divide the Night.* Johannesburg: Vintage Books.

_______________(2009). *October Killings.* Johannesburg: Vintage Books.

_______________(2019). *African Aftermath*. Johannesburg: Vintage Books.

Evans, M. et al. (2019). *Detecting the Social: Order and Disorder in Post-1970s Detective Fiction.* London: Palgrave Macmillan.

Freud, S. (1905). *Three Essays on the theory of Sexuality*. New York: Prentice-Hall.

Forster, E. M. (1986). *Aspects of the Novel.* London: Harcourt, INC.

Fowler, R. (1986). *Linguistic Criticism,* Oxford: Oxford University Press.

.Ganzel, E. (1972). *Ndoto ya Mwenda Wazimu.* Nairobi: East Africa Literature Bureau.

____________(1978). *Jogoo la Shamba.* Nairobi: East Africa Literature Bureau.

____________(1984). *Kitanzi*. Dar es Salaam: Utamaduni Publishers.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay in Method.* Ithaca: Cornell University Press.

Green, K. (1878). *The Leavenworth Case*. New York: G.P Putnam's Sons.

Gromov, M. D. (2008). *Swahili Popular Literature in Recent Years*. Katika *Swahili Forum* 15.

____________ (2008). 'Mahojano na Ben R. Mtobwa' katika *Swahili Forum* 15, uk.135-140.

____________ (2012). 'Generic Innovations in Recent Swahili Crime Fiction by Ben Mtobwa and Aristablus Elvis Musiba In Oed, A. na Matzke, C. (eds), *Life is a Thriller: Investigating African Crime Fiction.* Koln: rudiger Koppe Velarg.

Hartmann, J. (2008). *The Marketing of Edgar Allan Poe*. New York: Routledge.

Holman, C. H. (1972). *A Handbook To Literature.* Michigan: Odyssey Press.

Howard, H. (1942). *Murder for Pleasure; The Life and Times of the Detective Story*. London: Appleton-Century Company.

_______________ (ed.) (1992). *The Art of the Mystery Story: A Collection of Critical Essays*. New York: Carroll & Graf,pp.71-109

Hussein, E.N. (1971). "Ufundi wa M. S. Abdulla." Katika Topan. F. (mha). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Katalambulla, F. H. (1965). *Simu ya Kifo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Karin, B. (2018). *A History of African Popular Culture.* New york: Cambridge University Press.

Kassam M. K. (1982). *Mpango.* Dar es Salaam. International Publishers Agencies Limited.

Kezilahabi, E. (1975). “Riwaya za kiupelezi katika Afrika Mashariki” katika Jarida la Kiswahili, Juzuu 45/2. Dar es Salaam: TUKI.

____________(1980). “The Swahili Novel and the Common Man in East Africa” in *The East Africa Experience: Essays on English and Kiswahili Literature.* Schield, U.(ed).

Berlin: Reimer.

Kimura, E. (1992). *Mabadiliko ya Kijamii na Riwaya ya Upelelezi Tanzania*. Tokyo: Tokyo University of Foreign Studies Press.

Kiriamiti, J. (1984). *My Life With A Criminal.* Nairobi: SpearBook Publishers.

_____________(1984). *My life in Crime.* Nairobi: SpearBook Publishers.

Kisurulia E. S. (2012). “Point of View in the Kiswahili Novel; A Naratological Analysis of the Selected Texts”. Unpublished Ph.D dissertatio. University of Nairobi.

Kitereza, A. (1980). *Bwana Byombekera na Bibi Bugonoka: Ntulunalyo na Bulihwali*. Dar es Salaam: TanzaniaPublishing House.

Khamis, S.A.M (2012) ‘Is Abdulla’s Bwana Msa in *Mzimu wa Watu wa Kale* Conan Doyle’s Sherlock Holmes in Disguise? In Oed, A. na Matzke, C. (eds), *Life is a Thriller: Investigating African Crime Fiction.* Koln: rudiger Koppe Velarg.

Knight, S. (1980). .*Form and Ideology in Crime Fiction.* London: The Macmillan Press Ltd.

_____________(2003). *Crime Fiction, 1800-2000: Detection, Death, Diversity*. London: Palmagrave Macmillan.

Knox, R. A. (1992). ‘Detective Story Decalogue’, in *The Art of the Mystery Story: A Collection of Critical Essays*, ed. Howard Haycraft, New York.

Kurtz, J. R. (1998). *Urban Obsessions and Urban Fears: The Postcolonial Kenyan Novel*. Trenton: Africa World Press

Kwei, Q. (2009). *Wife of the Gods.* Accra: Random House Paperbacks.

___________(2011). *Children of the Street.* Accra: Random House Paperbacks.

____________(2014). *Murder at Cape Three Points.* Accra: Soho Crime Publications.

____________ (2020). *The Missing American.* Accra: Soho Crime Publications.

Leech, G. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry.* London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. & Short, M. (2007). *Style in Fiction: Linguistic Introduction to English Fiction Prose.* London: Longman Group Ltd.

Levi, G. (1975). *Mpelelezi Hodari na Genge la Wahalifu.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

_________(1985). *Fedheha ya Fedha*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Lukacs, G. (1972). *The Meaning of Contemporary Realism.* London: Merlin Press.

Madumullah, J. (1988). "Riwaya ya Kiswahili (Tanzania) katika Miaka ya Themanini", katika *Mulika, juzuu 20.* Dar es Salaam: TUKI.

Madumullah, J. S. na Mlacha, S. A. K. (1995) *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Dar Salaam University Press.

Mabala, R. (1989). "Popular Literature in Tanzania", Makala iliyosomwa katika Mkutano wa 15 wa Chama cha Fasihi ya Kiafrika. Dakar, Senegal.

Maillu, D. (1973). *Unfit For Human Consumption*. Nairobi: Combbooks.

_____________(1983). *My Dear Bottle.* Nairobi: Spear Books.

_____________(1974). *After 4:30.* Nairobi: Combbooks.

_____________(1974). *Trouble.* Nairobi: Combbooks.

_____________(1976). *No.* Nairobi: Combbooks.

_____________(1983). *Assassins on Safari.* Nairobi: Combbooks Publishers.

.Malmgren, C. (2001). *Anatomy of Murder: Mystery, Detection and Crime Fiction.* Bowling Green: Bowling Green University Press.

Mandel, E. (1984). *Delightful Murder: A Social History of the Crime Story.* Minneapolis: Universiy of Minnesota Press.

Mangua, C. (1971). *Son of Woman.* Nairobi: SpearBooks Publications.

______________(1984). *Son of Woman in Mombasa*. Nairobi: SpearBooks Publications.

Masondo, M. M. (1994). *Kanti Nawe?* Cape Town: Reach Out Publishers.

______________(1994). *Ngaze Ngazenza.*Cape Town: Reach Out Publishers.

______________(2004). *Sixololo.* Cape Town: Reach Out Publishers.

Massoud. S. M. (2013). "Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi katika Tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*". Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Mayers, D. (1999). *Dead Before Dying.* London. (Trans.M.Van. Bijon): Hodder and Stoughton Publishers.

___________(2003). *Heart of the Hunter*. London. (Trans.M.Van. Bijon): Hodder and Stoughton Publishers.

___________(2009). *Blood Safari.* London. (Trans.M.Van. Bijon): Hodder and Stoughton Publishers.

Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mbuthia, E. M, (2005). "A Stylistics and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories". Ph.D. dissertation. Deutschland:VDM Dr Muller Gmbh& Co.KG

Mbughuni, P. (1978). "From Oral to Written: The Politization of Kiswahili Literature".

Unpublished Ph.D. dissertation. University of Indiana

Meja, M. (1973). *Kill Me Quick.* Nairobi: East African Educational Publishers.

____________(1976). *Going Down Riverroad.* Nairobi: East African Educational Publishers. Publishers.

____________(1979). *Cockroach Dance.* Nairobi: East African Educational Publishers

Mgeni, A. (1983*). "The Elements of Mystery in the novels of Mohamed Said Abdalla".* Jarida la Kiswahili Toleo la 50/2. Dar es Salaam: TUKI.

Mkabarah, J. S. A. (1985). *Mbio za Kipofu*. Dar es Salaam: Utamaduni Publishers.

Mlacha. S. A na Madumulla. J. J. (1995) *Riwaya ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohamed, M. S. (1978). *Nyota ya Rehema.* Nairobi: Oxford University Press.

____________ (2000). *Kiu*. Longhorn Publishers.

Mohamed. S. A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili; Riwaya, Tamthilia na Hadithi Fupi*. Nairobi: East African Education Publishers.

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (1981). *Nitakuja kwa Siri.* Dar es Salaam. University of Dar es Salaam.

__________ (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: East. African.Education Publishers

Mtobwa, B. (1983). *Lazima Joram Ufe.* Nairobi: East African Educational Publishers.

__________(1993). *Najisikia Kuua Tena.* Nairobi: East African Educational Publishers.

___________(1993). *Salamu Kutoka Kuzimu*. Nairobi: East African Educational Publishers.

___________(1993). *Tutarudi na Roho Zetu?.* Nairobi: East African Publishers.

___________(2004). *Mtambo wa Mauti.* Nairobi: East African Publishers.

Mugenda, O. & Mugenda, G. (2003). *Research Methods: Quantitive and Qualitative Approaches*: Nairobi. ACTS Press.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. Nairobi: East Africa Education Publishers.

Mulokozi, M. (1996). ‘A Survey of Kiswahili Literature: 1970-1988’ katika *Afrika Focus*. Vol.8, Issue1 pp. 49-61.

.Musiba. A. E. (1981). *Njama.* Dar es Salaam: Continental Publishers.

__________(2000). *Uchu.* Dar es Salaam: East African Educational Publishers.

Mwamzandi, I. (2013). “Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi”, katika *Swahili Forum* 20.

Ndii, A. (1976). *A brief Assignment.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Newell, S. (2002). *Readings in African Popular Fiction*. Indianapolis: Indiana University Press.

Niccoye, M. (1983). *Manamba*. Dar es Salaam: International Publishers.

.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Wafula, R. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Obiechina, E. (2008). *Market Literature in Nigeria*. Online article accessed on 25.5.2020.http://ro.uow.edu.au/kunapipi/vol 30/iss2/11.

Oed, A. na Matzke, C. (eds) (2012). *Life is a Thriller: Investigating African Crime Fiction.* Koln: rudiger Koppe Velarg.

Ohly, R. (1981). *Aggressive Prose.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Park, J. K. (2004). "The Oral-Written Interface in the Kiswahili Ficional Prose". Unpublished, Ph.D. Dissertation. University of Nairobi.

Philips, B. (2016). "Crime Fiction: A Global Phenomenon." In *Journal of Literature and Librianship, Vol.5, Issue 1- Autumn 2016.*

Poe, E. A. (1841). "The Murders in the Rue Morgue" In *The Grahams Magazine*. London.

______________(1842). 'Mystery of Marie Roget' in *Burton's Gentleman's Magazine.* London.

______________(1844). 'The Purloined Letter' in *Burton's Gentleman's Magazine*. London.

Priestman, M. (1998). *Crime Fiction: From Poe to the Present*. Plymouth: Northcote House in Association with the British Council.

Reuster-Jahn (2012) *Police and judiciary corruption in Tanzanian crime novels* In Oed, A. na Matzke, C. (eds), *Life is a Thriller: Investigating African Crime Fiction.* Koln: rudiger Koppe Velarg.

Rimmo-Kenan, S. (2002). *Narrative Fiction: Contemporary Poetic.* London: Routlege.

Roberts, E. V. (1995). *Writing about literature*. New Jersey: Prentice Hall, Inc.

Robert. E. H. (1998). *Reading Illustrated Fiction in Late Imperial China.* Stanford: Stanford University Press.

Rodway, A. (1970). "Generic Criticism: The Approach Through Type, Mode and Kinds" in *Contemporary Criticism,* (eds) Brodbury, M. et al. London: Oxford University Press.

Romero, I. (2015). "Imperialism, Modernity and Literature: Why Detective Fiction Did Not Become Popular in Mexico". In the journal of Keio Communication Review No.37, 2015.

Rowland, S. (2001) *From Agatha Christie to Ruth Rendell: British Women Writers in Detective and Crime Fiction*. London: Palgrave Macmillan.

Ruheni, M. (1975). *The Mystery Smugglers.* Nairobi: Spear Book Publishers.

Said, E. (1977). *Orientalism*. London: Penguin Publishers.

Samantha E. B. (2014). 'The Production and Perception of Deon Mayer's Works; An Evaluation of the Factors Contributing To Bestseller's Status'. In *The Journal of Scrutiny 2*. University of Pretoria.

Sayers, D. L. (1992). 'Introduction to *The Omnibus of Crime*' (1928), in *The Art of the Mystery Story: A Collection of Critical Essays*, (ed), Howard. New York: Dover Publications

Scaggs, J. (2005). *Crime Fiction*. London & New york: Routledge Publications.

Senghor, L. (1976). *Prose and Fiction*. London: Heinemann Publishers.

Shaaban, R (1951) *Kusadikika*. Dar es Salaam. Nelson Publishers.

__________(1952). *Adili na Nduguze.*University of Califonia: MacMillan Publishers.

___________(1968). *Utubora Mkulima.* Dar es Salaam. Nelson Publishers.

Simbamwene, J. M. (1972). *Kwa Sababu ya Pesa.* Dar es Salaam: Longman

Simpson. P. (1993). *Language, Ideology and Point of View*. London: Routledge.

___________(2004). *Stylistics; A Students Handbook.* London: Routledge.

Smith. M. (2002). The *Kalahari Typing School for Men.* London: Polygon Books.

____________(2003). *The Full Cupboard of Life.* London: Polygon Books.

____________(2004). *In the Company of Cheerful Ladies.* London: Polygon Books.

Strinati, D. (2004). *An Introduction to the Theories of Popular Culture*. London: Routledge.

Svendsen,.F.H. & Pierce, K.A. (2010). .*A philosophy of Evil*. Chicago: Dalkey Archive Press.

Symons, J. (1993). *Bloody Murder: From the Detective Story to the Crime Novel*, (3rd revised edn). New York: The Mysterious Press.

Swaleh, A. (2011). "A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in Selected Swahili Novels". Unpublished Ph.D. dissertation: University of Nairobi.

Tiholwe, D. (2008). *Ancient Rites*. Cape Town: NB Publishers.

__________(2012). *Counting Coffins.* Cape Town: Kwela Publishers.

Todorov, T. (1977). *The Poetics of Prose*. Blackwell, Oxford: Oxford University Press.

Uspensky, B. (1973). *A Poetics of Composition.* Berkeley: University of California Press.

Van-Dine, S. S. (1992). 'Twenty Rules for Writing Detective Stories', in *The Art of the Mystery Story: A Collection of Critical Essays*, ed. Howard Haycraft, New York,Carroll & Graf.

Veseska, M. (2014). 'History, Development and Characteristics of British Detective Novel and the Significant Representatives of the Genre'. Unpublished Bachelors' Thesis: Palacky University Olomouc.

Wallek, R. & Warren. A. (1973). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.

Wamitila, K.W. (1999). 'What's In a Name: Towards Literary Onomastics In Kiswahili Literature'. In the Journal of *Swahili Forum*, Vol. 63.

______________(2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

______________(2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

______________ (2008). *Kanzi ya Fasihi 1*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Wanjala, C. L. (1978). *The Season of Harvest: Some Notes on East African Literature*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

___________ (1980). "Imaginative Writing since Independence: The East African Experience" in *The East African Experience: Essays on English and Kiswahili Literature.* Second Janheinz Jahn Symposium: Deitrich Reiner Verlag.

______________(1981). "The Growth of A Literary Tradition in East Africa", In Journal of Modern African Studies. Vol. 11.

Wright A. M. (1989) "On Defining the Short Story" in *Short Story Theory at Crossroads,* (eds) Lohaffers, et al. Lousiana. Lousiana State University.

Yenjela, D. (2017). "Narrated Histories in Selected Kenyan Novels 1963-2012". Unpublished Ph.D. dissertation. Stellenbosch University.